

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA KUMI NA TANO

Kikao cha Saba – Tarehe 10 Aprili, 2019

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa, tukae.

Katibu!

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, (SERA, BUNGE, KAZI, VIJANA, AJIRA NA WENYE ULEMAVU):

The follow-up Report on the Implementation of the Controller and Auditor General's Recommendations for the five performance Audit Reports Issued and tabled to the Parliament on April, 2015.

NAIBU WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):

(i) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali juu ya Taarifa za Fedha kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018 za Mamlaka za Serikali za Mitaa.

(ii) *Performance Audit Report on Monitoring of Building Works in Urban Areas as Performed by the President's Office – Region Administrations and Local Government.*

(iii) Taarifa ya Majibu ya Serikali na Mpango Kazi wa Utekelezaji wa Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2018.

(iv) Taarifa ya Majibu ya Serikali kuhusu Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (*LAAC*) kwa Mwaka wa Fedha 2016/2017.

(v) Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, UTUMISHI NA UTAWALA BORA:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 naomba kuwasilisha.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa na Majukumu ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka 2019/2020.

MHE. DANIEL E. MTUKA – K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGESA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA (K.n.y. MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA NA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA):

Taarifa ya Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kuhusu Makadirio na Mapato ya Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA:

- (i) Ripoti ya jumla ya Ukaguzi wa Ufanisi na Ukaguzi Maalum kwa kipindi kinachoishia tarehe 31 Machi, 2019.
- (ii) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Taarifa za Fedha za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018.
- (iii) Ripoti Kuu ya Mwaka ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018.
- (iv) Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kuhusu Ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha 2017/2018.
- (v) *The Annual General Report of the Controller and Auditor General on the Audit of Information Systems for the Year ended 30th June, 2018.*
- (vi) *The Performance Audit Report on Management of Bulk Procurement of Government of vehicles as performed by the Government Procurement service Agency.*
- (vii) Majumuisho ya majibu ya Hoja na Mpango wa kutekeleza Mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa

Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI:

- (i) *The Performance Audit Report on the Management of Water Projects in Rural Areas.*
- (ii) *The Performance Audit Report on the Management of Water Supply projects from Borehole Sources in Tanzania as Performed by the Ministry of Water.*

NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):

- (i) Ripoti ya Ukaguzi na Usimamizi wa Shughuli za Ujenzi wa Miradi ya Maji na Umwagiliaji, (*The Performance Audit Report on Management of Construction Activities on Irrigation Projects*).
- (ii) Ripoti ya Ukaguzi na Utendaji kuhusu Upatikanaji na uwezo wa kupata Pembejeo Bora za Kilimo, yaani mbegu na mbolea kwa Wakulima yaani *The Performance Audit Report on Availability and Accessibility of Good Quality Agricultural Inputs (seeds and fertilizers) to farmers*.

NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

- (i) Ripoti ya Ukaguzi kuhusu Utoaji wa Huduma za Dharura na Rufaa katika Hospitali za Rufaa (*The Performance Audit Report on Management of provision of Referral and Emergency Healthcare Services in Higher Level Referral Hospitals as performed by the Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children*).
- (ii) Ripoti ya Ukaguzi wa kuhusu utoaji huduma Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (*The Performance Audit on Management of Provision of National health Insurance service as Performed by The Ministry of Health, Community Development, Gender, Elderly and Children and National Health Insurance Fund*).

NAIBU WAZIRI WA NISHATI:

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018 kuhusu *Performance Audit Report on Maintenance of Power Generation Plants*.

NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:-

Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Juni, 2018 kuhusu Ufanisi juu ya Usimamizi wa Elimu kwa Wanafunzi Wenye Mahitaji Maalum (*The Performance Audit Report on Management of Education for Pupils with Special Needs. A Report of the Controller and Auditor General March, 2019*).

NAIBU SPIKA: Ahsante, Katibu.

NDG. STEPHEN KAGAIGAI – KATIBU WA BUNGE:

MASWALI NA MAJIBU

NAIBU SPIKA: Tunaanza na Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, swali lake litaulizwa kwa niaba yake na Mheshimiwa Omari Kigua.

Na. 53

Hitaji la Hosteli za Wanafunzi – Mufindi Kusini

MHE. OMARI M. KIGUA (K.n.y. MHE. MENDRAD L. KIGOLA) aliliza:-

Sekondari za Jimbo la Mufindi Kusini zinakabiliwa na tatizo la hosteli kwa ajili ya wanafunzi wanaotoka mbali:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kujenga hosteli kwa kila sekondari katika Jimbo la Mufindi Kusini?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mbunge wa Mufindi Kusini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi ina shule za sekondari 43 ambapo kati ya hizo shule 21 zina daharia (*hostel*). Katika mwaka wa fedha 2018/2019, shule nyingine mbili za sekondari za Ihowanza na Mninga zinaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa hosteli ili kufanya idadi ya shule zenye hosteli kufikia 23.

Aidha, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Halmashauri ya Wilaya ya Mufindi imetenga kiasi cha shilingi milioni 60 kuititia mapato ya ndani ili kusaidia ukamilishaji wa daharia zilizopo katika hatua ya ukamilishaji. Vilevile Lyara in Africa wamepanga kusaidia ujenzi wa hosteli katika Shule za Sekondari za Kiyowela na Idunda na CAMFED wamesaidia ujenzi wa hostei ya Ihowanza.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Omari Kigua, swali la nyongeza.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri sana ya Mheshimiwa Naibu Waziri lakini nina maswali mawili, kama ifutavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza, changamoto ya hosteli ambayo imejitokeza katika Jimbo la Mufundi Kusini haitofautiani sana na hali iliyopo katika Jimbo la Wilaya ya Kilindi. Ni ukweli usiopingika kwamba suala la hosteli ni kitu muhimu sana kwa sababu linachangia katika ufaulu wa watoto wetu. Je, Serikali iko tayari sasa kuhakikisha kwamba shule zote za vijijini ambazo watoto wanatembea kwa umbali mrefu zinakuwa na hosteli?

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili ni kwamba katika Jimbo la Kilindi ipo Shule ya Kwamkalakala ambayo ni miongoni mwa shule kumi za mwisho ambazo zimefanya vibaya kutokana na kutokuwa na hosteli. Je, Serikali ipo tayari kutoa msaada maalum kuhakikisha kwamba shule ile inajengewa hoteli? Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge wa Kilindi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la kwanza anataka kujua kama Serikali iko tayari kujenga hosteli kwenye shule zote za sekondari. Ni ukweli usiopingika kwamba hakuna mtu ambaye anapinga kutokuwa na hosteli katika shule zetu, zimeonesha tija na hasa kusaidia watoto wa kike waweze kupata muda mwingi wa kujisomea na kuweza kufanya vizuri katika masomo yao ambaao pia wamekuwa wakifanya vizuri wale ambaao wamebahatika kusoma vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunao mpango kuititia *EPforR*, tumepeleka fedha katika hosteli zetu na Kilindi wamepata hosteli moja ambayo nilienda kuitembelea. Tutaendelea kufanya hivyo kwa mwaka wa fedha huu ambaao tumeleta bajeti leo mezani kwenu, Waheshimiwa Wabunge watunge mkono ikishapita tutaangalia namna ya kuboresha.

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, tunawaomba wadau wote na Watanzania popote walipo hili jambo la kujenga hosteli za watoto wa kike katika shule zetu ni jambo shirikishi. Sisi Wabunge tushirikiane na wananchi wengine na Serikali tutasaidia kadri tutakavyokuwa na uwezo wa fedha wa kufanya jambo hilo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swalii la pili, Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swalii lake.

Na. 54

**Mchango wa Halmashauri kwa Vikundi vya
akina Mama- Kigoma**

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE aliuliza:-

Wanawake Mkoani Kigoma wameitikia wito wa kujunga katika vikundi vya ujasiriamali kama vile vikundi vya kilimo cha muhogo, kurina na kuchakata asali na VICOBA:-

Je, Halmashauri za Wilaya za Mkoa wa Kigoma zimechangia kiasi gani kwa vikundi hivyo kama sheria inavyotamka?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA
SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Josephine Johnson Genzabuke, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri za Mkoa wa Kigoma zilitoa shilingi milioni 250 kwa ajili ya vikundi vya wanawake na vijana. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 129 zilitolewa kwa vikundi vya wanawake. Aidha, katika mwaka wa fedha 2018/2019 hadi Februari 2019, Mkoa wa Kigoma umetoa shilingi milioni 249 kwa ajili ya vikundi 171 vya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu. Kati ya fedha hizo shilingi milioni 181 zimetolewa kwa vikundi 120 vya wanawake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Rais - TAMISEMI itaendelea kusimamia sheria inayozitaka Halmashauri kutenga, kutoa mikopo na kusimamia marejesho ya fedha hizo kutoka kwenye vikundi vilivyonufaika. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Josephine Genzabuke, swalii la nyongeza.

MHE. JOSEPHINE J. GENZABUKE: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu maswali mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kabla ya kuuliza swalii langu, naomba nichukue nafasi hii kupongeza Halmashauri ya Kusulu TC kwa kuweza kufanya vizuri kwa kutoa pesa hizo kila baada ya miezi mitatu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii langu la kwanza, kwa kuwa wanawake wengi, vijana pamoja na walemauvu wameweza kuhamasika kufungua vikundi lakini zipo Halmashauri ambazo zinasuasua na nyingine kutokupeleka pesa hizo kama sheria inavyotaka. Je, Wizara iko tayari sasa kutoa agizo ili Halmashauri hizo ziweze kutoa pesa kwa wakati? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili, zipo Halmashauri ambazo bado ni changa mfano Halmashauri ya Kakonko pamoja na Buhigwe, makusanyo yao sio mazuri sana, ni kidogo. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa kuzisaidia Halmashauri hizo? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Josephine, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum kwa kujali wanawake na kuwasemea ili waweze kupata mikopo na kujikwamua kiuchumi. Hii kazi inafanywa na Wabunge wote wa Viti Maalum kama nilivyosema jana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli wakati wa bajeti bahati nzuri nimehudhuria kikao cha Kamati ya Utawala wa TAMISEMI, naomba niwapongeze wajumbe wakiongozwa na Mwenyekiti, Mheshimiwa Rwekiza kwa kazi nzuri waliyofanya katika mjadala ule. Kila Mkoa, Halmashauri, Mkurugenzi, Katibu Tawala alihojija na kutoa maelezo namna ambavyo amesimamia ukusanyaji wa fedha na kupeleka kwenye vikundi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hoja ya kusuasua kutokupeleka fedha ni jambo la kisheria na maagizo yametoka naomba nirudie, Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa na Makatibu Tawala kwa maelekezo ya Kamati ya Utawala na TAMISEMI kwa mwaka wa fedha ujao kama kuna mtu atakuwa hajapeleka fedha hizi kikamilifu na kusimamia marejesho hali yake itakuwa mbaya sana. Haya ni maagizo ya Kamati na sisi kama Wizara tumeyachukua. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, maelekezo ni kwamba hakuna Halmashauri changa katika jambo hili, kama umekusanya Sh.100 umetoa makato yale ambayo ni ya msingi na makato mbalimbali ambapo yametolewa kwenye Halmashauri inayobaki 10% yake peleka kwenye vikundi vya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu. Kwa hiyo, hata kama utakuwa umekusanya Sh.5, ondoa makato yote ya msingi ambayo yameelekezwa na Serikali inayobaki 10% peleka, usipopeleka sheria itachukua mkondo wake. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swalı lake.

Na. 55

Wafugaji Kutengewa Maeneo yao – Mara

MHE. JOYCE B. SOKOMBI aliuliza:-

Mara ni mkoa ambao una makundi makubwa ya jamii ya wafugaji, wakulima na wavuvi lakini kwa sasa kuna shida kubwa ya ardhi kati ya wakulima na wafugaji:-

Je, ni lini wafugaji watapatiwa eneo kwa ajili ya kuendesha shughuli zao?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, majibu.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba kujibu swalii la Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mara unakadiriwa kuwa na ng'ombe 1,305,075, mbuzi 733,321, kondoo 437,387, nguruwe 5,802, punda 11,757 na kuku 1,524,653. Upande wa Nyanda za Juu katika Wilaya za Serengeti, Tarime, Rorya, Butiama na Bunda ndizo zenyeye ufugaji mkubwa wa mifugo ambapo Wilaya za Musoma, Rorya na Bunda kwa kiasi kikubwa zinashughulika na uvuvi hasa kwenye vijiji vya mwambao wa Ziwa Viktoria.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mkoa wa Mara kuititia Halmashauri 9 umeshatenga maeneo yenye jumla ya ukubwa wa hekta 15,588.55 kwa ajili ya malisho ya mifugo kuititia mpango wa matumizi ya ardhi ya vijiji. Mkoa kuititia Halmashauri utaendelea kutekeleza mpango wa matumizi ya ardhi kwa vijiji ili kuainisha matumizi ya ardhi kwa makundi

mbalimbali wakiwemo wafugaji na wakulima ili kuepusha migogoro. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Joyce Bitta Sokombi, swali la nyongeza.

MHE. JOYCE B. SOKOMBI: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Nilitegemea swali hili lingejibiwa na Wizara ya Mifugo na Kilimo lakini limejibiwa na TAMISEMI, kwa vile Serikali ni moja naamini tatizo la Mkoa wa Mara linaenda kutatuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu idadi ya ng'ombe nina mashaka nayo, kutohana na mabadiliko ya tabia nchi wafugaji wengi wageni toka sehemu mbalimbali wanaingia mkoani kwa ajili ya malisho kwa kufuata mbuga. Malisho ni shida sana katika Mkoa wa Mara, Mkoa umeelemewa na ndiyo sababu kubwa sana Hifadhi ya Taifa ya Serengeti na wakulima na wafugaji kuna mgogoro mkubwa sana. Kwa nini Serikali isione umuhimu wa kuweka sheria ya kuwasaidia wafugaji hawa?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wilaya ya Serengeti, Tarime, Ranya, Butiama, Bunda na Musoma Vijiji zimesahaulika ndio zenye wafugaji wengi sana na hakuna sehemu za malisho. Je, Serikali haioni umuhimu wa kutoa elimu kwa wafugaji hawa ili wafuge ufugaji wa kisasa ili kuweza kujikwamua katika mahitaji yao ya kila siku?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, majibu kwa maswali hayo.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Joyce Sokombi, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza namuomba Mheshimiwa Mbunge asiwe na wasiwasi kama alivyosema Serikali ni moja, ulipozungumza habari ya Halmashauri na vijiji

unazungumza TAMISEMI lakini pia tunafanya kazi pamoja na Wizara ya Mifugo na Uvuvi kuhakikisha kwamba mambo yanaenda sawasawa. Kwa hiyo, swali lipo sehemu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la msingi anasema idadi ya ng'ombe ina tatizo, sisi tumejiridhisha kwamba idadi hii ni kamili kwa sababu sensa imefanywa na Serikali na ni *data* kamili labda kama ana taarifa nyingine tofauti na hizi tutamkaribisha tu-*compare notes*.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumpongeze sana Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Dkt. John Pombe Joseph Magufuli baada ya kuona kwamba kuna shida kubwa ya malisho na migogoro mingi ya ardhi kati ya wafugaji na wakulima ameunda timu ya Mawaziri wanane wanaendelea na vikao vyao maeneo mahsus i yamependekezwa na wadau wameshirikishwa, Tarime, Serengeti, Bunda na maeneo mengine nchi nzima yatatengewa maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mpango huo kukamilika na taarifa kupewa Mheshimiwa Rais ataona itakavyofaa ili kuruhusu baadhi ya maeneo yawe kwa ajili ya wafugaji na wakulima na tunaamini baada ya zoezi hilo migorogoro ya wakulima na wafugaji itakuwa imefikia ukomo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili anazungumzia kuhusu kutoa elimu, nimemsikiliza mara kadhaa hapa Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Mpina na Mheshimiwa Ulega wametoa taarifa mara nyingi na mipango mbalimbali na ni kweli kwamba wafugaji wetu wanashauriwa kufuga kwa tija, afuge mifugo michache kulingana na eneo lake lakini yenye manufaa ya kusomesha na kupata kipato. Hiyo kazi inafanywa na Serikali na inaendelea kuleta tija kubwa sana. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed Mbunge wa Bumbwini, sasa aulize swali lake.

Na. 56

Upatikanaji wa Mafuta Nchini

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED aliuliza:-

Suala la mafuta ni la Muungano na kumekuwepo na taratibu mbalimbali zinazofanywa ili kutafuta mafuta nchini:-

Je, ni taratibu zipi zilizopaswa kufanyika ili kuthibitisha kwamba mafuta yanapatikana katika eneo husika?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba kwa mujibu wa Katiba iliyopo, suala la utafutaji na uzalishaji mafuta ghafi ni suala la Muungano. Hata hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar mwaka 2015 kwa nia njema ya kuongeza ufanisi na tija katika shughuli za kutafuta na kuzalishaji mafuta ghafi, zilikubaliana kuwa kila upande usimamie shughuli hizo kwa kutumia sheria na taasisi zake. Serikali zetu za pande zote mbili za Muungano zimefanya hivyo katika masuala ya bandari na viwanja vya ndege, pamoja na kuwa masuala hayo ni ya Muungano.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuthibitisha mafuta yanapatikana katika eneo husika, taratibu zifuatazo hufanya ikiwa ni pamoja na:

(a) Utafiti wa awali wa kukusanya sampuli za kijiolojia na kijiochemia;

- (b) Kukusanya data za kijiofizikia (*gravimetry* na *seismic*);
- (c) Kufanya tathmini (*interpretation*) ya data za kijiolojia na kijiofizikia;
- (d) Kutambua maeneo ya mashapo (*geological structures*) katika miamba tabaka ambapo mafuta au gesi inaweza kukusanyika kufuatia matokeo ya tathmini ya data za kijiolojia na kijiofizikia; na
- (e) Kuchimba visima vya utafiti (*exploration wells*) katika maeneo yalikotambulika mashapo ili kuthibitisha uwepo wa mafuta ghafi au gesi asilia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, swali la nyongeza.

MHE. MUHAMMED AMOUR MUHAMMED: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa kuuliza swali la nyongeza. Pamoja na majibu ya Serikali ambayo yanaonekana kuchupachupa kwa baadhi ya mambo, nina maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza ni *community based*, kwa kuwa *research* ni suala la Muungano na 2018 ilifanywa *research* kule Zanzibar nzima, ndani ya harakati za wale vijana kufanya *research* waliwaharibia wananchi wetu mazao yao. Je, ukizingatia *research* ni suala la Muungano Serikali ya Jamhuri ya Muungano ina namna gani ya kurejea nyuma angalau kuwapa mkono wa pole wale waliwaharibia mazao yao? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, Serikali imesema kwamba wamekubaliana mafuta na gesi kila upande ufanye kwa kutumia taasisi zake. Pamoja na Azimio ambalo limepitishwa na Baraza la Wawakilishi kule Zanzibar lakini bado suala la mafuta linabaki ni la Muungano. Je, hatuoni sasa ni wakati mwafaka sheria hii ambayo imo ndani ya

Katiba ya Muungano kwamba mafuta ni suala la Muungano tukalitoa sasa ili kurahisisha uwekezaji kule Zanzibar? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati, majibu.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Muhammed Amour Muhammed, Mbunge wa Bumbwini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa maswali mazuri. Swali lake la kwanza ameulizia namna gani Serikali ya Muungano inaweza ikawalipa fidia wananchi ambao mazao yao yaliharibiwa wakati wa utafiti. Kama liliyosema jibu langu la msingi, utafiti huu ulifanyika kwa ajili ya masuala ya mafuta au gesi; na kwa kuwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Zanzibar kwa nia njema ilipofika mwaka 2015 Bunge hili lilipitisha Sheria ya Mafuta na kifungu cha 2 kilianisha kabisa mamlaka ambazo zitatumika katika suala zima la utafutaji mafuta ni kwa pande zote mbali na ni kwa nia njema ya kupunguza urasimu. Kwa kuwa shughuli hizi za utafiti za mafuta na gesi zilifanyika upande wa Zanzibar ambao wana mamlaka na walipitisha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 labda nilichukue na kwa sababu tuna ushirikiano mzuri tutawasiliano na Wizara ya upande wa pili wa Muungano Zanzibar kuona hili jambo wanalfanyia kazi vipi lakini nia ilikuwa njema.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili ameuliza kwa kuwa suala hili liliifanyika kwa nia njema kwa nini lisifanyiwe marekebisho. Jambo la kufanya marekebisho katika Katiba limeundiwa utaratibu wake ndani ya Katiba hiyo hiyo lakini kwa sasa kwa nia njema Bunge hili hili lilitidha kupitisha Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015 na Baraza la Wawakilishi wakapitisha Sheria yao ya Mafuta ya mwaka 2016 kwa sasa shughuli zinaendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nilitaarifu Bunge lako walikuwa mashahidi tarehe 23 Oktaba, 2018, Serikali ya

Mapinduzi ya Zanzibar ilitiliana saini mkataba wa kugawana faida itakayopatikana wakati wa kuchimba mafuta au gesi na Kampuni ya *RAK Gaskutoka* nchi ya Ras Al Khaimah. Kwa hiyo, ni wazi kwamba tangu waingie mkataba huo kazi inaendelea na hakujatokea mgongano. Hata hivyo, hili naomba niliachie mamlaka zingine na Bunge hili kama itaona inafaa. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali, Mbunge wa Kilombero, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Upendo Peneza.

Na. 57

REA III- Kilombero

MHE. UPENDO F. PENEZA (K.n.y. MHE. PETER A. LIJUALIKALI) alijibu:-

Je, ni lini programu ya *REA III* itaanza kutekelezwa katika viji ya Wilaya ya Kilombero?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

***NAIBU WAZIRI WA NISHATI* alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Peter Ambrose Lijualikali, Mbunge wa Kilombero, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kuititia Wakala wa Nishati Vijiini (*REA*) ilianza kutekeleza Mradi wa Usambazaji Umeme Vijiini ikiwemo viji ya Wilaya ya Kilombero Julai, 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kampuni ya *State Grid Electrical and Technical Works Ltd* Novemba, 2018 ilikamilisha upimaji na usanifu katika viji 21 vya *REA III*, Mzunguko wa

Kwanza. Kwa sasa mkandarasi anaendelea na kazi ya ujenzi wa miundombinu katika Vijiji vya Kirama, Mbasa, Michenga, Mautanga, Ihanga na Miwanganani. Kazi za ujenzi wa mradi huu zitakamilka mwezi Juni, 2020.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za mradi wa Jimbo la Kilombero zinahusisha ujenzi wa njia ya umeme wa msongo wa Kilovoti 33 umbali wa kilomita 16.5, njia ya umeme wa msongo wa Kilovoti 04 urefu wa kilomita 28, ufungaji wa *transformer* 14 za KVA 50 na 100, pamoja na kuunganisha umeme wateja wa awali 497 na gharama ya mradi ni shilingi 1,700,060,000/=. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Upendo Peneza, swali la nyongeza.

MHE. UPENDO F. PENEZA: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Mbunge wa Jimbo husika Mheshimiwa Lijualikali anakubali kwamba ni kweli kazi inafanyika, lakini changamoto iliyopo ni kwamba umeme unawekwa kwa kurukaruka. Wakishafikisha kwenye *centre* vitongoji vingine havipati na kutoka kwenye *centre* kwenda kwenye vitongoji vingine kuna umbali mpaka wa kama kilomita sita mpaka kilomita nane, suala ambalo baadaye litakuwa gumu kwa wananchi kupeleka umeme katika hivyo vitongoji vingine.

Swali lake ni kwamba: Je, Serikali haioni umuhimu wa kuboresha usambazaji wa umeme kuhakikisha kwamba wanapopeleka kwenye kijiji basi wasambaze katika maeneo yote na vitongoji vyote vya kijiji hicho?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, naomba pia niulize kwa niaba ya wananchi wa Halmashauri ya Geita Mjini ambako mimi natoka. Serikali ilituahidi ndani ya Bunge kwamba kuna maeneo ambayo yamekuwa mitaa sasa na zamani yalikuwa ni vijiji, lakini kiuhalisia bado yana mazingira kama ya vijiji hivi; Serikali iliahidi kwamba bado wale wananchi ingawa wanaishi kwenye mitaa ingewapa umeme kwa kuititia mradi wa REA. Maeneo hayo ni katika Kata za

Ihanamilo; baadhi ya mitaa; Kata ya Kasamwa, Kata za Kanyara na Kata za Burela.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni lini sasa Serikali itatusaidia kupeleka umeme katika maeneo hayo na katika kata hizo kwa kupitia mradi huu wa *REA* kama ilivyoahidi ndani ya Bunge? Ahsante.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

MHE. NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kujibu maswali mawili ya nyongeza. Kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza napenda kushuruku kwamba Mheshimiwa Mbunge Lijualikali ametambua kazi mbalimbali ambazo zinaendelea katika Jimbo la Kilombero kuhusu mradi wa *REA* awamu ya tatu, mzunguko wa kwanza. Ametoa ushauri kwamba ni namna gani Serikali inaweza ikaboresha zaidi katika usambazaji wa umeme inapofika kwenye eneo fulani.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimtaarifu Mheshimiwa Mbunge, Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Magufuli imeliona hilo kwamba, kwa kuwa miradi hii ngazi yake kwanza ni ngazi ya kijiji, imetambua vijiji zaidi ya 3,559 kwa awamu hii ya kwanza, *REA* awamu ya tatu mzunguko wa kwanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, vijiji vina vitongoji. Kwa hiyo, Serikali ilibuni mradi ambao ilifanya majoribio ya ujazilizi kwa mikoa minane ambapo uligusa vitongoji 305 na iliwaunganisha wananchi kama 25,000 na mradi ule ulifanyika kwa mafanikio makubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuwa na mafanikio hayo, tutakuja na mradi mwingine *densification*

awamu ya pili katika Bunge hili la Bajeti linaloendelea. Kwa hiyo tutaomba mtuidhinishie, lakini mradi huu unakwenda kutatua tatizo la vitongoji vinavyoachwa. Kwa hiyo, nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge na Wabunge wengine, hilo linatambulika.

Mheshimiwa Naibu Spika, niendelee kuamini kwamba gharama za kupelekea umeme kwenye kijiji kimoja; kilimeta moja tu ni shilingi milioni 50. Kwa hiyo, Serikali ambayo inafanya mambo mengi ya kimaendeleo lazima kwenda hatua kwa hatua. Kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge waendelee kutuunga mkono na vitongoji vingine vitafikiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili Mheshimiwa Mbunge Upendo Peneza, ameелееza masuala ya Halmashauri ya Geita. Kwanza kata zote ambazo alizitaja, bahati nzuri na Mheshimiwa Mbunge mwenyewe wa Jimbo naye amelizungumzia, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili, lakini naye nimpongeze pia amelielezea. (*Makof!*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba maeneo yote ambayo yako katika Halmashauri za Miji na tunatambua kwamba bado yapo katika pia katika maeneo ya vijijini, kuna mradi unakuja *peri-urban* ambako maeneo ya kata ambazo zimetajwa zitashughulikiwa na bei ni ile ile shilingi 27,000/=.

Kwa hiyo, niwatoe hofu wakazi wa maeneo yote ya miji na mitaa, mradi wa ujazilizi na mradi wa wa *peri-urban* utakuja kutatua tatizo ambalo limebaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Eng. Ramo Matala Makani, Mbunge wa Tunduru Kaskazini, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Jerome Bwanausi.

Na. 58

Uhaba wa Maji Tunduru

MHE. JEROME D. BWANAUSI (K.n.y. MHE. ENG. RAMO M. MAKANI, aliuliza:-

(a) Je, nini mpango wa Serikali kukamilisha mradi wa maji safi unaoendelea katika Mji wa Tunduru ili kuwaondolea wananchi hao adha kubwa wanayoipata ya uhaba wa huduma hiyo?

(b) Jimbo la Tunduru Kaskazini lina vijiji 92 ambapo taarifa za Serikali na takwimu zinaonesha kiwango cha upatikanaji wa maji kuwa chini sana:-

Je, ni lini mpango wa Serikali wa kuongeza kiwango hicho cha upatikanaji wa maji katika vijiji hivyo kufikia kiwango kilichowekwa kwa mujibu wa mipango ya Serikali na llani ya CCM itatekelezwa?

MHE. NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Ramo Makani, Mbunge wa Jimbo la Tunduru Kaskazini, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2016/2017 Mji wa Tunduru ilitengewa fedha kiasi cha shilingi milioni 300 kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya maji Mjini Tunduru na kuongeza hali ya upatikanaji wa maji. Uboreshaji huo ulisaidia kuongeza huduma ya maji kutoka asilimia 52 mwaka 2017 kufikia asilimia 66 kwa sasa.

Aidha, kwa mwaka huu wa fedha 2018/2019, kupitia mamlaka ya majisafi na usafi wa mazingira Songea,

inaendelea na utaratibu wa kutekeleza mradi wa upanuzi wa miundombinu ya maji kwa mji wa Tunduru ambapo wananchi wengi zaidi watapata huduma ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba Jimbo la Tunduru Kaskazini lina jumla ya vijiji 92 vyenye vituo vya kuchotea maji 385 vinavyohudumia wakazi wapatao 58,250. Katika kuhakikisha huduma ya maji safi na salama inaongezeka katika vijiji vilivyopo, Jimbo la Tunduru Kaskazini, Serikali inatekeleza miradi miwili ya Nandemo ambaao umekamilika na mradi wa Matemanga ambaao umefikia asilimia 85 ya utekelezaji na utahudumia vijiji vya Matemanga, Milonde, Changarawe na Jaribuni. Lengo la Serikali ni kuhakikisha huduma ya maji vijijini inafikia asilimia 85 ifikapo mwaka 2020 kama inavyoelekeza llani ya CCM.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Jerome Bwanausi, swali la nyongeza.

MHE. JEROME D. BWANAUSI: Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

Swali la kwanza; kwa kuwa asilimia ya upatikanaji wa maji katika Mji wa Tunduru pamoja na vijiji vyake 92 ni wa chini sana; na kwa kuwa Serikali imekuwa ikitoa fedha kidogo kidogo katika mradi mkubwa wa Tunduru:-

Je, Serikali haioni sababu sasa ya kutafuta fedha za kutosha ili mradi huu ukamiliwa kwa haraka na wananchi waweze kupata maji kwa urahisi? (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, vijiji vya Lakalola, Nakachindu, Namwanga, Nangwale, Tupendane, vimikuwa vikikabiliwa na tatizo kubwa sana la maji katika Jimbo la Lulindi pamoja na kule Rivangu na Wakandarasi wako *site*; kuna *OBD and Companyna Sing Lyimo Enterprises*, lakini tangu wapeleke *certificate* mwezi Novemba, 2018 hadi sasa Wakandarasi hao hawajapata fedha zao ili kuendelea na kazi:-

Je, nini kauli ya Serikali? (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

NAIBU WAZIRI WA MAJI NA UMWAGILIAJI: Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote nimpongeze Mheshimiwa Mbunge. Niwe mkweli, tuna changamoto kubwa sana Tunduru na hata Mkoa wa Ruvuma, tulifanya ziara tukaona changamoto hiyo. Kubwa tunaloliona, tuna ubabaishaji mkubwa sana wa Mhandisi wetu wa Maji wa Mkaoa. Sisi kama Wizara tumeshamwondoa na tutaendelea kuwaondoa Wahandisi wote wababaishaji katika Wizara yetu ya Maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa tunatambua kabisa utekelezaji wa miradi ya maji inategemeana na fedha. Tullkuwa tuna madal zaidi ya shillingi bilioni 88 ya Wakandarasi. Tunashukuru sana Wizara ya Fedha imetupa shillingi bilioni 44, tumeshaanza kuwalipa Wakandarasi na mwezi huu wa Nne mwishoni watatupa shillingi bilioni 44 nyingine katika kuhakikisha tunawakamilishia Wakandarasi madai wanayotudai. Nataka niwahakikishie Waheshimiwa Wabunge, sisi kama Wizara ya Maji hatutakuwa kikwazo katika kuhakikisha miradi ya maji inakuwa endelevu na kuweza kuwashudumia wananchi. Ahsante sana.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Mheshimiwa Abdallah Ally Mtalea, Mbunge wa Temeke sasa aulize swali lake.

Na. 59

Uwekaji wa Matuta Barabarani

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA aliuliza:-

Serikali inajitahidi kujenga barabara ili kupunguza foleni pamoja na kurahisisha usarifi na usafirishaji, lakini barabara zinawekwa matuta ambayo siyo rafiki kwa vyombo vya usafiri jambo linalosababisha baadhi ya watumiaji wa

barabara hizo kuzikimbia, kwa mfano, matuta yaliyowekwa katika barabara ya Msata – Bagamoyo:-

Je, matuta ni sehemu ya alama za barabarani?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, alama za barabarani hutumika kutoa ujumbe wa matumizi sahihi ya barabara katika eneo husika. Alama hizo huwekwa kwenye milingoti pembezo mwa barabara au huchorwa katika uso wa barabara kutoa tafsiri sahihi ya matumizi ya barabara. Hata hivyo, kutohana na baadhi ya madereva kutozingatia alama za barabarani hususan, alama za ukomo wa mwendo (*speed limit*), Serikali hulazimika kujenga matuta katika maeneo ambayo ni harishishili ili kuwalazimisha madereva kupunguza mwendo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kutambua kuwa baadhi ya matuta ya barabarani siyo rafiki kwa vyombo vya usafiri, Serikali iliandaa mwongozo wa usanifu wa barabara wa mwaka 2011 *Road Geometric Design Manual, 2011* ambapo pamoja na mambo mengine, imeweka viwango bora vya ujenzi wa matuta barabarani. Kwa kuzingatia mwongozo huo, Wizara yangu kupitia *TANROADS* imepitilia upya matuta yote yaliyojengwa katika barabara kuu hapa nchini na kubaini kuwa matuta 323 siyo rafiki kwa vyombo vya usafiri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi ya uboreshaji wa matuta hayo inaendelea ambapo hadi sasa matuta 281

yemerekebishwa. Baadhi ya barabara ambazo matuta yamerekebishwa ni Kibaha - Mlandizi (6), Morogoro – Iringa (12), Mara – Simiyu (matuta 12), Igawa – Songwe (matuta matatu), Uyole – Kasumulu (matuta mawili) Mwanza – Simiyu (matuta tisa), Shelui – Nzega (matuta matano), Singida – Manyara (matuta 23), Mtukula – Bukoba (matuta saba) pamoja na maeneo mengine kwa ujumla (matuta 202).

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge na wananchi kwa ujumla kuwa matuta yote ambayo hayastahili kuwepo barabarani yataondolewa na yale ambayo hayakidhi kiwango yatajengwa upya. Aidha, natoa wito kwa madereva wote nchini kuzingatia alama za barabarani ikiwemo alama za ukomo wa mwendo (*Speed limit*).

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, swali la nyongeza.

MHE. ABDALLAH A. MTOLEA: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri ya Serikali ambapo imekiri uwepo wa matuta hayo ambayo siyo rafiki barabarani na wameanza kuchukua jithada, nilitaka kujua ni lini sasa Serikali itakuwa imemaliza kuyapitia na kuyarekebisha matuta yaliyopo kwenye barabara ya Msata – Bagamoyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; hivi karibuni Jeshi la Polisi kwa kupitia Kitengo chake cha Usalama Barabarani, wamekuwa wakifanya kazi nzuri ya kuwadhibiti madereva wakorofi. Je, pamoja na kazi nzuri hii ya Jeshi la Polisi bado tunaona kuna tija ya kuendelea kuweka matuta kwenye barabara kuu?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyojibu katika jibu langu la msingi, tunaendelea kuyatoa matuta yote ambayo yameonekana kwamba hayafai kulingana na

mwongozo ambao tumeutoa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Mt Olea kwamba muda siyo mrefu tutakamilisha kazi hii kwa sababu mpaka hivi ninavyoongea, tuko karibu asilimia 90 ya matuta yote ambayo tuliyatambua kwamba ni hatarishi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge uvute subira kwa sababu kuyatoa matuta haya pia ni gharama; tutaendelea kuyatoa matuta yote sehemu hiyo uliyosema kutoka Msata kwenda Bagamoyo na maeneo mengine nchini. Kwa hiyo, vuta subira kasi yetu ni nzuri, tutayatoa matuta yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, kwanza namshukuru sana Mheshimiwa Mt Olea kwa kutambua na kuona udhibiti wa madereva tunaoufanya Serikali kupitia Mambo ya Ndani na sisi upande wa ujenzi. Mimi kama Makamu wa Mwenyekiti wa Baraza la Usalama Barabarani, tunahakikisha kwamba kwanza wananchi wanabaki salama, watumiaji wengine wa barabara wanabaki salama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, Mheshimiwa tutaendelea kufanya udhibiti ili kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa salama kwanza, halafu tuendelee na hatua nyingine. Kwa hiyo, ni muhimu sana kuhakikisha watu wetu wanakuwa salama. Kwa hiyo, tutaendela kudhibiti na kuhakikisha kwamba wananchi wanakuwa salama.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Alhaj Abdallah Majurah Bulembo, Mbunge wa Kuteuliwa.

Na. 60

Upanuzi wa Uwanja wa Ndege Bukoba

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO aliuliza:-

Mheshimiwa Rais alipofungua Uwanja wa Ndege wa Bukoba alisema kuwa Uwanja wa Kanjunguti hautajengwa tena, badala yake shilingi bilioni tano zilizokusudiwa kutumika

huko Omukajunguti ziende kwenye upanuzi wa kiwanja cha Bukoba:-

- (a) Je, ni lini Serikali itatekeleza agizo la Mheshimiwa Rais?
- (b) Je, Serikali haioni ni tatizo kwa utuaji wa ndege kutokana na hali ya hewa ya eneo hilo?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO
(MHE. ELIAS J. KWANDIKWA) alijibu:-**

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Alhaj Abdallah Majurah Bulembo, Mbunge wa Kuteuliwa, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati wa uzinduzi wa kiwanja cha ndege cha Bukoba tarehe 6 Novemba, 2017, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, aliagiza ufanyike uchambuzi wa kina, kama kuna haja ya kujenga kiwanja kipyaa cha ndege katika eneo la Omukajunguti au kupanua kiwanja cha ndege kilichopo Bukoba, yaani kutoka Daraja la II C hadi Daraja la II C.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na agizo hilo la Mheshimiwa Rais, Serikali iliunda timu ya wataalam ili wafanye uchambuzi wa kina na hatimaye waweze kuishauri Serikali ipasavyo. Baada ya uchambuzi, timu hii ya wataalam ilibaini mambo yafuatayo:-

- (1) Kupanua kiwanja cha ndege cha Bukoga kutoka Daraja la II C hadi la III C, kutahitaji utoaji wa ardhi isiyopungua hekari 75 ambayo tayari imeendelezwa. Ardhi hii inayohitajika itagusa nyumba za makazi zipatazo 200, Kituo cha Afya Zamzam, Makanisa mawili (*WinnerS Chapel na Pentekoste*

Assembly of God), Msikiti, Shule za Msingi mbili, Zamzam na Bilele, barabara za Kashozi na Kashai pamoja na kuziba njia ya Mto Kanoni.

(2) Kupanua kiwanda hiki, kutasababisha jengo la abiria kuhamishwa ili kukidhi matakwa ya kiusalama ya usafiri wa anga. Pia kutakuwa na ugumu wa kupata eneo la kusimika taa za kumsaidi rubani kutua.

(3) Kutakuwa na ugumu wa kukiendeleza kiwanja hiki kufikia madaraja ya juu zaidi huko mbeleni.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kubaini mambo hayo, wataalam walitoa ushauri ufuataao kwa Serikali:-

(1) Kwa sasa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba hakina eneo la kutosha kwa Daraja la II C, tunakipandisha kwenda daraja la juu, ardhi zaidi itahitajika.

(2) Kwa sasa Kiwanja cha Ndege cha Bukoba kinafaa kusimikwa sehemu ya taa (*AGL System*) za kukiwezesha kufanya kazi usiku na mchana.

(3) Uongozi wa Mkoa wa Kagera ufanye utafiti wa kina (*detail survey*) kujua gharama na athari za utoaji wa ardhi inayotakiwa kwa ajili ya upanuzi wa kiwanja ndege cha Bukoba.

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati Serikali ikiendelea kushughulikia mapendekezo haya ya wataalam, sehemu ya fedha iliyokuwa itumike kulipa fidia kwenye eneo la Omukajunguti, zitatumika kusimika taa katika Kiwanja cha Ndege cha Bukoba ili zisaidie marubani wakati wa uwepo wa hali mbaya ya hewa, pia kukiwezesha kiwanja kutoa huduma usiku na mchana.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Abdallah Bulembo, swalii la nyongeza.

MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Maswali yangu mawili ya nyongeza.

(a) Pamoja na wataalam kuangalia athari ya fidia lakini wataalam hawa kwa nini hawakuangalia upande wa pili wa Mkao wa Kagera? Uwanja wa Mkao wa Kagera unaweza ukapakia *Airbus* kutoka Bukoba, ikajaa bila kwenda popote, kwa sababu watu wa Uganda, Burundi, Congo, wote wanapandia pale.

Je, upanuzi huu kwenda Daraja C mnategemea ufanyike lini? Naomba wataalam waangalie faida wasiangalie hasara peke yake. (*Makofii*)

(b) Kwa sababu kuna uwanja wa ambao ulikuwepo miaka yote, awamu zote kuanzia Mwalimu Nyerere zaidi ya miaka 41, Omukajunguti, leo hii Bukoba haiwezi kupanuliwa, kwa nini uwanja huu usiendelee kubaki ndani ya mamlaka ya viwanja vya ndege ili miaka ijayo mkitaka kupanua labda pesa zipo tusihangaike kutafuta mahali pa kwenda? (*Makofii*)?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, majibu.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia maendeleo siyo ya Bukoba peke yake, lakini ya nchi nzima. Nampongeza sana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli tumeliona hilo kwamba Uwanja wa Ndege wa Bukoba ni muhimu sana. Ndiyo maana katika mipango yetu na wakati mwingine Mheshimiwa Mbunge avute subira, ataona namna tulivyojipanga, kama nilivyosema kuuboresha uwanja huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumejipanga ili uwanja huu tuweze kuuwekea pia *VIP Lounge*, tumejipanga pia kwa ajili

ya kufanya maboresho kama nilivyosema ili tuweze kutoa huduma ya ndege nyingi. Kwa maana hiyo, ili kuweza kukidhi mahitaji ya matumizi ya uwanja huu, tutakapofanya maboresho, ikiwa ni pamoja na kuweka taa za kuongoza marubani, ina maana tutaongeza idadi ya miruko. Kwa sababu siyo suala la kuongeza ndege kubwa peke yake linaweza kukidhi mahitaji ya Bukoba, lakini ni pamoja na kuongeza idadi ya miruko katika uwanja huu. Kwa hiyo, tukifanya maboresho, idadi ya miruko tutaiongeza wakati tunatazama siku za usoni tufanye nini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu swali lake la pili, matumizi ya uwanja wa Omukajunguti, niseme tu uwanja huu bado unamilikiwa na Serikali na bado utaendelea kumilikiwa na Serikali kwa sababu maendeleo ya nchi hii yanakwenda kwa kasi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge, nasi wakati tunasonga mbele tunaendelea kutazama matumizi mazuri na maboresho ya uwanja huo wa Omukajunguti.

Nimhakikishie tu Mheshimiwa kwamba tunautazama vizuri na nitoe tu maelekezo kwa wenzetu upande wa TAA tuutazame uwanja huu kama kutahitaji kuweka uzio, tuweke kwa maana ya kuulinda. Pia niwasihii tu wananchi wa Bukoba na watu wanaozunguka eneo hili tusivamie eneo hili, eneo hili litakuja kutupa manufaa sisi na Watanzania wote kwa ujumla. Ahsante.

NAIBU SPIKA: Ahsante sana. Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali letu lililobaki, Wizara ya Katiba na Sheria. Mheshimiwa Fatma Hassan Tofiq, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 61

Kuandika Wosia

MHE. FATMA H. TOUFIQ aliuliza:-

Miongoni mwa sababu kubwa zinazosababisha wanawake na watoto kuporwa mali zao na ndugu za waume

zao ni kukosekana kwa wosia, jambo ambalo jamii haijaona umuhimu huo wakiamini kuwa kuandika wosia ni kujitakia kifo:-

(a) Je, Serikali ina mkakati gani endelevu wa kukabiliana na kadhia hii?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuelimisha jamii umuhimu wa kuandika wosia kama njia mojawapo ya kulikabili tatizo hili ambalo ni kubwa katika jamii?

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swalii la Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa kuandika wosia kama njia mojawapo ya kukabiliana na migogoro katika jamii inayohusiana na mgao wa mali za marehemu. Kwa kutambua hilo, mwaka 2008, Wizara yangu kupitia Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi (*R/IA*) iillanzisha huduma ya kuandika na kuhifadhi wosia ikiwa ni pamoja na kuuelimisha umma kuhusiana na huduma hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, tangu wakati huo, Wizara yangu kupitia Wakala wa Usajili, Udhamini na Ufilisi inaendelea kubuni na kutekeleza mikataba ya aina mbalimbali ili kuhakikisha na kufikisha elimu kwa wananchi kuhusu umuhimu wa kuandika na kuhifadhi wosia.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumekuwa tukitumia njia mbalimbali kutoa elimu ya kuandika wosia ikiwa ni pamoja na mikutano ya hadhara, radio, televisheni, vipeperushi, magazeti na mitandao ya kijamii. Pamoja na jitihada hiyo, mpaka sasa tumeweza kuandika na kuhifadhi wosia 578 kati ya hizo 32 tayari zimeshatumika. Hata hivyo, idadi hiyo ni ndogo ikilinganishwa na idadi kubwa ya Watanzania waliopo

kwa sasa. Bado kuna changamoto ya uelewa kwa wananchi wengi juu ya umuhimu wa suala hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kulithibitishia Bunge lako Tukufu kuwa Wizara yangu itaendelea kubuni njia mbalimbali za kuelimisha jamii kuwa umuhimu wa kuandika wosia ikiwa ni jitihada mojawapo ya kukabiliana na migogoro ya mgao wa mali za marehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba kutumia fursa hii kuwaomba Waheshimiwa Wabunge wote kuchangia katika juhudi zinazofanywa na Serikali za kuhamasisha wananchi kujijengea tabia na utamaduni wa kuandika na kuhifadhi wosia sehemu maalum hadi utakapohitajika. Endapo wananchi watahamasika, tutakuwa tumeondokana na migogoro isiyo ya lazima na hivyo kuruhusu maendeleo ya ustawi wa jamii. Hii ni njia muhimu ya kulinda haki za wanawake na watoto waliofiwa ndani ya familia.

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Fatma Hassan Toufiq, swalii nyongeza.

MHE. FATMA H. TOUFIQ: Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa ya kuuliza maswali ya nyongeza. Pia namshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri.

Mheshimiwa Naibu Sika, wosia wa mdomo au wa matamshi una changamoto nyingi. Kwa kuwa mazingira ya ndugu au mashuhuda huweza kubadili wosia kwa mtoa wosia, sasa hivi tuko kwenye ulimwengu wa sayansi na teknolojia, je, kwa nini Serikali isifanye utaratibu wa kurekodi wosia wa mdomo na kuhifadhi *RITA* ili wanawake na watoto wasipoteze haki zao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swalii la pili; kwa mujibu wa gharama za *RITA* kutunza wosia unatunza kulingana na mali aliyonayo mweka wosia ambayo ni kuanzia Sh.5,000 hadi Sh.50,000. Je, Serikali haioni umefikia wakati wa kufanya marejeo ya gharama hizo? Ahsante sana. (*Makofi*)

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, majibu.

WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa maswali ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge Kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tumefikia kipindi cha utaalam wa kisayansi, nakubaliana na yeyee kwamba wosia usiwe tu wa mdomo, lakini tutumie njia ya kurekodi wosia huo kutoka kwa wazazi, kutoka kwa jamii. Pia nataka kumhakikishia kwamba Ofisi za RITA ziko katika kila Wilaya kwenye Ofisi ya DASna tutajitahidi kama Serikali kuweza kuziwezesha kuwa na mashine za kurekodi wosia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nataka kumhakikishia kwamba kuna Mashirika mengi Yasiyo ya Kiserikali ambayo yamekuwa yanafanya kazi na jamii mbalimbali, kwanza kutoa elimu juu ya umuhimu wa kuweka wosia na pili jinsi ya kuandika wosia. Kwa hivyo Serikali yetu kwa kutumia sheria iliyopitishwa mwaka 2017 ya Misaada ya Sheria tutafanya pamoja ili kuhakikisha kwamba tunaboresha uandikaji wa wosia kwa wahusika. (*Makofii*)

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili, amesema sawa kwamba gharama kuanzia milioni 50, gharama ni Sh.5,000, kuanzia milioni 51 mpaka millioni 200 gharama za uandikishaji ni Sh.20,000. Kuanzia milioni 201 mpaka milioni 500 ni shilingi 30,000 na kuanzia hapo na kwenda juu ni shilingi 50,000. Ukitazama gharama hizi kwa kweli sio kubwa sana na kama tutapata mawazo kama uliyoyatoa hapo na kutoka kwa wananchi na kutoka kwenye ofisi zetu tunaweza tukatazama upya gharama hizi kulingana na mahitaji yatakavyojitekeza ili iwe ni motisha kwa wazazi, kwa ndugu kuweza kujandikisha na kutumia huduma hii ya Serikali na Mashirika Yasiyo ya Kiserikali. Ahsante. (*Makofii*)

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali na majibu. Nitaleta kwenu matangazo tuliyonayo. Tutaanza na matangazo ya

wageni waliopo siku ya leo na tutaanza kutangaza wageni waliopo jukwaa la Spika.

Kwanza ni wageni 22 wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ambaa ni viongozi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo wakiongozwa na Dkt. Laurian Ndumbaro ambaye ni Katibu Mkuu Utumishi. Karibu sana. (*Makofii*)

Yupo pia Dkt. Moses Kusiluka ambaye ni Katibu Mkuu Ikulu; Dkt. Francis Michael ambaye ni Naibu Katibu Mkuu Utumishi; Mheshimiwa Jaji Mstaafu Harold Nsekela ambaye ni Kamishna wa Madini; Dkt. Modestus Kipilimba ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Usalama wa Taifa; Ndugu Nyakimura Muhoji ambaye ni Katibu Tume ya Utumishi wa Umma; Dkt. Emmanuel Shindika ambaye ni Mkuu wa Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania; na Ndugu Waziri Kipacha ambaye ni Kamishna Msaidizi Maadili, karibuni sana. (*Makofii*)

Pia tunaye CP. Diwani Athumanii ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU; Brigedia Jeneralii John Mbung'o ambaye ni Naibu Mkurugenzi Mkuu TAKUKURU; Ndugu Ashery Mwanda ambaye ni Mkurugenzi wa Fedha na Mipango, Idara ya Usalama wa Taifa; Brigedia Jeneralii Machanga ambaye ni Mratibu Baraza la Usalama wa Taifa; Ndugu Ladislaus Mwamanga ambaye ni Mkurugenzi Mkuu TASAF; na Ndugu Seraphia Mgembe ambaye ni mratibu wa MKURABITA, karibuni sana. (*Makofii*)

Tunaye Profesa Joseph Semboja ambaye ni Mtendaji Mkuu Taasisi ya Uongozi; Ndugu Benjamin Ndimila ambaye ni Mtendaji Mkuu Wakala wa Ndege za Serikali; Ndugu Jabir Bakari ambaye ni Mtendaji Mkuu Wakala wa Serikali Mtandao; Ndugu Charles Senkondo ambaye ni Mtendaji Mkuu Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao; Ndugu Firmin Msiangi ambaye ni Kaimu Mtendaji Mkuu, Idara ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao; Ndugu Exaver Daud ambaye ni Mtendaji Mkuu Sekretarieti ya Ajira; Ndugu Mariam Mwaniilwa ambaye ni Mtendaji Mkuu Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma; na Dkt. Fred Msemwa

ambaye ni Mtendaji Mkuu Watumishi *Housing*, karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni 50 wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) ambao ni Viongozi wa Wizara na Taasisi zilizo chini ya ofisi hiyo wakiongozwa na *Engineer Joseph Nyamhanga* ambaye ni Katibu Mkuu; Dkt, Dorothy Gwajima ambaye ni Naibu Katibu Mkuu (Afya); Ndugu Tixon Nzunda ambaye ni Naibu Katibu Mkuu (Elimu); Ndugu Winifrida Rutahindurwa ambaye ni Katibu Tume ya Utumishi wa Walimu –TSC; Dkt. Mpamila Madale ambaye ni Mkuu wa Chuo *LGTI* Hombolo; Ndugu Robert Shilingi ambaye ni MKurugenzi Shirika la Elimu Kibaha; *Engineer Ronald Lwakatare* ambaye ni Mkurugenzi Mkuu, *DART*; *Engineer. Victor Seif* ambaye ni Mkurugenzi Mkuu *TARURA*; na Ndugu Hetson Msalale ambaye ni Mkurugenzi Shirika la Masoko ya Kariakoo, karibuni sana. (*Makofi*)

Wapo pia wageni wengine watano wa Mheshimiwa Suleiman Jaffo ambao ni familia yake wakiongozwa na mke wake ndugu Asha Shama Vuai, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wa Waheshimiwa Wabunge, tunaanza na wageni watatu wa Mheshimiwa Dkt. Harrison Mwakyembe, Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo ambao ni Watendaji wa Taasisi ya *Arise Africa* Mwenyekiti ndugu Kulthum Maabad, ndugu Rahma Issa na Ndugu Allya Mohamed, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa *Engineer Atashasta* Nditye ambaye ni Naibu Waziri wa Uchukuzi na Mawasiliano ambaye ni mpigakura wake kutoka Jimboni kwake Muhambo, Wilayani Kibondo, Mkoani Kigoma, Dkt. Emmanuel Mwasulama, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni watano wa Mheshimiwa Justin Monko ambao ni marafiki zake na wadau wa maendeleo kutoka Makete Njombe na Tanga wakiongozwa na Padri Marco Turra, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Flatei Massay ambaye ni mpigakura wake kutoka Mbulu Vijijiini, Mkoani Manyara ndugu Emmanuel Haali. Karibu sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Joseph Kasheku Musukuma ambaye ni Mwenyekiti wa CCM Mtaa wa Katoma, Mkoani Geita ndugu Simon Nyahinga, karibu sana (*Makofi*).

Tunao pia wageni watatu wa Mheshimiwa Japhary Michael ambaao ni familia yake kutoka Mkoani Kilimanjaro wakiongozwa na mke wake ndugu Neema Mushi, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wanne wa Waheshimiwa Wabunge Suzan Mgonokulima, Mheshimiwa Grace Tendega na Mheshimiwa Mchungaji Peter Msigwa ambaao ni Madiwani wa CHADEMA kutoka Manispaa ya Iringa wakiongozwa na Mheshimiwa Teodora Kalungwana. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa George Malima Lubeleje ambaao ni wajasiriamali kutoka Jijini Dodoma, ndugu Leonida Mkomoya na ndugu Magdalena Sumbali, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunaye pia mgeni wa Mheshimiwa Aida Khenani ambaye ni rafiki yake kutoka Makole Mkoani Dodoma ndugu Brighton Masalu, karibu sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni wawili wa Mheshimiwa Amina Mollel kutoka Jijini Dar es Salaam ambaao ni mume wake ndugu Leonida Farid Kidogo na shemeji yake ndugu Jovin Temba. Karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao pia wageni waliopo Bungeni kwa ajili ya mafunzo na huyu ni mgeni kutoka Jijini Dar es Salaama ambaye amekuja kujifunza jinsi Bunge linavyofanya kazi na huyu ni ndugu Kulwa Ndunguru. Karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni tulionao Bungeni siku ya leo, lakini lipo tangazo kutoka kwa Mheshimiwa Shally Raymond ambaye ni Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore hapa Bunge anawatangazia Waheshimiwa wote kwamba leo Jumatano tarehe 10 Aprili, 2019 kutakuwa na Ibada ya misa kwa Wakristo Wakatoliki mara baada ya kuahirisha shughuli za Bunge saa saba mchana katika ukumbi wa Pius Msekwa ghorofa ya pili. Aidha, Waheshimiwa Wabunge wengine wote wanaopenda kushiriki misa hiyo wanakaribishwa. Kwa hiyo mnatangaziwa na Mwenyekiti wa Jumuiya ya Mtakatifu Thomas Moore kwenda kuhuduria Ibada hiyo.

Baada ya kusema hayo, Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na utaratibu wetu uliopo.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mwongozo wa Spika...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mnyika unazifahamu vizuri Kanuni, ukizungumza Mwongozo wakati bado nimesimama unafahamu kanuni zetu zinasemaje, kwa hiyo subiri nikae ndiyo uzungumze.

Mheshimiwa Mnyika

MWONGOZO WA SPIKA

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Naibu Spika nashukuru. Mapema leo tumekabidhiwa orodha ya shughuli za leo ambayo pamoja na mambo mengine kuna hati zilizowasilishwa mezani ambapo takriban ripoti 17 za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali zimewekwa mezani. Sasa kwa mujibu wa utaratibu hati zikiwekwa mezani maana yake ni nyaraka zilizo wazi kwa umma na Wabunge tunapaswa tupewe nakala na utaratibu wa Wabunge kupewa nakala ni ama kupewa humu Bungeni au kuwekwa kwenye *pigeon holes*, lakini mpaka hivi sasa ninavyozungumza na wewe nyaraka hizi zote 17 bado hatujapatiwa nakala iwe kwa kuwekwa hapa Bungeni au kuwekwa katika *pigeon holes*. Sasa naomba mwongozo

wako kwamba hizi nakala tutapewa saa ngapi, lakini mwongozo wako kwenye jambo hili hili kwa sababu kwa utaratibu wa kawaida wa miaka yote nyaraka hizi...

NAIBU SPIKA: Mheshimiwa Mnyika, mwongozo ni mmoja tu, umeshaomba wa kwanza huo unasema ni wa pili. Mheshimiwa Joseph Mbilinyi.

MHE. JOSEPH O. MBILINYI: Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Bunge hili lilipitisha Azimio la kukataa kufanya kazi na *CAG* lakini sijashuhudia Azimio lingine lolote la kutengua Azimio lile la Bunge lako Tukufu ingawa kwenye *Order Paperya* leo nimeona kuna ripoti ya *CAG* imeletwa ili tufanyie kazi. Je, alishateuliwa *CAG* mpya au ni yuleyule Profesa Assad. (*Makofii/Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba mwongozo wako kwa sababu jambo hili linaendelea kulichanganya Taifa na tunapolichanganya Taifa ni hatari kwa usalama wa Taifa na kwa *stability* ya uchumi. Ahsante sana.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo.

NAIBU SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tumeombwa miongozo miwili hapa, mmoja umeombwa na Mheshimiwa Mnyika na mwingine na Mheshimiwa Joseph Mbilinyi. Mwongozo wa Mheshimiwa Mnyika unahusu Wabunge kutokupatiwa nakala ambazo Serikali imeziweka hapa Mezani. Ametoa maelezo ambayo sikusudii kuyarudia kwamba taarifa ikishawekwa hapo Mezani maana yake ni taarifa ya wazi na kwa mujibu wa taratibu Waheshimiwa Wabunge wanapaswa kupewa nakala, kwamba wanapewa saa ngapi, hilo halijasemwa popote.

Waheshimiwa Wabunge, hata hivyo, nakala hizi kwa kuwa zimeshaporelewa hapa maana yake ni kwamba Ofisi ya Spika imeshapokea taarifa hizi, itachukua utaratibu wa kawaida kabisa wa kuwakabidhi Wabunge nakala wanazostahili. (*Makofii*)

Waheshimiwa Wabunge, mwongozo mwingine ambao nimeombwa ni wa Mheshimiwa Joseph Mbilinyi, anasema kwamba taarifa nyingi zilizowekwa Mezani leo zinatokea Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na kwamba Bunge hili lilikwishapitisha uamuzi, kwa maelezo yake, wa kutofanya kazi na Ofisi ya CAG. Anauliza kama Bunge limebatilisha maamuzi yake ama vipi kwa kupokea taarifa hizi?

Waheshimiwa Wabunge, tunafahamu wazi kwamba Kanuni zetu hasa Kanuni ya 64(1)(c), kwa ujumla hii Kanuni inazungumzia mambo ambayo hayaruhusiwi Bungeni ikiwa ni pamoja na kuleta jambo ambalo lilikuwa limeshafanyiwa maamuzi na Bunge hili kama hukuleta hoja mahsus. Maana yake ni hii, Bunge lilishatoa maamuzi na Azimio ambalo analisema, anafahamu, kwamba Mheshimiwa Spika alitoa hapa ufanuzi ule ambao huko nje kuna watu kwa sababu zao binafsi walikuwa wakilipotosha. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Spika alisimama hapa siku ya pili yake na akatoa ufanuzi. Ufanuzi huo unaweza tu kubadilishwa mtu akileta hoja mahsus. Azimio la Bunge pia kama unataka libadilishwe unaleta hoja mahsus.

Kwa hiyo, mwongozo wangu ni kwamba hilo ni jambo ambalo haliruhusiwi Bungeni kwa kuwa Bunge lilishafanya maamuzi na hakuna hoja mahsus iliyoletwa kwa ajili ya jambo hilo. (*Makof*)

Waheshimiwa Wabunge, baada ya kupokea miongozo hiyo, Mwenyekiti wa Bunge atakuja kunipokea na kuendelea na ratiba.

Hapa Mwenyekiti (Mhe. Mussa A. Zungu) Alikalia Kiti

MWENYEKITI: Katibu.

NDG. NEEMA MSANGI - KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI. (*Makofii*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais-TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kupitisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, naomba hotuba yangu kama nilivyoiwasilisha Bungeni iingie kwenye Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kuiongoza Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambayo ina wajibu wa kuwashudumia wananchi kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake imara, wenye weledi na umakini katika utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 ambao umeiwezesha nchi yetu kupiga hatua

ya maendeleo katika utoaji wa huduma kwa sekta zote. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuongoza shughuli zote za Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipekee nikupongeze wewe Mwenyekiti, ambaye umekaa hapa leo lakini nimpongeze Mheshimiwa Spika na Naibu Spika...

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, ndani ukumbi tunaomba order. Waheshimiwa tunaomba utulivu ndani ya ukumbi. Ukinanyuka, ukitoka, uondoka kwa ustaarabu na kwa upole.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuwapongeza kwa hekima na busara mnazotumia kuliongoza Bunge hili la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanne Mchomba, Mbunge wa Viti Maalum na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kuchambua na kujadili Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Maoni, ushauri na ushirikiano uliotolewa na Kamati umewezesha Wizara yangu kukamilisha maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ufanisi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sasa napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Mpango na Makadirio ya Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019, ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili wa Mwaka 2016/2017 hadi 2020/2021, Agenda ya Dunia ya Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli, wakati akizindua Bunge la Kumi na Moja, Novemba, 2015, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015, dhana ya Upelekaji Madaraka kwa Umma na Sera mbalimbali za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri iliidhinishiwa jumla ya shilingi trilioni 6.58 kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya shilingi trilioni 4.13 ni Mishahara, shilingi bilioni 649.3 ni Matumizi Mengineyo na shilingi trilioni 1.80 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo, kiasi cha shilingi trilioni 1.27 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 527.1 ni fedha za nje. Hadi Februari, 2019, jumla ya shilingi trilioni 3.43 zilikuwa zimepokelewa sawa na asilimia 52 ya bajeti iliyoidhinishwa kwa mafungu yote ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maduhuli ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Mikoa. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mikoa iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya shilingi bilioni 22.7. Kati ya fedha hizo, shilingi milioni 20 ni maduhuli ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, shilingi bilioni 22.6 ni maduhuli ya Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na shilingi milioni 130.5 ni maduhuli ya Mikoa. Hadi Februari, 2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekusanya jumla ya shilingi milioni 7.9 sawa na asilimia 40 ya lengo, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI zimekusanya shilingi bilioni 9.8 sawa na asilimia 43 na Mikoa imekusanya jumla ya shilingi milioni 118.6 sawa na asilimia 85 ya lengo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato ya ndani ya Halmashauri. Katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 735.6 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya ndani. Hadi kufikia Februari, 2019, Halmashauri zilikuwa zimekusanya jumla ya shilingi bilioni 392.90 sawa na asilimia 53 ya makadirio. Kiasi kilichokusanywa ni ongezeko la shilingi bilioni 111.6 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 281.3 zilizokusanywa hadi Februari, 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ongezeko la makusanyo limechangiwa na kuimarishwa kwa usimamizi na udhibiti, elimu na hamasa kwa walipa kodi na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, mkakati uliowekwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI wa kuzishindanisha Halmashauri kila robo mwaka umesaidia kuongeza juhudzi ya ukusanyaji wa mapato ya ndani miongoni mwa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi, hadi Februari 2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 181.7 sawa na asilimia 45.2 ya bajeti ya shilingi bilioni 402.3. Aidha, katika kipindi hicho, Tume ya Utumishi wa Walimu ilikuwa imepokea jumla ya shilingi bilioni 5.6 sawa na asilimia 45 ya bajeti ya shilingi bilioni 12.5 zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Vilevile, Mikoa 26 imepokea jumla ya shilingi bilioni 144.3 kati ya bajeti ya shilingi bilioni 298.3 sawa na asilimia 48.4. Kadhalika, Halmashauri 185 zimepokea jumla ya shilingi triliioni 3.10 kati ya shilingi triliioni 5.88 zilizoidhinishwa sawa na asilimia 52.7.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utawala bora na demokrasia. Utawala bora ni nyenzo muhimu katika kuharakisha maendeleo endelevu ya nchi kwa kuzingatia misingi ya sheria, uwazi na uwajibikaji ili kutoa huduma bora kwa wananchi. Malengo ya kijamii na kiuchumi hayawezi kufikiwa endapo itakosekana misingi ya haki, usawa, uwazi na uwajibikaji. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inasimamia utekelezaji wa shughuli za utawala bora kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 146(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa

Tanzania ya mwaka 1977 inayohusu ugatuaji wa madaraka kwa wananchi ili kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuimarisha utawala bora na demokrasia ikiwa ni pamoja na maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019, ujenzi wa majengo ya utawala katika Mikoa, Halmashauri, Tarafa, Kata, Mitaa na Vijiji ili kuboresha mazingira ya kufanya kazi, kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo viongozi na Watendaji kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuimarisha misingi ya uwazi, uwajibikaji na usawa katika matumizi ya fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ibara ya 146(1) na (2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya mwaka 1977 inaelekeza uimarishaji wa demokrasia kwa wananchi na kuwawezesha wananchi kushiriki katika kujiletea maendeleo. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatekeleza matakwa hayo ya Kikatiba kwa kuhakikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unafanyika kila baada ya miaka mitano kwa kuzingatia Sheria za Serikali za Mitaa Sura 287 na 288.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 utakuwa wa sita tangu ulipofanyika kwa mara ya kwanza chini ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa mwaka 1994. Viongozi watakaochaguliwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 ni Wenyeviti na Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Wajumbe wa Kamati za Mitaa na Wenyeviti wa Vitongoji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekamilisha zoezi la uhakiki wa maeneo ya utawala ambayo yatashiriki katika uchaguzi huo katika Halmashauri zote 184 ukiondoa Jiji la Dar-es-Salaam kwa kushirikisha Wizara za Kisekta, Mikoa na Halmashauri. Lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kujiridhisha na usahihi wa maeneo hayo kwa idadi na majina kabla ya kutoa Tangazo la Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa. Usahihi wa takwimu hizo ni

muhimu kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya uchaguzi na mahitaji muhimu kwa ajili ya uchaguzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekamilisha maandalizi ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa mwaka 2019 ambazo zimeandaliwa kwa kuwashirikisha wadau mbalimbali wakiwemo Wakuu Mikoa 26, Makatibu Tawala wa Mikoa 26, Wakurugenzi wa Halmashauri 184, Maafisa Uchaguzi 184, Vyama vyta Siasa vyenye usajili wa kudumu na Taasisi za Dini na Asasi Zisizo za Kiserikali. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatoa wito kwa wadau mbalimbali na wananchi kujandikisha na kuchukua fomu za kugombea na kujitokeza kwa wingi wakati wa kupiga kura ili kutumia haki yao ya kidemokrasia ya kuchagua au kuchaguliwa katika uchaguzi huo muda utakapofika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jukumu la msingi la Ofisi ya Rais-TAMISEMI ni kuzijengea uwezo Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Mafunzo yametolewa kwa Wakuu wa Wilaya 27 walioteuliwa Oktoba, 2018, Wakuu wa Mikoa 26 na Makatibu Tawala wa Mikoa 26, Wakurugenzi wapya wa Halmashauri 39, walioteuliwa walifanyiwa mafunzo juu ya utawala bora kupitia Taasisi ya Uongozi kuhusu utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Serikali. Vilevile, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mipango na Uratibu 26 wa Mikoa na Maafisa Mipango 185 wa Halmashauri walipatiwa mafunzo kuhusu mipango na bajeti. Mafunzo mengine yalitolewa kwa wataalam 2,602 wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakiwemo Maafisa Utumishi, Maafisa Mipango, Maafisa Elimu, Waganga Wakuu, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Lishe, Wakaguzi wa Ndani na Maafisa Ugavi. Mafunzo yametolewa pia kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa 1,614. Mafunzo hayo yamesaidia kuboresha utendaji kazi ndani ya mamlaka ya Serikali na kutatua kero za wananchi ili kuboresha utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA iliyopo na kubuni mifumo mipya ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa

shughuli za Serikali. Mifumo iliyobuniwa ni pamoja na Mfumo wa Usajili wa Maeneo ya Utawala kwa ajili ya utambuzi wa maeneo ya utawala ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za utoaji wa huduma kwa wananchi, Mfumo wa Kusajili Wadau wa Maendeleo na Vibali vya Tafiti ambao unatumika kuratibu Wadau wa Maendeleo ili kuwatambua na kujuu kazi wanazotekeliza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mifumo mingine iliyosanifiwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ni pamoja na Mfumo wa Daftari la Wakazi (*Electronic Population Register System*) ambao umeanza kutumika kwa majoribio kusajili taarifa za wakazi katika Mikoa ya Songwe na Pwani, Mfumo wa Kuchagua Kidato cha Kwanza na Tano ambao unafanya kazi, Mfumo wa Kielektroniki wa Uhamisho wa Watumishi ambao unaendelea kukamilishwa na Mfumo wa Kielektroniki wa Ufuatilaji na Tathmini ambao umejumuisha viashiria kutoka kwenye sekta zote ambazo utekelezaji wake unafanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mmfumo ya kielektroniki unaotumika katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa umechangia kuboresha hali ya upatikanaji wa taarifa kwa wakati, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, Tawala za Mikoa zimetumia jumla ya shilingi bilioni 31.64 kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Ofisi na nyumba za viongozi katika Mkoa, Wilaya na Tarafa. Kati ya Fedha hizo, shilingi bilioni 20.6 zimetumika kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Tarafa na shilingi bilioni 11.04 zimetumika kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa nyumba za viongozi kwenye Mikoa, Wilaya na Tarafa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa umefanyika katika Mikoa ya Katavi, Simiyu, Njombe, Geita, Pwani, Arusha, Ruvuma, Dodoma na Singida kwa għarama ya shilingi bilioni 7.2. Aidha, ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya umefanyika katika Wilaya 29. Aidha, Ofisi 60 za Maafisa Tarafa zimejengwa kwa għarama ya shilingi bilioni 3.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile zimejengwa nyumba za viongozi 72 katika Mikoa na Wilaya kwa ajili ya Wakoo wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Tarafa. Hadi Februari 2019, ujenzi na ukarabati wa nyumba hizo umegharimu jumla ya shilingi bilioni 11.04.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Halmashauri 78 zimeendelea na ujenzi wa majengo ya utawala zikiwemo Halmashauri 55 zilizotengewa bajeti ya shilingi bilioni 61.7 kuanzia mwaka wa Fedha 2015/16 hadi 2017/18. Ujenzi wa majengo hayo upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Halmashauri 23 zilizoanzishwa mwaka 2014 ziliidhinishiwa jumla ya shilingi bilioni 52.9 katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri. Hadi Februari, 2019 Halmashauri 23 zimepokea jumla ya shilingi billioni 23 sawa na asilimia 43.4 kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika sekta ya afya, huduma bora za afya ni msingi wa kuondoa umaskini na kuharakisha maendeleo ya wananchi. Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kutekeleza llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya mwaka 2015 inayoelekeza kuwa na Hospitali kila Wilaya, Kituo cha Afya kila Kata na Zahanati kila Kijiji. Lengo la mpango huo wa maendeleo ni kuongeza upatikanaji wa huduma za afya ya msingi katika ngazi zote ili kuboresha maisha ya wananchi na kuchochea ukuaji wa uchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha 2018/2019, ziliidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 100.5 kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Hospitali 67 za Halmashauri. Hadi Februari 2019, fedha zote zilikuwa zimepokelewa kwenye Halmashauri na ujenzi unaendelea kwa kutumia utaratibu wa "Force Account" kwa kuzingatia Kanuni ya 167 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za mwaka 2013 pamoa na marekebisho yake ya mwaka 2016.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ujenzi wa Hospitali hizo za Hamashauri unahusisha majengo saba ambayo yamejengwa kwa kutumia shilingi bilioni 1.5 kwa kila Halmashauri zilizowekwa kwa kila Halmashauri. Majengo hayo ni ya Utawala, majengo ya nje, stoo ya madawa, maabara, jengo la mionzi, jengo la kufulia na jengo la wazazi. Aidha, ujenzi huo unatarajiwa kukamilika ifikapo Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi na ukarabati wa Vituo vya Afya nchini ni mkakati wa Serikali wa kuboresha huduma ya Afya ya Msingi yaani (*Primary Health Care*) ili kupunguza msongamano katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na zile za Kanda.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeendelea na ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma afya. Ujenzi na ukarabati huo unahusisha vituo vya kutolea huduma ya afya 352 ambao umegharimu jumla ya shilingi 184.67. Ujenzi na ukarabati huo umehusisha ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto, nyumba moja ya mtumishi, jengo la wagonjwa wa nje na chumba cha kuhifadhi maiti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeendelea kutoa fedha nyingi kwa kutumia utaratibu wa "*Force Account*" ambapo gharama zimepungua kutoka Shilingi bilioni 2.5 hadi Shilingi milioni 400 au 500 kwa kila Kituo cha Afya. Sambamba na ujenzi na ukarabati, Serikali imetoea jumla ya Shilingi bilioni 41.6 kwa ajili ya ununuzi wa vifaa tiba. Vilevile, Wataalam wa Usingizi zaidi ya 200 wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya kuimarisha huduma na upasuaji kwenye vituo vya afya vilivyojengwa na kukarabatiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti; sambamba na ujenzi wa miundombinu, Serikali imeajiri watumishi wa kada ya afya wapatao 8,447 waliopangiwa kufanya kazi katika vituo vilivyojengwa na watumishi 2,267 walioajiriwa mwaka wa fedha 2016/2017 na watumishi 6,180 walioajiriwa katika mwaka wa

fedha 2018/2019. Vilevile Taasisi ya Benjamini Mkapa imeajiri watumishi 300 na kuwapanga katika maeneo ya kipaumbele kwenye vituo vilivyokarabatiwa ili wawenze kutoa huduma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kuhakikisha huduma bora za afya zinapatikana, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeratibu uanzishwaji wa Mfumo wa Mshirini katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara ikiwa ni utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya na utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015. Mfumo wa Mshirini umeviwezesha vituo vya kutolea huduma ya afya kupata mahitaji ya vifaa, vifaa tiba, dawa na vitendanishi kutoka kwa Wauzaji Binafsi walioteuliwa pindi mahitaji yanapokosekana kutoka Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika wa mpango wa lishe, nchi yetu bado inakabiliiwa na matatizo ya lishe duni ambapo viwango vya udumavu katika Mikoa mingi bado siyo ya kuridhisha. Kwa mujibu wa daftari la Hali ya Afya nchini kwa mwaka 2016/2017 inaonesha hali ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano ni asilimia 34.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali kwa kushirikiana na jamii na Wadau wa Maendeleo inatekeleza Mpango Jumuishi wa Taifa ya Taifa ya Lishe wa Miaka Mitano ambao umejielekeza katika kutekeleza afua mbalimbali za lishe likiwemo tatizo la utapiamlo. Serikali imeweka kipaumbele na kuongeza rasilimali fedha za utekelezaji afua za lishe kutoka Shilingi bilioni 11 zilizoishia mwaka wa fedha 2017/2018 hadi Shilingi bilioni 15 katika mwaka wa fedha 2018/2019 sawa na ongezeko la asilimia 3.6.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, katika kipindi hicho wadau wa maendeleo walitoa kiasi cha shilingi bilioni 4.96 zilizotumika kutekeleza afua za lishe katika baadhi ya Mikoa na Halmashauri nchini. Ongezeko la rasilimali fedha limesaidia kuongeza kiwango cha utoaji wa huduma ya matone ya vitaminini A kutoka asilimia 93 mwaka 2017 hadi asilimia 97 kwa mwaka 2018; na utoaji wa dawa za minyoo umeongezeka

kutoka asilimia 92 mwaka 2017 hadi asilimia 96 kwa mwaka 2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imesaini mkataba na utendaji kazi na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri ili kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika utekelezaji wa afua za lishe nchini. Mikataba hiyo inafanyiwa tathmini kila baada ya miezi sita ili kupima kufanikiwa kwa malengo ya kutokomeza utapiamlo. Vilevile Serikali imeimarisha maeneo ya rasilimali watu hasa wataalam wa lishe ambapo jumla ya wataalam wapatao 113 wameajiriwa ili kuboresha mkakati wa utekelezaji wa afua za lishe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la ulinzi na usalama wa mtoto, katika hatua ya kuendelea kulimarisha ulinzi na usalama wa mtoto kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Wataalam wa Ustawi wa Jamii wapatao 505 kati ya 738 wamepatiwa mafunzo kuhusu namna ya kutoa huduma ya ulinzi na usalama wa mtoto katika maeneo yao. Hadi Februari, 2019, watoto wapatao 389,012 wanaoishi katika mazingira magumu wametambuliwa ikilinganishwa na watoto 201,382 waliotambuliwa hadi Machi, 2018 na kupatiwa huduma mbalimbali ikiwemo kuunganishwa na familia zao, vifaa vya shulen na ada za kujiunga na vyuo vya mafunzo ya ufundi ikiwemo vyuo vya *VETA*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika upande wa Watu Wenye Ulemavu waliotambuliwa walikuwa ni 405,426. Jumla ya Watu Wenye Ulemavu 217,932 kati ya 405,426 ya waliotambuliwa, walipatiwa huduma ya Afya kwa gharama ya shilingi milioni 102.1 na kati yao 3,226 walipatiwa kadi ya Bima ya Afya ya Jamii (*CHF*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa huduma za wazee, hadi Februari, 2019 jumla ya wazee 750,622 walitambuliwa ikilinganishwa na wazee 300,000 waliotambuliwa hadi Februari, 2018. Kati ya hao, wazee 247,705 walipatiwa vitambulisho vya matibabu bure, sawa

na asilimia 33 ya wazee wote walio tambuliwa. Aidha, kati ya hao, wazee 502,917 wamepatiwa kadi ya matibabu ya Afya ya Jamii (*CHF*) sawa na asilimia 67.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI imeboresha utaratibu wa usimamizi wa fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya kwa kuzipeleka fedha moja kwa moja kwenye Vituo vya Kutolea Kuduma ya Afya ambapo wananchi wanashirikishwa kuititia Kamati za Usimamizi wa Vituo vya Kutolea Huduma za Afya. Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeanzisha mfumo wa kielektroniki ujulikanao kama *FFARS* ambao unatumika kusimamia fedha hizo na kurahisisha upatikanaji wa taarifa ya matumizi ya fedha hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa Mpango wa Malipo Kulingana na Ufanisi (*Result Based Financing*) ulianza kutekelezwa mwaka 2015 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga kwa majoribio na baadaye kwa mwaka 2016, Programu hiyo ilianza kutekeleza katika Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga. Kwa sasa Mpango wa Malipo Kulingana na Ufanisi unatekelezwa katika Mikoa minane ya Shinyanga, Mwanza, Pwani, Simiyu, Tabora, Kagera, Geita na Kigoma yenye jumla ya Halmashauri 59 na vituo 1,655 vya kutolea huduma ya afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mikoa hiyo ilichaguliwa kutokana na uwepo wa vifo vya mama wajawazito vilivyosababishwa na kukosekana na huduma za msingi pamoja na idadi ndogo ya wataalam wa afya kwenye maeneo hayo. Mpango huo unahuishi ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya na kujenga uwezo wa Timu za Usimamizi wa huduma ya afya ngazi ya Mkoa na Wilaya.

Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Februari, 2019 jumla ya shilingi bilioni 26.1 zimetumika kutekeleza mpango huo katika shughuli za usimamizi ngazi ya Mkoa na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma ya afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utekelezaji wa mpango huo umesaidia kuboresha huduma za afya ambapo Mikoa hiyo sasa inafanya vizuri katika kiwango cha utoaji wa huduma ya afya kutoka mwaka 2015 hadi 2018. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuimarika kwa ushirikishwaji wa wananchi kupitia kuongezeka kuundwa kwa Bodi ya Afya za Halmashauri kutoka asilimia 50 hadi asilimia 86.2. Vituo vya Afya vyenye nyota sifuri vimepungua kutoka asilimia 42.5 hadi asilimia 3.1 na vituo vyenye nyota zaidi ya tatu vimeongezeka kutoka asilimia 0.8 hadi asilimia 23.2. Aidha, kiwango cha ubora wa takwimu kimeongezeka kutoka asilimia 70 hadi asilimia 89.5 kwenye Mikoa minane ya utekelezaji wa mpango huo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika suala zima la Utekelezaji wa Elimu Msingi Bila Malipo, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha, kuimarisha na kuinua kiwango cha Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa lengo la kuhakikisha elimu katika ngazi zote inakuwa na ubora unaostahili. Lengo ni kuwa na jamii iliyoelimika yenye maarifa, uzalendo na ujuzi wa kutosha kumudu ustawi wa maisha yao na kuhimili ushindani wa ndani na wa Kimataifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti; kwa upande wa Elimu ya Awali, uandikishaji wa wanafunzi wapya katika mfumo rasmi wa elimu nchini umeonesha kuwa hadi Machi, 2019 wanafunzi wa elimu ya awali walioandikishwa ni 1,278,816 sawa na asilimia 92.48 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,382,761. Aidha, kati ya hao walioandikishwa, wanafunzi 1,372 ni wenye mahitaji maalum. Vilevile, wanafunzi wapya walioandikishwa kuanza Darasa la Kwanza ni 1,670,919. Kati ya hao, wanafunzi wenye mahitaji maalum walioandikishwa ni 3,028.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kushirikiana na wananchi na wadau wa maendeleo katika kuboresha miundombinu ya Shule za Awali na Msingi. Hadi Februari, 2019 ujenzi wa vyumba vya madarasa 2,840 kwa Shule za Msingi umefanyika ambapo

vyumba nya madarasa 6,637 viko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Vilevile, jumla ya matundu ya vyoo 7,067 kwa vyoo nya wanafunzi 6,445 na vile nya Walimu 622 yamejengwa katika Shule za Msingi. Aidha, matundu ya vyoo 3,004 yameendelea kujengwa na yanatarajiwa kukamilika kabla ya Juni, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kazi nyingine za kuboresha miundombinu ya elimu zilizofanyika pia ni pamoja na ujenzi wa nyumba za Walimu 720 na kuongeza idadi ya nyumba hizo kutoka 44,320 mwaka 2018 hadi 45,040 Februari, 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, madawati ya wanafunzi watatu watatu yameongezeka kutoka madawati 2,858,982 yaliyokuwepo mwezi Machi, 2018 hadi madawati 2,994,266 Februari, 2019 sawa na ongezeko la madawati 135.284.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2019...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri una dakika tano, kwa hiyo, weka yale muhimu, halafu useme yote yaingie kwenye Hansard.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi si saa nzima au! Najua tuna present saa moja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Sasa hayo makofi ya nini?

WABUNGE FULANI: Aendelee.

MWENYEKITI: Mimi ndio referee hapa. Nusu saa Utawala Bora, nusu saa TAMISEMI.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante.

MWENYEKITI: Mnataka kutoka nje? (*Kicheko*)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Bajeti wa Mwaka wa Fedha 2019/2020 umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano (2016/2017 mpaka 2020/2021), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais TAMISEMI na Taasisi zake, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Serikali za Mitaa imepanga kutekeleza mipango mbalimbali kama inavyoainishwa kiundi katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya malengo mahsusii yaliyopangwa kutekelezwa katika mwaka mwaka wa fedha 2019/2020 ni kama yafuatavyo:-

Kuanza ujenzi wa Hospitali mpya 27 za Halmashauri. Hospitali hizo zitajengwa na kuboreshwa katika Halmashauri mbalimbali kama zinavyoainisha katika kitabu changu; kuendelea na ujenzi wa Hospitali 67 ambazo zimeishia katika bajeti mwaka wa fedha 2018/2019; ujenzi wa Vituo vya Afya vipyta 52; kutekeleza Mpango wa Elimu ya Msingi Bila Malipo ambaao utagharimu shillingi bilioni 288.7; ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba 364; ujenzi wa Sekondari mpya za wasichana 26; ununuzi wa magari mapya 26; ujenzi wa nyumba 800 na madarasa; ujenzi wa mabweni 300; Ujenzi wa matundu ya choo 1,000; ujenzi wa majengo 50; na Ujenzi wa kumbi 200.

Vile vile ukarabati wa shule kongwe 15; ununuzi wa vifaa kwa shule maalum 70; ununuzi wa magari 40 kwa ajili ya Halmashauri mbalimbali; ujenzi wa nyumba 1,200 vya madarasa kwa Shule za Msingi; ujenzi wa matundu ya vyoo 2,000; ujenzi wa mabweni 10; kuendelea na majengo ya majengo ya utawala katika Halmashauri 62 ambaao

utagharimu ya shilingi bilioni 56.5; kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala katika Mikoa mitano; kuanza ujenzi wa jengo upya katika Mkoa wa Mbeya; ununuzi wa magari 13 kwa ajili ya Halmashauri; na kuendelea na utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika Halmashauri zilizokidhi vigezo;

Pia Kufanya matengenezo ya barabara zenyе urefu wa kilometa 21,525; ujenzi wa madaraja 113, ujenzi wa makalvati makubwa 270 na makalvati madogo 2,403; ujenzi wa barabara za lami ya kilometa 15.5; ujenzi wa barabara za lami za kilometa 25 kwa mpango katika Jiji la Dae es Salaam na kuweza kutoa mikopo kwa vikundi vyę wanawake ambao utagharimu shilingi bilioni 62.5

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wangu sasa naomba kutoa shukrani kubwa sana kwa watu wote walioshiriki kwa pamoja hasa nikiwashukuru Kamati ikiongozwa na Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa. Nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati kwa kazi kubwa waliyofanya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini pia nawashukuru Manaibu wangu Mawaziri ambao ni Mheshimiwa Josephat Kandege, pamoja Mheshimiwa Mwita Waitara kwa kazi kubwa walioifanya. Namshukuru pia Katibu Mkuu wangu Bwana Nyamhanga kwa kazi kubwa aliyoifanya Dorothy Gwajima na Dickson Mzunda. Nawashukuru Wakuu wote wa Taasisi mbalimbali ambazo ziko chini ya Ofisi yangu ambao wamefanya kazi kubwa sana katika mchakato huu wa bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika napenda kuwashukuru wadau wote wa maendeleo ambao hapa kutokana muda sitaweza kuwataja. Nawashukuru kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. Vilevile naishukuru familia yangu kwa msaada mkubwa walionipa katika kutekeleza majukumu yangu. Nawashukuru wananchi wangu wa Kisarawe kwa kazi kubwa waliyofanya na kunipa moyo katika kipindi chote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kuzungumza hayo, tutarajie katika Mwaka wa Fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake na Mikoa 26 na Halmashauri 185 inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya shilingi 802,160,498,164/=. Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, ada za wanafunzi, marejesho na kodi za ushuru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa matumizi Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Taasisi zake, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa 26 na Halmashauri 185 imepanga bajeti ya matumizi kama ifuatavyo:-

Mishahara shilingi 3,807,104,425,000/=. Katika upande wa matumizi mengineyo, shilingi 707,951,000,000/=. Katika Miradi ya Maendeleo tunatarajia kutumia shilingi 1,692,937,354,769.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020 jumla ya shilingi 6,207,992,779,769/= kwa ajili ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI - Fungu Na. 56; Tume ya Utumishi wa Walimu - Fungu Na. 02; na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojumuisha Halmashauri 185.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hotuba hii, yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Taasisi zake, Mikoa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii inapatikana pia kwenye tovuti ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI ambayo ni
www.tamisemi.go.tz

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja.

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA, MHESHIMIWA SELEMANI SAIDI JAFO (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAPITIO, MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20
– KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

A. UTANGULIZI

- 1. *Mheshimiwa Spika***; kufuatia taarifa iliyowasilishwa leo ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, naomba kutoa hoja kwamba Bunge lako Tukufu likubali kupokea na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Ofisi ya Rais-TAMISEMI) kwa Mwaka wa Fedha 2018/19. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu lijadili na kuitisha Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.
- 2. *Mheshimiwa Spika***; napenda kuchukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijalia afya njema na kuniwezesha kutekeleza majukumu yangu ya kuiongoza Ofisi ya Rais-TAMISEMI ambayo ina wajibu wa kuwashudumia wananchi kiuchumi na kijamii.
- 3. *Mheshimiwa Spika***; kwa heshima kubwa naomba kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa uongozi wake imara, wenye weledi na umakini katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 ambao umeiwezesha nchi yetu kupiga hatua ya maendeleo katika utoaji wa huduma kwa Sekta zote. Aidha, nawapongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, na Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa (Mb), Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna wanavyomsaidia Mheshimiwa Rais kusimamia na kuongoza shughuli zote za Serikali ya Awamu ya Tano.
- 4. *Mheshimiwa Spika***; kipekee nakupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa hekima

na busara mnazotumia kuongoza Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vilevile, napenda kuipongeza Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaab inayoongozwa na Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijini, na Makamu Mwenyekiti, Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mbunge wa Viti Maalum, na Wajumbe wote wa Kamati hiyo kwa kuchambua na kujadili Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Maoni, ushauri na ushirikiano uliotolewa na Kamati umewezesha Wizara yangu kukamilisha maandalizi ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 kwa ufanisi.

5. *Mheshimiwa Spika*; naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wote waliochaguliwa kwenye Chaguzi Ndogo akiwemo Mheshimiwa Mwita Waitara, Mbunge wa Ukonga, ambaye kwa sasa ni Naibu Waziri, Ofisi ya Rais-TAMISEMI anayeshughulikia huduma za Elimu na Utawala; Mheshimiwa Julius Kalanga Laizer, Mbunge wa Monduli; Mheshimiwa Timotheo Paul Mnzava, Mbunge wa Korogwe Vijijini; Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Serengeti; Mheshimiwa Mhandisi Christopher Kajoro Chizza, Mbunge wa Buyungu; Mheshimiwa Joseph Michael Mkundi, Mbunge wa Ukerewe; Mheshimiwa James Kinyasi Millya, Mbunge wa Simanjiro; Mheshimiwa Pauline Philipo Gekul, Mbunge wa Babati Mjini; na Mheshimiwa Abdallah Ally Mtalea, Mbunge wa Temeke.

6. *Mheshimiwa Spika*; katika Mwaka 2018, Bunge lako Tukufu lilipata simanzi kutokana na kifo cha Mheshimiwa Stephen Hilal Ngonyani aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Korogwe Vijijini na Mheshimiwa Kasuku Bilago aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Buyungu. Natoa pole kwako Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge na familia za marehemu kwa kuondokewa na wapendwa wao. Aidha, kwa masikitiko makubwa natumia fursa hii kuwapa pole wote waliopatwa na majanga ya ajali na kufiwa na ndugu, jamaa na wapendwa wao katika matukio mbalimbali hapa nchini. Mwenyezi Mungu awapokee na kuwahifadhi mahali pema peponi. Amina.

7. ***Mheshimiwa Spika***; baada ya kusema hayo, sasa napenda kutoa maelezo ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 na Mpango na Makadirio ya Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

B. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/19

8. ***Mheshimiwa Spika***; utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19, ulizingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025, Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano Awamu ya Pili wa Mwaka 2016/17 hadi 2020/21, Agenda ya Dunia ya Malengo Endelevu ya Maendeleo ya Mwaka 2030, Hotuba ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, katika Mkutano wa 11 wa Bunge wa Novemba 2015, Sheria ya Bajeti Na. 11 ya Mwaka 2015 na dhana ya Upelekaji Madaraka kwa Umma na Sera mbalimbali za Serikali.

9. ***Mheshimiwa Spika***; katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri iliidhinishiwa kutumia **Shilingi trilioni 6.58** kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizo, jumla ya **Shilingi trilioni 4.13** ni Mishahara, **Shilingi bilioni 649.3** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi trilioni 1.80** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha za maendeleo kiasi cha **Shilingi trilioni 1.27** ni fedha za ndani na **Shilingi bilioni 527.1** ni fedha za nje. Hadi Februari, 2019, jumla ya **Shilingi trilioni 3.43** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 52** ya Bajeti iliyoidhinishwa kwa mafungu yote ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

Maduhuli ya OR-TAMISEMI na Mikoa

10. ***Mheshimiwa Spika***; katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Mikoa iliidhinishiwa kukusanya maduhuli ya **Shilingi bilioni 22.7**. Kati ya fedha **Shilingi milioni**

20.0 ni Maduhuli ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, **Shilingi bilioni 22.6** ni Maduhuli ya Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI na **Shilingi milioni 130.5** ni maduhuli ya Mikoa. Hadi Februari, 2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekusanya jumla ya **Shilingi milioni 7.9** sawa na **asilimia 40** ya lengo, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI zimekusanya **Shilingi bilioni 9.8** sawa na **asilimia 43** na Mikoa imekusanya jumla ya **Shilingi milioni 118.6** sawa na **asilimia 85** ya lengo.

Mapato ya Ndani ya Halmashauri

11. *Mheshimiwa Spika*; katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya jumla ya **Shilingi bilioni 735.6** kutoka kwenye vyanzo mbalimbali vya ndani. Hadi kufikia Februari, 2019, Halmashauri ziliikuwa zimekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 392.90** sawa na asilimia **53** ya makadirio (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 1*). Kiasi kilichokusanya ni ongezeko la **Shilingi bilioni 111.6** ikilinganishwa na kiasi cha **Shilingi bilioni 281.3** zilizokusanya hadi Februari, 2018. Ongezeko la makusanyo limechangiwa na kuimarishwa kwa usimamizi na udhibiti, elimu na hamasa kwa walipa kodi na matumizi ya mifumo ya kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, mkakati uliowekwa na OR-TAMISEMI wa kuzishindanisha Halmashauri kila robo mwaka umesaidia kuongeza juhudii ya ukusanyaji wa mapato ya ndani mionganoni mwa Halmashauri.

Matumizi

12. *Mheshimiwa Spika*; majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI yanatekelezwa katika ngazi ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI Makao Makuu, Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ofisi ya Rais-TAMISEMI Makao Makuu na Mikoa ina jukumu la kuratibu na kusimamia utekelezaji unaofanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

13. *Mheshimiwa Spika*; hadi Februari 2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zilizo chini yake ziliikuwa zimepokea jumla ya **Shilingi bilioni 181.7** sawa na **asilimia 45.2** ya bajeti ya **Shilingi bilioni 402.3**. Vilevile, hadi Februari 2019, Tume ya

Utumishi wa Walimu ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 5.6** sawa na **asilimia 45** ya Bajeti ya **Shilingi bilioni 12.5** zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu. Aidha, Mikoa 26 imepokea jumla ya **Shilingi bilioni 144.3** kati ya bajeti ya **Shilingi bilioni 298.3** sawa na **asilimia 48.4**. Kadhalika, Halmashauri 185 zimepokea jumla ya **Shilingi triliuni 3.10** kati ya **Shilingi triliuni 5.88** zilizoidhinishwa sawa na **asilimia 52.7**.

Utawala Bora na Demokrasia

14. *Mheshimiwa Spika;* utawala bora ni nyenzo muhimu katika kuharakisha maendeleo endelevu ya nchi kwa kuzingatia misingi ya Sheria, uwazi na uwajibikaji ili kutoa huduma bora kwa wananchi. Malengo ya kijamii na kiuchumi hayawezi kufikiwa endapo itakosekana misingi ya haki, usawa, uwazi na uwajibikaji. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inasimamia utekelezaji wa shughuli za utawala bora kwa kuzingatia matakwa ya Ibara ya 146(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977 inayohusu Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi ili kuboresha utoaji wa huduma za kijamii na maendeleo. Mamlaka za Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi vyenye Mamlaka ya kushiriki na kuwashirikisha wananchi katika mipango na utekelezaji wa shughuli za maendeleo katika maeneo yao. Dhana ya ugatuaji wa Madaraka kwa Umma inatekelezwa kuititia misingi mikuu minne ambayo ni ugatuaji wa madaraka ya Kisiasa, Ugatuaji wa Rasilimali Watu, ugatuaji wa rasilimali fedha na mahusiano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

15. *Mheshimiwa Spika;* katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuimarisha utawala bora na demokrasia ikiwa ni pamoja na maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019, ujenzi wa majengo ya utawala katika Mikoa, Halmashauri, Tarafa, Kata, Mitaa na Vijiji ili kuboresha mazingira ya kufanya kazi, kutoa mafunzo ya kuwajengea uwezo Viongozi na Watendaji kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuimarisha misingi ya uwazi, usawa na uwajibikaji katika matumizi ya fedha kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019

16. *Mheshimiwa Spika:* Ibara ya 146 (1) na (2)(c) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania ya Mwaka 1977 inaelekeza uimarishaji wa Demokrasia kwa Wananchi na kuawezesha Wananchi kushiriki katika kujiletea maendeleo. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatekeleza matakwa hayo ya Kikatiba kwa kuhakikisha Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unafanyika kila baada ya miaka mitano kwa kuzingatia Sheria za Serikali za Mitaa Sura 287 na 288. Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 utakuwa wa sita tangu ulipofanyika kwa mara ya kwanza chini ya Mfumo wa Vyama Vingi vya Siasa Mwaka 1994. Viongozi watakaochaguliwa katika Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 ni Wenyeviti na Wajumbe wa Halmashauri za Vijiji, Wenyeviti wa Mitaa, Wajumbe wa Kamati za Mitaa na Wenyeviti wa Vitongoji.

17. *Mheshimiwa Spika:* Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekamilisha zoezi la uhakiki wa maeneo ya utawala ambayo yatashiriki katika uchaguzi huo katika Halmashauri zote 184 ukiondoa Jiji la Dar-es-Salaam kwa kushirikisha Wizara za Kisikta, Mikoa na Halmashauri. Lengo la zoezi hilo lilikuwa ni kujiridhisha na usahihi wa maeneo hayo kwa idadi na majina kabla ya kutoa Tangazo la Serikali kupitia Waziri mwenye dhamana na Serikali za Mitaa. Usahihi wa takwimu hizo ni muhimu kwa ajili ya maandalizi ya bajeti ya uchaguzi na mahitaji mengine muhimu kwa ajili ya uchaguzi.

18. *Mheshimiwa Spika:* vilevile Ofisi ya Rais-TAMISEMI imekamilisha maandalizi ya Kanuni za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa wa Mwaka 2019 ambazo zimeandaliwa kwa kuwashirikisha Wadau mbalimbali wakiwemo Wakuu Mikoa 26, Makatibu Tawala wa Mikoa 26, Wakurugenzi wa Halmashauri 184, Maafisa Uchaguzi 184, Vyama vya Siasa vyenye usajili wa kudumu na Taasisi za Dini na Asasi Zisizo za Kiserikali. Kanuni hizo zitatumika kusimamia uchaguzi huo ambaeo utafanyika Novemba, 2019. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inatoa wito kwa wadau mbalimbali na wananchi kujandikisha, kuchukua fomu za kugombea na kujitekeza kwa wingi wakati wa kupiga kura ili kutumia haki yao ya

kidemokrasia ya kuchagua au kuchaguliwa katika uchaguzi huo muda utakapofika.

Kuzijengea Uwezo Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

19. *Mheshimiwa Spika*; jukumu la msingi la Ofisi ya Rais-TAMISEMI ni kuzijengea uwezo Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi. Mafunzo yametolewa kwa Wakuu wa Wilaya 27 walioteuliwa Oktoba, 2018 katika nyanja za mifumo, taratibu za mawasiliano Serikalini na mahusiano baina ya Taasisi za Serikali. Mafunzo hayo yameimarisha utendaji kazi wa Wakuu wa Wilaya katika usimamizi wa miradi ya maendeleo, utawala bora na utatuzi wa kero za Wananchi. Vilevile, Mwezi Desemba 2018, Wakuu wa Mikoa **26** na Makatibu Tawala wa Mikoa **26**, Wakurugenzi wapya wa Halmashauri **39** walioteuliwa walifanyiwa mafunzo juu ya utawala bora kupitia Taasisi ya Uongozi kuhusu utekelezaji wa majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Serikali. Vilevile, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mipango na Uratibu **26** wa Mikoa na Maafisa Mipango **185** wa Halmashauri walipatiwa mafunzo kuhusu mipango na Bajeti. Mafunzo hayo yamesaidia kuboresha utendaji ndani ya Serikali na kutatua kero za wananchi ili kuboresha utoaji wa huduma.

20. *Mheshimiwa Spika*; mafunzo mengine yametolewa kwa Wataalam **2,602** wa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa wakiwemo Maafisa Utumishi, Maafisa Mipango, Maafisa Elimu, Waganga Wakuu, Maafisa Ustawi wa Jamii, Maafisa Lishe, Wakaguzi wa Ndani na Maafisa Ugavi. Mafunzo yametolewa pia kwa Maafisa Watendaji wa Vijiji na Mitaa **1,614**. Mafunzo hayo yalihu uzingatiaji wa Sheria ya Ununuzi wa Umma na Sheria mbalimbali, Kanuni, Taratibu na Miongozo mbalimbali ya Utumishi wa Umma, misingi ya utawala bora, utoaji huduma, usimamizi na uendeshaji, tathmini ya utekelezaji wa mipango na bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19 na maandalizi ya mipango na bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20.

Matumizi ya Mifumo ya TEHAMA

21. Mheshimiwa Spika; Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuboresha mifumo ya TEHAMA iliyopo na kubuni mifumo mipyä ili kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Mifumo iliyobuniwa ni pamoja na Mfumo wa Usajili wa Maeneo ya Utawala kwa ajili ya utambuzi wa maeneo ya utawala ili kurahisisha utekelezaji wa shughuli mbalimbali za utoaji wa huduma kwa wananchi, Mfumo wa Kusajili Wadau wa Maendeleo na Vibali vya Tafiti ambao unatumika kuratibu Wadau wa Maendeleo ili kuwatambua na kujua kazi wanazotekeliza.

22. Mheshimiwa Spika; mifumo mingine iliyosanifiwa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI ni pamoja na Mfumo wa Daftari la Wakazi (*Electronic Population Register System*) ambao umeanza kutumika kwa majaribio kusajili taarifa za wakazi katika Mikoa ya Songwe na Pwani na Mfumo wa Kuchagua Kidato cha Kwanza na Tano ambao unafanya kazi. Aidha, Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inakamilisha maandalizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Uhamisho wa Watumishi. Mfumo huo utaimarisha uwazi, uwajibikaji na kuondoa usumbufu kwa mtumishi kulazimika kusafiri kwa ajili ya kushughulikia uhamisho.

23. Mheshimiwa Spika; Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesanifu mfumo wa kielektroniki wa ufuatiliaji na tathmini ambao umejumuisha viashiria kutoka kwenye sekta zote ambazo utekelezaji wake unafanya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfumo huo utaiwezesha Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Wizara za kisekta kupata taarifa kuhusu utekelezaji wa masuala ya kisera na kicutendaji kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mfumo uko katika hatua za mwisho za maandalizi ili uanzesha kutumika.

24. Mheshimiwa Spika; mfumo wa kusimamia huduma za afya wa GoTHOMIS unatumika katika vituo vya kutolea huduma za afya **381** ambavyo vinajumuisha Hospitali za Rufaa za Mikoa **23**, Hospitali za Halmashauri **89**, Vituo vya Afya

178 na Zahanati **91**. Lengo ni kuwa na taarifa sahihi za afya, kuimarisha ukusanyaji wa mapato na kuboresha utoaji wa huduma za afya.

25. Mheshimiwa Spika; mifumo imeunganishwa ili iwasiliane na kubadilishana taarifa kuititia *Muongano Gateway* ukiwemo Mfumo Funganishi wa Usimamizi na Udhhibit wa Matumizi ya Fedha (Epicor), Mfumo wa Mipango na Utoaji wa Taarifa (PlanRep), Mfumo wa kukusanya Mapato ya Ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (LGRCIS), Mfumo wa Kihasibu wa Mapato na Matumizi na Utoaji Taarifa na Mfumo wa GoT-HOMIS unaotumika katika vituo vya kutolea huduma za afya kwa ajili ya usimamizi na ukusanyaji wa mapato yanayotokana na uchangiaji wa huduma za afya.

26. Mheshimiwa Spika; mifumo ya kielektroniki inayotumika katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa imechangia kuboresha hali ya upatikanaji wa taarifa kwa wakati, kuongeza ukusanyaji wa mapato, kuimarika kwa uwazi na uwajibikaji katika utendaji kazi ndani ya Serikali.

Ujenzi wa Majengo ya Utawala na Nyumba za Viongozi Katika Mikoa na Halmashauri

27. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Tawala za Mikoa zimetumia jumla ya **Shilingi bilioni 31.64** kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Ofisi na nyumba za Viongozi katika Mkoa, Wilaya na Tarafa. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi bilioni 20.6** zimetumika kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Tarafa na **Shilingi bilioni 11.04** zimetumika kwa ajili ya ukarabati na ujenzi wa nyumba za Viongozi kwenye Mikoa, Wilaya na Tarafa.

28. Mheshimiwa Spika; ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa umefanyika katika Mikoa ya Katavi, Simiyu, Njombe, Geita, Pwani, Arusha, Ruvuma, Dodoma na Singida kwa gharama ya **Shilingi bilioni 7.2**. Aidha, ujenzi na ukarabati wa Ofisi za Wakuu wa Wilaya umefanyika katika Wilaya **29** ambazo ni Busega, Wanging'ombe, Nyang'hwale, Mbogwe, Dodoma Mjini, Buhigwe, Hai, Ruangwa, Malinyi, Gairo,

Nyamagana, Tunduru, Mtwara, Mbanga, Pangani, Kilindi, Korogwe, Muleba, Biharumulo, Kaliua, Kigoma, Ubungo, Nyasa, Kalambo, Muheza, Igunga, Mkalama, Lushoto na Kinondoni ambazo zimegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 10.1**. Aidha, Ofisi **60** za Maafisa Tarafa zimejengwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 3.3**.

29. *Mheshimiwa Spika*; vilevile zimejengwa nyumba za Viongozi 72 katika Mikoa na Wilaya kwa ajili ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya, Makatibu Tawala Wasaidizi wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Tarafa. Hadi Februari 2019, ujenzi na ukarabati wa nyumba hizo umegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 11.04**.

30. *Mheshimiwa Spika*; Mkoa wa Njombe umepokea jumla ya **Shilingi milioni 401.01** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa, Katibu Tawala wa Mkoa, Ofisi na nyumba ya Mkuu wa Wilaya ya Wanging'ombe. Nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa zipo katika hatua ya umaliziaji. Aidha, Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Wanging'ombe imekamilika na inatumika na nyumba ya Mkuu wa Wilaya ipo katika hatua ya umaliziaji. Mkoa wa Geita umepokea **Shilingi bilioni 2.5** kwa ajili ya ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Geita na Ofisi ya Mkuu wa Wilaya. Mkandarasi amepatikana na kazi ya ujenzi wa Ofisi hizo itaanza Aprili, 2019.

31. *Mheshimiwa Spika*; Mkoa wa Katavi umepokea jumla ya **Shilingi milioni 675.00** ambazo zimetumika kuanza ujenzi wa nyumba ya Katibu Tawala wa Mkoa, nyumba ya Mkuu wa Wilaya, nyumba ya Katibu Tawala wa Wilaya na nyumba ya Afisa Tawala wa Wilaya ya Mlele. Ujenzi uko katika hatua ya msingi. Mkoa wa Songwe umepokea **Shilingi bilioni 1.3** kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mkoa na Katibu Tawala wa Mkoa, ukamilishaji wa nyumba ya Mkuu wa Wilaya, Katibu Tawala wa Wilaya na nyumba za Maafisa Waandamizi katika Wilaya ya Momba, ujenzi wa nyumba za Maafisa Waandamizi wa Wilaya upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji. Nyumba ya Katibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Waandamizi zinajengwa kwa kutumia

utaratibu wa *Force Account*. Aidha, ujenzi wa nyumba ya Mkuu wa Mko na Katibu Tawala wa Mko wa Songwe uko katika hatua ya kutangaza Zabuni.

32. *Mheshimiwa Spika*; Mko wa Simiyu unaendelea na ukamilishaji wa nyumba ya Mkuu wa Mko na Katibu Tawala wa Mko, ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega na nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya za Busega na Itilima kwa gharama ya **Shilingi bilioni 1.48** ambapo ujenzi umekamilika katika nyumba ya Mkuu wa Mko na Katibu Tawala wa Mko. Aidha, ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Busega na nyumba za Makatibu Tawala wa Wilaya za Busega na Itilima upo katika hatua ya kutangaza zabuni.

33. *Mheshimiwa Spika*; Halmashauri **78** zinaendelea na ujenzi wa majengo ya utawala zikiwemo Halmashauri **55** zillzotengewa bajeti ya **Shilingi billioni 61.7** kuanzia Mwaka wa Fedha 2015/16 hadi 2017/18. Ujenzi wa majengo hayo upo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Halmashauri 23 zilizoanzishwa Mwaka 2014 ziliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 52.9** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri. Hadi Februari, 2019 Halmashauri **23** zimepokea jumla ya **Shilingi bilioni 23** sawa na **asilimia 43.4** kwa ajili ya kuendeleza ujenzi wa majengo ya utawala ya Halmashauri.

Huduma za Afya

34. *Mheshimiwa Spika*; huduma bora za afya ni msingi wa kuondoa umaskini na kuharakisha maendeleo ya wananchi. Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kutekeleza Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 inayoelekeza kuwa na Hospitali kila Wilaya, Kituo cha Afya kila Kata na Zahanati kila Kijiji. Lengo la mpango huo wa maendeleo ni kuongeza upatikanaji wa huduma za Afya ya msingi katika ngazi zote ili kuboresha maisha ya wananchi na kuchochaea ukuaji wa uchumi.

Ujenzi wa Hospitali za Halmashauri

35. *Mheshimiwa Spika*; katika Mwaka wa Fedha 2018/19, ziliidhinishwa jumla ya **Shilingi bilioni 100.5** kwa ajili ya kuanza

ujenzi wa Hospitali 67 za Halmashauri. Hadi Februari 2019, fedha zote zilikuwa zimepokelewa kwenye Halmashauri na ujenzi unaendelea kwa kutumia utaratibu wa "Force Account" kwa kuzingatia Kanuni ya 167 ya Kanuni za Ununuzi wa Umma za Mwaka 2013 pamoja na marekebisho yake ya Mwaka 2016. Matumizi ya utaratibu wa "Force Account" yamezingatia uzoefu uliopatikana katika ujenzi wa vituo vya Afya kwenye Halmashauri ambao umeleta manufaa makubwa katika kupunguza gharama endapo Makandarasi wangetumika kutekeleza miradi hiyo. Aidha, utaratibu huo umeongeza hamasa kwa wananchi kushiriki kwa hali na mali katika kujenga miundombinu ya huduma za kijamii katika maeneo yao na hivyo kujenga dhana ya kujitegemea, kumiliki na kuwa na sauti katika maendeleo ya huduma za afya.

36. *Mheshimiwa Spika*; ujenzi wa Hospitali za Halmashauri unahusisha majengo saba (7) ambayo yanajengwa kwa kutumia **Shilingi bilioni 1.5** zilizotolewa kwa kila Halmashauri. Majengo hayo ni ya utawala, wagonjwa wa nje, stoo ya dawa, maabara, jengo la mionzi (X-Ray), jengo la kufulia nguo na jengo la wazazi. Aidha, ujenzi huo utakamilika ifikapo Juni, 2019.

Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Afya na Zahanati

37. *Mheshimiwa Spika*; ujenzi na ukarabati wa Vituo vya afya nchini ni mkakati wa Serikali kuboresha huduma za afya ya msingi (Primary Health Care) ili kupunguza msongamano katika Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Taifa za Kanda. Hivyo, mpango huo unaboresha mfumo wa rufaa kwa wagonjwa kuanzia ngazi ya Zahanati, Vituo vya afya, Hospitali za Halmashauri, Hospitali za Rufaa za Mikoa na Hospitali za Rufaa za Kanda.

38. *Mheshimiwa Spika*; katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea na ukamilishaji wa ujenzi, ukarabati na ununuzi wa vifaa na vifaa tiba kwa ajili ya vituo vya kutolea huduma za afya. Mpango wa uboreshaji wa vituo hivyo, unazingatia upatikanaji wa huduma za upasuaji kwa mama wajawazito ili kupunguza vifo vya mama na mtoto.

Ujenzi na ukarabati huo unahusisha vituo vya kutolea huduma za afya **352**, zikiwemo Hospitali **9**, Vituo vya Afya **304** na Zahanati **39**. Vilevile, ujenzi na ukarabati wa nyumba za watumishi **301** unaendelea. Kipaumbele kiliwekwa katika kukamilisha maboma yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi.

39. *Mheshimiwa Spika*; utekelezaji wa mpango huo wa ujenzi na ukarabati wa vituo vya afya na zahanati umegharimu jumla ya **Shilingi bilioni 184.67**. Vigezo vilivyotumika kubainisha vituo vitakavyokarabatiwa vilijumuisha umbali kutoka Makao Makuu ya Halmashauri ya Wilaya, gharama za vifaa vya ujenzi katika eneo husika, hali au uwepo wa miundombinu na makubaliano na Wafadhili waliota fedha za ukarabati. Ujenzi na ukarabati huo umejumuisha ujenzi wa jengo la Mama na Mtoto, nyumba moja ya mtumishi, jengo la wagonjwa wa nje na chumba cha kuhifadhi maiti. Serikali imeweza kuokoa fedha nyingi kwa kutumia utaratibu wa "*Force Account*" ambapo gharama zimepungua kutoka **Shilingi bilioni 2.5** hadi **Shilingi milioni 400 au 500** kwa kituo. Sambamba na ujenzi na ukarabati, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 41.6** kwa ajili ununuzi wa vifaa na vifaa tiba. Vilevile, Wataalam wa Usingizi zaidi ya **200** wamepatiwa mafunzo kwa ajili ya kuimarisha huduma za upasuaji kwenye vituo vipyta vya afya vilivyojengwa na kukarabatiwa.

40. *Mheshimiwa Spika*; ukarabati wa Vituo vya afya unafanyika kwa awamu kulingana na upatikanaji wa fedha. Awamu ya Kwanza ilifanyika Oktoba 2017 hadi Aprili, 2018 ambayo ilihusisha ukarabati wa vituo vya afya **44** vilivyogharimu jumla ya **Shilingi bilioni 22.0**. Vituo hivyo vimekamilika na vimeanza kutoa huduma. Awamu ya Pili ilifanyika Januari hadi Juni, 2018 na kuhusisha vituo vya afya **139** vilivyogharimu jumla ya **Shilingi bilioni 59** ambavyo vimekamilika kwa zaidi ya **asilimia 90**. Awamu ya Tatu imefanyika kuanzia Mei hadi Novemba, 2018 na kuhusisha vituo **27** vilivyokarabatiwa kwa gharama ya **Shilingi bilioni 12.5** na Awamu ya Nne na ya Tano imehusisha ukarabati wa vituo **114** vilivyopokea jumla ya **Shilingi bilioni 42.45**. Fedha hizo

zimepelekwa moja kwa moja kwenye vituo kupitia Akaunti za vituo kwa kutumia Mfumo wa kihasibu wa Mapato na Matumizi kwenye Vituo vya Kutolea Huduma (FFARS) ambao umeimarisha uwazi, uwabijikaji, ushirikishwaji na ukusanyaji wa mapato.

Watumishi wa Kada ya Afya

41. *Mheshimiwa Spika;* ujenzi na ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya unafanyika sambamba na ajira za watumishi ili kuvivezesha vituo hivyo kuanza kutoa huduma. Kati ya Mwaka wa Fedha 2016/17 hadi 2018/19, Serikali iliajiri watumishi wa kada za afya **8,447** waliopangwa kufanya kazi katika vituo vilivyoko kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Idadi hiyo inajumuisha watumishi **2,267** walioajiriwa Mwaka wa Fedha 2016/17 na watumishi **6,180** walioajiriwa katika Mwaka wa Fedha 2018/19. Villevile, Taasisi ya Benjamin Mkapa imeajiri watumishi **300** na kuwapanga katika maeneo ya kipaumbele kwenye vituo vilivyokarabatiwa ili vianze kutoa huduma. Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto na Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ili kuhakikisha watumishi wengi zaidi wa afya wanaajiriwa kukidhi viwango vya utoaji wa huduma za afya kwa wananchi.

Upatikanaji wa Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba

42. *Mheshimiwa Spika;* Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeratibu uanzishwaji wa Mfumo wa Mshiriki katika Mikoa 26 ya Tanzania Bara ikiwa ni utekelezaji wa Awamu ya Nne ya Mpango Mkakati wa Sekta ya Afya na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015. Mfumo wa Mshiriki unaviwezesha vituo vya kutolea huduma za afya kupata mahitaji ya vifaa, vifaa tiba, dawa na vitendanishi kutoka kwa Wauzaji Binafsi walioteuliwa pindi mahitaji yanapokosekana katika Bohari Kuu ya Dawa (*MSD*). Vituo vya kutolea huduma za afya nchini vitaendelea kuagiza mahitaji ya bidhaa za afya kutoka MSD kama ulivyo utaratibu na pale vituo vitakapokosa mahitaji hayo MSD ndipo

vinaruhusiwa kuagiza kutoka kwa Mshitiri Mteule wa Mkoa kwa kutumia mapato ya ndani au fedha za makusanyo za uchangiaji za papo kwa papo. Mshitiri atavipatia vituo vya afya bidhaa za afya kulingana na uhitaji kwa bei ambazo zimekubalika kwa mujibu wa mkataba.

43. *Mheshimiwa Spika*; ili kuimarisha usimamizi na matumizi sahihi ya mfumo wa Washitiri, mafunzo yametolewa kwa Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na Wataalam ngazi ya Wizara kuhusu matumizi ya mfumo huo ambao umeanza kufanya kazi. Vilevile, watoa huduma za afya **103** ngazi ya Kitaifa, **431** kutoka ngazi ya Mkoa, **540** kwenye Hospitali za Halmashauri na Wafanyabiashara **142** wanaojihusisha na biashara ya bidhaa za dawa za walipatiwa mafunzo.

Huduma za Lishe

44. *Mheshimiwa Spika*; nchi yetu bado inakabiliwa na matatizo ya lishe duni ambapo viwango vya udumavu katika Mikoa mingi bado siyo ya kuridhisha. Kwa mujibu wa utafiti wa Hali ya Afya Nchini (TDHS) wa mwaka 2015/16 zinaonesha hali ya udumavu kwa watoto chini ya miaka mitano ni **asilimia 34**. Serikali kwa kushirikiana na jamii na wadau mbalimbali wa maendeleo inatekeleza Mpango Jumuishi wa Taifa wa Lishe wa Miaka Mitano ambao umejielekeza katika kutekeleza afua mbalimbali za lishe likiwemo tatizo la utapiamlo. Serikali imeweka kipaumbele na kuongeza rasilimali fedha za kutekeleza afua za lishe kutoka **Shilingi bilioni 11.0** zilizoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2017/18 hadi **Shilingi bilioni 15** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 sawa na ongezeko la **asilimia 3.6**. Vilevile, katika kipindi hicho Wadau wa Maendeleo walitoa kiasi cha **Shilingi bilioni 4.96** zilizotumika kutekeleza afua za lishe katika baadhi ya Mikoa na Halmashauri nchini. Ongezeko la rasilimali fedha limesaidia kuongeza kiwango cha utoaji wa huduma ya matone ya vitaminini A kutoka **asilimia 93** Mwaka 2017 hadi **97** Mwaka 2018 na utoaji wa dawa za minyoo umeongezeka kutoka **asilimia 92** Mwaka 2017 hadi **asilimia 96** Mwaka 2018. Vilevile, **asilimia 79** ya watoto wenye umri chini ya miaka mitano

walipimwa hali zao za lishe, **asilimia 75** ya akina mama wajawazito wamepatiwa vidonge vya kuongeza wekundi wa damu kwa lengo la kupunguza vifo vya akina mama wakati wa kujifungua vinavyosababishwa na upungufu wa damu.

45. *Mheshimiwa Spika;* Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesaini mkataba wa utendaji kazi na Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Wakurugenzi wa Halmashauri ili kuimarisha usimamizi na uwajibikaji katika utekelezaji wa afua za lishe nchini. Mikataba hiyo inafanyiwa tathmini kila baada ya miezi sita ili kupima kufikiwa kwa malengo ya utokomezaji wa utapiamlo. Vilevile, Serikali imeimarisha eneo la rasilimali watu hasa wataalam wa lishe ambapo jumla ya wataalam wa lishe **113** wameajiriwa ili kuboresha mkakati wa utekelezaji wa afua za lishe kama utoaji wa matone ya Vitamin A, utoaji wa madini ya chuma, vyakula tiba, na elimu ya lishe kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Huduma za Ustawi wa Jamii

46. *Mheshimiwa Spika;* utekelezaji wa shughuli za ustawi wa jamii kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Mtoto Na.21 ya Mwaka 2009, Sheria ya Ndoa Na. 5 ya Mwaka 1971, Sheria ya Watu Wenye Ulemavu Na.9 ya Mwaka 2010, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Biashara Haramu ya Binadamu 2008, Sheria ya makosa ya kujamiana Na. 4 ya mwaka 1998, Sera ya Taifa ya Wazee ya Mwaka 2003, Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu ya 2004, na Mwongozo uliotolewa na Ofisi ya Rais-TAMISEMI Mwaka 2017 kuhusu ustawi wa jamii.

47. *Mheshimiwa Spika;* maeneo ya utekelezaji wa huduma za Ustawi wa Jamii ni pamoja na familia na watoto; malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto; marekebisho ya Tabia na Haki za Mtoto kisheria; huduma kwa Wazee na Watu Wenye Ulemavu na Uimarishaji wa Mifumo ya kielektroniki ya ustawi wa jamii. Serikali imeweka kipaumbele na kuongeza rasilimali fedha za kutekeleza utoaji

huduma za Ustawi wa Jamii katika maeneo tajwa kutoka **Shilingi bilioni 9** zilizoidhinishwa Mwaka wa Fedha 2017/18 hadi **Shilingi bilioni 11.4** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 sawa na ongezeko la **asilimia 6.6**.

Ulinzi na Usalama wa Mtoto

48. *Mhesimiwa Spika*; katika hatua ya kuendelea kuimarisha Ulinzi na Usalama wa Mtoto kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mtoto na Mwanamke zimeundwa katika Mikoa **26**, Halmashauri **184**, Kata **2,490** kati ya **4,420**, Vijiji **7,900** kati ya **16,626** ili kutekeleza kampeni za kutokomeza mimba na ndoa za utotoni. Aidha, Wataalam wa Ustawi wa Jamii 505 kati ya 738 wamepatiwa mafunzo kuhusu namna ya kutoa huduma ya Ulinzi na Usalama wa Mtoto katika maeneo yao

49. *Mheshimiwa Spika*; juhudi za kutokomeza ukatili dhidi ya Watoto na Wanawake umeamsha mwitikio chanya kwa wananchi hivyo kuongeza kesi za utakili wa Watoto na Wanawake zinazotolewa taarifa katika Ofisi za Ustawi wa Jamii, Dawati la Polisi la Jinsia na Ofisi za Watendaji wa Mitaa/ Vijiji. Aidha, mashauri ya ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto yaliyoripotiwa kuhusu akina mama ni **4,187** na watoto ni **6,782** ambayo yamefanyiwa kazi. Kati ya mashauri hayo, jumla ya kesi **1,973** zilifkishwa mahakamani na kesi **711** zilitolewa hukumu.

Huduma kwa Watoto Walio Katika Mazingira Hatarishi

50. *Mheshimiwa Spika*; hadi kufikia Februari, 2019, tumefanikiwa kuongeza idadi ya utambuzi wa watoto walio katika mazingara hatarishi, ambapo watoto **389,012** wametambuliwa ukilinganisha na watoto **201,382** walotambuliwa katika kipindi cha Machi, 2018 hivyo kufikisha idadi ya Watoto **1,495,049** wanaoishi katika mazingira hatarishi walitambuliwa, wanawake wakiwa ni **724,105** na wanaume **770,944** na kupatiwa huduma mbalimbali ikiwemo kuunganishwa na familia zao, vifaa vyta shule na ada ya

kujiunga vyuo vya Mafunzo ya Ufundi ikiwemo chuo cha VETA.

Huduma kwa Watu Wenyewe Ulemavu

51. ***Mheshimiwa Spika;*** Watu Wenyewe Ulemavu waliotambuliwa ni **405,426** ambapo wanawake **191,116** wanaume **214,220** katika Halmashauri **184**. Kamati za Watu Wenyewe Ulemavu zimeundwa katika Vijiji **11,954** kati ya Vijiji **12,545** sawa na **asilimia 95** na Mitaa **4,011** kati ya Mitaa **4,420** sawa na **asilimia 90.7**. Jumla ya Watu Wenyewe Ulemavu **217,932** kati ya **405,426** ya waliotambuliwa walipatiwa huduma za Afya kwa gherama ya **Shilingi milioni 102.1** na kati ya hao **3,226** walipatiwa kadi za Bima ya Afya ya Jamii (CHF).

Huduma za Wazee

52. ***Mheshimiwa Spika;*** hadi Februari, 2019 jumla ya Wazee **750,622** wametambuliwa ikilinganishwa na Wazee **300,000** waliotambuliwa hadi Februari, 2018. Kati ya hao, wazee **247,705** wamepatiwa vitambulisho vya matibabu bure, sawa na asilimia **33** ya wazee wote waliotambuliwa. Aidha, kati ya hao, wazee **502,917** wamepatiwa kadi za matibabu za Afya ya Jamii (CHF) sawa na asilimia **67**.

Mpango wa Uimarishaji wa Mifumo ya Taarifa ya Ustawi wa Jamii

53. ***Mheshimiwa Spika;*** hadi Machi, 2019 tumefanikiwa kusambaza na kuanza kutumia mfumo wa kielektroniki wa ukusanyaji na utunzaji wa taarifa za watoto walio katika mazingira hatarishi na wale wanaoishi na kufanya kazi mtaani katika Halmashauri **147** kati ya **184**. Mfumo umesaidia kuwa na takwimu sahihi za matukio ya ukatili dhidi ya watoto na kuongeza uwazi katika usimamizi wa shughuli za watoto. Kupitia Mradi wa USAID Kizazi Kipyaa zimenunuliwa na kusambazwa Kompyuta, *Printer*, na Modem **101** zenye thamani ya **Shilingi milioni 257.6** kwa Mikoa **23** na Halmashauri **78** Awamu ya Kwanza kwa ajili ya matumizi ya Mfumo wa Kielektroniki wa Taarifa za Ustawi wa Jamii.

Mfuko wa Pamoja wa Afya

54. ***Mheshimiwa Spika;*** Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeboresha utaratibu wa usimamizi wa fedha za Mfuko wa Pamoja wa Afya kwa kuzipeleka moja kwa moja kwenye vituo vya kutolea huduma za afya ambapo wananchi wanashirikishwa kupitia kamati za usimamizi wa vituo vya kutolea huduma za afya. Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo imeanzisha mfumo wa kielektroniki unaojulikana kama FFARS ambao unatumika kusimamia fedha hizo na kurahisisha upatikanaji wa taarifa za matumizi ya fedha hizo. Katika Mwaka wa Fedha 2017/18, jumla ya vituo 5,136 vya kutolea huduma vilipokea kiasi cha **Shilingi bilioni 69.0** zilizotumwa moja kwa moja kupitia kwenye mfumo huo. Vilevile, katika Mwaka wa Fedha 2018/19, jumla ya **Shilingi bilioni 19** kati ya bajeti ya **Shilingi bilioni 104.7** zimepelekwa kwenye vituo **5,437**. Ili kuimarisha usimamizi wa fedha hizo, Serikali imearajiri Wahasibu Wasaidizi **535** ambao wanasimamia matumizi ya mfumo katika ngazi ya vituo na kutoa taarifa kila Robo Mwaka.

Mpango wa Malipo Kulingana na Ufanisi (*Result Based Financing*)

55. ***Mheshimiwa Spika;*** Mpango wa Malipo Kulingana na Ufanisi (Result Based Financing-RBF) uliana kutekelezwa Mwaka 2015 katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu Mkoani Shinyanga kwa majaribio na baadaye Mwaka 2016, Programu hiyo ilianza kutekelezwa katika Halmashauri zote za Mkoa wa Shinyanga. Kwa sasa Mpango wa Malipo Kulingana na Ufanisi unatekelezwa katika Mikoa nane (8) ya Shinyanga, Mwanza, Pwani, Simiyu, Tabora, Kagera, Geita na Kigoma yenye jumla ya Halmashauri **59** na vituo **1,655** vya kutolea huduma za afya. Mikoa hiyo ilichaguliwa kutokana na uwepo wa vifo vya Mama Wajawazito vilivuosababishwa na kukosekana na huduma za msingi pamoja na idadi ndogo ya wataalam wa afya kwenye maeneo hayo. Mpango huo unahuisha ukarabati wa vituo vya kutolea huduma za afya na kujenga uwezo wa Timu za Usimamizi wa huduma za afya ngazi ya Mkoa na Wilaya. Katika kipindi cha kuanzia Julai,

2018 hadi Februari, 2019 jumla ya **Shilingi bilioni 26.10** zimetumika kutekeleza mpango huo katika shughuli za usimamizi ngazi ya Mkoa na uboreshaji wa miundombinu ya kutolea huduma za afya kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa.

56. *Mheshimiwa Spika*; utekelezaji wa mpango huo umesaidia kuboresha huduma za afya ambapo Mikoa hiyo sasa inafanya vizuri katika viwango vya utoaji wa huduma za afya kutoka mwaka 2015 hadi 2018. Mafanikio mengine yaliyopatikana ni pamoja na kuimarika kwa ushirikishwaji wa wananchi kupitia kuongezeka kuundwa kwa Bodi za Afya za Halmashauri kutoka **asilimia 50** hadi **asilimia 86.2**. Aidha, upatikanaji wa dawa umeongezeka kutoka **asilimia 41.06** hadi **asilimia 86.2**. Vituo vya afya vyenye nyota **0** vimepungua kutoka **asilimia 42.5** hadi **asilimia 3.1** na vituo vyenye nyota zaidi ya **3** vimeongezeka kutoka **asilimia 0.8** hadi **asilimia 23.2**. Aidha, kiwango cha ubora wa takwimu kimeongezeka kutoka asilimia 70 hadi asilimia 89.5 kwenye Mikoa nane (8) ya utekelezaji wa mpango.

Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF)

57. *Mheshimiwa Spika*; Ofisi ya Rais- TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia Wazee na Watoto, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya pamoja na Wadau wa Maendeleo imefanya maboresho ya mfuko huo ili wananchi waweze kupata huduma za matibabu ya rufaa hadi kwenye hospitali za rufaa za Mikoa. Utengenezaji wa kanzidata kwa ajili ya utunzaji wa kumbukumbu za wanachama nchi nzima umekamilika. Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa umeanza rasmi kutumika Aprili, 2018. Hadi Machi, 2019, Mikoa ilioanza kusajili wanachama wa Mfuko wa Afya ya Jamii ulioboreshwa imefikia **13** na zoezi hilo linaendelea.

Mfuko wa Dunia wa UKIMWI, Kifua Kikuu na Malaria

58. *Mheshimiwa Spika*; Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea na utekelezaji wa shughuli za UKIMWI, Malaria na Kifua Kikuu

katika kipindi cha Mwaka 2018-2020 baada ya kufikia ukomo katika kipindi cha Mwaka 2015-2017. Kazi kubwa zinazofanyika zinahusisha shughuli za uratibu, usimamizi shirikishi, mikutano na mafunzo kuititia timu za uendeshaji huduma za afya kwenye Mikoa na Halmashauri (RHMTs na CHMTs), ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za UKIMWI na kuimarisha mifumo ya kutolea taarifa za fedha katika vituo vya kutolea huduma za afya. Katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi bilioni 2.88** kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za UKIMWI na Kifua Kikuu. Kati ya Fedha hizo **Shilingi bilioni 2.76** sawa na **asilimia 96** zilikuwa zimepokelewa hadi Februari, 2019 kwa ajili ya utekelezaji wa programu kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Usimamizi na Uendeshaji wa Elimu ya Msingi na Sekondari

59. *Mheshimiwa Spika*; Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuboresha, kuimarisha na kuinua kiwango cha Elimu ya Awali, Msingi na Sekondari kwa lengo la kuhakikisha elimu katika ngazi zote inakuwa na ubora unaostahili. Lengo ni kuwa na jamii iliyoelimika yenyе maarifa, uzalendo na ujuzi wa kutosha kumudu ustawi wa maisha yao, na kuhimili ushindani wa ndani na kimataifa.

Elimu ya Awali na Msingi

60. *Mheshimiwa Spika*; uandikishaji wa wanafunzi wapya katika mfumo rasmi wa elimu nchini unaonesha kuwa hadi Machi, 2019 wanafunzi wa elimu ya awali walioandikishwa ni **1,278,816** sawa na asilimia **92.48** ya lengo la kuandikisha wanafunzi **1,382,761**. Aidha, kati ya hao walioandikishwa, wanafunzi **1,372** ni wenyе mahitaji maalum. Uandikishaji huo umepungua kwa **asilimia 0.4** ikilinganishwa na wanafunzi **1,283,790** walioandikishwa mwaka **2018**. Vilevile, wanafunzi wapya walioandikishwa kuanza Darasa la Kwanza ni **1,670,919** hadi kufikia Machi, 2019 ikilinganishwa na wanafunzi **1,751,221** walioandikishwa hadi Mwaka **2018** sawa na upungufu wa asilimia **4.5**. Kati ya hao, wanafunzi wenyе mahitaji maalum walioandikishwa ni **3,028**. Upungufu wa

uandikishaji unatokana na mafanikio ya Mpango wa Elimusingi Bila Malipo ambao katika kipindi cha miaka mitatu kuanzia 2016 hadi 2018 umewezesha wanafunzi wenyewe umri wa kwenda shule kuandikishwa kila mwaka kutokana na kuondolewa kwa vikwazo vya ada na michango mbalimbali.

61. *Mheshimiwa Spika*; Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kushirikiana na Wananchi na Wadau wa Maendeleo katika kuboresha miundombinu ya shule za awali na msingi. Hadi Februari, 2019 ujenzi wa vyumba vya madarasa **2,840** kwa shule za msingi umefanyika na kuongeza idadi ya vyumba vya madarasa kutoka **119,647** viliviyokuwepo Machi 2018 hadi madarasa **122,487** kufikia Februari, 2019 sawa na ongezeko la **asilimia 2.3**. Aidha, vyumba vya madarasa **2,637** viko katika hatua mbalimbali za ukamilishaji. Vilevile, jumla ya matundu ya vyoo **7,067** (vyoo vya wanafunzi matundu **6,445** na vyoo vya Walimu matundu **622**) yamejengwa katika shule za msingi na kuongeza matundu ya vyoo kutoka **190,674** yaliyokuwepo Machi, 2018 hadi kufikia matundu ya vyoo **197,741** mwezi Februari, 2019 hili ni ongezeko la **asilimia 3.5**. Aidha, matundu ya vyoo **3,004** yanaendelea kujengwa na yanatarajiwa kukamilika kabla ya Juni, 2019.

62. *Mheshimiwa Spika*; kazi nyingine za uboreshaji miundombinu ya elimu zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa nyumba za walimu **720** na kuongeza idadi ya nyumba hizo kutoka **44,320** mwaka **2018** hadi nyumba **45,040** Februari, 2019. Aidha, madawati ya wanafunzi watatu watatu yameongezeka kutoka madawati **2,858,982** yaliyokuwepo Machi, 2018 hadi madawati **2,994,266** Februari, 2019 sawa na ongezeko la madawati **135,284**. Aidha, kupitia Programu ya *Equip-T*, Serikali imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 18.5** kwa ajili ya ujenzi wa vituo shikizi **251** ambapo jumla ya vyumba vya madarasa **502**, ofisi za walimu **251**, matundu ya vyoo **1,255**, maktaba **34**, matanki ya maji **1,255** pamoja na ukamilishaji wa maboma **263** ya vyumba vya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yametekelizwa katika Mikoa **9** yenye Halmashauri **63**.

Ajira za Walimu wa Shule za Msingi

63. *Mheshimiwa Spika;* Serikali imeajiri walimu **4,811** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 ambao walipangwa kufundisha katika shule za msingi nchini. Walimu hao wamepangwa katika Halmashauri zenyе upungufu mkubwa isipokuwa shule zilizoko katika Halmashauri za Majiji, Manispaa na Miji ambazo zina walimu wengi ikilinganishwa na maeneo ya vijijini. Ajira hizo zimeongeza idadi ya walimu wa shule za msingi waliopo kutoka **164,618** waliokuwepo Februari, 2018 hadi **179,429** waliopo Februari, 2019. Aidha, Serikali imetoa kibali cha ajira ya walimu **3,175** wa shule za msingi ambapo mchakato wa ajira unaendelea na mara baada ya zoezi hilo kukamilika watapangwa katika maeneo yenye upungufu mkubwa wa walimu na hasa yale ya vijijini. Ajira hizo zitatoa kipaumbele kwa walimu wenye mahitaji maalum na kwa walimu waliosomea Elimu Maalum.

64. *Mheshimiwa Spika;* katika kuongeza ari ya utendaji kazi, Serikali inatoa posho ya madaraka kwa Walimu Wakuu wa Shule za Msingi **16,159** na Maafisa Elimu Kata **3,895** kila mwezi. Aidha, Maafisa Elimu Kata wamepewa pikipiki **2,894** ili kuimarisha uratibu, usimamizi na ufuatiliaji wa elimu kwenye maeneo yao.

Upimaji na Mtihani wa Taifa

65. *Mheshimiwa Spika;* katika mwaka 2017, watahiniwa **1,192,655** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Upimaji wa Darasa la Nne. Wanafunzi **1,158,499** walifanya Mtihani huo ambapo kati ya hao, wanafunzi **1,086,156** walifaulu sawa na **asilimia 93.57** ikilinganishwa na wanafunzi **1,362,642** waliosajiliwa kufanya Mtihani Mwaka 2018 ambapo kati yao wanafunzi **1,302,461** sawa na **asilimia 93.14** walifaulu mtihani huo. Aidha, jumla ya wanafunzi **957,904** walisajiliwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Kuhitimu Darasa la Saba mwaka 2018 na wanafunzi **733,103** sawa na **asilimia 77.72** kati ya wanafunzi **944,218** waliofanya Mtihani huo walifaulu ikilinganishwa na wanafunzi **662,035** waliofaulu Mtihani huo kwa mwaka 2017 sawa na **asilimia 72.76**. Ufaulu wa mtihani umeongezeka kwa

asilimia 4.96 kutoka **asilimia 72.76** Mwaka 2017 hadi **asilimia 77.72** mwaka **2018**. Kuimarika kwa ufaulu huo kumetokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, usimamizi mzuri wa viongozi wa elimu, ushiriki wa wazazi, wadau na mwamko wa walimu kufanya kazi kwa misingi ya weledi ikiwa ni pamoja na kukamilisha muhtasari ndani ya muda uliopangwa.

Elimu ya Sekondari

66. *Mheshimiwa Spika*; katika mwaka 2019 jumla ya wanafunzi **710,436** walichaguliwa kuijunga Kidato cha Kwanza ikilinganishwa na wanafunzi **595,427** waliojunga Kidato cha Kwanza mwaka 2018 sawa na ongezeko la wanafunzi **115,009** ambaoni **asilimia 116.2**. Hadi Februari, 2019 wanafunzi **575,187** sawa na **asilimia 80.96** walikuwa wameripoti katika shule walizopangiwa.

67. *Mheshimiwa Spika*; Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuboresha miundombinu ya shule ili kuhakikisha wanafunzi wote waliochaguliwa wanapata fursa ya kuendelea na masomo ya sekondari. Hadi Februari, 2019 Serikali kuititia mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R) imetoa jumla ya **Shilingi bilioni 52.22** kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa **938**, matundu ya vyoo **2,141**, mabweni **210**, nyumba za walimu **47**, majengo ya utawala **13**, maabara za sayansi **22**, maktaba **39**, mabwalo ya chakula **76**, ukarabati na umaliziaji wa vyumba vya madarasa **219** na ujenzi wa visima **10** vya maji.

68. *Mheshimiwa Spika*; Aidha, jumla ya vyumba **1,607** vya madarasa vimejengwa na kuongeza idadi kutoka vyumba vya madarasa **40,720** Machi, 2018 hadi **42,327** Februari, 2019 na ukamilishaji wa madarasa **1,223** unaendelea. Vilevile, jumla ya matundu ya vyoo **1,978** yamejengwa na kuongeza idadi ya matundu ya vyoo kufikia **56,466** ikilinganishwa na matundu **54,488** yaliyokuwepo Machi, 2018.

69. *Mheshimiwa Spika*; kazi nyingine za uboreshaji miundombinu ya elimu zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa

nyumba za walimu **159**, maabara za sayansi **123**, ununuzi wa viti **605** na meza **727** kwa ajili ya wanafunzi. Aidha, Serikali imetoea jumla ya **Shilingi bilioni 29.9** kwa ajili ya ukamilishaji wa maboma **2,392** ya madarasa yatakayowezesha kuongeza idadi ya wanafunzi **133,747** wa Kidato cha Kwanza waliokosa nafasi.

Ajira za Walimu wa Shule za Sekondari

70. Mheshimiwa Spika; Serikali imeajiri walimu **2,189** katika Mwaka wa Fedha 2018/19 ambao walipangwa kufundisha katika shule za sekondari nchini. Kati ya walimu hao, walimu wenye mahitaji maalum ni **29**, walimu wa hisabati na sayansi **1,900**, walimu wa lugha (Literature in English) **100**, na mafundi sanifu wa maabara **160**. Walimu hao wamepangwa katika Halmashauri zenyе upungufu mkubwa wa walimu. Ajira hizo zimeongeza idadi ya walimu wa shule za sekondari kutoka **82,023** waliokuwepo Februari, 2018 hadi **84,212** waliopo Februari, 2019. Aidha, Serikali imetoea kibali cha ajira ya walimu **1,374** wa shule za sekondari ambapo mchakato wa ajira unaendelea na mara baada ya zoezi hilo kukamilika watapangwa katika maeneo yenye upungufu mkubwa na kipaumbele kitatolewa kwa walimu wenye mahitaji maalum na waliosomea Elimu Maalum.

Upimaji na Mitihani ya Taifa

71. Mheshimiwa Spika; idadi ya wanafunzi waliofaulu mtihani wa Taifa wa Upimaji wa Kidato cha Pili imeendelea kuongezeka mwaka hadi mwaka. Katika mwaka 2017, jumla ya wanafunzi **486,423** walifanya mtihani ambapo kati yao wanafunzi **433,453** sawa na asilimia **89.05** walifaulu ikilinganishwa na ufaulu wa **asilimia 89.68** wa wanafunzi walifanya mtihani huo mwaka 2018 ambapo jumla ya wanafunzi **506,235** walifanya mtihani huo na waliofaulu walikuwa wanafunzi **452,273**.

72. Mheshimiwa Spika; idadi ya wanafunzi waliosajiliwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka 2017 walikuwa **385,767** ambapo walifanya mtihani huo walikuwa

wanafunzi **317,777** na wanafunzi **245,274** walifaulu sawa na **asilimia 77.18**. Aidha, mwaka 2018 walisajiliwa wanafunzi **368,037** ambapo, waliofanya mtihani huo walikuwa wanafunzi **360,510**, wanafunzi waliofaulu walikuwa **284,126** sawa na **asilimia 78.81**. Vilevile, ufaulu wa wanafunzi waliofanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Sita umeendelea kuimarika. Kati ya wanafunzi **62,725** waliofanya mtihani mwaka 2017, wanafunzi **61,533** walifaulu sawa na **asilimia 98.1** ikilinganishwa na wanafunzi **83,581** waliofaulu mtihani huo mwaka 2018 kati ya wanafunzi **86,105** waliofanya mtihani sawa na ufaulu wa **asilimia 97.07**. Kuimarika kwa ufaulu huo kumetokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya kufundishia na kujifunzia, kuimarika kwa usimamizi wa elimu, ushiriki wa wazazi na wadau mbalimbali na mwamko wa walimu kufanya kazi kwa misingi ya weledi ikiwa ni pamoja na kukamilisha muhtasari ndani ya muda uliopangwa.

Utoaji wa Elimumsingi Bila Ada

73. *Mheshimiwa Spika*; Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada ulioanza Desemba, 2015. Katika mwaka wa fedha 2018/19 hadi kufikia Februari, 2019, Serikali ilikuwa imetoa fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 166.44** kutekeleza Mpango wa Elimumsingi Bila Ada. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi bilioni 77.20** zilipelekwa katika Shule za Msingi na **Shilingi bilioni 89.23** zimetumika kutekeleza mpango katika Shule za Sekondari. Maeneo yanayohusika na fedha za Elimumsingi Bila Ada ni ruzuki ya uendeshaji kwa kila mwanafunzi, fedha za chakula kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum wa shule za msingi na wanafunzi wa bweni wa shule za sekondari kidato cha 1 hadi 6, fidia ya ada kwa wanafunzi wa kutwa na bweni kidato cha 1 hadi 4, na posho ya madaraka kwa Wakuu wa Shule za Msingi na Sekondari na Maafisa Elimu Kata. Mpango wa Elimumsingi Bila Ada umewezesha wanafunzi wapya wanaoingia kwenye elimu ya mfumo rasmi kuongezeka mwaka hadi mwaka.

Elimu ya Watu Wazima na Nje ya Mfumo Rasmi

74. *Mheshimiwa Spika*; Serikali inaendelea na utekelezaji na usimamizi wa Elimu ya Watu Wazima kwa njia ya vikundi vyta uzalishaji mali. Katika mwaka 2018 jumla ya vikundi **208**

vilifikiwa kwa ajili ya masomo ya ujasiriamali, na ujifunzaji wa Kusoma, Kuandika na Kuhesabu. Idadi ya wanakisomo **63** walipatiwa vyeti nya kuhitimu mafunzo yao. Wanakisomo **13,008** wanatarajija kufuzu mafunzo hayo mwezi Agosti, 2019.

75. *Mheshimiwa Spika*; idadi ya wanafunzi **14,033** wa MEMKWA kundirika la kwanza wanapatiwa masomo sawa na wanafunzi walio katika mfumo rasmi. Kati ya hao waliosajiliwa kufanya mtihani wa darasa la nne mwaka 2018 ni **6,019**, waliofanya mtihani ni **5,900** na waliofaulu kuingia darasa la tano ni **3,217**. Hadi Machi, 2019 jumla ya wanakisomo walioandikishwa ni **17,024**. Aidha, Programu ya Elimu Changamani kwa vijanabalehe wenye umri wa miaka 14 – 19 kundirika la pili, imeanzishwa kwa majaribio katika Mikoa **8** ambayo ni Kigoma, Tabora, Iringa, Njombe, Mbeya na Songwe, Dodoma na Dar es Salaam inatarajia kuanza Julai, 2019. Programu hii inatarajija kuwanufaisha walengwa **10,000**.

76. *Mheshimiwa Spika*; walengwa wa programu hiyo ni Vijana ambao hawakuwahi kwenda shule, Wanafunzi walioacha shule ya Msingi, waliomaliza darasa la saba na kukosa fursa ya kuendelea na masomo, waliomaliza kupitia programu ya MEMKWA, wasichana walioacha shule kwa changamoto mbalimbali kama vile ujauzito na ndoa za utotoni.

Elimu Maalum

77. *Mheshimiwa Spika*; hadi Februari, 2019 wanafunzi **49,655** wenye mahitaji maalum wameandikishwa ikilinganishwa na wanafunzi **42,786** walioandikishwa Februari, 2018 wakiwemo, wanafunzi **viziwi, wasioona, wenye uoni hafifu, wenye usonji, wenye ulemavu wa viungo, na wenye ulemavu wa akili**. Aidha, mwaka 2019 jumla ya wanafunzi **1,407** sawa na asilimia **71.9** ya wanafunzi **1,956** wenye mahitaji maalum walihitimu elimu ya msingi na kuchaguliwa kujunga Kidato cha Kwanza.

Elimu kwa Michezo

78. *Mheshimiwa Spika*; OR-TAMISEMI imeendelea kuratibu na kusimamia michezo katika Shule za Msingi na Sekondari

kuanzia ngazi ya shule hadi Taifa. Katika mwaka 2018 OR-TAMISEMI iliendeleza jitihada za kuimarisha uendeshaji wa mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA. Katika kipindi hicho jumla ya wanafunzi **2,120** wa Shule za Msingi, wanafunzi **2,360** wa Shule za Sekondari na zaidi ya walimu na viongozi **1,500** walishiriki mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA iliyofanyika Mkoani Mwanza.

79. *Mheshimiwa Spika*; kuimarika kwa mashindano hayo kumeendelea kuonesha mafanikio makubwa kwa Timu ya Taifa ya Soka kwa vijana wenyewe umri chini ya miaka **17** (Serengeti Boys) ambayo mwaka 2017 ilifanikiwa kushiriki fainali za Afrika zilizofanyika nchini Gabon. Aidha, Timu hiyo itakuwa mwenyeji kwenye fainali za **Kombe la Mataifa ya Afrika (AFCON)** kwa vijana yatakayofanyika nchini Tanzania mwaka 2019. Timu hiyo ya Vijana wa Serengeti inaundwa na wachezaji waliotokana na mashindano ya michezo ya UMITASHUMTA na UMISSETA kwa zaidi ya asilimia **85**. Vijana hao wamekuwa wakichaguliwa wakati wa michezo hiyo inayofanyika kila mwaka tangu Mwaka 2014. Michezo hiyo imekuwa ni chachu ya kupata wachezaji bora ambao wanajunga kwenye vilabu vya michezo na hatimaye kwenye Timu ya Taifa.

80. *Mheshimiwa Spika*; Tanzania inatarajiwa kuwa mwenyeji wa mashindano ya michezo ya shule za sekondari na shule za msingi (FEASSSA) kwa nchi za Afrika ya Mashariki yaliyopangwa kufanyika Mkoani Arusha Agosti, 2019. Zaidi ya washiriki **5,000** kutoka katika nchi wanachama wa Jumuia ya Afrika Mashariki wanatarajiwa kuwepo Arusha kushiriki michezo hiyo. Michezo itakayoshindaniwa ni pamoja na soka, netiboli, mpira wa kikapu, mpira wa mikono, mpira wa kengele, riadha, *Rugby* na kuogelea.

81. *Mheshimiwa Spika*; Ofisi ya Rais-TAMISEMI itaendelea na kuimarisha michezo kwa kuandaa mkakati wa Taifa na maendeleo ya elimu ya michezo katika shule. Aidha, Mwaka 2019, Ofisi ya Raís-TAMISEMI imepanga kuendesha mashindano ya UMMISETA na UMITASHUMTA yatakayofanyika Mkoani Mtwara ili kutoa fursa kwa vijana kuonesha vipaji vyao

katika fani mbalimbali za michezo na soka. Michezo itakayoshindaniwa ni pamoja na soka, netiboli, mpira wa kikapu, mpira wa mikono, mpira wa wavu, riadha, mpira wa kengele, kwaya na ngoma. Jumla ya wanafunzi **2,000** wa shule za msingi na **2,200** wa shule za sekondari wakiwemo wenye mahitaji maalum, wanatarajiwu kushiriki mashindano hayo Mkoani Mtwara.

Mkataba wa Utendaji Kazi kwa Walimu

82. *Mheshimiwa Spika*; katika uimarishaji na uendeshaji wa elimu OR - TAMISEMII imeandaa utaratibu wa mkataba wa utendaji kazi kwa walimu (Performance Contract) ambapo kupitia mkataba huo walimu watapimwa kwa kuangalia idadi ya vipindi walivyofundisha kulingana na ratiba ya masomo shulenii, ukamilishaji wa mihtasari, ufaulu kwenye masomo, uandaaji wa masomo na maazimio ya kazi. Lengo la mikataba hii ni kuongeza uwajibikaji na nidhamu ya kazi kwa Walimu.

Uendelezaji wa Sekta ya Kilimo

83. *Mheshimiwa Spika*; Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili ulianza kutekelezwa Julai, 2018 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2018/19 hadi mwaka wa fedha 2022/23. Utekelezaji wa mpango huo unafanyika kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa 185 kupitia Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (*District Agricultural Development Projects*).

84. *Mheshimiwa Spika*; Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019 OR – TAMISEMII kwa kushirikiana na Wizara zinazoratibu Sekta ya Kilimo imeandaa Mwongozo wa kuandaa Mipango ya Maendeleo ya Kilimo ya Wilaya (DADPs) ikiwa ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo ya Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Mwongozo huo umesambazwa katika Mikoa 26 na Halmashauri 185. Aidha, OR TAMISEMII kwa kushirikiana na Shirika la Mapinduzi ya Kijani Afrika (Alliance for Green Revolution in Africa- AGRA) imeandaa Mkakati uliowezesha

kupata fedha kiasi cha **Shilingi bilioni 3.34** kwa ajili ya kuwajengea uwezo Maafisa Ugani katika mafunzo na vitendea kazi, Waratibu ngaziza Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Viwanda, Biashara na Uwekezaji

85. Mheshimiwa Spika: ujenzi wa viwanda unafanyika kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuifikiha Tanzania katika uchumi wa kati uliofungamanishwa na maendeleo ya watu ifikapo Mwaka 2025. Mamlaka za Serikali za Mitaa zina jukumu la kuboresha mazingira ya uwekezaji ili kujenga misingi itakayorahisisha na kuvutia ukuaji wa sekta ya viwanda. Katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais-TAMISEMI ilipanga kutenga ekari **228,543** kwa ajili ya viwanda vidogo, vyat kati na vikubwa kwenye Mikoa 26. Hadi kufikia Desemba 2018, jumla ya hekta **777,110.48** zillikuwa zimeainishwa zikiwemo hekta **367,077.21** kwa ajili ya ujenzi wa viwanda vikubwa, viwanda vyat kati na viwanda vidogo; hekta **204,488.28** kwa ajili ya shughuli za kilimo na skimu za umwagiliaji, hekta **143,000** kwa ajili ya malisho ya mifugo na hekta **62,545** kwa ajili ya uwekezaji mwingine. Serikali imeunda timu ya wataalam kwa ajili ya kuhakiki maeneo hayo kama yanafaa kwa ajili ya uwekezaji na hayana migogoro.

86. Mheshimiwa Spika: OR-TAMISEMI ilizindua Kampeni ya ujenzi wa viwanda katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kote nchini ikiwa na kaulimbiu ya *Mkoa Wetu, Viwanda Vyetu*. Lengo kuu la kaulimbiu hiyo ilikuwa ni kutoa hamasa kwa Viongozi na wananchi kushiriki kikamilifu kuwezesha uwepo wa viwanda katika maeneo yao ili kukuza uchumi na ustawi wa maisha ya wananchi. Kaulimbiu ya Mkoa Wetu, Viwanda Vyetu imeleta msukumo mpya wa ujenzi wa viwanda na kuongeza idadi ya viwanda vikubwa, vyat kati na vidogo kufikia **4,877** sawa na **asilimia 187.6** ya lengo la kujenga viwanda **2,600** kuanzia Novemba, 2017 hadi Februari, 2019. Viwanda vikubwa vilivyojengwa kwa kipindi hicho ni **108**, viwanda vyat kati **236**, viwanda vidogo **2,522** na viwanda vidogo sana **2,011**.

87. **Mheshimiwa Spika;** Mkoa wa Dar es Salaam ndio ulioongoza kwa kujenga viwanda vikubwa **46** ukifuatiwa na Mkoa wa Pwani wenyewe viwanda **8**. Vilevile, Mkoa wa Dar es Salaam umeongoza kwa kujenga viwanda vidogo **245** ukifuatiwa na Mkoa wa Pwani wenyewe viwanda **219**. Mkoa wa Geita umeongoza kwa kujenga viwanda nya katika **57** ukifuatiwa na Mkoa wa Mbeya uliofanikiwa kujenga viwanda **40**. Viwanda nya katika vilivyojengwa katika Mikoa ya Mbeya na Geita ni vile vinavyojishughulisha na uchenjuaji wa madini ya dhahabu ambayo hupatikana kwa wingi katika Mikoa hiyo. Vilevile, Mkoa wa Lindi umefanya vizuri katika ujenzi wa viwanda vidogo kwa kuanzisha viwanda **452** vinavyojihusisha na ubanguaji wa korosho ukifuatiwa na Mkoa wa Mara wenyewe viwanda **377**. Kwa ujumla kumekuwa na mwitikio mkubwa wa uanzishaji wa viwanda katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ambavyo vimeajiri watu **35,796**.

Miradi ya Kimkakati Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa

88. **Mheshimiwa Spika;** utaratibu wa utekelezaji wa Miradi ya kimkakati uliana katika Mwaka wa Fedha 2017/18. Kupitia utaratibu huo, Halmashauri zinaandaa maandiko ya miradi ambayo inapatiwa fedha za utekelezaji baada ya kukidhi vigezo. Miradi hiyo inapaswa kuwa na sifa ya kuiwezesha Halmashauri kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri ili kuziwezesha kujitegemea kimapato na kupunguza utegemezi wa Ruzuku ya Serikali Kuu. Hadi Februari, 2019 jumla ya Halmashauri **29** zenyе miradi **37** zimekidhi vigezo nya kupatiwa jumla ya **Shilingi bilioni 268.84** kwa ajili ya kutekeleza miradi ya kimkakati.

89. **Mheshimiwa Spika;** katika Awamu ya Kwanza, Halmashauri 18 zenyе miradi **23** zilikidhi vigezo nya kupatiwa jumla ya **Shilingi bilioni 131.46**. Kati ya Fedha hizo, **Shilingi bilioni 31.36** zimepokelewa kwenye Halmashauri hizo ambazo zimesaini mikataba ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati. Fedha hizo zitatumika kutekeleza miradi ya ujenzi wa masoko, viwanda, machinjio, vituo nya mabasi na maghala ya kuhifadhi mazao.

90. **Mheshimiwa Spika**; katika Awamu ya Pili, Halmashauri nyingine 12 zenyé miradi 15 zimekidhi vigezo vya kupatiwa jumla ya **Shilingi bilioni 137.37** mwezi Januari, 2019. Halmashauri zimesaini mikataba ya utekelezaji wa miradi hiyo itakayohusisha ujenzi wa masoko ya kisasa, machinjio ya kisasa, vituo vya mabasi, uendelezaji wa ufukwe wa Oysterbay, kiwanda cha kusindika korosho na ujenzi wa kitega uchumi kwenye kituo cha mabasi Kange Mkoani Tanga. Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango inaendelea kujenga uwezo kwa Halmashauri kuziwezesha kuibua miradi, kufanya upembuzi yakinifu ili miradi hiyo iweze kukidhi vigezo na kupata fedha na kuitekeleza kwa ufanisi.

Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi

91. **Mheshimiwa Spika**; kufuatia marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 Kifungu cha **37A** Mikopo inayotokana na **asilimia 10** ya mapato ya ndani sasa inatolewa bila riba kuanzia Julai, 2018 kwa kuzingatia mgawanyo wa **asilimia 4** kwa Wanawake, **asilimia 4** kwa Vijana na **asilimia 2** kwa Watu Wenye Ulemavu. Uwezeshaji wa Wananchi kiuchumi umeendelea kufanyika ikiwa ni utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 Sura ya Tano (5) inayohusu Uwezeshaji wa Wananchi Kiuchumi. Hadi Februari, 2019, jumla ya **Shilingi bilioni 13.2** kati ya **Shilingi bilioni 54.08** sawa na **asilimia 24.4** zimetolewa kama mikopo kwa vikundi **5,628** kati ya vikundi **28,025** vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 8.04** zimetolewa kwa vikundi **3,835** vya Wanawake, **Shilingi bilioni 4.7** zimetolewa kwa vikundi **1,606** vya Vijana na **Shilingi milioni 415.96**, zimetolewa kwa vikundi **187** vya Watu Wenye Ulemavu.

92. **Mheshimiwa Spika**; kuitia Programu ya Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (*Local Investment Climate -LIC*), Ofisi ya Rais-TAMISEMI imeendelea kuwezesha wananchi kiuchumi katika Sekta za Kilimo, Biashara na Uvuu katika Mikoa ya Kigoma na Dodoma. Maeneo ya kipaumbele

ni uzalishaji na uchakataji wa mazao ya Michikichi, Zabibu, Mbogamboga, Muhogo, Mpunga, Alizeti na Ufugaji wa Samaki. Miradi 44 imeibuliwa katika Halmashauri za Mikoa ya Dodoma na Kigoma yenye thamani ya **Shilingi bilioni 6.2**.

93. Mheshimiwa Spika; miradi hiyo inahusisha ukarabati wa miundombinu ya skimu za umwagiliaji 7 zikiwemo 4 za Mikoa wa Dodoma maeneo ya Mpunguzi na Bahi na skimu 3 za Mikoa wa Kigoma katika maeneo ya Nyindera na Mgambazi, masoko 7, minada 6, machinjio 7 ya kisasa, viwanda vidogo 5 na ujenzi wa Vituo 13 vya kutolea huduma za pamoja za biashara (*One Stop Business Centres*). Vituo hivyo vimesaidia kuongeza ufanisi ambapo leseni za biashara zinatolewa kwa wastani wa siku 1 au 2 ikilinganishwa na wastani wa siku 7 za awali. Hadi Februari 2019, jumla ya wafanyabiashara **16,173** wamepatiwa leseni za biashara katika Halmashauri za Mikoa wa Dodoma na wafanyabiashara **5,051** wamepatiwa leseni katika Halmashauri za Mikoa wa Kigoma. Vilevile, mradi wa LIC umesaidia upatikanaji wa vifaa vya kukusanya mapato (*Point of Sale Machine -POS*) **505** katika Mikoa ya Dodoma na Kigoma ili kuimarisha makusanyo ya mapato ya ndani ya Halmashauri.

94. Mheshimiwa Spika; utekelezaji wa miradi hiyo umechochea ukuaji wa uchumi kwenye maeneo husika pamoja na kuongeza ajira zipatazo **18,896** ambapo Wanawake ni **6,586** na Wanaume **12,310**. Aidha, Wafugaji na Wakulima wapatao **2,300** wamepatiwa mafunzo ya ujasiriamali kuhusu kuandaa maandiko ya miradi na kuwaunganisha na Taasisi mbalimbali za Fedha kwa lengo la kupata mikopo ili kukuza mitaji yao na ajira. Aidha, utoaji wa Vitambulisho kwa Wafanyabiashara Wadogo unaendelea ambapo hadi tarehe 25 Machi, 2019 vitambulisho **1,850,000** vimetolewa kwa Wakuu wa Mikoa. Kati ya vitambulisho hivyo, vitambulisho **820,104** tayari vimetolewa kwa wafanyabiashara wadogo sawa na **asilimia 44** ambapo hadi Machi, 2019 jumla ya **Shilingi 16,402,080,000.00** zilikuwa zimekusanya kutokana mauzo ya vitambulisho hivyo.

Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma

95. Mheshimiwa Spika; Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa kushirikiana na Wadau wa Maendeleo inaendelea na utekelezaji wa Awamu ya Tano ya Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma katika Mikoa 26 kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka wa fedha 2017/18 hadi mwaka wa fedha 2021/22. Wadau wanaoshirikiana na Serikali katika utekelezaji wa programu ni Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID) na Nchi za Norway na Sweden.

96. Mheshimiwa Spika; utekelezaji wa programu unahusisha shughuli za kuimarisha mifumo ya upangaji mipango na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa, usimamizi wa mapato na matumizi na ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Halmashauri, utekelezaji wa bajeti na uandaaji wa taarifa, usimamizi wa matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa na kuimarisha mifumo ya usimamizi, udhibiti na uwazi.

97. Mheshimiwa Spika; hadi Februari 2019, programu imeimarisha Mfumo Funganishi wa Usimamizi na Udhibiti wa Matumizi ya Fedha ambao umefungwa katika Halmashauri 184 ili kuhakikisha mfumo huo unakuwa endelevu. Aidha, umeandaliwa mwongozo wa ukusanyaji mapato ya ndani ya Halmashauri na kusambazwa kwenye Halmashauri hizo ili kuziwezesha kubuni vyanzo vipyta ya mapato na kusimamia makusanyo katika vyanzo vilivyopo. Vilevile, Mashine **6,000** za kukusanya mapato (*Point of Sale Machine-POS*) zimenunuliwa ili kuziwezesha Halmashauri zenye uwezo mdogo kuweza kukusanya mapato zaidi.

Uendelezaji wa Vijiji na Miji

98. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2018/19, ustawi wa jamii yetu uliendelea kuimarika sambamba na uendelezaji uliofanyika Vijijini na Mijini. Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaendelea na jukumu la kuhakikisha kuwa Mamlaka za Upangaji (Majiji, Manispaa, Halmashauri za Wilaya, Miji na Mamlaka za Miji Midogo) na Vijiji zinaandaa Mipango ya

Uendelezaji wa maeneo hayo kwa kuzingatia Sera na Sheria zinazohusu Uendelezaji wa Vijiji na Miji.

99. Mheshimiwa Spika; miji nchini inakua kwa kasi na mingine mipya inachipukia. Uendelezaji na uendeshaji wa miji unaimarika japokuwa zipo changamoto za utoaji wa huduma kutokana na maeneo mengi kutopangwa vizuri. Takriban asilimia 60 ya nyumba mijini zimejengwa kwenye maeneo yasiyo rasmi ambapo asilimia 80 ya wakazi wa miji wanaishi kwenye maeneo hayo. Wakazi mijini wameongezeka kutoka watu **555,535 (5.3%)** mwaka **1961** hadi kufikia **12,694,875 (29.1%)** mwaka **2012**. Idadi hiyo ina nguvukazi yenye uwezo wa kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kijamii nchini na ambayo inahitaji iwekewe mazingira mazuri ili ilete mabadiliko chanya ya kimaendeleo kwa nchi.

100. Mheshimiwa Spika; Ofisi ya Rais – TAMISEMI inatambua mchango wa utekelezaji wa programu, miradi na mikakati ya uendelezaji wa miji kuititia uimarishaji wa miundombini, Mifumo ya Taarifa za Kijiografia na TEHAMA, ukusanyaji na udhibiti wa mapato, usafi na takangumu, utunzaji wa mazingira, ukuzaji kipato na ustawi wa jamii. Katika kuendeleza juhudhi hizo Serikali inaiwezesha Miji kuwa na jamii iliyoelimika vizuri, shirikishi, shindani na yenye utangamano na Vijiji katika kuleta maendeleo nchini.

101. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Ofisi ya Rais - TAMISEMI ilikamilisha uandaaji wa Mwongozo wa Utoaji wa Vibali vya Ujenzi na Usimamizi wa Ukaguzi wa Majengo wa Machi, 2018 na kuusambaza kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara. Kila Halmashauri imeanzisha kituo kimoja (*One Stop Centre*) cha utoaji wa Vibali vya Ujenzi kuititia Kamati Ndogo za Wataalam. Tathmini ya matokeo kwenye Halmashauri 184 yamebainisha kupungua kwa muda wa kutoa Vibali vya Ujenzi kutoka siku **60** hadi siku **7** kwa majengo ya kawaida na siku **30** kwa majengo makubwa. Katika kipindi cha Julai 2018 hadi Februari 2019 Vibali vya Ujenzi **9,469** vilitolewa kwenye Halmashauri. Idadi hiyo imeongezeka kwa wastani wa mara

4 ikilinganishwa na kipindi kama hicho kwa Mwaka wa Fedha 2017/18 ambapo Vibali **2,341** vilitolewa.

102. *Mheshimiwa Spika;* Ofisi ya Rais - TAMISEMI inaratibu na kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Anwani za Makazi na Postikodi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano. Kazi zinazofanyika kwenye Halmashauri zote **185** ni kutoa elimu na kuihamasisha jamii, kuainisha na kuyahakiki majina ya barabara na mitaa, na namba za nyumba. Uwekaji miundombinu ya Mfumo wa Anwani za Makazi umefanyika katika Halmashauri **13** za Majiji ya Mwanza, Dodoma na Tanga, Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Moshi na Shinyanga, Halmashauri za Miji ya Kibaha na Geita na Halmashauri za Wilaya za Chato, Chamwino, Bahi, Buchosa na Sengerema zimechaguliwa kuanza kuweka miundombinu hiyo. Manufaa ya mpango huu ni kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi kwa kuyatambua maeneo mbalimbali na kuyafikia kwa urahisi.

103. *Mheshimiwa Spika;* katika kuendeleza Vijiji na Miji, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imeendelea kuimarisha matumizi ya Mfumo wa Taarifa za Kijografia (*Geographical Information System - GIS*) kwenye Mikoa na Halmashauri zote nchini. Mfumo huu umeongeza ufanisi na uwazi katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu za kijografia, ukusanyaji wa mapato, kusimamia masuala ya uendelezaji Vijiji na Miji. Hadi sasa Mamlaka za Serikali za Mitaa **148** kati ya **184** sawa na asilimia **80** zinatumia Mfumo huu. Mfumo umewezesha kuainisha **Miji Midogo Inayochipukia 1,165** ili iweze kuendelezwa kutoka Vijiji kuwa Miji Midogo kwa kuwa ina fursa za maendeleo na ndiyo ngazi ya msingi ya ukuaji wa Miji na ustawi wa Vijiji.

104. *Mheshimiwa Spika;* Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliendelea kuratibu uandaaji wa Mipango ya Jumla (General Planning Schemes) ya Uendelezaji Miji ambapo hadi kufikia Februari 2019, Mipango Kabambe ya Miji 10 ya Manispaa za Singida, Musoma, Mtwara, Iringa, Tabora na Songea; Miji ya Korogwe, Kibaha, Tunduma, na Bariadi imekamilika. Mipango hiyo itaongoza uendelezaji wa Miji na kudhibiti ujenzi holela.

Mipango Kabambe ya Majji ya Dar es Salaam, Dodoma, Mbeya, Mwanza na Arusha pamoja na Halmashauri zilizobaki iko kwenye hatua za uandaaji. Serikali inatumia mbinu na utaalalm mbalimbali wa kisasa katika kufanya marekebisho ya uendelezaji wa miji iwe himilivu na ya kisasa.

Utekelezaji wa Mpango wa Serikali Kuhamia Dodoma

105. *Mheshimiwa Spika;* Ofisi ya Rais-TAMISEMI imesimamia utungwaji wa Sheria ya Kulitangaza Jiji la Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi ambapo Muswada wa Sheria hiyo ulijadiliwa na Bunge lako Tukufu katika Mkutano wa 12 wa Bunge mwezi Septemba, 2018 na kuitishwa kuwa sehemu ya Sheria za Nchi. Kutungwa kwa Sheria hiyo ni utekelezaji wa uamuzi wa Serikali uliotolewa Mwaka 1973 wa kuhamisha Makao Makuu ya Nchi kutoka Dar es Salaam kwenda Dodoma. Aidha, huu ni utekelezaji wa llani ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 katika Ibara ya 151 (a) iliyoelekeza Serikali Kutunga Sheria itakayotambua Mji wa Dodoma kuwa Makao Makuu ya Nchi. Uamuzi huo uliofanywa na Serikali ya Awamu ya Tano umeleta hamasa kubwa ya maendeleo kwa wananchi wa Mkoa wa Dodoma na Watanzania wote kwa kuanza kujenga nyumba bora za makazi, kuongezeka kwa uwekezaji wa huduma mbalimbali za jamii na uboreshaji wa miundombinu ya kiuchumi ya barabara, viwanja vyta ndege na ujenzi wa Mji wa Serikali.

106. *Mheshimiwa Spika;* Halmashauri ya Jiji la Dodoma imekabidhiwa dhamana ya kusimamia uendelezaji na uendeshaji wa Makao Makuu ya Nchi. Kazi kubwa zilizofanyika ni kuongeza kasi ya upimaji wa maeneo ili kuhakikisha uendelezaji unafanyika kwa kuzingatia Sheria ya Mipango Mji ya Mwaka 2007. Vilevile, Halmashauri kwa kushirikiana na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) inaendelea kujenga barabara za lami na changarawe kurahisisha upitikaji katika maeneo yote likiwemo eneo la Mji wa Serikali.

107. *Mheshimiwa Spika;* katika kutekeleza azma ya Serikali kuhamia Dodoma, Ofisi ya Rais – TAMISEMI inashiriki katika

kutekeleza Mpango wa Kuendeleza Makao Makuu ya Nchi. Mpango Kabambe wa Jiji la Dodoma unafanyiwa mapitio ili kuandaa Mpango Kabambe ambao utakidhi na kuendana na uendelezaji wa Makao Makuu ya Nchi.

C. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA TAASISI ZILIZO CHINI YA OFISI YA RAIS-TAMISEMI

Tume ya Utumishi wa Walimu

108. *Mheshimiwa Spika;* Tume ya Utumishi wa Walimu kupitia vikao vya Kisheria ilipokea na kujadili mashauri ya kinidhamu **1,917** na kuyatolea uamuzi kwa kuzingatia Sheria na Kanuni za Utumishi wa Umma. Kati ya mashauri hayo **529** yalihitimishwa, **812** yapo katika hatua ya uchunguzi na **576** yatahitimishwa kabla ya Juni, 2019. Aidha, rufaa **114** zilipokelewa na kujadiliwa ambapo rufaa **62** zilihitimishwa na rufaa **52** zipo kwenye hatua za uhitimishwaji.

109. *Mheshimiwa Spika;* katika Mwaka wa Fedha 2018/19, Tume imefanya ufuatilaji katika Wilaya za Tanga, Muheza, Ubungo, Ilala, Temeke, Kinondoni, Kisarawe na Kibaha ili kuangalia utekelezaji wa majukumu yake na changamoto zinazoikibili katika ngazi ya Wilaya. Matokeo ya ufuatilaji huo umeiwezesha Tume kuratibu upatikanaji wa taarifa za kiutumishi za Walimu **95,578** ambapo Walimu wa Shule za Msingi ni **70,768** na Walimu wa Shule za Sekondari ni **24,810**. Jumla ya walimu **1,652** walithibitishwa kazini wakiwemo wa Shule za Msingi **1,124** na Shule za Sekondari **528**. Aidha, Walimu wanaojiendeza ni **8,643** ambapo kati yao, Walimu wa Shule za Msingi ni **5,911** na Walimu wa Shule za Sekondari ni **2,732**.

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

110. *Mheshimiwa Spika;* Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini unasimamia mtandao wa barabara zenyе urefu wa kilometra **108,946.19** ambazo zinajumuisha barabara za lami kilometra **1,449.55**, barabara za changarawe **kilometra 24,405.40** na barabara za udongo **kilometra 83,091.24** pamoja

na ujenzi wa **madaraja 2,760** na **makalvati 52,454**. Lengo la Wakala ni kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja ili kufungua fursa za kuchumi na kijamii Vijijini na Mijini.

Mapokezi ya Fedha za Mfuko wa Barabara

111. Mheshimiwa Spika; hadi kufikia Machi, 2019 Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) ulikuwa umepokea **Shilingi bilioni 136.02** kati ya **Shilingi bilioni 243.27** za Mfuko wa Barabara zilizoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/19 sawa na **asilimia 56**. Aidha, TARURA imeweza kujenga **kilomita 5,565.30** za barabara, **madaraja 167**, Makalvati makubwa (Box Culverts) 27, *drift 59* na mifereji ya maji yenye urefu wa **mita 51,347**. Vilevile, katika mwaka wa fedha 2018/19, TARURA imenunua magari **22** ili kuimarisha usimamizi wa barabara katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa. TARURA pia inaendelea na ujenzi wa jengo la utawala la Makao Makuu katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba Jijini Dodoma.

112. Mheshimiwa Spika; TARURA imefanikiwa kununua Mashine (POS) **664** za kukusanya ushuru wa matumizi ya maeneo ya hifadhi za barabara na maegesho ya magari ili kuungeza mapato yatakayowezesha Wakala kumudu utekelezaji wa majukumu yake. Hadi Machi, 2019, TARURA imekusanya jumla ya **Shilingi bilioni 8.71** sawa na **asilimia 78.20** ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 11.14** kutokana na matumizi maeneo ya hifadhi ya barabara zilizo chini ya TARURA na maegesho ya magari. Mafanikio hayo yanatokana na ushirikiano madhubuti kati ya TARURA na Wadau kupitia Kamati za Ushauri za Wilaya na Mikoa. TARURA inaendelea kufanya mipango ya kujimarisha ili kuungeza maeneo mengine ya ukusanyaji wa mapato. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaendelea kuimarisha ufuatiliaji na usimamizi ili kuhakikisha TARURA inatekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

Programu ya Uboreshaji wa Barabara Vijijini

113. Mheshimiwa Spika; kupitia Programu ya Uboreshaji wa Barabara Vijijini inayofadhiliwa na DfID, jumla ya barabara

zenye urefu wa **kilometra 151** zimejengwa kwa kiwango cha changarawe pamoja na madaraja **3** na makalvati makubwa **42** katika Halmashauri za Wilaya za Iramba, Kyela, Kyerwa, Rungwe, Bahi, Gairo, Kishapu, Babati, Mpwapwa, Magu, Busokelo, Bariadi, Kondoa, Kisarawe, Kibiti, Ushetu, Songwe na Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa gharama ya **Shilingi bilioni 28.88**. Aidha, Halmashauri ya Manispaa ya Iringa inaendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa daraja la Tagamenda na Halmashauri ya Wilaya ya Kilombero imekamilisha ujenzi wa barabara ya Chita hadi Melela.

114. Mheshimiwa Spika; kupitia Programu inayofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (*Road Transport Sector Policy Support Programme RTSPSP II*), jumla ya **kilometra 219.6** za barabara zimejengwa ambapo kati ya hizo **kilometra 21.3** zimejengwa kwa kiwango cha lami na **kilometra 198.3** zimejengwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya **Shilingi bilioni 16.07**. Mradi unatekelezwa katika Halmashauri za Wilaya za Chamwino, Kilolo, Kondoa, Kisarawe, Songea, Mbanga, Mwanga, Mbulu, Kongwa, Mbogwe, Busokelo, Kalambo, Iringa, Ludewa, Hanang, Kiteto na Halmashauri ya Manispaa ya Temeke. Mara baada ya kukamilika kwa barabara hizo zitarahisisha usafiri na usafirishaji.

115. Mheshimiwa Spika; Serikali kwa kushirikiana na USAID kupitia Programu ya *Feed the Future* inatekeleza miradi ya uboreshaji wa miundombinu ya barabara katika Halmashauri za Wilaya za Kongwa, Kiteto, Mvomero na Kilombero. Hadi Februari 2019, kilometra **152.1** za barabara zimejengwa kwa kiwango cha changarawe kwa gharama ya **Shilingi bilioni 7.56**. Mradi huo utakapokamilika utawezesha wakazi wa Halmashauri hizo kusafirisha mazao kwa urahisi hadi kwenye masoko na hivyo kukuza kipato.

Mradi wa Kuendeleza Jiji la Dar es Salaam (DMDP)

116. Mheshimiwa Spika; kupitia mradi huu, Serikali imeweza kujenga jumla ya kilometra **75.5** kati ya kilometra **210** za barabara zinazotarajiwani kujengwa kwa kiwango cha lami na Ofisi 3 zenye maabara ya kisasa. Aidha, umeandaliwa

Mpango Kabambe wa Maji ya Mvua na Maji taka utakaotekelawa kwa kipindi cha miaka kumi na saba (17) kuanzia Mwaka 2018 hadi 2035 kwa ajili ya kutatua changamoto za mafuriko katika Jiji la Dar es Salaam.

117. Mheshimiwa Spika; kazi nyingine zilizofanyika ni kuweka taa **5,000** za barabarani za mfumo wa jua na mitaro ya maji ya mvua kilomta **2.8**, ujenzi wa madaraja makubwa mawili ya Vimbili na Ulongoni katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilala, masoko **10**, vizimba **54**, vituo **7** vya huduma ya vyoo, vituo **6** vya maeneo ya mapumziko, vituo **12** vya huduma ya maji safi na ujenzi wa njia za waenda kwa miguu zenyne urefu wa **kilometra 5**, ununuzi wa samani, ujenzi wa Kituo cha Afya cha Buza katika Halmashauri ya Manispaa ya Temeke na masoko kumi **(10)** ya kisasa ambayo yapo katika hatua za ujenzi. Utekelezaji wa miradi hii unagharimu jumla ya **Shilingi billioni 207**.

118. Mheshimiwa Spika; hivi sasa Ofisi ya Rais-TAMISEMI inakamilisha maandalizi ya mikataba kwa ajili ya kujenga barabara zenyne urefu wa kilometra **61.3**, mifereji mikubwa (storm water drains) yenye urefu wa kilometra **40** kwenye maeneo ya mto ya Sinza, Kiboko, Gerezani na Kizinga; Bonde la Sungura, Mafuriko, Yombo, Buguruni Kisiwani, Msimbazi Tenge-Liwiti pamoja na ujenzi wa mabwawa makubwa **4** ya kuhifadhi maji ya mvua. Aidha, vizimba **12** vitajengwa kwa kwa ajili ya kuhifadhi taka ngumu, kuweka huduma za maji katika vituo **8** na kuweka taa za barabarani **1,054**.

Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)

119. Mheshimiwa Spika; kupitia mradi huo unaotekelawa katika Majiji ya Tanga, Arusha, Mbeya, Dodoma, Mwanza na Halmashauri za Manispaa za Mtwara-Mikindani, Kigoma Ujiji na Illemela, miradi ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara zenyne urefu wa kilometra **80.22** inaendelea kutekelezwa. Miradi mingine inayoendelea kutekelezwa ni pamoja na ujenzi wa madampo ya kisasa mawili (2), ujenzi wa maeneo ya kuwekea makontena ya kukusanya taka ngumu kwenye mitaa, ujenzi wa maeneo mawili ya

mapumziko (Public Parks), ujenzi wa mitaro mikubwa ya maji ya mvua kilometa **16.47** na ujenzi wa kituo kimoja cha kuegesha malori.

120. Mheshimiwa Spika; kazi nyingine zilizotekelezwa kupitia Mradi wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP) ni ujenzi wa vivuko sita (6) vya waenda kwa miguu, ujenzi wa kituo kikubwa kimoja cha mabasi katika Jiji la Dodoma, stendi mbili (2) za daladala katika Manispaa ya Mtwara-Mikindani na masoko makubwa mawili ya kisasa katika Jiji la Dodoma na Manispaa ya Mtwara Mikindani. Gharama za miradi hiyo ni **Shilingi bilion 214.74.**

Programu ya Kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa za Miji 18 (ULGSP)

121. Mheshimiwa Spika; kupitia Programu hii Serikali imeweza kujenga barabara zenyet urefu wa kilometa **116.6** kati ya kilometa **155.7** zinazotarajiwa kujengwa kwa kiwango cha lami katika Halmashauri za Manispaa za Morogoro, Tabora, Moshi, Sumbawanga, Shinyanga, Songea, Iringa, Mpanda, Lindi, Singida, Musoma na Bukoba na Halmashauri za Miji ya Kibaha, Babati, Geita, Korogwe, Bariadi na Njombe. Aidha, magari makubwa 26 yamenunuliwa kwa ajili kusombea taka ngumu; mitambo mikubwa minane (8) kwa ajili ya kupakilia taka na ukarabati wa dampo moja (1). Vilevile, vituo tisa (9) vya mabasi vinajengwa ambapo kati ya hivyo, vituo vitano (5) vimekamilika. Vituo hivyo, vinajengwa katika Halmashauri za Manispaa za Songea (2), Singida (2) na Iringa na Halmashauri za Miji ya Njombe Bariadi, Korogwe, Kibaha na machinjio nne (4) za kisasa katika Halmashauri za Manispaa za Lindi, Songea, Shinyanga na Halmashauri ya Mji wa Geita.

122. Mheshimiwa Spika; kazi nyingine zinazotekelezwa chini ya Programu hii ni ujenzi wa masoko matatu (3) ya kisasa katika Manispaa za Morogoro, Iringa na katika Mji wa Njombe na ujenzi wa kituo kimoja cha malori katika Manispaa ya Sumbawanga. Vilevile mradi umewezesha ununuzi wa picha za anga (Satellite Images) za Miji 18 kwa ajili ya kuboresha

mfumo wa Mipango Miji na Mfumo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Miji.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam

123. Mheshimiwa Spika; Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART) umekamilisha maandalizi ya utekelezaji wa Awamu ya Pili ya ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka itakayohusisha barabara za Kilwa, Kawawa, Sokoine, Gerezani, Bandari na Chang'ombe yenye urefu wa kilometra **20.3**. Utekelezaji wa mradi huo unafanyika kwa mkopo wa masharti nafuu kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Wananchi na Taasisi **90** kati ya **105** wamelipwa fidia ya **Shilingi bilioni 28.52** kati ya **Shilingi bilioni 34.19** zilizopangwa kulipwa ili kupisha utekelezaji wa mradi.

124. Mheshimiwa Spika, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART) umeanza maandalizi ya utekelezaji wa Awamu ya Tatu itakayohusisha barabara za Azikiwe na Maktaba, Bibi Titi na Nyerere kupitia Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) hadi Gongo la Mboto; kituo kikuu cha mabasi Kariakoo Gerezani kupitia Mtaa wa Lindi, Shaurimoyo na Uhuru kupitia Buguruni hadi TAZARA zenye urefu wa kilometra **23.6**. Aidha, wananchi wapatao **78** (PAPS) wanaoguswa na mradi mali zao zimethaminiwa kwa ajili ya kulipwa fidia. Vilevile, Serikali imetoa eneo la Gongo la Mboto kwa ajili ya ujenzi wa karakana ya mabasi (*bus depot*), eneo ndani ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere kwa ajili ya kujenga kituo cha mabasi kuunganisha uwanja huo na huduma ya Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam na eneo la kujenga kituo mlisho cha Banana karibu na eneo zilipo ofisi za TCAA.

Chuo cha Serikali za Mitaa - Hombolo

125. Mheshimiwa Spika; Chuo cha Serikali za Mitaa kilichopo Hombolo kimedahili wanafunzi wapatao **5,943** ikilinganishwa na lengo la kudahili wanafunzi **3,500** sawa na

asilimia 169.8. Ongezeko la udahili huo limetokana na Serikali kuanua wanafunzi waliokosa nafasi ya kuijunga na Kidato cha Tano Mwaka 2018 kuijunga na Vyuo mbalimbali kikiwemo Chuo cha Serikali za Mitaa-Hombolo. Vilevile, Chuo kimepata ithibati ya kuanza kufundisha Shahada mbili za Utawala na Rasilimali Watu na Utawala na Uongozi katika Serikali za Mitaa ambazo zitaanza kudahili wanafunzi katika mwaka wa masomo 2019/20.

126. *Mheshimiwa Spika*; Chuo kimeendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu na mfupi kwa watumishi wa Chuo na Watendaji na Viongozi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari 2019, Chuo kimegharamia mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi 39 na mafunzo ya muda mfupi kwa watumishi 106 ili kujenga uwezo wa Chuo kutekeleza majukumu yake. Aidha, Chuo kimetoa mafunzo kwa watumishi **266** kutoka katika Halmashauri **18** kuhusu utawala bora, uendeshaji wa miradi ya ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi, ukusanyaji wa mapato, uendeshaji wa vikao vyya kisheria, usimamizi wa miradi na uzingatiaji wa masuala ya jinsia katika mipango na bajeti.

127. *Mheshimiwa Spika*; ili kuboresha mazingira ya utoaji wa mafunzo, katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019, Chuo kimenunua viti **458** vikiwemo viti **168** visivyohamishika na viti **290** vinavyohamishika, *projector* **8** na *braille* mashine **4** kwa ajili ya wanafunzi wenyewe mahitaji maalum. Vilevile, katika kipindi hicho Chuo kimenunua eneo la ekari **2.7** katika Halmashauri ya Jiji la Dodoma kwa gharama ya **Shilingi milioni 74.7** kwa ajili ya kujenga kituo cha mihadhara na mafunzo ya muda mfupi katika eneo la lyumbu.

128. *Mheshimiwa Spika*; Chuo kimefanya tafiti katika nyanja za ukusanyaji wa mapato, uchumi wa viwanda, ukatili na unyanyasajii wa jinsia pamoja na dawati la kushughulikia malalamiko kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tafiti hizo zimesaidia kutoa mchango katika mipango ya Serikali kwa ajili ya kuboresha ustawi wa wananchi na maendeleo ya kiuchumi.

Shirika la Elimu Kibaha

129. Mheshimiwa Spika; Shirika kupitia Chuo cha Maendeleo ya Wananchi Kibaha linatoa mafunzo na kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo kwa lengo la kulijengea uwezo Shirika. Chuo kimeendelea kutoa mafunzo katika fani za kilimo na ufugaji, majengo na ujenzi, uchomeleaji na uundaji wa vifaa vya chuma, ufundi umeme, ushonaji, usimamizi wa hoteli, ufundi wa magari pamoja na udereva. Chuo kina uwezo wa kuchukua jumla ya wanafunzi **400** kwa mwaka. Shirika limeanzisha shamba la mifugo lenye Ng'ombe **71** wenye uwezo wa kuzalisha lita **13,640** za maziwa ghafi kwa miezi mitatu.

130. Mheshimiwa Spika; Shirika lina shule moja ya msingi iitwayo Tumbi yenye wanafunzi **916**. Vilevile, Shirika lina shule tatu za sekondari ambazo ni Kibaha Sekondari (wavulana) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **840**, Shule ya Sekondari Tumbi (Mchanganyiko) yenye wanafunzi **659** na Shule ya Sekondari ya Kibaha (Wasichana) yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi **320**. Shirika linaendelea kusimamia shule hizo ikiwa ni mpango wa kupambana na adui ujinga kwa kuhakikisha fursa mbalimbali za elimu zinatolewa kwa jamii.

Shirika la Masoko Kariakoo

131. Mheshimiwa Spika; Shirika la Masoko Kariakoo katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Februari, 2019 limekusanya mapato kiasi cha **Shilingi bilioni 1.7** katи ya lengo la kukusanya **Shilingi bilioni 3.49** sawa **asilimia 48.7** ya makadirio. Vilevile, katika kipindi hicho, Shirika limefanikiwa kujenga maduka **94** kuzunguka jengo la Soko Kuu ili kuongeza makusanyo ya mapato ya Shirika. Ujenzi wa maduka hayo umeongeza uwezo wa Shirika kukusanya mapato **Shilingi milioni 602.98** kwa mwaka.

132. Mheshimiwa Spika; Shirika limefanikiwa kufunga mfumo wa kielektroniki (*Local Government Revenue Collection Information System- LGRCIS*) na kununua mashine mpya (*Point of Sale Machine-POS*) 27 zinazotumika kukusanya

mapato. Matumizi ya mfumo wa kielektroniki yamechangia kuimarisha makusanyo kufikia **Shilingi bilioni 1.7** hadi Februari, 2019 ikililinganishwa na makusanyo halisi ya **Shilingi bilioni 1.62** yaliyokusanywa hadi Februari, 2018 sawa na ongezeko la **Shilingi milioni 80**. Makusanyo ya mapato hayo yanatokana ushuru wa mazao, ada ya kutumia soko na ada ya maegesha katika eneo la soko. Mapato hayo yametumika kuboresha hali ya soko na kuliwezesha Shirika kukusanya mapato zaidi kutokana na vyanzo hivyo.

133. Mheshimiwa Spika; Shirika limeandaa mkakati wa uwekezaji katika viwanja vilivyoko Mbezi Beach, Tabata na eneo la Soko Kuu kwa kufanya uwekezaji mkubwa ambapo tayari Shirika limeyatangaza maeneo hayo kwa shughuli za uwekezaji kwa mfumo wa ubia baina ya Serikali na Sekta Binafsi. Makampuni mbalimbali yameonesha nia ya kuwekeza katika viwanja hivyo. Utekelezaji wa mpango huo utaliwezesha Shirika kuongeza mapato na kuboresha utoaji wa huduma kwa wadau wake.

Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

134. Mheshimiwa Spika; kwa kipindi cha Julai, 2018 hadi Februari, 2019 Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imesimamia na kuratibu urejeshwaji wa mikopo kutoka Halmashauri ambapo Halmashauri zimerejesha mikopo kiasi cha **Shilingi milioni 616.63** kutokana na mikopo iliyotolewa. Kati ya fedha hizo, **Shilingi milioni 177.8** ni makusanyo ya mapato ya ndani yanayojoumuisha riba ya mikopo, kodi ya nyumba za Bodi na gawio la hisa, **Shilingi milioni 244.8** ni marejesho ya mikopo kutoka kwenye Halmashauri zilizokopeshwa na **Shilingi milioni 194.03** ni Michango ya Akiba kutoka kwenye Halmashauri. Aidha, Bodi imewekeza kiasi cha **Shilingi bilioni 2.1** katika akaunti za amana za muda maalum kwenye Benki za Biashara ili kukuza mtaji wa Bodi kutoa huduma ya mikopo kwa wadau wake.

**D. MPANGO NA MAKADIRIO YA MATUMIZI YA KAWAIDA
NA MAENDELEO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

135. Mheshimiwa Spika; Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 umeandaliwa kwa kuzingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17-2020/21), Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2015, Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030, Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20, maelekezo ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, wakati wa kuzindua Bunge Mwaka 2015 na maelekezo ya Viongozi wengine wa Kitaifa, Sera na Nyaraka mbalimbali za Serikali na Mipango Mikakati ya Taasisi.

Ofisi ya Rais-TAMISEMI

136. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kuratibu shughuli za Wizara za Kisekta na Wadau wengine, na kusimamia shughuli za Serikali katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- ii) Kuratibu na kusimamia shughuli za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika mwishoni mwa mwaka 2019;
- iii) Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Huduma za Afya ya Msingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- iv) Kuratibu na kusimamia Utekelezaji wa shughuli za utoaji wa Elimumsingi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- v) Kuandaa Sera na Mkakati wa kusimamia na kutekeleza dhana ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Umma;

- vi) Kufanya marekebisho mbalimbali ya Sheria za Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- vii) Kutekeleza mkakati wa kudhibiti rushwa;
- viii) Kudhibiti maambukizi mapya ya VVU na UKIMWI na kuendelea kuwasaidia walioathirika;
- ix) Kuratibu na kusimamia shughuli za Uendelezaji Vijiji na Miji iwe yenye ufanisi hususan Miji Midogo Inayochipukia;
- x) Kuratibu shughuli za lishe katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xi) Kukamilisha ujenzi wa Ofisi mpya ya OR-TAMISEMI katika Mji wa Serikali eneo la Mtumba Jijini Dodoma;
- xii) Kufanya ukaguzi, ufuatiliaji na tathimini kuhusu upolekaji wa fedha na utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xiii) Kuratibu na kusimamia mkakati wa kuongeza juhudzi za ukusanyaji wa mapato na matumizi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambapo kila Mkuu wa Idara amepewa Mkoa wa kusimamia;
- xiv) Kuratibu na kusimamia mifumo ya TEHAMA katika ngazi zote za OR-TAMISEMI;
- xv) Kuratibu na kusimamia masuala ya kiutumishi katika ngazi zote za OR-TAMISEMI;
- xvi) Kuratibu shughuli na utendaji kazi wa Taasisi zilizopo chini ya OR- TAMISEMI;
- xvii) Kuratibu shughuli za uboreshaji wa mazingira ya biashara katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo utoaji wa vitambulisho kwa wafanyabiashara wadogo;

xvii) Kuratibu na kusimamia uibuaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika Halmashauri zote nchini; na

xix) Kuratibu na kusimamia mkakati wa ujenzi na uanzishaji wa viwanda **100** kwa kila Mikoa.

Tawala na Mikoa

137. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Tawala za Mikoa zinazojumuisha Sekretarieti za Mikoa, Wilaya na Tarafa zitatekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kudumisha amani, utulivu na usalama;
- ii) Kuratibu utoaji wa huduma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa katika Sekta za Afya, Elimu na sekta nyingine;
- iii) Kuendeleza ujenzi, ukarabati na ukamilishaji wa Ofisi na Makazi ya Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Wilaya na Maafisa Tarafa;
- iv) Kuendelea kusimamia na kuimarisha Utawala Bora katika Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- v) Kuratibu Maandalizi ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa ajili ya viongozi wa ngazi za msingi za Vijiiji, Mitaa na Vitongoji utakaofanyika mwishoni mwa mwaka 2019;
- vi) Kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Ugatuaji wa Madaraka kwa Wananchi na Sera nyingine za kisekta ili kuimarisha utoaji wa huduma kwa wananchi;
- vii) Kuratibu, kusimamia na kutoa ushauri katika ujenzi wa miundombinu ya kutolea huduma za kiuchumi na kijamii katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- viii) Kuratibu na kusimamia uibuaji na utekelezaji wa miradi ya kimkakati katika Halmashauri;

- ix) Kuratibu na kusimamia shughuli za lishe katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- x) Kuziwezesha na kuzijengea uwezo Mamlaka za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake;
- xi) Kuratibu Masuala Mtambuka yanayotekelawa kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- xii) Kuratibu uanzishwaji wa viwanda na ushiriki wa sekta binafsi kwa kuendelea kuweka mazingira wezeshi ya kufanya biashara mijini na vijiji;
- xiii) Kutatua migogoro inayotokana na matumizi ya ardhi na mipaka kwenye Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; na
- xiv) Kuratibu na kusimamia Mkakati wa ujenzi na uanzishaji wa viwanda 100 katika Mkoaa.

Mamlaka za Serikali za Mitaa

138. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Mamlaka za Serikali za Mitaa zimepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- i) Kusimamia utawala bora, amani na utulivu katika ngazi zote za Halmashauri;
- ii) Kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utakaofanyika Mwaka 2019;
- iii) Kuendelea kuwawezesha wanawake, vijana na watu wenyewe ulemavu kwa kutenga na kutoa mikopo kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri;
- iv) Ukamilishaji wa miradi viporo ikiwemo majengo ya Ofisi na makazi ya viongozi na watumishi hasa katika maeneo mapya ya utawala;

- v) Ujenzi, Ukarabati na ukamilishaji wa miundombinu ya kutolea huduma za kijamii na kiuchumi katika sekta zote hususan Hospitali za Halmashauri, Vituo vya Afya, zahanati, maabara, nyumba za watumishi, matundu ya vyoo na vyumba vya madarasa;
- vi) Kuendesha mikutano ya kisheria na kutekeleza maazimio ya vikao;
- vii) Kusimamia rasilimaliwatu na fedha katika Halmashauri;
- viii) Kubuni na kutekeleza miradi ya kimkakati itakayosaidia kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri ili kupunguza utegemezi;
- ix) Kusimamia shughuli za lishe katika Halmashauri;
- x) Kuimarisha matumizi ya mifumo ya kielektroniki kwa ajili ya kuongeza ufanisi wa makusanyo katika vyanzo vya mapato;

- xi) Kusimamia Mpango wa utoaji wa Elimumsingi Bila Ada katika Shule za Msingi na Sekondari;
- xii) Kutenga maeneo ya uwekezaji kwa ajili ya viwanda vidogo, vya kati na viwanda vikubwa na maeneo ya wafanyabiasha wadogo;
- xiii) Kusimamia na kuwezesha uendeshaji wa ngazi za msingi na maeneo ya kutolea huduma katika Halmashauri;
- xiv) Kuendelea kusimamia matumizi ya fedha za Mfuko wa Kuchochera Maendeleo ya Jimbo kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za Mfuko;
- xv) Kuratibu shughuli za usafi wa mazingira na utunzaji wa vyanzo vya maji;
- xvi) Kusimamia na kuratibu shughuli za Mipango Miji na Matumizi ya Ardhi; na

xvii) Kubuni mikakati ya uanzishaji wa viwanda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa.

E. MALENGO YA TAASISI ZILIZO CHINI YA OR-TAMISEMI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

Tume ya Utumishi wa Walimu

139. *Mheshimiwa Spika;* katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Tume ya Utumishi wa Walimu imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kutoa uamuzi wa mashauri ya nidhamu, rufaa na malalamiko ya Walimu kwa mujibu wa Sheria na kwa wakati;
- ii) Kusimamia taaluma ya ualimu ili kuhalikisha uwepo wa Walimu wenye sifa na wenye kuleta tija na kuongeza ufanisi katika sekta ya elimu ili kutatua changamoto zinazolikabili Taifa;
- iii) Kusimamia maadili na nidhamu kwa taaluma ya Ualimu kwa Shule za Msingi na Sekondari;
- iv) Kuimarisha mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kusimamia masuala ya Walimu nchini; na
- v) Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanyia kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Tume Makao Makuu na Wilayani pamoja na kuendeleza rasilimali watu kwa kuwaongezea ujuzi na vitendea kazi.

Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA)

140. *Mheshimiwa Spika;* katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) utatekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kujenga uwezo wa Ofisi za Mikoa na Wilaya katika kutekeleza majukumu ya Wakala;

- ii) Kufanya matengenezo ya kawaida **kilometa 13,098.61**, matengenezo ya maeneo korofi **kilometa 5,565.79**, matengenezo ya muda maalum **kilometa 2,860.64** na matengenezo ya makalvati madogo **2,403**, madaraja **113**, makalvati makubwa **273** na mifereji yenze urefu wa mita **82,627.81**.
- iii) Kuhimiza Misingi ya Utawala Bora na Uwajibikaji kwa Makandarasi na Wafanyakazi wa TARURA;
- iv) Kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Wakala;
- v) Kutunza mtandao wa barabara za Vijiini na Mijini ili zipitike kwa nyakati zote za mwaka;
- vi) Kushiriki katika uhakiki wa mtandao wa barabara za Mijini na Vijiini;
- vii) Kuendelea na matengenezo ya barabara za vijiini na mijini ili zipitike nyakati zote za mwaka kwa kutumia fedha za Mfuko wa Barabara;
- viii) Kusimamia utekelezaji wa kazi za ujenzi wa Barabara kwa Miradi ya Maendeleo kuititia Wadau wa Maendeleo (EU, DfID,USAID and Benki ya Dunia);
- ix) Kushirikiana na Wadau wa Maendeleo kuwezesha matengenezo ya barabara za vijiini na mijini kulingana na miongozo inayotolewa;
- x) Kufanya utafiti kwa lengo la kuwezesha utekelezaji wa mipango ya Wakala;
- xi) Kuimarisha Mfumo wa Usimamizi wa Matengenezo ya Barabara (DROMAS);
- xii) Kuanzisha na kuendesha mizani ya barabara ili kudhibiti uzito wa magari katika barabara za vijiini na mijini;

xiii) Kuimarisha Mfumo wa Kudhibiti Matumizi ya Fedha katika Ofisi za Mikoa na Halmashauri; na

xiv) Kuimarisha Masuala Mtambuka katika maeneo yenye miradi ya ujenzi wa barabara kwa kutoa elimu ya Maambukizi ya Virusi vya Ukimwi, Rushwa, Jinsia, Watu Wenye Ulemavu, Vijana na Wazee, pamoja na Mazingira.

Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam (DART)

141. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka utatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kushiriki katika utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Awamu ya Pili inayotekelawa kupitia Mkopo wa Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB). Ujenzi miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Pili unahusisha barabara zenyen urefu wa **kilometra 20.3** katika barabara za Kilwa, Kawawa, Sokoine, Gerezani, Bandari na Chang'ombe. Mradi huo utahusisha pia ujenzi wa barabara za juu (flyovers) katika makutano ya Chang'ombe na Uhасibу;

(ii) Kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi waliopisha ujenzi wa miundombinu ya mfumo wa Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Tatu. Ujenzi wa miundombinu utahusisha barabara za Nyerere kutoka katikati ya Jiji la Dar es Salaam hadi Gongo la Mboto, Bibi Titi na Mitaa ya Uhuru, Shaurimoyo, Lindi, Azikiwe na Maktaba.

(iii) Kufanya tathmini ya gharama za kuhamisha miundombinu ya kijamii na fidia kwa wananchi watakaopisha utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT) Awamu ya Nne ambayo itahusisha ujenzi wa barabara za Bagamoyo hadi Tegeta, Bibi Titi, Ali Hassani Mwinyi na Sam Nujoma zenyen urefu wa kilometra 25.9 na Awamu ya Tano itakayohusisha ujenzi wa barabara za Mandela kuanzia eneo la Ubungo kupitia TAZARA, Uhасibу

kuungana na barabara ya daraja la Kigamboni na barabara ya kuanzia Tabata Relini hadi Segerea;

(iv) Ukamilishaji wa taratibu za ununuzi ili kumpata Mto Huduma kamili (*Service Provider-SP*) kwa Awamu ya Kwanza ya Mabasi Yaendayo Haraka (BRT). Mabasi yanayotarajiwa yatakuwa 305 na barabara za mlisho zitakuwa 11 ikilinganishwa na huduma ya mpito yenyе mabasi 140 na barabara za mlisho mbili; na

(v) Kuendelea kusimamia kwa karibu Mfumo wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato wa Serikali za Mitaa (*Local Government Revenue Collection Information System-LGRCIS*) katika ukusanyaji wa mapato kwa Awamu ya Kwanza.

Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo

142. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Chuo cha Serikali za Mitaa kitakeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kudahili wanafunzi wapya 5,000;
- ii) Kuendeleza na kuboresha mazingira ya kufundishia na kujifunzia kwa wanafunzi wa kozi za muda mrefu (kununua kompyuta 80 na vitabu 600) kutoa mafunzo ya muda mfupi yenyе kuzingatia uhitaji;
- iii) Kuanzisha kozi moja ya shahada ya Utawala na Menejimenti katika Serikali za Mitaa (*Bachelor Degree in Local Government Administration and Management*);
- iv) Kufanya tafiti na kutoa ushauri wa kitaalam katika masuala yanayohusu Mamlaka za Serikali za Mitaa;
- v) Kutekeleza majukumu ya kuwa Chuo kiongozi cha mafunzo (*Lead Training Institution*) katika kusimamia ubora wa mafunzo yanayotolewa katika ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa (*LGAs*);

- vi) Kuendeleza watumishi katika ngazi mbalimbali za mafunzo;
- vii) Usimamizi wa shughuli za uendeshaji wa Chuo;
- viii) Kufanya mapitio ya Sera mbalimbali za Chuo ili ziendane na mazingira ya sasa mfano mitaala ya kufundishia na mafunzo na maendeleo ya watumishi.
- ix) Kusimamia ukusanyaji wa mapato, matumizi na kudhibiti malimbikizo ya madai na madeni;
- x) Ukarabati wa miundombinu ya Chuo na utunzaji wa mazingira yake;
- xi) Ujenzi wa hostel ya wanafunzi wa kike yenyewe uwezo wa kuchukua wanafunzi 200;
- xii) Kuendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara (lecturer theatre) wenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 500;
- xiii) Kuhamisha makaburi katika eneo la upanuzi wa Chuo,
- xiv) Kuimarisha matumizi ya TEHAMA katika shughuli za Chuo ikiwa ni pamoja na ununuzi wa kompyuta mpya 80; na
- xv) Kupima na kufuatilia upatikanaji wa hati ya umiliki wa ardhi ya eneo la Chuo lenye ukubwa wa ekari **592** ikiwa ni pamoja na kurejea Michoro ya Mpango wa matumizi wa eneo hilo (Master Plan).

Shirika la Elimu Kibaha

143. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Shirika la Elimu Kibaha limepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kuziwezesha shule zilizopo (Shule ya Chekechea moja, Shule ya Msingi moja na Shule za Sekondari tatu) kutoa elimu na malezi bora kwa wanafunzi **2,765** na kutoa huduma za maktaba kwa wadau **40,000**;

- ii) Kuendelea kupambana na adui umaskini kwa kutoa elimu ya ufundi stadi kwa wanachuo **400**, kuendeleza shamba la ng'ombe wa maziwa na kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa wadau **400**; na
- iii) Kupanua miundombinu ya Chuo cha Afya na Sayansi shirikishi kukidhi mahitaji ya utoaji wa mafunzo katika Chuo hicho.

Shirika la Masoko Kariakoo

144. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Shirika la Masoko Kariakoo litatekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kuboresha eneo la Mabucha lilioko ndani ya Jengo la Soko Kuu kwa kujenga maduka yapatayo hamsini na mbili (52);
- ii) Kujenga maduka madogo yapatayo ishirini na mbili (22) eneo la Mtaa wa Tandamti;
- iii) Kujenga Soko eneo la Mbezi Beach- Makonde;
- iv) Kufanya ukarabati wa miundombinu ya Soko, Ofisi na nyumba za Shirika;
- v) Kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa kutumia Mfumo wa Kielektroniki na kubuni vyanzo vipyta vyatia mapato pamoja na kuimarisha usimamizi wa matumizi ya rasilimali za Shirika;
- vi) Kuboresha maslahi ya Watumishi ikiwemo kulipa stahiki za Watumishi kwa wakati;
- vii) Kulipa madeni; na
- viii) Kufanya uwekezaji wa ubia katika viwanja ambavyo vinamilikiwa na Shirika.

Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa

145. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imepanga kutekeleza shughuli zifuatazo:-

- i) Kupokea, kuchambua na kutoa mikopo kwa Halmashauri zitakazokidhi vigezo;
- ii) Kuendelea kutoa mafunzo ya kuzijengea uwezo Halmashauri 84 kuandaa maandiko ya miradi bora inayokopesheka;
- iii) Kuweka mkakati wa ufuutiliaji wa urejeshwaji wa mikopo na uwasilishwaji wa michango kutoka Halmashauri zinazodaiwa kwa lengo la kuongeza mtaji wa Bodi;
- iv) Kubuni vyanzo vipyta vya mapato; na
- v) Kutoa elimu kwa wadau mbalimbali ili waweze kufahamu majukumu ya Bodi na huduma zinazotolewa.

F. MALENGO MAHSUSI YALIYOPANGWA KUTEKELEZWA KATIKA MWAKA WA FEDHA 2019/20

146. Mheshimiwa Spika; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Ofisi ya Rais-TAMISEMI imepanga kutekeleza kazi maalum kama ifuatavyo:-

- (i) Kuanza ujenzi wa Hospitali mpya **27** za Halmashauri ambazo hazina Hospitali. Hospitali hizi zitajengwa katika Halmashauri za Karatu, Chalinze, Kondoa, Kongwa, Mbogwe, Biharamulo, Nsimbo, Kigoma, Kakonko, Liwale, Serengeti, Mbeya, Kilombero, Kaliua, Babati, Mvomero, Newala, Sengerema, Kwimba, Madaba, Msalala, Ikungi, Handeni, Mkinga, Halmashauri ya Mji wa Tunduma na Halmashauri za Manispaa za Sumbawanga na Tabora. Vilevile, Hospitali **67** za Halmashauri zilizoanza kujengwa katika mwaka wa fedha 2018/19 zitaendelea na ujenzi katika mwaka wa fedha 2019/20. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi**

bilioni 46.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali hizo za Halmashauri (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 6*);

(ii) Ujenzi wa Vituo vya Afya vipya **52** katika baadhi ya Kata ambazo hazina vituo ili kuboresha huduma za uzazi kwa kuboresha huduma za Mama na Mtoto na hali ya utoaji wa huduma za afya kwa ujumla. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 10.40** kwa ajili ya ujenzi wa vituo hivyo vya afya (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 7*);

(iii) Kuendelea kutekeleza Mpango wa Utoaji Elimumsingi Bila Ada kwa Shule za Msingi na Shule za Sekondari hadi Kidato cha Nne. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 288.47** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa Elimumsingi Bila Ada. Kati ya fedha hizo, **Shilingi bilioni 134.31** zimetengwa kwa Shule za Msingi (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.8*) na Shilingi bilioni **154.16** zimetengwa kwa Shule za Sekondari (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na.9*);

(iv) Ukamilishaji wa ujenzi wa nyumba **364** za walimu katika Shule za Msingi. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 9.10** kwa ajili ya ujenzi wa nyumba hizo za walimu (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 10*);

(v) Kupitia Mpango wa Uboreshaji wa Elimu ya Sekondari (SEQUIP) zitajengwa Shule za Sekondari **26** maalum za wasichana sawa na shule moja kila Mkoa. Ujenzi wa shule hizo utafanyika sambamba na ujenzi wa maktaba kwa kila shule. Aidha, yatanunuliwa magari **26** kwa ajili ya kuimarisha usimamizi wa shule hizo **26**;

(vi) Kupitia Mpango wa Lipa Kulingana na Matokeo (EP4R), kazi sitiatazo zitatekelezwa:-

a) Ujenzi wa Vyumba **800** vya Madarasa ya Shule za Sekondari;

- b) Ujenzi wa Mabweni **300** ya Shule za Sekondari;
 - c) Ujenzi wa matundu **1,000** ya vyoo ya Shule za Sekondari;
 - d) Ujenzi wa majengo **50** ya utawala ya Shule za Sekondari;
 - e) Ujenzi wa kumbi **200** kwenye Shule **100** za Sekondari;
 - f) Ukarabati wa Shule kongwe **15** za Sekondari;
 - g) Ununuzi wa vifaa maalum vya maabara katika Shule 70 za Sekondari;
 - h) Ununuzi wa magari **40** kwa ajili ya Halmashauri zenyne mazingira magumu;
 - i) Ujenzi wa vyumba **1,200** vya madarasa ya Shule za Msingi,
 - j) Ujenzi wa matundu ya vyoo **2,000** katika Shule za Msingi;
 - k) Ujenzi wa mabweni **10** katika shule **10** za Elimu maalum;
- (vii) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala katika Halmashauri **62** zinazoendelea na ujenzi. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 56.50** kwa ajili ya ujenzi wa majengo ya utawala kwenye Halmashauri hizo (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 11*);
- (viii) Kuendelea na ujenzi wa majengo ya utawala katika Mikoa mitano (5) ambayo ni Simiyu, Katavi, Geita, Songwe na Njombe. Aidha, Mkoa wa Mbeya umetengewa fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa jengo la utawala;
- (ix) Halmashauri kumi na tatu (13) za Wilaya ambazo ni Nsimbo, Kakonko, Mbogwe, Nyang'hwale, Kigoma, Mlele, Buhigwe, Busokelo, Gairo, Madaba, Bumbuli, Ileje na Mbulu zimepewa kipaumbele cha ununuzi wa magari ya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2019/20;

(x) Kuendelea na utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati katika Halmashauri zilizokidhi vigezo. Jumla ya **Shilingi bilioni 70** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 12*);

(xi) Kufanya matengenezo ya barabara zenye urefu wa **kilometa 21,525.04** na matengenezo ya makalvati madogo **2,403**, madaraja **113**, makalvati makubwa **273** na mifereji yenye urefu wa mita **82,627.81**. Jumla ya **Shilingi bilioni 224.94** zilimetengwa kwa ajili ya kutekeleza kazi hizo kupitia fedha za Mfuko wa Barabara (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 13*).

(xii) Vilevile, kwa mwaka wa fedha 2019/20, Mfuko wa Barabara umetengewa **Shilingi bilioni 22.44** kwa ajili ya ujenzi wa barabara za lami **kilometa 15.1**, ukarabati wa barabara za changarawe **kilometa 185.7** na ujenzi wa **madaraja 23** (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 14*).

(xiii) Katika Mwaka wa Fedha 2019/20, jumla ya kilometa **25.69** za barabara zitajengwa kwa kiwango cha lami kupitia mradi wa DMDP pamoja na ununuzi wa vifaa vya kuzoa taka ngumu katika Manispaa za llala, Temeke na Kinondoni. Jumla ya **Shilingi bilioni 90.50** zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi wa DMDP;

(xiv) Kuendelea kutoa mikopo kwa vikundi vya Vijana, Wanawake na Watu Wenye Ulemavu. Katika mwaka wa fedha 2019/20, zimetengwa **Shilingi bilioni 62.25** kwa ajili ya mikopo ya vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu (*Mchanganuo umeoneshwa katika Kiambatisho Na. 15*).

G. SHUKRANI

147. *Mheshimiwa Spika*; kabla ya kuhitimisha Hotuba yangu, natumia fursa hii kukushukuru sana wewe Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi imara katika kutekeleza shughuli za Bunge. Vilevile, naishukuru sana Kamati ya

Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa inayoongozwa na Mwenyekiti wa Kamati Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Bukoba Vijijiini, na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Mcemba, Mbunge wa Viti Maalum, kwa kazi nzuri katika kusimamia utendaji wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

148. *Mheshimiwa Spika*; nichukue fursa hii pia kuzishukuru Nchi na Mashirika mbalimbali ya Kimataifa wanaoendelea kushirikiana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI katika kutekeleza mipango na programu mbalimbali katika kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Washirika hao wa Maendeleo ni pamoja na Benki ya Dunia (WB), Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), Jumuiya ya Ulaya (EU), Shirika la Maendeleo la Ubelgiji (BTC), *Global Partnership for Education*, Shirika la Maendeleo la Uingereza (DfID), Shirika la Maendeleo la Canada (CIDA), Shirika la Maendeleo la Marekani (USAID), Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ), Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF), Shirika la Umoja wa Mataifa la Makazi (UN-Habitat), UNEP, *CAMFED*, Africities, Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu (UNFPA), *World Food Programme* (WFP), Nchi ya Sweden, Shirika la Mapinduzi ya Kijani Afrika (AGRA), Shirika la DALBERG na Nchi zote zinazochangia kupitia Mfuko wa Pamoja wa Kusaidia Bajeti ya Serikali. Ofisi ya Rais-TAMISEMI inaahidi kuendelea kushirikiana na Wadau mbalimbali wa Maendeleo katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI yaliyojikita katika kuboresha utoaji huduma za kijamii na kiuchumi ili kupunguza umaskini. Aidha, ninawashukuru Wananchi kwa mchango mkubwa katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mafanikio katika utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI yametokana na ushirikiano mzuri baina ya Wadau wa Maendeleo, Wananchi na Viongozi katika ngazi mbalimbali za usimamizi.

149. *Mheshimiwa Spika*; napenda kutambua mchango mkubwa wa Viongozi wenzangu katika kufanikisha utekelezaji

wa majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Kipekee nawashukuru Naibu Mawaziri, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege (Mb.) na Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara (Mb.) kwa msaada mkubwa wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI. Aidha, namshukuru Katibu Mkuu, Mhandisi Joseph M. Nyamhanga, Naibu Makatibu Wakuu Bw. Tixon T. Nzunda na Dkt. Dorothy O. Gwajima na Katibu wa Tume ya Utumishi wa Walimu Bi. Winfrida Rutaindurwa. Aidha, nawashukuru Wakuu wa Mikoa, Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI, Wakurugenzi wa OR-TAMISEMI na Wakurugenzi wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa pamoja na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais-TAMISEMI kwa ushirikiano wanaonipa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais-TAMISEMI.

150. *Mheshimiwa Spika*; nitakuwa mchoyo wa fadhila nisipowashukuru Viongozi wenzangu katika Ofisi ya Rais wakiongozwa na Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mheshimiwa George Huruma Mkuchika na Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais- Menjeimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa katika kutekeleza majukumu ya Ofisi ya Rais. Aidha, nawashukuru sana Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Dkt. **Francis Michael, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais-Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao.**

151. *Mheshimiwa Spika*; kipekee nawashukuru wananchi wa Jimbo la Kisarawe kwa kunitia moyo katika utekelezaji wa majukumu haya ya Kitaifa. Ninawaahidi kuendelea kuwatumikia kwa nguvu zangu zote ili kuboresha utoaji wa huduma kwa wananchi. Aidha, naishukuru familia yangu kwa uvumilivu muda wote nilipokuwa mbali nao katika utekelezaji wa majukumu haya ya Kitaifa.

H. MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/20

Maduhuli na Makusanyo ya Mapato ya Ndani

152. *Mheshimiwa Spika*; katika Mwaka wa Fedha 2019/20, OR - TAMISEMI, Taasisi zilizo chini yake, Mikoa 26 na Halmashauri 185 inaomba idhini ya kukusanya maduhuli na mapato ya ndani jumla ya **Shilingi Bilioni Mia Nane na Mbili, Milioni Mia Moja Sitini, Mia Nne Tisini na Nane Elfu, Mia Moja Sitini na Nne (Shilingi 802,160,498,164.00)**. Makusanyo hayo yatatokana na mauzo ya vifaa chakavu, nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, ada za wanafunzi, marejesho ya masurufu na mishahara na kodi na ushuru mbalimbali unaotozwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kulingana na Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290. Mchanganuo wa makusanyo ya mapato hayo ni kama ifuatavyo:-

Jedwali Na. 1: Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo kwa Mwaka wa Fedha 2019/20	
OFISI/TAASISI	MAKADIRIO
OR-TAMISEM	20,000,000.00
Taasisi	36,444,195,252.00
Mkoa	213,302,912.00
Halmashauri	765,483,000,000.00
	802,160,498,164.00

153. *Mheshimiwa Spika*; sasa naomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 jumla ya **Shilingi Trillioni Sita, Bilioni Mia Mbili na Saba, Milioni Mia Tisa Tisini na Mbili, Laki Saba na Sabini na Tisa, Mia Saba Sitini na Tisa (Shilingi 6,207,992,779,769.00)** kwa ajili ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI Fungu Na. 56, Tume ya Utumishi wa Walimu Fungu Na. 02 na Mafungu 26 ya Mikoa yanayojojumuisha Halmashauri 185. Mchanganuo wa fedha zinazoombwba kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 ni kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na.2.**

Jedwali Na.2: Muhtasari wa Makadirio ya Mpango na Bajeti ya OR – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2019/20

AINA Y A M ATUMIZI	FEDHA ZINAZOOMBWA
OR - TAMISEMI	
Mishahara	
Makao Makuu	10,836,663,200.00
Ta a sisi	33,385,105,800.00
Jum la Mishahara	44,221,769,000.00
Matumizi Mengineyo	
Makao Makuu	7,896,530,195.00
Ta a sisi	1,318,870,805.00
Jum la Matumizi Mengineyo	9,215,401,000.00
JUMLA OR - TAMISEMI	53,437,170,000.00
Tume ya Utumishi wa Walimu	
Mishahara	9,899,012,000.00
Matumizi Mengineyo	6,002,155,000.00
Jum la	15,901,167,000.00
MIKO A	
Mishahara	83,654,030,000.00
Matumizi Mengineyo	41,803,829,000.00
Jum la	125,457,859,000.00
HALMASHAURI	
Mishahara	3,669,329,614,000.00
Matumizi Mengineyo (SK)	190,390,615,000.00
Mapato ya Ndani (OS)	460,539,000,000.00
Jum la Ndogo	4,320,259,229,000.00
MIRADI YA MAENDELEO	
OR - TAMISEMI	463,563,123,910.00
Mikoa	67,333,480,032.00
Halmashauri (SK)	857,096,750,827.00
Mapato ya ndani (OS)	304,944,000,000.00
Jum la Miradi ya Maendeleo	1,692,937,354,769.00
JUMLA KUU	6,207,992,779,769.00

*SK – Serikali Kuu OS – Own Source

154. Mheshimiwa Spika, pamoja na hotuba hii yapo majedwali ambayo yanafafanua kwa kina makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya OR-TAMISEMI, Taasisi, Mikoa na Halmashauri.

155. Mheshimiwa Spika, hotuba hii inapatikana pia kwenye Tovuti ya OR-TAMISEMI ambayo ni www.tamisemi.go.tz

156. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

NAIBU WAZIRI WA NISHATI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono. Ni taarifa nzuri ya kazi Serikali iliyofanya na Waheshimiwa Wabunge mmeshapewa taarifa hizo kwenye meza zenu, msiwe wavivu wa kusoma. Msingoje kila siku kusomewa. Someni na ninyi wenyewe mjue kilichoandikwa na mazuri ya Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Waziri, Utumishi na Utawala Bora.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mhesnimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na mafungu tumeyataja hapo. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kuitisha Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mhesnimiwa Mwenyekiti, awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uwezo wa kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi. Namshukuru pia Mheshimiwa Rais, kwa kuendelea kuniamini katika nafasi ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya

Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Namwahidi kuwa nitatekeleza wajibu wangu kwa ufanisi na uadilifu wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru wapigakura wangu wa Jimbo la Newala Mjini kwa kuendelea kuniamini kushirikiana nami wakati wote ninapokuwa naendelea kuwawakilisha katika Bunge ninapotumwa pia katika shughuli za Kitaifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishukuru familia yangu wakiongozwa na mke wangu Anna na watoto wangu na wajukuu zangu kwa uvumilivu wanaonipa, wajukuu wangependa kucheza nami lakini muda mwingu babu hayupo anatekeleza majukumu ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpongeza Mwenyekiti wetu wa Kamati na Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa kuchaguliwa tena kwenye Kamati kuendelea kutuongoza, nawapongeza kwa kazi nzuri ambazo wanafanya na ushauri wanaotupa katika Kamati yetu unaowezesha kutekeleza majukumu yetu vizuri. Nawapongeza Wajumbe wapya ambao wamejunga nasi katika Kamati na majina yao nimeyatata.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa na Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijiji na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mwanne Ismail Mcchemba, Mbunge wa Viti Maalum, Tabora kwa ushirikiano wanaotupa katika shughuli za Kamati yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha wa 2018/2019; Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fedha kwa Mwaka wa Fedha wa 2019/2020. Maoni na ushauri wa Kamati hiyo yametuwezesha na yataendelea kutuwezesha kutekeleza majukumu ya kuwahudumia wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, naomba kutumia nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa

wetu, Rais wetu mpendwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa uongozi wake mahiri unaohimiza uadilifu, uwajibikaji, uchapakazi na utendaji wenye matokeo katika Utumishi wa Umma na usimamizi wa miradi mikubwa ya kimkakati. Pia, napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wetu wa Rais pamoja na Mheshimiwa Majaliwa, Waziri wetu Mkuu ambaye pia ni Kiongozi wetu hapa wa shughuli za Serikali Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua fursa hii pia kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo na kuimarisha Muungano wa Tanzania, amani na utulivu. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Balozi Self Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa ushupavu na uadilifu mkubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Spika, Wenyeviti wa Kamati kwa jinsi mnavyotuongozza katika Bunge letu Tukufu na kufanikisha malengo na kutekeleza majukumu ya Bunge letu. Naomba nikupongeze binafsi wewe Mwenyekiti pamoja na Spika, Naibu Spika na ninyi Wenyeviti kwa kumsaidia Mheshimiwa Spika kuliendesha Bunge letu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapongeza Mawaziri wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio wanayopaya katika utekelezaji wa llani ya Uchaguzi ya CCM, Chama Tawala na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Kwa namna ya pekee, nampongeza naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wabunge wapya wote waliochaguliwa, orodha ipo ndani ya hotuba yangu, kwa kunusuru muda muelewe tu kwamba nimewapongeza na nimewaandika katika *book* langu la hotuba ya leo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuchukua fursa hii kuwapongeza tena Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu

Waziri walioteuliwa kuongoza Serikali yetu kumsaidia Mheshimiwa Rais katika sekta mbalimbali. Majina yao yamo ndani ya *book*, siyasomi kwasababu ya kunusuru muda. Vile vile Lakini nichukue nafasi hii nimpongeze Naibu wangu, Mheshimiwa Marry Machuche Mwanjelwa kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Naamini kwamba Mheshimiwa Rais aliona mzigo uliopo katika Wizara akaona nipate msaidizi. Nakupongeza Marry, chapa kazi nami nipo pamoja nawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru Watendaji wa Serikali wakiongozwa na Balozi, Injinia Kijazi ambaye ni Katibu Mkuu Kiongozi, yeye anafanya kazi lkulu na mimi ni Waziri wa Rais (lkulu). Nampongeza yeye, Makatibu Wakuu wote, Wakurugenzi na Watendaji Wakuu wote ambao wanaongoza Taasisi za Serikali na wale wanaohusika na Wizara yangu mmewasikia tumewatambulisha leo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee nazishukuru nchi mbalimbali ambazo zimetoa ushirikiano na Serikali yetu kuititia Wizara yangu na orodha ya nchi mbalimbali na Mashirika ya Kimataifa yameorodheshwa katika hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho kabisa napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa Watumishi wote wa umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi mkubwa. Uzalendo na imani yao kwa Uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi kwa ufanisi. Mimi ndiyo Waziri wenu Watumishi wa umma, nawapongezeni wale mlion waadilifu, nawapongezeni kwa kazi nzuri mnayofanya kukusanya mapato, kuhudumia wagonjwa, kutengeneza barabara na zote mnazofanya watumishi wa umma nchi hii Rais ana imani na ninyi, Waziri wenu ana imani na ninyi, chapeni kazi. Madege tusingenunua, barabara tusingetengeneza na kazi nydingi zimewezekana kwa sababu watumishi wa umma wamekusanya vizuri mapato ya Serikali. Tunataka mfanye

vizuri zaidi, nchi inajivunia kuwa na watumishi wa umma wa aina ya kwenu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kulithibitishia Bunge lako Tukufu kwamba, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma itatekeleza majukumu yake ipasavyo kwa mujibu wa mgawanyi wa kazi wa Wizara kama ulivyotolewa na Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu, Viongozi na Watumishi wa Umma waliopoteza maisha yao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki ikiwemo ajali za Magari matatu ya watumishi wa umma ambao wamepata ajali na wakapoteza maisha wakati wakielekea Dodoma, wakitoka Dodoma kutekeleza majukumu ya Serikali. Mwenyezi Mungu aziweke roho zao mahali pema peponi. Amina.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu itazungumzia maeneo makuu mawili ambayo ni Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha wa 2018/2019 pamoja na Mpango wa Utekelezaji na Maombi ya Fedha kwa Mwaka 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Mwaka wa Fedha 2018/2019, mwaka wa fedha 2018/2019, ulizingatia dira kama tulivyosema ya maendeleo, llani ya Uchaguzi na kadhalika. Nitazungumzia kwa kifupi Ofisi zangu zote, Ofisi ya Rais, Ikulu na Taasisi zake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Fungu 20 - Ofisi ya Rais, Ikulu ilidhinishiwa bilioni 22.6 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na kufikia Machi, 2019 Shilingi bilioni 16.1 zilitolewa. Ili kutekeleza majukumu katika Mwaka wa Fedha wa 2018/2019, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri - Fungu 30 iliyojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, ilidhinishiwa Shilingi bilioni 576. Kati ya hizo, Shilingi bilioni 401 kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, Shilingi bilioni 175 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia

Machi, 2019, Shilingi bilioni 427 zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo Shilingi bilioni 304 tuliwaeleza kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Shilingi bilioni 123 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo ya kila Taasisi:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Ikulu inaendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, kazi zifuatazo zilitkelezwa. Tumeeleza pale huduma zilizotolewa kwa Mheshimiwa Rais, ushauri ulitolewa kwa Mheshimiwa Rais, tumeeleza vikao vya Baraza la Mawaziri, vikao vya Makatibu Wakuu, vikao vya Sekretarieti vilivyo fanyika kufanya maandalizi wka ajili ya kushauri Baraza la Mawaziri. Kwa hiyo, kazi zilizofanywa katika Ofisi ya Rais, Ikulu tumeziandika katika kitabu, kama nilivyosema kwa kunusuru muda, naomba nisisome vyote. Kazi zingine zilizotekelzwa katika fungu hili zipo katika ukurasa wa 10 hadi 11 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa; matokeo ya juhudini zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya uongozi shupavu wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kukabiliana na rushwa nchini yameleta mafanikio makubwa kwa kuongeza nidhamu na uwajibikaji kwa watumishi wa umma, kujengeka kwa uadilifu katika biashara, ukusanyaji mapato na matumizi ya umma. Mafanikio yameijengesha Serikali msingi mpana wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma za msingi kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa mbalimbali zinazotolewa na taasisi za kimataifa na za kitaifa kuhusiana na hatua zinazochukuliwa na Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa zimedhihirisha Tanzania inapiga hatua kubwa katika kudhibiti vitendo vya rushwa na ujisadi hapa nchini. Kwa kutolea mifano michache, kiashiria cha *Transparency International* kimeonesha kuwa kwa mwaka 2018/2019, Tanzania imefanya vizuri kwa kiwango cha juu ya wastani ukilinganisha na nchi nyingine za Kusini mwa Jangwa la Sahara kwa kufikisha kiwango cha asilimia 36 na kushika nafasi

ya 99 kati ya nchi 180 Duniani ikilinganishwa na nafasi ya 103 ya mwaka 2017/2018. Kwa hiyo Tanzania tunakaribia kuwa katika nusu ya kwanza ya nchi zile duniani ambazo zinafanya vizuri katika suala la kupambana na rushwa na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, *Afrobarometer* mwaka 2014 walionesha kuwa asilimia 66 ya waliohojiwa walisema kuwa kiwango cha rushwa kimeongezeka. Hata hivyo, matokeo ya utafiti walioufanya hao hao mwaka 2017 yanaonesha kwamba asilimia 72 ya waliohojiwa walisema kuwa kiwango cha rushwa nchini kimepungua.

Aidha, matokeo ya utafiti uliofanywa na TWaweza mwaka 2017 nao ulibainisha kuwa asilimia 85 ya wananchi waliohojiwa walieleza kuwa rushwa imepungua ukilinganisha na asilimia 11 ya waliosema mwaka 2014. Kwa hiyo, tunaendelea kufanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa, siku hizi kila Mtanzania anaewala kwamba ukiuza kitu toa risiti, ukinunua kitu dai risiti. Utamaduni huo kwa Watanzania sasa umeanza kukolea na nawaomba Watanzania tuendelee hivyo, mwelewe kwamba mtu ambaye anafanya biashara hatoi risiti anatuibia fedha ambazo zingetumika kununulia madawa na kuwapeleka watoto shule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kipindi cha mwezi Julai, 2018 hadi Machi, 2019 shughuli zifuatazo zilitkelezwa:-

Uchunguzi wa majalada na kuomba kibali cha kufungua kesi, shilingi milioni 977.92 ziliokolewa kutokana na TAKUKURU kuingilia kati malipo ambayo yalikuwa haramu, malipo hewa; Elimu kuhusu athari za rushwa zimeendelea kutolewa na hapa nataka niwaombe tena Watanzania wenzangu; kazi za TAKUKURU ziko tatu; kupambana na rushwa, kuzuia rushwa na kuelimisha. Sasa sisi tumeomba na Waziri Mkuu pia ameshaagiza Watumishi wa Serikali wakiwa na Makongamano, warsha, semina, kitu gani ilimradi kuna mkusanyiko wamekaa kutwa siku mbili, wawaite wataalam wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa waje kutoa elimu. Utekelezaji wa jambo hili siyo mzuri sana. Tumeomba

Mabaraza ya Madiwani watoa mada wako huko Wilayani. Kila Wilaya tuna Maafisa wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa tuwatumie hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taasisi ya Uongozi; Taasisi ya Uongozi imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha utaalam wa hali ya juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika nzima kwa ujumla. Taasisi inafanya vizuri, Taasisi tumeiomba mara kwa mara kuendesha semina kwa makundi mbalimbali mnakaribishwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha Mwaka 2018/2019, kwa muhtasari kazi zifuatazo zimetekelizwa. Tumezieleza Kozi saba (7) za muda mfupi zimetolewa, watu gani wamehudhuria hayo mafunzo, Wakuu wa Wilaya, Wakuu wa Mikoa, Wakurugenzi na Makundi mbalimbali waliomba Taasisi na wakatoa mafunzo hayo. Taarifa kwa kina ipo katika kitabu changu cha hotuba ukurasa wa 21 hadi wa 27 wa hotuba yangu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali, Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA); Mango wa MKURABITA umeendelea kutekelezwa. Jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara nchini unatambulika na kukubalika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2018 hadi Machi, 2019, MKURABITA imejengea uwezo Vyama vyta Wakulima uwezo wa kutumia Hati Miliki za Kimila kupata mtaji katika Benki na Taasisi nyingine. Maelezo ya shughuli zake yako katika ukurasa wa 27 mpaka 31.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*); Mfuko huu umeendelea kutekeleza awamu ya tatu kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya Ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini. Takwimu zinaonesha kwamba asilimia 28.2 ya Watanzania ni maskini. Serikali ya Awamu ya Tano imepata mafanikio makubwa kuitia mpango huu wa *TASAF*, watoto waliokuwa hawaendi shule wanakwenda, watoto ambao walikuwa hawapati uji asubuhi wanapata,

mafanikio yao darasani sasa yameanza kubadilika, majumba mengine yamejengwa. Maelezo kuhusu mpango huu wa *TASAF* tumeyaeleza katika kitabu kwa urefu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka niwatoe hofu Watanzania wenzangu, wako watu wengi ambao wanahitaji kuhudumiwa na *TASAF* lakini uwezo wetu Kiserikali tulifika asilimia 70 tu. Asilimia 30 ya walengwa wa *TASAF* bado hatujawafikia. Tunaandaa mpango katika mwaka huu unaokuja tuweze kumaliza asilimia 30 yote iliyobaki na kufika katika vijiji vyote. Kazi nyininge zilizotekelawa katika kipindi hiki zipo katika ukurasa wa 31 hadi 37 wa kitabu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mfuko wa Rais wa Kujitegemea; Mfuko huu umetoea huduma mbalimbali ya mikopo kwa wajasiriamali wadogo na wa kati. Aidha, Mfuko huu utakamillsha kazi zake katika mwaka wa fedha 2018/2019 baada ya hapo hautakuwepo kwa mwaka 2019/2020 kwa sababu shughuli zake zitakuwa zimefungwa kuanzia wakati huo. Maelezo yake mengine yako ukurasa wa 37 na 38.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi, katika kipindi cha Julai mpaka Machi baadhi ya shughuli zilizotekelawa tumeziorodhesha kutoka kifungu cha kwanza pale mpaka cha pili, kupokea malalamiko, kupokea fomu za kutangaza mali na kadhalika. Kazi nyininge zilizotekelawa zipo katika ukurasa wa 38 hadi 42 katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na wakala zilizopo chini yake. Katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma, Fungu 32 inayojumuisha wakala zilizo chini yake iliidhinishiwa jumla ya fedha shilingi bilioni 41, takwimu za fedha zilizopata na zilizotumika tumeziorodhesha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kipindi cha kuanzia Julai 2018 hadi Machi 2019, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo, tumezieleza

toka moja pale, mbili, tatu, nne. Hii ndiyo Ofisi ya Katibu Mkuu, Utumishi, kwa hiyo kuna mambo mengi sana nikisema niyasome yote ndani ya nusu saa niliyopewa inaweza ikaniwia vigumu kwangu. Haya ndiyo masuala yaliyotekelawa na ofisi hiyo. Taarifa ya kina ya shughuli zilizotekelawa ziko katika ukurasa wa 42 hadi 51 katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma (*Tanzania Public Service College*). Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa ili kutoa mafunzo, ushauri, kufanya utafiti na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za Uongozi, Menejimenti ya Utumishi na Utawala. Tumeeleza kozi mbalimbali zilizoendeshwa na Chuo cha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa nataka kutoa rai moja, ukisema rai labda unawabembeleza, nataka kutoa agizo, sheria iliyoanzisha chuo hiki inataka kila mtumishi wa umma anayepata ajira Serikalini kabla hajaanza kufanya kazi apelekwe akasome Chuo cha Utumishi wa Umma. Waajiri hamuwapeleki watumishi wenu, kule wanafundishwa Kiswahili kizuri, ndiyo maana siku hizi jambo la kawaida kabisa kumpata mtumishi badala ya kusema 'fulani hajambo' unasema 'fulani ajambo' anaanza na 'a' badala ya 'h'.

Mheshimiwa Mwenyekiti, watumishi wengi wa umma hawajui taratibu za Serikali na jinsi inavyofanya kazi. Kwa hiyo, natoa rai kwa waajiri wote na bahati nzuri nawafahamu kwa sababu mnapotaka kuaajiri mnakuja kuomba ruhusa kwangu, sisi ndiyo tunawafanyia *interview*, tunawateua baada ya pale eleza unawapeleka lini kusoma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukienda nchi nyingine, nenda Kenya hapa jirani zetu wana chuo pale Kenya *School of Government* kazi yake ni kufundisha watumishi namna ya kufanya kazi Serikalini. Pale ndiyo wanajifunza *Government moves on paperna kadhalika*. Leo watumishi wana matatizo wanapeleka *SMS* kwa Mheshimiwa Waziri, kwa Mheshimiwa Katibu Mkuu, mimi siwezi kuchukua hatua kwa *SMS* ulioileta

kwa sababu sina uhakika kama unayosema ni kweli, lakini ukileta barua inawekwa katika faili tunafuatilia, tunakujibu. Nasema kuanzia sasa nitafuatilia mimi mwenyewe waajiri wote mnaoajiri na wale ambao mna viporo mliwaajiri lakini hamjawapeleka kwenda kusoma Chuo cha Utumishi wa Umma fanyeni hivyo mara moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (*E-Government*), niwaeleze tu kwamba tutafanya mpango, tutaleta Muswada hapa Bungeni wa kubadili Wakala huu kuwa mamlaka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, omiba pesa.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba hotuba yangu yote hii kama tulivyowasilisha Mezani iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, jumla kuu ya bajeti nayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka 2019/2020 ni kama ifuatavyo: Jumla kuu ya Matumizi ya Kawaida ni Sh.483,705,000. Jumla kuu Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh.199,867,255,617. Jumla kuu ya fedha nazoliomba Bunge lako hili liidhinishe kwa ajili ya Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) ni Sh.683,543,960,617.

Mheshimiwa Mwenyekiti na Waheshimiwa Wabunge, mwisho, naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaiddinisha ili twende tukachape kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kutoa hoja. (*Makof*)

WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naafiki.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

MWENYEKITI: Hoja imeungwa mkono, ahsante Mheshimiwa kwa taarifa na kazi nzuri mnazofanya. Sasa namuita MwenyeKITI wa Kamati ya Kudumu, Bunge, Utawala na Serikali za Mitaa. (*Makofi*)

MHE. JASSON S. RWEIKIZA – MWENYEKITI KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE, UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa MwenyeKITI, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu mwangi wa rehema kwa kuturuzuku uhai tangu tulipokamilisha kujadili Bajeti ya Ofisi ya Rais -TAMISEMI kwa mwaka wa fedha unaoisha hadi leo tena tunapokutana katika kujadili Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha ujao. Wapo wenzetu ambao hawakupata nafasi hii, hivyo sisi tuliohatika kuipata tunapaswa kumrejeshea shukurani Maulana yechee pekee aliyetukuka.

Mheshimiwa MwenyeKITI, kutokana na ufinyu wa muda naomba taarifa yote hii iingie katika Kumbukumbu Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa MwenyeKITI, kwa mujibu wa Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, naomba kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 pamoja na maoni ya Kamati kuhusu makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa MwenyeKITI, sehemu ya utangulizi wa taarifa hii imeeleza majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016 pamoja na kazi ambazo zilitkelezwa na Kamati kwa kuzingatia Kanuni hizo. Aidha, sehemu hii imegusia kwa kifupi dhana ya ugatuaji wa madaraka kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kupongeza juhudhi za Serikali katika kuzingatia dhana hii kwa kuunga mkono nguvu za wananchi. Kamati inashauri iendelee kujikita katika kujenga mfumo imara wa kuwahudumia wananchi ambao utazingatia misingi ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi ambao Ibara ya 8(a) ya Katiba inawataja kuwa wao ndiyo

msingi wa madaraka yote ya Serikali na Serikali itapata madaraka na mamlaka yote kutoka kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Kamati inashauri Serikali ihakikishe inagatua rasilimali fedha za kutosha na kuzipeleka kikamilfu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji wake unafanyika na kuziwezesha Mamlaka hizo kutimiza wajibu wake kwa wananchi. Sehemu ya utangulizi ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 1 hadi 3 wa kitabu cha taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kutekelezwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa mwaka 2018/2019. Katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais - TAMISEMI iliidhinishiwa na Bunge hilli Tukufu Sh.1,799,000,000 kwa ajili ya utekelezaji wa Mirdi ya Maendeleo. Kamati ilitembelea na kukagua miradi ifuatayo, Mradi Na.6403 Mpango wa Uandaaji wa Miji ya Kimkakati Tanzania (*TSCP*). Mradi huu unagharamiwa na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia na ruzuku kutoka Serikali ya Denmark na utekelezaji wake uko katika awamu ya pili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, awamu ya kwanza ilianza mwaka wa fedha 2010/2011 hadi 2015/2016 kwa jumla ya Dola za Kimarekani milioni 225.7 na awamu ya pili ilianza mwaka wa fedha 2017/2018 na inaendelea hadi kufikia mwaka wa fedha 2020 kwa gharama ya Dola za Kimarekani milioni 130.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Manispaa ya Mtwara Mikindani ambao unatekelezwa chini ya kifungu 8091, Fungu la 80, Mkoa wa Mtwara. Mradi unahusisha uboreshaji wa miundombinu ya huduma za Miji na uimarishaji wa mfumo wa Halmashauri katika kutoa huduma bora kwa jamii. Katika uboreshaji wa huduma za Miji, barabara zenye urefu wa kilomita 15.78 zimejengwa kwa kiwango cha lami kwa jumla ya shilingi bilioni 24. Barabara hizo ni bandari

kilometra 2.75, Zambia kilometra 3.75, Mikindani kilometra 2, Chuno kilometra 5.78 na Kunambi kilometra 1.6. Aidha, ujenzi wa dampo la kisasa, vizimba 25 vya kukusanya taka na ununuzi wa mitambo na vifaa vya kusafirishia taka viligharimu jumla ya shilingi bilioni 4.9 vilijengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya mradi huo Manispaa ya Mtwara Mikindani ilipata nyongeza ya shilingi bilioni 8.8 ambazo zimefanikisha shughuli kadhaa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mifereji ya maji yenye urefu wa kilomita 7.4, maegesho ya magari katika dampo, mizani za kupimia taka na uwekaji wa taa za nishati ya juu katika barabara ya Chuno. Aidha, jumla shilingi bilioni 21.6 zitatumika katika awamu ya pili ya mpango kwa kujenga barabara kilomita 4.1, mfereji wa kupeleka maji bahrini kilomita 3.4, kuboresha maeneo ya wazi, maduka makubwa, stendi ya daladala ya Mikindani na ujenzi wa soko la Chuno.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na.46 *Local Govenment Authority Own Source Projects*, Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu. Mradi huu ilitengewa jumla ya shilingi bilioni 3.01 na ulipangwa kutekelezwa chini ya Fungu 80, Mkao wa Mtwara. Mradi huu ni sehemu ya mkakati wa Serikali Awamu ya Tano ya kuwawezesha kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kupitia asilimia 10 ya mapato la ndani ya kila Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini Tanzania (*TARURA*). *TARURA* inahudumia mtandao wa barabara wenye kilomita zaidi ya 108,946,000 nchi nzima na ina majukumu makubwa ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za vijiji na mijini pamoja na madaraja na mpango mkakati wa kuondoa vikwazo ili barabara ziweze kuitika muda wote. Aidha, *TARURA* inatarajiwa kuimarisha barabara zinazopita kwenye maeneo muhimu yenye viwanda na kilimo na hivyo kusaidia shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Mkoani Lindi ambako *TARURA* inahudumia barabara yenyе urefu wa kilomita 693.1. Barabara zilizokaguliwa na Kamati ni kipande cha Nyengendi (Km.1) kinajengwa kwa kiwango cha lami ambacho ni sehemu ya barabara ya Nyengendi – Mnara - Lutamba yenyе urefu wa kilomita 48 na kipande cha Kituo cha Mabasi - Nyangao Hospitali (Km. 0.8) ambacho ni sehemu ya barabara ya Nyangao – Namupa - Mihima yenyе urefu wa kilomita 23.2. Matokeo ya ukaguzi. Matokeo ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotekelawa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 9 - 12 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Kutokana na ziara ya ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo katika Mikoa ya Lindi na Mtwara, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri wa jumla kama ifuatavyo:-

- (i) Wakala wa Barabara za Vijijini na Mjini (*TARURA*) unakabiliwa na ufinyu wa bajeti hivyo unahitaji kuongezewa fedha ili uweze kutekeleza kazi zake kwa ufanisi kutokana na kuwa na mtandao mkubwa wa barabara.
- (ii) Upungufu wa wataalamu wa ujenzi na uhaba wa vitendea kazi unaathiri utendaji wa *TARURA* katika maeneo mbalimbali nchini.
- (iii) Hazina itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa miradi inayopangwa na hivyo kuendelea kuwakosesha wananchi huduma zilizokusudiwa.
- (iv) Kukosekana kwa programu endelevu ya elimu ya ujasiliamali na uwezeshaji wa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu unasababisha vikundi vingi vinavyopatiwa mikopo kushindwa kuendelea na kukuza miradi illyokusudiwa.
- (v) Kukosa umakini katika usanifu wa awali (*feasibility study*) wa miradi ya maendeleo kunaathiri

utekelezaji na hivyo kuongezeka għarama kutokana na kubadilisha michoro.

(vi) Hatua ya Mfuko wa Kuwezesha Kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu Wenye Ulemavu kutungiwa sheria, Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa, Sura 290 ambayo ilifanyiwa marekebishesha na Sheria ya Fedha ya mwaka 2018, kutafanya utaratibu wa usimamizi wa mfuko huo kuwa na nguvu za kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa mpango wa bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa. Uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka 2018/2019 ni kama inavyoonekana katika ukurasa wa 14 hadi 20 wa taarifa hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Mpango wa Makadirio wa Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Taarifa ya mpango wa bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI inajumuisha mafungu 28; Fungu 56, Fungu 2 na mafungu 26 ya mikoa yote ya Tanzania Bara imeandaliwa na kuzingatiwa yafuatavyo:-

(i) Mwongozo wa Taifa wa kuandaa mpango na bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na maelekezo mbalimbali ya viongozi wa Kitaifa.

(ii) Vipaumbele vilivyoainishwa katika llani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 - 2020.

(iii) Malengo endelevu ya maendeleo 2030 (*Sustainable Development Goals*).

(iv) Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo ya Miaka Mitano.

(v) Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais - TAMISEMI uliofanyiwa mapitio mwaka 2016.

(vi) Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipozindua Bunge la Kumi na Moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imepanga kutekeleza malengo yake kwa kuzingatia vipaumbele 10 kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 21 - 22 wa taarifa ya Kamati. Baadhi ya vipaumbele hivyo ni pamoja na haya yafuatayo:-

(i) Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na ugatuaji wa madaraka kwa umma (*D by D*).

(ii) Kusimamia maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa ya mwaka huu 2019.

(iii) Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya maendeleo ya utawala wa Mikoa, Wilaya na Halmashauri mpya na za zamani ambazo hazina majengo ya utawala.

(iv) Kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa fedha katika Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya mapato. Katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinakadiria kukusanya jumla ya shilingi bilioni 802.1, mapato hayo yameongezeka kwa shilingi bilioni 43.8 sawa na asilimia 6 ikilinganisha na makusanyo ya mwaka wa fedha unaoisha. Jedwali Na.4 linatoa ufanuzi zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ingawa kumekuwa na ongezeko la makusanyo katika maeneo haya inatarajiwa

kwamba Halmashauri zitachangia kwa kiasi kikubwa kutokana na maduhuli yake kuongezeka kwa takribani shilingi bilioni 29.9 sawa na asilimia 4.1 ikilinganishwa na makusanyo ya Halmashauri katika mwaka uliotangulia. Ni mtazamo wa Kamati kwamba huenda ongezeko hilo limechangiwa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa kuendelea kubuni vyanzo vipyta vya mapato ili kufidia pengo la vyanzo vilivyochukuliwa na Serikali Kuu na kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa makadirio ya matumizi. Katika mwaka wa fedha wa 2019/2020, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa pamoja zinaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya shilingi trillioni 6.2 kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyopangwa kutekelezwa. Kati ya fedha hizo shillingi trillioni 4.5 ni kwa Matumizi ya Kawaida na shillingi trillioni 1.7 ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Kwa upande wa fedha za Maendeleo, Kamati imebaini upungufu wa asilimia 5.2 kutoka shilingi trillioni 1.8 kwa mwaka unaoisha hadi trillioni 1.7 kwa mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kulinganisha bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI na Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, uchambuzi umeibaini kwamba wakati bajeti ya Taifa ikiongezeka kwa asilimia 1.9 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/2019 bajeti TAMISEMI katika kipindi hicho imepungua kwa asilimia 5.7. Aidha, bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMSEMI ni sawa na asilimia 18.7 ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umeendelea kupungua katika kipindi cha miaka minne mfululizo kutoka asilimia 24 mwaka 2015/2016 hadi kiwango cha sasa. Kwa ujumla uwiano huo umepungua kwa zaidi ya asilimia 5 ndani ya kipindi cha miaka minne ya fedha kiwango ambacho ni kikubwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, inashangaza kwamba licha ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kusimamia sekta nyingi sana katika ngazi za Mamlaka ya Serikali za Mitaa bajeti yake imepungua. Ni kwa mantiki hiyo Kamati inahojii ni kwa vipi maboma ya

shule za msingi na sekondari za kata, zahanati, vituo vya afya, hospitali za Wilaya na kadhalika yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi yatakamailika. Ni wazi hilo halitawezekana kwa mwenendo wa bajeti kupungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ingetamani kuona ofisi hii inaongezewa fedha katika bajeti yake huku Serikali ikiendelea kujikita katika kujenga mfumo imara wa kuwashudumia wananchi ambaa ndio msingi wa madaraka yote ya Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8(a) katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Njia madhubuti ya kujenga mfumo huo ni Serikali kuhakikisha inagatua rasilimali fedha za kutosha, yaani kuongeza bajeti na kuzipeleka kikamilifu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji wake unafanyika na ikiwezekana mamlaka hizo kutimiza wajibu wake kwa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kufanya ziara kwenye miradi ya maendeleo na kupitia Taarifa ya Utekelezaji, Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

(1) Kamati inapongeza hatua ya Serikali kutunga sheria kwa ajili ya kusimamia mikopo ya uwezeshaji kiuchumi wanawake, vijana na watu wenye ulemavu kutohana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri. Sheria hiyo imetungwa kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2018 na imefafanua kuhusu mgawanyo wa makundi hayo na kwamba mikopo hiyo haitolewi riba. Kamati inaishauri Serikali iharakishe kukamilisha mchakato wa kuanda Kanuni za Sheria hiyo ili ianze kutumika ipasavyo.

(2) Halmashauri nyingi hazijaanza kuzingatia Sheria ya Kusimamia Mikopo ya Uwezeshaji kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu, kutohana na kushindwa kutenga fedha na kuzipeleka kikamilifu fedha hizo kwenye vikundi husika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa jambo hilo na Wakurugenzi wa

Halmashauri ambao hawatazingatia sheria hii wachukuliwe hatua stahiki.

Aidha, Halmashauri ziwezeshwe kufungua Akaunti Maalum kwa ajili ya fedha za asilimia 10 ili ziweze kusimamiwa kwa ufanisi zaidi. Vilevile, Halmashauri ziandae na kutunza takwimu kuhusu idadi ya vikundi, pamoja na kuonesha usimamizi wa fedha zinazorejeshwa na vikundi vilivyokopeshwa.

(3) Kamati inashauri Halmashauri ziwezeshe vikundi vinavyopata fedha kutoptaka na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri, kubuni miradi mikubwa ya kiuchumi ili kuweza kujikwamua dhidi ya umasikini. Kamati inapongeza Halmashauri zote za Mkoa wa Simiyu ambazo zimeamua kutumia fedha hizo kununua mashine kutoka Shirika la Viwanda (*SIDO*) kwa lengo la kuwezesha vikundi hivyo kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya uzalishaji na Halmashauri ya Mji Mafinga, Mkoani Iringa ambayo imetumia fedha hizo kuanzisha kiwanda kikubwa cha kutengeneza sabuni za kufulia za kipande na za maji aina ya *Mafinga Soap* ambacho tayari kimeanza uzalishaji.

(4) Serikali iendelee kuhimiza Halmashauri kubuni vyanzo vipyta vya mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Kamati imebaini kwamba Halmashauri 30 zimeweza kubuni miradi ya kimkakati 38 ambayo iliidhinishiwa jumla ya shilingi billioni 268.4 kwa ajili ya utekelezaji na kuongeza mapato ya ndani. Idadi hiyo ambayo ni sawa na asilimia 16.2 ya Halmashauri zote nchini ni ndogo sana, hivyo juhudhi zaidi zinahitajika ili kusaidia Halmashauri nyingine kubuni miradi ya kimkakati ili ziweze kupatiwa fedha za utekelezaji.

(5) Serikali ihmize Halmashauri kuongeza juhudhi katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwani mwenendo wa ukusanyaji kwa baadhi ya Halmashauri siyo mzuri. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba kwa wastani Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ilikusanya kwa asilimia 57.6 hadi kufikia mwezi Februari, mwaka huu. Mikoa Sita katika hiyo ilifanya vibaya zaidi kwa kukusanya chini ya asilimia 50 ya lengo kama inavyoonekana kwenye Jedwali Na. 07. Aidha, Halmashauri

tatu za Mkoa wa Mtwara ziliongoza kwa makusanyo hafifu ikilinganishwa na Halmashauri zote nchini. Halmashauri hizo ni Masasi, Nanyumbu na Tandahimba ambazo wastani wa makusanyo yao ulikuwa asilimia 11.5. Aidha, Halmashauri nyingine zilizokusanya mapato ya ndani kwa kiwango cha chini ni Nsimbo, Mlele Mkoani Katavi pamoja na Nyasa na Tunduru Mkoani Ruvuma. Kamati inashauri Serikali kuelekeza nguvu katika mikoa hiyo sita kwa lengo la kubaini chanzo cha udhaifu huo katika makusanyo na kutafuta suluhisho.

(6) Serikali iendelee kutenga na kupeleka kikamilifu fedha kwa ajili kukamilisha ujenzi wa maboma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo yamejengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi. Kamati inatambua juhudzi za Serikali katika kutenga fedha za maendeleo. Hata hivyo, changamoto kubwa imekuwa upatikanaji wa fedha hizo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2018/2019 jumla ya shillingi trilliuni 1.7 ziliidhinishwa kwa ajili ya maendeleo. Hadi mwezi Februari, mwaka 2019 takribani robo ya tatu ya mwaka wa fedha ni asilimia 38 tu ya fedha hizo ambayo ilipelekwa kwenye Halmashauri hizo. Hii inaashiria kwamba miradi ya maendeleo itaendelea kusuasua na hivyo kuwacheleweshea wananchi huduma ambazo zingetokana na miradi hiyo. Aidha, hali hiyo inawavunja moyo wananchi katika kushiriki kwenye miradi ya maendeleo.

(7) Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuondoa kodi ya taulo za kike kuitia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018 kwa lengo kuwasaidia watoto wa kike kushiriki kikamilifu katika masomo. Hata hivyo, Kamati inashauri Halmashauri nchini kubuni namna ya kuwasaidia watoto wa kike kutoka familia masikini kupewa taulo hizo bure ili waweze kuhuduria masomo kikamilifu wakati wote. Aidha, Kamati inahimiza ujenzi wa vyumba maalum kwa ajili ya watoto wa kike kujihudumia wanapokuwa katika siku zao. (*Makofii*)

(8) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuanza ujenzi wa Vituo vya Afya 350 na Hospitali za Wilaya 67 katika mwaka unaoisha na kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa Vituo vya Afya na hospitali zaidi katika

mwaka wa fedha ujao. Aidha, Kamati inashauri kwamba pamoja na kujianadaa kuanza ujenzi katika maeneo mapya, Serikali itoe fedha kikamilifu ili kuendeleza na kukamilisha ujenzi wa majengo yaliyoanza ili yakamiliike upesi na wananchi wa maeneo hayo waanze kupata huduma ya matibabu. (*Makofij*)

(9) Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kujenga wodi maalum, Mama Ngojea, 84 katika mikoa 20 kati ya 26 ya Tanzania Bara ili kuwezesha Wajawazito kutoka maeneo ya mbali na huduma hiyo kupata uangalizi wa karibu kutoka kwa Wataalam wa afya hasa wanapokaribia kujifungua. Hatua hiyo itasaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua (*maternity mortality deaths*) ambavyo huchangiwa na kukosa huduma za msingi za afya kama vile upasuaji (*operation*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kujenga wodi hizo katika mikoa iliyosalia ambayo ni Katavi, Tanga, Mtwara, Rukwa, Mara na Dar es Salaam ili kuendelea kueneza huduma hiyo. Aidha, bado idadi hiyo ya wodi ni ndogo. Kwa hiyo, Kamati inashauri angalau tufikie kiwango cha kuwa na wodi hizo za aina hiyo katika kila Halmashauri nchini.

(10) Serikali ihmize Halmashauri nchini kuchangia kikamilifu katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, kwani kiwango cha uchangiaji kiko chini sana na kimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Hadi kufikia mwezi Februari, mwaka huu, Halmashauri zilikuwa zimechangia shilingi milioni 616.7 sawa na asilimia 11 kwa lengo liliowekwa.

(11) Ofisi ya Rais, TAMISEMI isimamie na kuhakikisha Halmashauri ambazo zinadaiwa na Waheshimiwa Madiwani posho stahiki za vikao na za mwezi zinawalipa viongozi hao ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao vizuri. Halmashauri Sita za Mkoa wa Singida zinaongoza kwa kudaiwa na Madiwani ambapo kwa ujumla wake zinadaiwa zaidi ya shilingi milioni 620 na Benki za CRDB na NMB ikiwa ni mikopo ya Madiwani waliyochukua kwa dhamana ya posho zao.

Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni peke yake inadaiwa shilingi milioni 112.1 kati ya kiasi hicho.

(12) Serikali ichukue hatua za makusudi ili kukabili tatizo la upatikanaji wa fedha kidogo za maendeleo kutoka Hazina, kwani unaathiri na kukwamisha kabisa utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi kufikia Februari, mwaka huu asilimia 44 tu ya fedha za maendeleo ndiyo ilikuwa imepokelewa ikilinganishwa na asilimia 50 ya fedha za matumizi ya kawaida iliyopokelewa katika kipindi hicho.

(13) Serikali isaidie Mikoa na Halmashauri nchini kupata majengo ya ofisi, watumishi na vitendea kazi ili kuwezesha watendaji wake kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Mfano, Wakuu wa Wilaya za Mkalama Mkoa wa Singida, Wakurugenzi Halmashauri tano za Mkoa wa Singida, Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama, Wilaya ya Singida, Singida Mji, Halmashauri ya Wilaya ya Iramba na Halmashauri ya Wilaya ya Bukoba katika Mkoa wa Kagera hawana magari, hivyo ni wazi inaathiri utendaji wao.

(14) Kamati inapongeza kazi nzuri iliyotekelizwa na Wakala wa Barabara Vijiji na Mijini (*TARURA*) katika kujenga na kuboresha miundombinu katika maeneo hayo. Hata hivyo, kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Wakala huo ni kidogo sana ikilinganishwa na mtandao wa barabara, zaldi ya kilomita 108,000 inazozihudumia. Kamati inashauri kwamba *TARURA* iongezewe fedha na Serikali. Aidha, mgawo wa fedha wa asilimia 30 ambaao *TARURA* inapewa uongezewe hadi kufikia asilimia 50. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho, napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika, Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu ya kuliendesha Bunge letu Tukufu kwa umakini na ustadi. Aidha, ninawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti hii ambaao umewezesha kukamilisha taarifa hizi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii inashughulikia mafungu mengi ya Bajeti; mafungu 36 na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya uchambuzi, ni wazi katika kipindi hicho Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi. Licha ya mazingira magumu, bado walitekeleza uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, ikiwa ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa namna ya pekee ningetamani sana kuwatambua majina yao, hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda, ninaomba majina yao yaingizwe katika kumbukumbu za *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati napenda kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Mheshimiwa Selemani Saidi Jafo, Mbunge na Naibu Mawaziri wake, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, na Mheshimiwa Waitara Mwita Mwikwabe kwa ushirikiano mkubwa kwa Kamati ambao umesaidia Kamati kuweza kutekeleza shughuli zake. Viongozi hawa ni ni hazina kubwa katika ustawi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na maendeleo ya Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Mhandisi Joseph Nyamuhanga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, akisaidiana na Naibu Makatibu Wakuu Dickson Nzunda na Dkt. Dorothy Gwajima, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa uchambuzi wa Kamati hii. (*Makofii*)

Aidha, shukrani zangu za pekee ziwaendee Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini kwa utendaji wao makini katika utekelezaji wa bajeti ya mwaka unaoisha na kwa uwasilishaji mzuri wa Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai,

Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi wa Huduma za Mambo ya Jumla, Ndugu Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndugu Chacha na Ndugu Eunike, wakisaidiwa na Ndugu Modesta kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile, nawashukuru watumishi wote wa Idara ya *Hansard* wakiongozwa na Bi Hanifa Masaninga kwa kuandaa na kutoa Taarifa hii ya vitabu hivi kwa wakati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kama yalivyowasilishwa na Mtoha hoja hapo awali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. (*Makofii*)

TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Kwa mujibu wa Kifungu cha 6(4) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 Kamati hii imepewa jukumu la kuisimamia Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora (OR - UUB) pamoja na Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR - TAMISEMI). Aidha, Kifungu cha 7(1) (a), kinaipa Kamati jukumu mahususi la kushughulikia Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Mheshimiwa Spika, Kamati ilizingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kwa kufanya ziara ya kukagua miradi ya maendeleo iliyotekelawa na Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha unaoisha.

Kamati ilitekeleza jukumu hilo kwa siku zisizozidi saba (7), kabla ya kuanza uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Taarifa hii inahusisha mapitio na uchambuzi wa jumla ya mafungu ishirini na nane (28) yafuatayo: -

- i. Fungu 56 - Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa;
- ii. Fungu 02 - Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC);
- iii. Fungu 36 – Mkoa wa Katavi;
- iv. Fungu 47 – Mkoa wa Simiyu;
- v. Fungu 54 – Mkoa wa Njombe;
- vi. Fungu 63 – Mkoa wa Geita;
- vii. Fungu 70 – Mkoa wa Arusha;
- viii. Fungu 71 – Mkoa wa Pwani;
- ix. Fungu 72 – Mkoa wa Dodoma;
- x. Fungu 73 – Mkoa wa Iringa;
- xi. Fungu 74 – Mkoa wa Kigoma;
- xii. Fungu 75 – Mkoa wa Kilimanjaro;
- xiii. Fungu 76 – Mkoa wa Lindi;
- xiv. Fungu 77 – Mkoa wa Mara;
- xv. Fungu 78 – Mkoa wa Mbeya;
- xvi. Fungu 79 - Mkoa wa Morogoro;
- xvii. Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara;

- xviii. Fungu 81 – Mkoa wa Mwanza;
- xix. Fungu 82 – Mkoa wa Ruvuma;
- xx. Fungu 83 – Mkoa wa Shinyanga;
- xxi. Fungu 84 – Mkoa wa Singida;
- xxii. Fungu 85 – Mkoa wa Tabora;
- xxiii. Fungu 86 – Mkoa wa Tanga;
- xxiv. Fungu 87 – Mkoa wa Kagera;
- xxv. Fungu 88 – Mkoa wa Dar es Salaam;
- xxvi. Fungu 89 – Mkoa wa Rukwa;
- xxvii. Fungu 90 – Mkoa wa Songwe; na
- xxviii. Fungu 95 – Mkoa wa Manyara.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya utekelezaji wa Bajeti kwa mwaka wa fedha unaoisha pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya bajeti kwa mwaka wa fedha unaoanza, ulifanyika kuanzia tarehe 20 hadi 29 Machi, 2019. Taarifa hii ya Kamati kuhusu Ofisi ya Rais – TAMISEMI inajikita katika maeneo manne (4) yafuatayo: -

- i) Matokeo ya Ugaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa fedha 2019/2020; na
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kamati hii ndiyo yenye dhamana ya kuisimamia Serikali katika masuala ya Serikali za Mitaa, nigosie kidogo kuhusu dhana ya ugatuvi wa madaraka au upelekaji wa madaraka kwa wananchi (*Devolution by Decentralization – D by D*) ambayo msingi wake ni Ibara ya 145 na 146 za Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977.


Ibara ya 146 (1) inasisitiza kwamba, vyombo vya serikali za mitaa (Halmashauri, Kata, Vijiji, Mitaa na Vitongoji) vitakuwa na haki na mamlaka ya kuwashirikisha wananchi katika

mipango na shughuli za utekelezaji wa maendeleo katika sehemu zao na nchini kote kwa ujumla.

Utekelezaji wa dhana hiyo ya kikatiba kupitia sera iliyotungwa mwaka 1998 umekuwa na manufaa kadhaa ikiwa ni pamoja na kusogezwa kwa huduma karibu na wananchi, na ushiriki wa wananchi katika kutathmini, kupanga, kuamua na kutekeleza mipango mbalimbali kwa kuzingatia matatizo yanayowakabili kwa kutumia mbinu ya fursa na vikwazo kwa maendeleo.

Ni kwa mantiki hiyo wananchi kwa nguvu zao na uungwaji mkono wa Serikali wamefanikiwa kujenga shule za msingi, shule za sekondari za kata, zahanati, vituo vya afya, hospitali za wilaya, miradi ya maji, uhifadhi endelevu wa misitu, n.k

Mheshimiwa Spika, Kamati inapongeza juhudzi za Serikali za kuunga mkono nguvu za wananchi, na inashauri iendelee kujikita katika kujenga mfumo imara wa kumhudumia mwananchi ambao utazingatia misingi ya upelekaji wa madaraka kwa wananchi ambao Ibara ya 8(a) ya Katiba inawataja kuwa wao ndiyo msingi wa madaraka yote na Serikali itapata madaraka na mamlaka yake yote kutoka kwa wananchi. Aidha, Serikali ihakikishe inagatua rasilimali fedha za kutosha na kuzipeleka kikamilifu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji unafanyika ili kuziwezesha mamlaka hizo kutimiza wajibu wake kwa wananchi.



Ufunguo:

- Mchoro **A** :- Mamlaka na utoaji wa huduma vinahodhiwa sehemu moja (hakuna ugatuzi wa madaraka);
- Mchoro **B**:- Mamlaka na utoaji wa huduma vimekasimiwa katika maeneo mbalimbali (kuna ugatuzi wa madaraka).

2.0 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA NA KUTEKELEZWA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

2.1 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, illidhinishiwa na Bunge jumla ya **Shilingi 1,799,436,057,500** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Ili kuzingatia Kanuni ya 98 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotekelawa na Ofisi hii katika mwaka wa fedha 2018/2019. Miradi iliyotembelewa ni pamoja na, Mpango wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati (*Tanzania Strategic Cities Programme -TSCP*), Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) na Mfuko wa Maendeleo wa Wanawake, Vijana na Watu wenye Ulemavu (Asilimia 10 ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri), kama ifuatavyo: -

2.1.1 Mradi Na. 6403 Mpango wa Uendelezaji wa Miji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)

Mheshimiwa Spika, usimamizi wa mradi huu uko chini ya Kifungu 1009 "Infrastructure Development Division "chini ya Fungu 56 – Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Mradi huu unagharamiwa na fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia na ruzuku kutoka Serikali ya Denmark na utekelezaji uko katika awamu ya pili. Awamu ya kwanza ilianza mwaka

wa fedha 2010/2011 hadi 2015/2016 kwa jumla ya Dola za Marekani milioni 225.7, na awamu ya pili ilianza mwaka wa fedha 2017/2018 na itaendelea hadi katika maka wa fedha 2020 kwa gharama ya Dola za Marekani milioni 130.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu katika Manispaa ya Mtwara Mikindani ambako unaotekelzeza chini ya Kifungu 8091, Fungu 80 – Mkoa wa Mtwara. Mradi unahusisha uboreshaji wa miundombinu ya huduma za mijii na uimarishaji wa mifumo ya halmashauri katika kutoa huduma bora kwa jamii.

Katika uboreshaji wa miundombinu ya huduma za mijii, barabara zenyе urefu wa kilomita 15.78 zimejengwa kwa kiwango cha lami kwa jumla ya **shilingi bilioni 24.01**. Barabara hizo ni Bandari (kilomita 2.75), Zambia (kilomita 3.75), Mikindani (kilomita 1.9), Chuno (kilomita 5.78) na Kunambi (kilomita 1.6).

Aidha, ujenzi wa dampo la kisasa na vizimba 25 vya kukusanya taka, pamoja na ununuzi wa mitambo na vifaa vya kusafirisha taka kutoka kwenye vizimba hadi dambo viligharimu jumla ya **shilingi bilioni 4.96**.

Mheshimiwa Spika, kutohana na ufanisi mkubwa katika utekelezaji wa awamu ya kwanza ya miradi hiyo, Manispaa ya Mtwara Mikindani ilipata nyongeza ya **shilingi bilioni 8.8** ambazo zimefanikisha shughuli kadhaa ikiwa ni pamoja na ujenzi wa mifereji ya maji yenye urefu wa kilomita 7.4, maegesho ya magari katika dampo, mizani ya kupimia taka, na uwekaji wa taa za nishati ya jua katika barabara ya Chuno.

Aidha, jumla ya **shilingi bilioni 21.68** zitatumika katika awamu ya pili ya mpango kwa kujenga barabara (kilomita 4.1), mfereji wa kupeleka maji baharini (kilomita 3.4), kuboresha maeneo ya wazi, maduka makubwa, stendi ya dalada ya Mikindani, na ujenzi wa soko la kisasa la Chuno. Kazi hizo zinatekelezwa na Mkandarasi M/s Jiangxi Geo Engineering Group ya nchini China, chini ya usimamizi wa mradi unafanywa na Kampuni ya LEA International ya Canada.

2.1.2 Mradi Na. 4946 - Local Government Authority Own Source Projects "Uwezesaji Kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyе Ulemavu"

Mheshimiwa Spika, mradi huu ilitengewa jumla ya **shilingi bilioni 3.01** na ulipangwa kutekelezwa chini ya **Fungu 80** - Mkoa wa Mtwara. Mradi huu ni sehemu ya mkakati wa Serikali ya Awamu ya Tano wa kuwawezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyе Ulemavu kupitia asilimia (10%) ya mapato ya ndani ya kila Halmashauri nchini.

Kupitia utaratibu huu ambao unatekelezwa kwa mujibu wa Sheria ya Fedha ya Serikali za Mitaa (Sura 290) ambayo ilifanyiwa marekebisho na Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018, makundi hayo ya kijamii yanawezeshwa kupata mafunzo na mitaji ya kutekeleza shughuli za kiuchumi kwa lengo la kujikwamua dhidi ya umaskini. Hadi Desemba, 2018 jumla ya vikundi 1,213 kutoka makundi hayo, vilikuwa vimenufaika na kiasi hicho cha fedha kilichotengwa.

Kamati ilitaka kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mfuko huu na hivyo ilitembelea Vikundi vitatu ambavyo ni Tunalekane Women Group (Wanawake); Tuvamo Group (Vijana) na Wajibu Group (Watu wenyе Ulemavu) katika Manispaa ya Mtwara Mikindani.

2.1.3 Kikundi cha Wanawake cha Tunalekane (Tunalekane Women Group)

Mheshimiwa Spika, kikundi hiki chenye wanachama watano (5) kilianzishwa mwaka 2012 na kinajishughulisha na kutoa mafunzo ya utengenezaji wa sabuni za maji na vipande, mafuta ya mgando na batiki kwa wajasiriamali wengine. Aidha, kinafuga kuku, kupika vyakula kwenye sherehe na kuuza vifaa nya utengenezaji wa sabuni na batiki.

Tangu kuanzishwa kikundi hiki kimeishapata mikopo yenye thamani ya **shilingi milioni 12** kwa awamu tatu na kupokea mafunzo ya ujasiriamali kutoka Manispaa ya Mtwara Mikindani, ambavyo vimeweza wanakikundi kujikwamua

kiuchumi wao pamoja na familia zao. Aidha, kikundi kimeanzisha ufugaji wa kuku wa kienyeji, upishi wa chakula kwenye sherehe na kutoa mafunzo kwa wajasiriamali zaidi ya 670 katika mikoa ya Mbeya na Mtwara.

Kupitia kipato wanachopata, wanakikundi hao wamemudu kucomesha watoto, kupata mahitaji ya nyumbani na pia mtaji kwa kila mwanachama ili kuendesha shughuli za kiuchumi nje ya kikundi.

2.1.4 Kikundi cha Vijana cha Tuvamo (Tuvamo Group)

Mheshimiwa Spika, kikundi hiki kilianzishwa mwaka 2016 na kina jumla ya vijana watano (5) wa kiume ambao waliamua kujinga pamoja na kuanzisha shughuli ya kutengeneza na kuza samani, kukarabati majengo (upauaji, kufunga jipsum) na kukopesha wanachama kwa hiyari.

Kikundi kilianza kwa mtaji wa **shilingi 2,000,000/=** na sasa kina mtaji unaofikia **shilingi 14,000,000** kutokana na mkopo uliotolewa kwa kikundi hiki mwaka 2018 kupitia Mfuko wa kuwezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyе Ulemavu.

Kuptia miradi hii kikundi kimeweza kutoa ajira kwa vijana wanne (4) ambao ni mafundi; kuongeza uzalishaji wa samani na hivyo kukuza kipato cha kila mwanakikundi sambamba na kuchangia mapato ya Serikali kwa kulipa kodi.

2.1.5 Kikundi cha Watu wenyе Ulemavu cha Wajibu (Wajibu Disabled Group)

Mheshimiwa Spika, kikundi cha Wajibu ni kikundi cha watu wenyе ulemavu, kinachooundwa na wanachama watano (5) wanaume watatu na wanawake wawili. Kikundi hiki kilichoanzishwa mwaka 2018 kinajishughulisha na Uchomeleaji (welding), Ushonaji (tailoring) na Biashara ndogondogo sokoni.

Kikundi kilianza shughuli zake kwa mkopo usio na riba kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya Halmashauri

ya Manispaa ya Mtwara Mikindani, wa **shilingi milioni 4.7** na kimekuwa kikitekeleza shughuli zake kwa ufanisi ambapo hadi sasa kimeisharejesha **shilingi 558, 000** na lengo ni kuhakikisha fedha zinarejeshwa ndani ya muda uliowekwa.

Shughuli za kikundi zimewezesha wanachama wake kujimudu kiuchumi kwa kupata mahitaji muhimu ya chakula, matibabu, mavazi; kusaidia kuondoa hali ya unyanyapaa kwa wanachama kutokana na ulemavu walio nao.

2.1.6 Wakala wa Barabara za Vijiji na Mijini Tanzania (TARURA)

Mheshimiwa Spika, Wakala huu ulianzishwa kwa mujibu wa Sheria ya Wakala za Serikali, Sura 245 na kuanza kutekeleza majukumu yake tarehe 2 Julai, 2017. Kuanzishwa kwa wakala huu ni muendelezo wa utekelezaji wa mabadiliko (*reforms*) kwenye sekta ya ujenzi na barabara yaliyoanza mwaka 1998 ambayo ni pamoja na marekebisho ya Road Tolls Act, kuanzishwa kwa Mfuko wa Barabara (RF), TANROADS na sasa TARURA.

TARURA ambayo inahudumia mtandao wa barabara wenye jumla ya kilomita 108,946 nchi nzima ina majukumu makubwa ya ujenzi, ukarabati na matengenezo ya barabara za Vijiji na Mijini pamoja na madaraja na mpango mkakati wa kuondoa vikwanzo ili barabara ziweze kuitika muda wote. Aidha, TARURA inatarajiwa kuimarisha barabara zinazopita kwenye maeneo muhimu yenye viwanda na kilimo na hivyo kusaidia shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhidha na utekelezaji wa shughuli za TARURA Kamati ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Lindi, Mkoani Lindi ambapo Wakala inahudumia barabara zenye urefu wa kilomita 693.1 ambazo zimeingizwa kwenye mfumo wa usimamizi na ufuatiliaji wa barabara (DROMAS). Barabara zilizokaguliwa na Kamati ni kipande cha Nyengendi (1km) kinachojengwa kwa kiwango cha lami ambacho ni sehemu ya barabara ya Nyengendi – Mnara – Rutamba yenye urefu wa kilomita 48, na kipande cha Nyangao kituo cha Mabasi –

Nyangao Hospitali (0.8 km) ambacho ni sehemu ya barabara ya Nyangao – Namupa – Mihima yenyewe urefu wa kilomita 23.2

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa kipande cha Nyengendi unatekelezwa na Nyumbani Construction Company Ltd. kwa gharama ya **shilingi milioni 302.02** na utekelezaji umefikia asilimia 32. Inatarajiwa kwamba, kukamilika kwa kipande hiki cha barabara kutarahisisha huduma ya usafiri kutoka barabara kuu ya Lindi – Mtwara kwenda eneo la Rondo ambako kuna Msitu wa Hifadhi ya Taifa na hivyo kuchache shughuli za utalii.

Aidha, ujenzi wa kipande cha Nyangao kituo cha Mabasi – Nyangao Hospitali pia unatekelezwa na Nyumbani Construction kwa gharama ya **shilingi milioni 229.91** na umefikia asilimia 45 ya utekelezaji. Inatarajiwa kwamba, kukamilika kwa kipande hiki kutarahisisha usafiri kwa wakazi wa Kata za Nyangao na Namupa, kutoka barabara kuu ya Lindi – Masasi kwenda Hospitali teule ya Wilaya (Nyangao – DDH) kupata huduma za matibabu.

2.2 Matokeo ya Ukaguzi

Mheshimiwa Spika, kutohana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo hiyo inayotekelizwa na Ofisi ya Rais - TAMISEMI katika mwaka wa fedha 2018/2019, naomba kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tufuku kuhusu mambo ambayo Kamati iliyabaini kama ifuatavyo: -

2.2.1 Mradi Na. 6403 - Mpango wa Uendelezaji wa Mji ya Kimkakati Tanzania (TSCP)

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani ambako Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa mradi huu wa kuimarisha miundombini, mambo yafuatayo yalibainika: -

a) Mafanikio;

- i) Kuongezeka kwa kilomita 18.8 za lami katika Mji wa Mtwara na kuufanya kuwa na barabara zenyewe jumla ya urefu wa kilomita 43.5;

- ii) Kuimarika kwa usalama wa mji kutokana na uwepo wa taa za barabarani;
- iii) Kuongezeka kwa usafi wa mji kutokana na utaratibu wa usafishaji na usafirishaji wa taka kwenda kwenye dampo la kisasa, jambo ambalo limepunguza magonjwa ya mlipuko;
- iv) Kuongezeka kwa biashara na uwekezaji katika maeneo ya mji kutokana na wananchi kufanya biashara nyakati za usiku;
- v) Kuongezeka thamani ya ardhi na pango la nyumba na maeneo ya biashara na makazi yaliyo jirani na barabara zinazojengwa;
- vi) Kupungua kwa mafuriko katika maeneo ya Skoya – Nabwada – Shakuru – Mtepwezi kutokana na ujenzi wa mifereji yenye urefu wa kilomita 3.1; na
- vii) Kuongezeka kwa mapato kutokana na kodi ya leseni kwa watu wanaofanya biashara katika maeneo ya kupumzikia (public parks) na michezo kwa watoto.

b) Changamoto;

- i) Kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa mfereji mkuu wa kupeleka maji baharini kutokana na kuchelewa kuhamishwa kwa miundombinu ya huduma za jamii;
- ii) Kasi ndogo ya ujenzi wa barabara zilizo katika mradi kutokana na msimu wa mvua;
- iii) Kuchelewa kuanza kwa ujenzi wa stendi ya daladala ya Mikindani kutokana na kuchelewa kukamilika kwa zoezi la ulipaji fidia kwa wananchi waliohama ili kupisha mradi; na
- iv) Mabadiliko ya michoro katika mradi wa uboreshaji maeneo ya wazi na ujenzi wa soko la kisasa la Chuno.

2.2.2 Mradi Na. 4946 - Local Government Own Source Projects. (Uwezeshaji Kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyе Ulemavu)

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa Kamati katika mradi katika Manispaa ya Mtwara Mikindani, ulibaini mambo kadhaa ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto kama ifuatavyo: -

(a) Mafanikio:

- i. Ajira imepatikana kwa Wanawake, Vijana na Watu wenyе Ulemavu ambao ni wanachama wa vikundi viliviyotembelewa na Kamati;
- ii. Kuongezeka kwa mapato ya Manispaa kutokana na vikundi vyote vitatu (3) kuchangia mapato kwa kulipa kodi stahiki kutokana na miradi yao;
- iii. Wanavikundi wamewezeshwa kumudu maisha kutokana na kipato wanachokipata katika miradi wanayoitekeleza;
- iv. Watu wenyе Ulemavu wamepata fursa ya kuidhihirishia jamii kwamba, pale wanapowezeshwa wanaweza kutoa mchango wao katika jamii. Mfano ni Kijana Hamza Ndambilo ambaye ana ulemavu wa kusikia (Bubu) lakini ameweza kubuni na kutengeneza vitu kutokana na ujuzi wa kuchomelea "*welding skills*" ambao anao. Aidha, mafundi wa nguo nao wameweza buni na kushona nguo, licha ya ulemavu walio nao; na
- v. Wanavikundi hasa wa Tunalekane wametumia ujuzi wao kutoa mafunzo kwa Wasiriamali zaidi ya 670 katika mikoa ya Mbeya na Mtwara.

(b) Changamoto:

- i. Wateja wanaokopa bidhaa zinazozalishwa na vikundi kushindwa kulipa madeni yao kwa wakati;

- ii. Ukosefu wa masoko ya uhakika kwa biadhaa zinazozalishwa na vikundi. Mfano ni samani zinazozalishwa na kikundi cha Tuvamo ambazo wakati mwingine zinalazimika kukaa muda mrefu zikisubiri wateja;
- iii. Kukosekana kwa malighafi ya kutengeneza batiki mkoani Mtwara, na hivyo kikundi cha Tunalekane kulazimika kuzifuata mkoani Dar es Salaam;
- iv. Muda wa mwaka mmoja uliotengwa kwa ajili ya urejeshaji wa mkopo ni mfupi sana hasa kwa kuzingatia kwamba, mzunguko wa fedha ni mdogo hivyo biashara haziendi kwa haraka; na
- v. Kukosekana kwa elimu ya ujasiriamali jambo linalowasababisha wanavikundi kushindwa kukuza miradi yao kutokana na kukosa ujuzi wa kubuni, kuanzisha na kuendeleza.

2.2.3 Wakala wa Barabara za Vijijiini na Mijini Tanzania (TARURA)

Mheshimiwa Spika, ukaguzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa shughuli za TARURA katika Halmashauri ya Wilaya ya Lindi ulibaini mafanikio na changamoto kama ifuatavyo: -

Mafanikio;

- i. Kurahisisha usafiri wa kutoka barabara kuu ya Lindi – Masasi kwenda katika Hospitali Teule ya Wilaya (Nyangao DDH) kwa ajili ya kupata huduma za matibabu;
- ii. Kukamilika kwa vipande vinavyotengenezwa kwa kiwango cha lami kutapunguza gharama za matengenezo katika barabara hizo ambazo zinahudumia jumla ya Kata Sita;

- iii. Kuongezeka kwa thamani ya maeneo ya ardhi yaliyo jirani na barabara zinazojengwa kwa kiwango cha lami; na
- iv. Kurahisisha usafiri kutoka barabara kuu ya Lindi – Masasi kwenda eneo la Msitu wa Hifadhi ya Taifa wa Rondo na hivyo kuchochaea shughuli za kitalii.

(a) Changamoto;

- i. Ufinyu wa bajeti kwa ajili ya matengenezo ya barabara ikilinganishwa na mahitaji halisi ya matengenezo;
- ii. Kukosekana kwa usafiri wa uhakika utakaowezesha kufuatilia na kusimamia ujenzi wa barabara kutokana na gari liliopo kuwa chakavu kiasi cha kutotengenezeka;
- iii. Upungufu wa wataalam wa ujenzi. Ofisi ya Meneja wa TARURA katika Halmashauri ya Lindi ina watumishi Wahandisi watatu (3) na Fundi Sanifu mmoja (1) ambao ni wachache; na
- iv. Kuchelewa kwa utekelezaji wa kazi za ujenzi kutokana na msimu wa mvua;

2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, kutokana na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika mikoa ya Lindi na Mtwara, Kamati iliweza kubaini mambo mbalimbali na ingependa kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

- i. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) unahitaji kuongezewa fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya barabara kutokana na kuwa na mtandao mkubwa wa barabara;
- ii. Hazina itoe fedha za miradi ya maendeleo kwa wakati ili kutoathiri utekelezaji wa miradi iliyopangwa na hivyo kuendelea kuwakosesha wananchi huduma zilizokusudiwa;

- iii. Kukosekana kwa programu endelevu ya elimu ya ujasiriamali na uwezeshaji kwa Wanawake, Vijana na Watu wenyе Ulemavu, kunasababisha vikundi vingi vinavyopatiwa mikopo kushindwa kuendeleza na kukuza miradi ilioanzishwa;
- iv. Urasimu (*cumbersome procedures*) usio wa lazima Serikalini umeendelea kuchelewesha utekelezaji wa miradi. Mfano, utaratibu wa watoa huduma na wakandarasi kuwasilisha madai kwa njia ya cheti (*certificates*) umekuwa ukichelewesha malipo na hivyo kukwamisha utekelezaji wa miradi;
- v. Kukosa umakini katika usanifu wa awali (*feasibility study*) wa miradi ya maendeleo kunaathiri utekelezaji na hivyo kuongeza gharama kutokana na kubadilisha michoro;
- vi. Hatua ya Mfuko wa kuwezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyе ulemavu kutungiwa sheria (Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290) ambayo ilifanyiwa marekebisho na Sheria ya Fedha ya Mwaka, 2018 kutafanya uratibu na usimamizi wa mfuko huo kuwa na nguvu ya kisheria;
- vii. Muda wa mwaka mmoja uliotengwa kwa ajili ya Vikundi vinavyopata fedha kutoka Mfuko wa kuwezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyе Ulemavu (10% ya Mapato ya ndani ya Halmashauri) kurejesha fedha hizo ni mfupi; hivyo uangaliwe uwezekano wa kutoa muda zaidi.

3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

3.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo na mwenendo wa

upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zilizopangwa kutekelezwa.

Njia kubwa zilizotumika katika uchambuzi huu ni kwa kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati, pamoja na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

Kwa ufanuzi wa ziada kuhusu uchambuzi huu, Kamati imetumia majedwali ili kurahisisha maelezo yake wakati wa kuonesha taarifa, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji.

3.1.1 Uchambuzi wa Taarifa kuhusu ukusanyaji Maduhuli

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI (Fungu 56) pamoja na Taasisi zilizo chini yake (LGTI, KEC, DART na LGLB) ilipanga kukusanya jumla ya **Shilingi 22,643,519,061** kutoka vyanzo vya ndani. Mapato hayo yanatokana na kuuza vifaa chakavu na zabuni kwa upande wa makao makuu (Fungu 56) na ada za wanafunzi, ukusanyaji wa madeni, tozo, ushuru na mauzo ya bidhaa mbalimbali kwa upande wa taasisi.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 kiasi cha **Shilingi 9,848,994,774.41** kilikuwa kimekusanywa, sawa na **asilimia 44** ya malengo yaliyowekwa. Kamati ilitaka kujua ni kwanini kumekuwa na makusanyo hafifu ya maduhuli, na sababu zilizotolewa ni pamoja na:-

- i. Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa (LGLB) kushindwa kupata **shilingi bilioni 1.2** ilizotarajia kutoka Benki ya CRDB;
- ii. Baadhi ya Halmashauri kushindwa kuwasilisha michango yao kwenye Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; na
- iii. Mauzo hafifu ya nyaraka za zabuni na vifaa chakavu;

Mheshimiwa Spika, uchambuzi unaonesha kwamba, kiasi kilichokusanywa kimeongezeka kwa asilimia 0.3 ikilinganishwa

na asilimia 43.7 iliyoshuhudiwa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Ingawa kiwango kilichokusanya kiko chini ya asilimia 70 iliyopaswa kuwa imefikiwa katika robo ya tatu, bado ni kikubwa hasa kwa kuzingatia kwamba malengo yaliyowekwa yalikuwa makubwa zaidi ikilinganishwa na malengo ya mwaka wa fedha uliotangulia.

Aidha, uchambuzi umebaini kwamba, makusanyo yamekuwa yakiongezeka katika kipindi cha miaka mitatu ya fedha (2016/17, 2017/18 na 2018/19).

Kwa mtazamo wa Kamati ni vigumu kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato kwa kipindi kilichosalia, na hivyo upo uwezekano wa kutetereka kwa shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa fedha za ndani.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mikoa hadi kufikia mwezi Februari, 2019 makusanyo yalikuwa ni **shilingi 139,059, 708**, kiasi ambacho ni sawa na asilimia 85 ya lengo liliowekwa.

Aidha, Halmashauri ziliidhinishiwa kukusanya **shilingi 735,588,629,000** na hadi kufikiwa mwezi Februari, 2019 zilikuwa zimekusanya asilimia 53 ya lengo.

Wastani wa makusanyo katika Mikoa na Serikali za Mitaa katika kipindi hicho ulifikia asilimia 69, kiwango ambacho kinapaswa kuwa kimefikiwa katika kipindi kama hicho cha mwaka wa bajeti.

Bado kiasi cha ukusanyaji katika Halmashauri kimeendelea kuwa kikubwa ikilinganishwa na maeneo mengine kutokana na ukweli kwamba, huko ndiko kwenye watu wengi na vyanzo vingi vya mapato ikilinganishwa na mikoa na makao makuu (Fungu 56) pamoja na taasisi zake.

3.1.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI umebaini kwamba,

hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako

Tukufu kwa mwaka wa fedha 2018/19 na kiasi kinachotolewa na Hazina.

Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba: -

- i. Fedha zinazotolewa zimeendelea kupungua kwa mwaka wa tatu mfululizo; mwaka wa fedha 2016/17 (asilimia 57), mwaka wa fedha 2017/18 (asilimia 53) na mwaka wa fedha 2018/19 (asilimia 45.2);
- ii. Fedha zinazotolewa ni kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa fedha (*cash flow plan*) uliowekwa;
- iii. Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa wingi ikilinganishwa na matumizi ya maendeleo; na
- iv. Fedha hazitolewi kwa wakati, jambo linaloathiri utekelezaji wa mipango ya bajeti kwa Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulibaini kuwa, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Ofisi ya Rais – TAMISEMI pamoja na Taasisi zilizo chini yake, ilikuwa imepokea **Shilingi 181,733,988,946.36/=** kutoka Hazina kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 45.2** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Ofisi hii. Mwenendo wa upatikanaji wa fedha unaonesha kwamba, kiasi hicho kilichopatikana katika kipindi hicho kimepungua kwa takribani asilimia 7.8 ikilinganishwa na kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambapo ilikuwa ni asilimia 53.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida hadi kufikia Februari, 2019 ofisi hiyo na taasisi zake ilikuwa imepokea **shilingi 21,749,442,225.51**, sawa na asilimia 50.6 ya fedha iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimepungua kwa asilimia 18.4 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/18.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2019, Ofisi ya Rais - TAMISEMI na taasisi zake ilikuwa imepokea kutoka Hazina jumla ya **shilingi 159,984,546,720.00**, sawa na asilimia 44.5 ya fedha yote iliyoidhinishwa. Kiasi hicho kimepungua kwa asilimia 7.5 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho mwaka wa fedha 2017/18.

Mheshimiwa Spika, Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu Na.02) katika mwaka wa fedha 2018/19 iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 12,515, 260,000/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida. Kati ya fedha hizo, **shilingi 7,893,118,000/=** ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi 4,622,142,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Tume ilikuwa imepokea **shilingi 5,663,988,000/=** sawa na asilimia 45 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha zilizopokelewa **shilingi 3,649,225,000/=** ni kwa ajili ya mishahara, na **shilingi 2,014,763,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, katika mwaka wa fedha 2018/19 ziliidhinishiwa bajeti ya **shilingi 5,888,072,708,500/=** kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya fedha hizo **shilingi 3,942,713,089,000/=** ni kwa ajili ya mishahara, **shilingi 580,252,615,000/=** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo na shilingi **1,365,107,004,000/=** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 fedha za matumizi ya kawaida zilikuwa zimepokelewa kwa asilimia 57, wakati fedha za maendeleo zilikuwa zimepokelewa kwa asilimia 38.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa kina wa Kamati umebaini kwamba kwa wastani upatikanaji wa fedha (Matumizi ya Kawaida na Maendeleo) kwa Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Taasisi zake katika mwaka wa fedha 2018/19 ulikuwa ni **asilimia 47.55**, kiwango ambacho kimepungua sana ikilinganishwa na wastani wa **asilimia 60.5** katika miaka miwili ya fedha iliyopita (2016/17 na 2017/18).

Kwa tafsiri ya kawaida ni kwamba, badala ya upatikanaji wa fedha kuongezeka ili kufikia lengo la angalau asilimia 25 kwa kila robo katika mwaka fedha, sasa wastani umeshuka hadi kufikia asilimia 15 kwa robo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mamlaka za Serikali za Mitaa, uchambuzi umebaini kwamba, wastani wa upatikanaji wa fedha ulikuwa ni kwa asilimia 47.5. Aidha, bado fedha za matumizi ya kawaida zimeendelea kupatikana kwa kiwango cha juu ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Hii inaashiria kwamba utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaendelea kusuasua kutokana na fedha kucheleweshwa na kutolewa kwa kiasi kidogo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilifanya ulinganisho wa uwiano wa kiasi cha fedha kilichoidhinishwa kwa ajili ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamkala za Serikali za Mitaa na kiasi kilichopatikana hadi kufikia mwezi Februari, 2019, kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida (Mishahara na Matumizi Mengineyo) na Miradi ya Maendeleo. Ufanuzi zaidi kwa baadhi ya maeneo hayo umeoneshwa kuititia **Jedwali Na. 01 & Jedwali**

Mgawanyo wa Bajeti	Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2018/19	Kiasi Kilichopokelewa hadi Februari, 2019	Asilimia ya Kiasi kilichopokelewa hadi Februari, 2019
OC	19,215,401,095	6,497,806,480.15	33.7
Mshahara	23,652,841,905.00	15,251,635,745.36	64.48
Maendeleo	345,113,541,000.00	159,984,546,720.00	44.5
Jumla	387,981,784,000.00	181,733,988,946.00	53

Jedwali Na.02: Bajeti iliyoidhinishwa kwa Mamlaka za Serikali za Mitaa ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana hadi Februari, 2019

Chanzo Jedwali Na 01 & 02: Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI Mwaka wa Fedha 2019/2020.

3.1.3 Mapito ya Utekelezaji wa Ushauri wa Kamati

Mheshimiwa Spika, katika uchambuzi na mapitio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Kamati ilitoa maoni na ushauri wa mambo kumi (10) ili ofisi hii iweze kuyazingatia katika utekelezaji wa vipaumbele vya bajeti ili kuleta ufanisi na tija;

Mheshimiwa Spika, napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa baada ya kupitia majibu yaliyowasilishwa na Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Kamati imeridhishwa na jitihada zilizooneshwa katika kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati kwa kutatua changamoto zillizobainishwa. Uzingatiaji wa maoni na ushauri wa Kamati umechangia uboreshaji wa huduma za msingi kwa maendeleo ya jamii.

Hata hivyo, bado Kamati inaitaka Serikali kuendelea kufanyia kazi maoni na ushauri kwa baadhi ya maeneo yaliyosalia ili kuendelea kuboresha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

Mheshimiwa Spika, baadhi ya maeneo ambayo yameboreshwa kwa kuzingatia ushauri na maoni ya Kamati ni pamoja na: -

- i. Serikali iwasilishe Bungeni Muswada wa Sheria utakaowezesha kusimamia kikamilifu asilimia kumi (10) ya mapato ya ndani ya Halmashauri kwa ajili ya kuwezesha kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu, ambapo Sheria ya kusimamia Mikopo ya Uwezeshaji Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu imetungwa kupitia Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, Sura 290 iliyofanyiwa marekebisho kwa kuongeza kifungu cha 37 A, na sheria hiyo ilianza kutumika Julai, 2018. Aidha, maandalizi ya Kanuni za utekelezaji wa Sheria hiyo yako katika hatua za mwisho za ukamilishaji;
- ii. Serikalia iangalie uwezekano wa kupunguza au kuondoa kabisa kodi ya taulo za kike ili kuwezesha watoto wa kike hasa kutoka familia maskini kumudu gharama ya taulo hizo na kuweza kuhudhuria masomo kikamilifu, ambapo Serikali imeondoa kodi ya taulo za kike kupitia marekebisho yaliyofanyika katika Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018; na
- iii. Halmashauri ziendelee kubuni vyanzo vipyta vya mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu, ambapo Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango imebuni miradi ya kimkakati ili kuziwezesha Halmashauri kuongeza mapato ya ndani. Hadi kufikia Februari, 2019 Halmashauri 30 zimekidhi vigezo vya miradi 38 ambayo iliidhinishiwa **shilingi bilioni 268.4**;

Mheshimiwa Spika, licha ya baadhi ya maoni kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyaboresha zaidi ili kuleta ufanisi katika utendaji. Maoni hayo ni pamoja na: -

- i. Kuhakikisha Halmashauri zinatenga kikamilifu fedha za asilimia Kumi (10%) ya Mapato ya Ndani ya Halmashauri na kuzipeleka kwenye Vikundi vya Wanawake, Vijana na Watu wenyewe ulemavu. Aidha, Halmashauri ziandae na kutunza takwimu sahihi kuhusiana na idadi ya vikundi vilivyopokea pesa, na kusimamia urejeshaji wa fedha hizo;

- ii. Serikali iendelee kutoa fedha kwa ajili ya kukamilisha ujenzi wa maboma katika halmashauri nchini ambayo yalijengwa kwa kushirikisha nguvu za wananchi. Ni muhimu kukamilisha majengo hayo ili kutowakatisha tamaa wananchi katika kushiriki kazi za maendeleo. Serikali iliidhinisha **shilingi trilioni 1.36** kwa ajili ya miradi ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, lakini hadi Desemba, 2018 ni asilimia 38 tu ya fedha hizo ndiyo ilikuwa imetolewa. Hii inaashiria kwamba, ukamilishaji wa miradi ikiwa ni pamoja na maboma utaendelea kusuasua; na
- iii. Serikali iendelee kusaidia mikoa mipya na Halmashauri nchini kupata majengo ya ofisi, watumishi na vitendea kazi na kuboresha miundombinu ya barabara ili lengo la kuanzishwa kwa maeneo hayo mapya liveze kutimia. Kamati inatambua hili linatekelezwa kwa kadri fedha zinavyopatikana, ambapo mwaka 2018/19 zilitengwa **shilingi bilioni 11.58**, hata hivyo kiasi hicho hakiwezi kukidhi mahitaji, hivyo ni muhimu Serikali ikaendelea kuongeza bajeti kwa ajili ya maeneo hayo mapya.

4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mpango na Bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020, kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI inayojumuisha Mafungu 28 (Fungu 56; Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) imeandalowiwa kwa kuzingatia yafuatayo:-
i. Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na maelekezo mbalimbali ya Viongozi wa Kitaifa;

ii. Vipaumbele vilivyoanishwa katika llani ya Uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi ya Mwaka 2015 – 2020;

iii. Malengo Endelevu ya Maendeleo 2030 (*Sustainable Development Goals 2030*);

- iv. Mpango wa Pili wa Taifa wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21;
- v. Mpango Mkakati wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI uliofanyiwa mapitio mwaka 2016; na
- vi. Hotuba ya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzaia kwenye uzinduzi wa Bunge la 11.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais - TAMISEMI), imepanga kutekeleza malengo yake kwa kuzingatia vipaumbele kumi (10). Baadhi ya vipaumbele hivyo ni hivi vifuatavyo:-

- i. Kusimamia shughuli za utawala bora, kukuza demokrasia, ushirikishwaji wa wananchi na ugatuaji wa madaraka kwa umma (D by D);
- ii. Kusimamia maandalizi ya uchaguzi wa serikali za mitaa wa mwaka 2019 ;
- iii. Kuchochea na kuhimiza ukuaji wa uchumi kwa maendeleo ya wananchi na Taifa kwa ujumla kwa kuiwezesha mikoa na mamlaka za serikali za mitaa kuweka mazingira mazuri ya biashara na uwekezaji hasa katika kilimo na viwanda ;
- iv. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya msingi ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ikiwa ni pamoja na kufanya ufuatiliaji na tathmini kuhusu utekelezaji wa shughuli za Serikali, Taasisi, programu na miradi katika ngazi ya mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ;
- v. Kuratibu ujenzi wa miundombinu ya maeneo ya utawala ya mikoa, wilaya, na halmashauri mpya na za zamani ambazo hazina majengo ya utawala ;
- vi. Kuimarisha uwajibikaji na usimamizi wa fedha katika mikoa na mamlaka za serikali za mitaa ; na

vii. Kuratibu shughuli za kuboresha mazingira ya kufanya kazi kwa watumishi wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI (ujenzi wa ofisi, mtumba), mikoa na mamlaka za serikali za mitaa pamoja na kuapatia vitendea kazi.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Halmashauri, zinaomba kuidhinishiwa jumla ya **Shilingi 6,207,992,779, 769/=**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,515,055,425,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida, na **Shilingi 1,692,937,354,769/=** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **Shilingi 3,807,104,425,000/=** sawa na asilimia 61.33 ya bajeti yote ni kwa ajili ya mishahara, na **Shilingi 707,951,000,000/=** sawa na asilimia 11.40 ya bajeti yote ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Bajeti ya maendeleo imechukua asilimia 27.27 ya bajeti yote ya Ofisi hii. **Jedwali Na. 03** linafafanua zaidi juu ya Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

Jedwali Na. 03 Mgawanyo wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Chanzo: Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI (2019/2020)

4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, zinakadiria kukusanya jumla ya **Shilingi 802,160,498,164/=**. Mapato hayo ni ongezeko la **Shilingi 43,789,290,395/=** sawa na **asilimia 6** ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka wa fedha 2018/2019. Ulinganisho wa makusanyo kati ya mwaka wa fedha 2018/19 na 2019/20 umefafanuliwa zaidi katika **Jedwali Na. 04**.

Mheshimiwa Spika, makusanyo hayo yanatarajiwa kutokana na kuuza vifaa chakavu pamoja na nyaraka za zabuni, faini mbalimbali, ada, tozo, marejesho ya masurufu na mishahara kwa makao makuu. Aidha, kwa upande wa Halmashauri, makusanyo yatatokana na ushuru na kodi mbalimbali na vyanzo vingine vya mapato vilivypo kwa mujibu wa sheria.

Jedwali Na.4 Mchanganuo wa Maduhuli na Makusanyo ya ndani

Ofisi/Taasisi	Bajeti 2018/2019	Bajeti 2019/2020	Tofauti	Asilimia
OR – TAMISEM na Taasisi		36,464,195,252	13,820,676,191	61.08
Mkoa	22,643,519,061			
Halmashauri	139,059,708	213,302,912	74,243,204	53.39
	735,588,629,000	765,483,000,000	29,894,371,000	4.06
Jumla	758,362,711,799	802,160,498,164	43,789,290,395	5.77

Chanzo: Randama ya Ofisi ya Rais –TAMISEMI (2019/2020)

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa uchambuzi wa Kamati makusanyo yote yanatarajiwa kuongezeka kwa **shilingi 43,789,290,395/=** ikilinganishwa na mwaka wa fedha unaomalizika. Kiasi hicho ni sawa na ongezeko la asilimia 5.8. Aidha, ingawa kumekuwa na ongezeko la makusanyo katika maeneo yote, inatarajiwa kwamba Halmashauri zitachangia kwa kiasi kikubwa kutokana na maduhuli yake kuongezeka kwa takribani **shilingi 29,894,371,000** sawa na asilimia 4.1 ikilinganishwa na makusanyo ya Halmashauri katika mwaka wa fedha unaomalizika.

Ni mtazamo wa Kamati kwamba, huenda ongezeko hilo limechangiwa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuendelea kubuni vyanzo vipyta vya mapato ili kufidia pengo la vyanzo vilivyochochukuliwa na Serikali Kuu, na kuimarisha matumizi ya mashine za kielektroniki katika ukusanyaji wa mapato. Aidha, idadi kubwa ya wananchi na vyanzo vingi vya mapato kupatikana katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, inaweza kuwa sababu isiyopingika katika kuchangia mapato mengi kwenye Halmashauri.

4.3 Uchambuzi wa Makadirio ya Matumizi

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha ujao 2019/2020, Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, kwa pamoja zinaomba kuidhinishiwa na Bunge lako Tukufu jumla ya **Shilingi 6,207,992,779,769/=** kwa ajili ya kutekeleza majukumu mbalimbali yaliyopangwa kutekelezwa. Kati ya fedha hizo **shilingi 4,515,055,425,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,692,937,354,769** ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Aidha, katika fedha hizo zinazoombwba kuidhinishiwa na Bunge, **Shilingi 15,901,167,000/=** ni kwa ajili ya Mishahara na Matumizi Mengineyo kwa Tume ya Utumishi wa Walimu (TSC) – Fungu 02.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla wake bajeti inayoombwa kuidhinishiwa na Bunge lako tukufu kwa Ofisi ya Rais - TAMISEMI, Tume ya Utumishi wa Walimu, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa, imepungua kwa **Shilingi 374,954,071,694**

sawa na asilimia 5.69 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha unaomalizika wa 2018/2019. Kwa upande wa fedha za maendeleo, Kamati umebaini upungufu wa asilimia 5.92 kutoka **shilingi 1,799,436,057,500/=** kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi **shilingi 1,692,937,354,769/=** katika mwaka wa fedha ujao wa 2019/2020. Uchambuzi umebaini kwamba, upungufu huo wa bajeti ya jumla, na ile ya maendeleo umebadili kabisa mwelekeo wa bajeti kwa ofisi hii ambayo kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita ilikuwa ikiongezeka. Katika miaka hiyo mitatu bajeti ya jumla kwa ofisi hii iliongezeka kwa asilimia 12 (mwaka 2016/17); asilimia 8.5 (mwaka 2017/18) na asilimia 6.5 (mwaka 2018/19).

Mheshimiwa Spika, katika kulinganisha bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI na Bajeti ya taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 uchambuzi umebaini kwamba, wakati bajeti ya Taifa iklongezeka kwa asilimia 1.93 kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/19, bajeti ya TAMISEMI katika kipindi hicho imepungua kwa asilimia 5.69. Aidha, bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI ni sawa na asilimia 18.74 ya bajeti ya Taifa. Uwiano huo umeendelea kupungua katika kipindi cha miaka minne mfululizo kutoka mwaka wa fedha 2015/16 ambapo uwiano ulikuwa ni asilimia 24 hadi kiwango hicho cha sasa. Kwa ujumla uwiano huo umepungua kwa zaidi ya asilimia 5 ndani ya kipindi cha miaka minne ya fedha, kiwango ambacho ni kikubwa. Ulinganisho zaidi wa Uwiano wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI na Bajeti ya Taifa umefafanuliwa zaidi kupitia **Jedwali Na. 05.**

Mheshimiwa Spika, inashangaza kwamba, licha ya Ofisi ya Rais - TAMISEMI kusimamia sekta nyingi katika ngazi za mamlaka za Serikali za Mitaa, bajeti yake imepungua, na uwiano wa bajeti hii ikilinganishwa na bajeti ya Taifa umeendelea kupungua kwa mwaka wa nne mfululizo. Ni kwa mantiki hiyo, Kamati inahoji kama bajeti ya ofisi hii inashuka ni kwa vipi juhudzi za wananchi katika shughuli za maendeleo zitaungwa mkono. Ni kwa vipi maboma ya shule za msingi na sekondari za kata, zahanati, vituo vyatya afya, hospitali za wilaya, n.k, yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi

yatakamilika! Ni wazi hilo halitawezekana kwa mwenendo wa bajeti kupungua.

Mheshimiwa Spika, Kamati ingetamani kuona Ofisi hii inaongezewa fedha katika bajeti yake, huku Serikali ikiendelea kujikita katika kujenga mfumo imara wa kuwahudumia wananchi ambao ndiyo msingi wa madaraka yote ya Serikali kwa mujibu wa Ibara ya 8(a) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ya mwaka 1977.

Njia madhubuti ya kujenga mfumo huo ni Serikali kuhakikisha inagatua rasilimali fedha za kutosha (kuongeza bajeti) na kuzipeleka kikamilifu kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa ambako utekelezaji unafanyika ili kuziwezesha mamlaka hizo kutimiza wajibu wake kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, aidha, mgawanyo wa makadirio ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mikoa na Mamlaka ya Serikali za Mitaa umefafanuliwa zaidi kuititia **Jedwali Na. 06**. ambalo ni Kiambatisho “A” cha Taarifa hii ya Kamati

Jedwali Na. 05: Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI dhidi ya Bajeti ya Taifa, kwa mwaka wa fedha 2019/20

Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa, na Randama ya Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/2020

5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kufanya ziara kwenye miradi ya maendeleo na kupitia Taarifa ya utekelezaji wa Ofisi ya Rais – TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Kamati inatoa maoni na ushauri kama ifuatavyo:

-

- i. Kamati inapongeza hatua ya Serikali kutunga Sheria kwa ajili ya kusimamia Mikopo ya Uwezeshaji kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu kutokana na **asilimia 10** ya mapato ya ndani ya halmashauri. Sheria hiyo imetungwa kupitia Sheria ya Fedha za Serikali Mitaa, Sura 290 ambayo ilifanyiwa marekebisho na Sheria ya Fedha yam waka 2018 na imefafanua kuhusu mgawanyo wa makundi hayo na kwamba, mikopo itatolewa bila riba. Kamati inashauri Serikali iharakishe kukamilisha mchakato wa kuandaa Kanuni za utekelezaji wa Sheria hiyo ili zianze kutumika na hivyo kuwezesha jambo hili kutekelezwa kwa mujibu wa utaratibu;
- ii. Kamati imebaini kwamba, Halmashauri nyingi hazijaanza kuzingatia Sheria ya Kusimamia Mikopo ya Uwezeshaji kiuchumi Wanawake, Vijana na Watu wenyewe Ulemavu, kutokana na kushindwa kutenga kikamilifu fedha hizo na kuzipeleka kwenye vikundi husika. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kusimamia kikamilifu utekelezaji wa jambo hili, na Wakurugenzi wa Halmashauri ambazo hazitazingatia sheria hii kikamilifu wachukuliwe hatua stahiki. Aidha, Halmashauri ziwezeshe kufungua Akaunti Maalum kwa ajili ya fedha za asilimia 10 ili ziweze kusimamiwa kwa ufanisi zaidi. Vilevile, Halmashauri ziandae na kutunza takwimu kuhusu idadi ya vikundi, pamoja na kuonesha usimamizi wa fedha zinazorejeshwa na vikundi vilivyokopeshwa;
- iii. Kamati inashauri Halmashauri ziwezeshe vikundi vinavyopata fedha kutokana na asilimia 10 ya mapato ya ndani ya halmashauri, kubuni miradi mikubwa ya kiuchumi ili kuweza kujikwamua dhidi ya umaskini. Kamati inapongeza

Halmashauri zote za Mkoa wa Simiyu ambazo zimeamua kutumia fedha hizo kununua mashine kutoka Shirika la Viwanda Vidogo (SIDO) kwa lengo la kuwezesha vikundi hivyo kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya uzalishaji; na Halmashauri ya Mji Mafinga, Mkoani Iringa ambayo imetumia fedha hizo kuanzisha kiwanda kikubwa cha kutengeneza sabuni za kufulia za kipande na maji aina ya "**Mafinga Soap**" ambacho tayari kimeanza uzalishaji;

iv. Serikali iendelee kuhimiza Halmashauri kubuni vyanzo vipyta vya mapato ili kupunguza utegemezi wa ruzuku kutoka Serikali Kuu. Kamati imebaini kwamba, Halmashauri 30 zimeweza kubuni miradi ya kimkakati 38 ambayo iliidhinishiwa jumla ya **shilingi bilioni 268.4** kwa ajili ya utekelezaji ili kuongeza mapato ya ndani. Idadi hiyo ambayo ni sawa na asilimia 16.21 ya halmashauri zote nchini ni ndogo sana, hivyo juhudu zaidi zinahitajika ili kusaidia halmashauri nyingine kubuni miradi ya kimkakati ili ziweze kupatiwa fedha za utekelezaji;

v. Serikali ihimize halmashauri kuongeza juhudu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani kwani mwenendo wa ukusanyaji kwa baadhi ya halmashauri siyo mzuri. Uchambuzi wa Kamati ulibaini kwamba, kwa wastani Mikoa yote 26 ya Tanzania Bara ilikusanya kwa asilimia 57.63 hadi kufikia mwezi Februari, 2019. Mikoa Sita kati ya hiyo ilifanya vibaya zaidi kwa kukusanya chini ya asilimia 50 ya lengo kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 07**;

Aidha, halmashauri tatu za Mkoa wa Mtwara zilongoza kwa makusanyo hafifu ikilinganishwa na halmashauri zote nchini. Halmashauri hizo ni Masasi (10.95); Nanyumbu (10.44) na Tandahimba (13.22) ambazo wastani wa makusanyo ulikuwa asilimia 11.53. Aidha, Halmashauri nyingine zilizokusanya mapato ya ndani kwa kiwango cha chini ni Nsimbo (23.5%) na Mlele (26.3) za Mkoani Katavi; pamoja na Nyasa (26.19) na Tunduru (27%) za mkoani Ruvuma. Kamati inashauri Serikali kuelekeza nguvu katika mikoa hiyo sita kwa lengo la kubaini chanzo cha udhaifu huo katika makusanyo, na kutafuta suluhisho;

Jedwali Na.07: Mikoa iliyokusanya mapato chini ya asilimia 50

Moa	Mwara	Ruvuma	Simiyu	Kigoma	Katai	Singida
Asilimia (%)	25.23	37.91	43	468	47.5	47.9
Nafasi	1	2	3	4	5	6

Chanzo: Randama za Mikoa kwa mwaka wa fedha 2019/2020

vi. Serikali iendelee kutenga na kupeleka kikamilifu fedha kwa ajili kukamilisha ujenzi wa maboma, katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ambayo yamejengwa kwa kushirikisha nguvu za Wananchi. Kamati inatambua juhudzi za Serikali katika kutenga fedha za maendeleo, hata hivyo changamoto kubwa imekuwa upatikanaji wa fedha hizo. Kwa mfano katika mwaka wa fedha 2018/19 jumla ya **shilingi trillioni 1.37** zilliidhinishwa kwa ajili ya maendeleo, lakini hadi mwezi Februari, 2019 (takribani robo ya tatu ya mwaka wa fedha) ni asilimia 38 tu ya fedha hizo ndiyo ilipelekwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ajili ya miradi iliopangwa. Kiwango hicho ni kidogo, na kinaashiria kwamba utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaendelea kusuasua na hivyo kuendelea kuwacheleweshea Wananchi huduma ambazo zingetokana na kukamilika kwa miradi husika. Aidha, hali hiyo inawavunja moyo wananchi katika kushiriki kwenye miradi ya maendeleo;

vii. Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kuondoa kodi ya taulo za kike kupitia marekebisho ya Sheria ya Fedha ya Mwaka 2018 kwa lengo kuwasaidia watoto wa kike kushiriki kikamilifu katika masomo. Hata, hivyo Kamati inashauri halmashauri nchini kubuni namna ya kuwasaidia watoto wa kike kutoka familia maskini kupata taulo hizo bure ili waweze kuhuduria masomo kikamilifu wakati wote. Utafiti uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) Mwaka 2008 ulibaini kwamba, asilimia 10 ya watoto wa kike katika shule za msingi na sekondari, Kusini mwa Jangwa la Sahara huacha masomo kwa kushindwa kumudu kununua taulo za kike Pads/Tampos. Aidha, Kamati inahimiza ujenzi

wa vyumba maalumu kwa ajili ya Watoto wa kike kujihudumia wanapokuwa katika siku zao;

viii. Kamati inapongeza hatua ya Serikali kuanza ujenzi wa Vituo vya Afya (350) na Hospitali za Wilaya (67) katika mwaka wa fedha 2018/19 na kutenga fedha kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vituo na hospitali zaidi katika mwaka ujao wa fedha. Aidha, Kamati inashauri kwamba, pamoja na kuijandaa kuanza ujenzi katika maeneo mapya, Serikali itoe fedha kikamilifu ili kuendeleza na kukamilisha ujenzi wa majengo yaliyoanza ili yakamilike upesi na wananchi wa maeneo hayo waanze kupata huduma ya matibabu;

ix. Kamati inapongeza hatua ya Serikali ya kujenga wodi maalum (Mama Ngojea) 84 katika mikoa 20 kati ya 26 ya Tanzania Bara ili kuwezesha Wajawazito kutoka maeneo ya mbali na huduma za afya, kupata uangalizi wa karibu kutoka kwa Wataalam wa afya hasa wanapokaribia kujifungua. Hatua hiyo itasaidia kupunguza vifo vya mama na mtoto wakati wa kujifungua (*maternity mortality deaths*) ambavyo huchangiwa na kukosa huduma za msingi za afya kama vile upasuaji (*operation*);

Hata hivyo, Kamati inashauri Serikali kujenga wodi hizo katika mikoa iliyosalia ambayo ni Katavi, Tanga, Mtwara, Rukwa, Mara na Dar es Salaam ili kuendelea kueneza huduma hiyo. Aidha, bado idadi hiyo ya wodi ni ndogo, hivyo Kamati inashauri angalau tufikie kiwango cha kuwa na wodi za aina hiyo katika kila halmashauri nchini;

x. Serikali ihimize Halmashauri nchini kuchangia kikamilifu katika Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, kwani kiwango cha uchangiaji kiko chini sana na kimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 halmashauri zilikuwa zimechangia **shilingi milioni 616.7** sawa na asilimia 11 ya lengo liliowekwa. Kiwango hiko kimepungua kwa asilimia 9 zaidi ikilinganishwa na kiwango kilichokuwa kimekusanywa katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha uliopita ambacho kilifikia asilimia 20. Hali hiyo inakwamisha bodi hiyo kutekeleza majukumu yake kikamilifu

na hivyo inapaswa kuangaliwa kwa kuchukua hatua stahiki kwa halmashauri ambazo hazichangii kikamilifu;

xi. Ofisi ya Rais, TAMISEMI isimamie na kuhakikisha halmashauri ambazo zinadaiwa na Waheshimiwa Madiwani posho stahiki za vikao na za mwezi zinawalipa viongozi hao ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao vizuri. Aidha, hali hiyo itasaidia kuondoa migogoro baina ya viongozi hao na taasisi za fedha na benki ambazo wamechukua mikopo kwa dhamana ya posho wanazolipwa, lakini hakuna urejeshajii wa fedha kwa mujibu wa makubaliano. Halmashauri Sita (6) za Mkoa wa Singida zinaongoza kwa kudaiwa na Madiwani ambapo kwa ujumla wake zinadaiwa zaidi ya **shilingi milioni 620** na Benki za CRDB na NMB ikiwa ni mikopo ya Madiwani waliyochukua kwa dhamana ya posho zao. Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni pekee yake inadaiwa **shilingi milioni 112.13** kati ya kiasi hicho;

xii. Serikali ichukue hatua za makusudi ili kukabili tatizo la upatikanaji wa fedha kidogo za maendeleo kutoka Hazina, kwani unaathiri au kukwamisha kabisa utekelezaji wa miradi iliyokusudiwa. Hadi mwezi Februari, 2019 ni asilimia 44.5 tu ya fedha za maendeleo ndiyo ilikuwa imepokelewa ikilinganishwa na asilimia 50.6 ya fedha za matumizi ya kawaida iliyopokelewa katika kipindi hicho;

xiii. Serikali isaidie Mikoa na Halmashauri nchini kupata majengo ya ofisi, watumishi na vitendea kazi ili kuwawezesha watendaji wake kutekeleza majukumu yao kikamilifu. Kwa mfano; baadhi ya viongozi katika maeneo hayo hawana magari, na hivyo kulazimika kuazima magari ya wataalam, jambo linalokwamisha shughuli za kitaalam. Katika mkoa wa Singida pekee Wakuu wa Wilaya za Mkalama na Singida; na Wakurugenzi watano 5 (H/W Ikungi, H/W Mkalama, H/M Singida, H/W Singida, na H/W Iramba) hawana magari, hivyo ni wazi inaathiri utendaji wao; na

xiv. Kamati inapongeza kazi nzuri inayotekelzwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) katika kujenga na kuboresha miundombinu katika maeneo hayo.

Hata hivyo, kiasi cha fedha kinachotengwa kwa Wakala huu ni kidogo sana ikilinganishwa na mtandao wa barabara (zaidi ya kilomita 108,000) inazohudumia. Ni ushauri wa Kamati kwamba, TARURA iongezewe fedha na Serikali. Aidha, mgawo wa fedha wa asilimia 30 ambaao TARURA inapata kutoka Mfuko wa Barabara (Road Fund) uongezwe hadi asilimia 50.

6.0 **HITIMISHO**

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika, na Wenyeviti wa Bunge, kwa namna ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu ya kuliendesha Bunge letu Tukufu kwa umakini na ustadi.

Aidha, ninawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii ambaao umewezesha kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Ninaamini tutaendelea kushirikiana kikamilifu katika kutekeleza shughuli za Kamati, na hivyo kutimiza wajibu wetu wa kikatiba wa kuwakilisha wananchi na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa shughuli za Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii inashughulikia mafungu mengi ya Bajeti (Mafungu 36) na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya uchambuzi, ni wazi katika kipindi hicho Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi wakati mwingine hadi jioni kabisa. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa namna yoyote ile kwa Wajumbe, na badala yake walitekeleza jukumu la uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, ikiwa ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa namna ya pekee ningetamani sana kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda, ninaomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanne Ismail Mcchemba, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe. George Malima Lubeleje, Mb
6. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba,Mb
7. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
8. Mhe. Hamad Salim Maalim, Mb
9. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate,Mb
10. Mhe. Mwatum Dau Haji,Mb
11. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum,Mb
12. Mhe. Salum Khamis Salum,Mb
13. Mhe. Venance Methusela Mwamoto,Mb
14. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb
15. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
16. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
17. Mhe. Lusia Ursula Michael, Mb
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
19. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb
20. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
22. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
23. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
24. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb
25. Mhe. Mansoor Hirani Shanif, Mb
26. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati napenda kumshukuru sana Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais – TAMISEMI, Mhe. Seleman Said Jafo (Mb) kwa ushirikiano mkubwa alionunesha kwa Kamati hii ambao umechangia kwa sehemu kubwa Kamati kuweza kutekeleza shughuli zake. Yeye pamoja na Naibu Mawaziri wake, Mhe. Josephat Sinkamba Kandege (Mb) na Mhe. Waitara Mwita Mwikwabe (Mb) ni hazina kubwa katika ustawi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa na maendeleo ya Taifa hili.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Mhandisi Joseph Nyamuhanga, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais TAMISEMI, akisaidiana na Naibu Makatibu Wakuu Tickson

Nzunda na Dkt. Dorothy Gwajima, kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Aidha, shukrani zangu pia ziwaendee Wakuu wa Mikoa yote ya Tanzania Bara, Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri zote nchini, kwa utendaji wao makini katika utekelezaji wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha, na kwa uwasilishaji mzuri wa Taarifa ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa mwaka ujao wa fedha.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai, Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Mambo ya Jumla, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Modesta Kipiko, kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

Vilevile, nawashukuru watumishi wote wa Idara ya Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard), wakiongozwa na Bi. Hanifa Masaninka, kwa kuandaa na kutoa vitabu vya taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kama yalivowasilishwa na Mto Hoja hapo awali.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Jasson S. Rweikiza (Mb)

MWENYEKITI

KAMATI YA BUNGE YA UTAWALA

NA SERIKALI ZA MITAA

10 Aprili, 2019

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Ni wewe mwenyewe? Mheshimiwa Mwamoto, Balozi. (*Makofii*)

MHE. JASSON RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba yangu ya pili ya Kamati ya TAMISEMI na Utawala Bora, kuhusu Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, itasomwa na Mheshimiwa Daniel Mtuka.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mtuka. Aah, Mheshimiwa Mwamoto, Balozi. (*Makofii*)

MHE. VENANCE M. MWAMOTO - K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote namshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kuturuzuku uhai tangu tulipokamilisha kujadili bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha unaoisha hadi leo tena tunapokutana kujadili bajeti ya ofisi hii kwa mwaka wa fedha ujao. Wapo wenzetu hawakupata nafasi hii, hivyo sisi tuliobahatika kuipata tunapaswa kumshukuru Mwenyezi Mungu na kumrejeshea shukrani Maulana, yeeye pekee aliyetukuka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na ufinyu wa muda, naomba taarifa hii yote liingie katika kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge, *Hansard*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sehemu ya utangulizi wa taarifa hii imeeleza majukumu ya Kamati kwa mujibu wa

Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 pamoja na kazi zilizotekelawa na Kamati kwa kuzingatia kanuni hizo ambazo ni pamoja na uchambuzi wa bajeti, maeneo ambayo Kamati hii ilijikita kuyaelekeza. Sehemu ya utangulizi inapatikana katika ukurasa wa kwanza na wa pili wa taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa shilingi bilioni 119.9 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu matano yaliyoonekana katika ukurasa wa tatu wa taarifa hii ya Kamati. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelawa chini ya mipango ya kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge Tanzania (MKURABITA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania. Ufafanuzi kuhusu miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

Mradi Namba 4921, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 1,500,000,000/= na ulitekelezwa chini ya Kifungu Na. 1003 - *Policy and Planning*, Kifungu Na. 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Mpango huu umewezesha wanyonge kurasimisha ardhi na biashara na kuvitumia kama dhamana ya kupata mikopo ambayo imewawezesha kukuza mitaji ya shughuli za kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA imewajengea wakulima 362 na viongozi 88 na vyama vya wakulima uwezo wa kutumia hati za Hakimiliki za Kimila kupata mitaji katika benki katika Halmashauri za Wilaya za Mvomero na Magu. Kutokana na mafunzo hayo, wakulima 100 wameweza kufungua akaunti katika benki mbalimbali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa Zanzibar urasimishaji wa biashara katika Wilaya ya Magharibi na Unguja na Mkoani Pemba umeanza ambapo

wafanyabiashara 100 watapata mafunzo na kusajili biashara zao. Napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea Mkoani Lindi ili kujiridhisha kuhusu hali ya utekelezaji wa MKURABITA.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mradi Na. 6220 - *Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF)* ulitengewa jumla ya shilingi 74,360,989,000/= ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu Na. 1003 - *Administration and Human Resource Management*, cha Fungu Na. 30 Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Mfuko huu ulitekelezwa katika mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar na uko katika awamu ya tatu ya utekelezaji wake ambapo inahusu mpango wa ruzuku kwa kaya masikini ili kuzisaidia kupunguza umasikini na kuinua ubora wa maisha. Hadi sasa kaya masikini 1,007,588 zenye jumla ya Watanzania millioni tano zimeandikishwa na kunufaika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mpango huu, Kamati ilitembelea na kukagua Kijji cha Namela kilichopo Kata ya Msanga Mkuu, Tarafa ya Ziwani, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Mkoani Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma (*TPSC*) kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo, ushauri na kufanya utafiti tumizi na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za uongozi na menejimenti na utawala. Aidha, chuo kinaendesha kozi za kitaalam kwa ngazi ya astashahada, stashahada na shahada katika nyanja za Uhazili, Utunzaji wa Kumbukumbu, Menejimenti ya Raslimali Watu, Utawala na Manunuvi ya Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo katika Kampasi Sita zilizoko katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Tanga, Singida, Mbeya na Mtwara.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo hiki, Kamati ilitembelea Kampasi ya Mtwara ili kupata taarifa na kukagua mazingira ya chuo. Matokeo ya ukaguzi mradi Na. 4921 – Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA). Katika Halmashauri ya Nachingwea Kamati ilipokea taarifa za

utekelezaji wa mpango huu katika Vijiji vya Mbondo, Nahimba na Nakalonji, ambavyo kutokana na mafunzo ya vitendo jumla ya mashamba 2,328 yameweza kupimwa na Hati za Haki Miliki za Kimila 2180 kuandaliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika Kijiji cha Mbondo mashamba 1304 yamepimwa na hati 750 zimeandaliwa na Kamati ilikabidhi hati 100 kati ya hizo. Jedwali namba moja linatoa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mpango huo katika Halmashauri ya Nachingwea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mradi Na. 6220 – *Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF)* - Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini. Kamati ilitembelea Kijiji cha Namela kilichopo Wilayani Mtwara ambacho hiki kina jumla ya Kaya 117 zinazonufaika na mpango huu. Kaya hizo zimepokea ruzuku ya shillingi millioni 109.99 kutokana na awamu 30 za uhawillishaji tangu kuanza kwa mpango huo Julai – Agosti, 2014 hadi Februari, 2019. Aidha, TASAF imewezesha Kijiji cha Namela kutekeleza miradi yenye thamani ya shillingi milioni 36.5 na kutoa ajira za muda kwa kaya zote 117 za walengwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati ilitembelea wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini Abdallah Ismail Hamadi Tungwalu na Bi. Fatuma Shamte Abdallah (81), ambao wametumia ruzuku wanayoipata kuwa chachu ya kujenga na kuboresha makazi pamoja na hali ya uchumi wa familia. Wanufaika hao wanafuga kuku, mbuzi, wanajenga nyumba bora kutokana na ruzuku wanazozipata. Akiongea kwa kujamini Bi. Fatuma anasema, "*TASAF ndiye bwana wangu. Mimi na wajukuu wangu tumetoka kula mlo mmoja, hadi sasa tunakula milo mitatu. Ninavaa kitenge kizuri, wajukuu zangu wanasoma bila hofu kwani wanapata mahitaji muhimu ya shule*". Haya ndio mambo ya TASAF.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Chuo cha Utumishi wa Umma; Chuo hiki kilianzishwa rasmi kama Wakala wa Serikali, Agosti, 2000 kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997, baada ya kuunganishwa kwa vyuo viwili, Chuo cha Watumishi wa Serikali (*Civil Service Training Centre*)

kilichokuwa Dar es Salaam na Chuo cha Uhazili Tabora (*Tabora Secretarial College*) na sasa kina matawi sita. Matokeo ya ukaguzi wa miradi iliyobaini mafanikio na changamoto yameelezwa kwa kina katika ukurasa wa 7 -13 wa taarifa hii ya kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni ya jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019; moja Wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini wanaweza kujikwamua kiuchumi iwapo watatumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi midogo midogo ya kiuchumi kama vile biashara, ufugaji au kilimo. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Jamii katika halmashauri isaidie kuwaelimisha walengwa hao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; iwapo *TASAFitahakiki* na kusajili kaya maskini zilizosahaullika katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, itasaidia kupunguza au kuondoa malalamiko mionganoni mwa wanajamii. Tatu, Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umechangia kuboresha mahudhurio ya watoto wa kaya maskini shulenii na kliniki. Nne, bajeti finyu kwa MKURABITA inaathiri utendaji wa mpango huo na hivyo kukwamisha zoezi la urasimishaji, hivyo tunaomba MKURABITA pia waongezewe bajeti.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano; Watendaji wa halmashauri walijengewa uwezo na MKURABITA, wanaweza kuendeleza zoezi la urasimishaji iwapo watawezeshe kwa kupatiwa vifaa na raslimali fedha. Sita benki na taasisi za fedha zikielimishwa kuhusu hadhi ya Hati za Hakimiliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo, zitatoa mikopo kwa wananchi wanaomiliki ardhi kwa hati hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba; Halmashauri zikipatiwa wataalam wa ardhi, zitasaidia MKURABITA kuharakisha zoezi la kurasimisha ardhi na kutoa Hati za Hakimiliki kwa wahusika; nane, iwapo Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Mtwara kitawezeshwa kumiliki viwanja Na. 41 na 46 vilivyo jirani na kampasi hiyo, kitawezwa

kujenga mabweni na hivyo kuondoa usumbufu kwa wanafunzi wanaolazimika kupanga vyumba mbali na chuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti na uzingatiaji wa mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2018/2019. Uchambuzi wa Kamati katika utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ya mwaka 2018/2019 ulizingatia makusanyo ya maduhuli kwa kulinganisha na malengo ya mwenendo wa upatikanaji wa fedha kwa matumizi ya shughuli zilizopangwa kwa kutekelezwa. Uchambuzi wa taarifa na uzingatiaji wa maoni ya Kamati kwa mwaka 2018/2019 ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 15 – 18 wa taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa mpango wa Makadirio ya matumizi ya mwaka fedha 2018/2020. Taarifa ya mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayojumuisha Mafungu Nane (20, 30, 32, 33, 67, 94, 09 na 04) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika:-

- (i) Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 ya Chama Tawala;
- (ii) Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja; na
- (iii) Maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla ofisi hii pamoja na mafungu yake imepanga kutekeleza malengo 177 katika mwaka wa fedha ujao na baadhi ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 19 - 21 wa taarifa hii ya Kamati.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuweza kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishiwa

jumlah ya shilingi bilioni 683.5. Kati ya fedha hizo shilingi bilioni 483.7 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 199.9 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, shilingi bilioni 35.4 sawa na asilimia 7.31 ni kwa ajili ya mishahara na shilingi bilioni 44.8 sawa asilimia 92 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwaa kuidhinishwa katika mwaka ujao wa fedha imeongezeka kwa shilingi bilioni 14.4 sawa na asilimia 2.6 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambayo ilikuwa shilingi bilioni 669. Ongezeko hilo la fedha limebadili mwenendo wa bajeti ya ofisi hii kwa miaka miwili ya fedha iliyopita (2017/2018 na 2018/2019) ambapo bajeti hiyo ilikuwa ikipungua. Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi umebaini kwamba kiasi kinachoombwa kuidhinishwa nacho kimeongezeka kwa kwa shilingi bilioni 3.9 sawa na asilimia 1.99 ikilinganishwa na kiasi cha shilingi bilioni 1.95 kilichoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi zaidi umebaini kwamba, ingawa ongezeko hilo limebadili mwenendo wa bajeti ya maendeleo ambayo imekuwa ikipungua kwa miaka miwili ya fedha iliyopita (2017/2018 na 2018/2019), bado kiasi kilichoongezeka ni kidogo ikilinganishwa na kiasi kilichoongezeka katika fedha za matumizi ya kawaida. Licha ya ongezeko, bajeti ya maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha ni takribani asilimia 51.12 tu ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi wa bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2019/2020. Uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Uchambuzi umelenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika

mwaka ujao wa fedha. Jedwali namba mbili na chati mraba namba moja na mbili zimefafanua zaidi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uchambuzi huu ulibaini mambo yafuatayo. Moja, bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ni shilingi bilioni 683 sawa na asilimia 2.06 ya Bajeti ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2019/2020 ni shilingi bilioni 33.15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 1.93, ikilinganishwa na mpango wa bajeti kwa mwaka 2018/2019; ilihali bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/2020 imeongezeka kwa asilimia 2.16 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia mbili katika fedha za maendeleo, ambazo ni sawa na asilimia 37 ya bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo ni sawa na asilimia 0.60 ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa asilimia 1.9 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maoni na ushauri wa Kamati. Baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja; Serikali iongeze kiasi inachotoa kuchangia utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini, kwani mchango wake ni mdogo sana. Tangu kuanza kwa mpango huu katika mwaka wa fedha 2013/2014, hadi taarifa hii inaandaliwa Serikali imechangia shilingi bilioni

4.35 tu kati ya shilingi bilioni 66.5 ilizopaswa kuchangia, sawa na asilimia 6.54 kwa ufanuzi ufuatao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili; Serikali iwezeshe wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini walioamua kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*), kutumia kadi hizo kupata huduma ya matibabu nje ya maeneo waliyosajiliwa. Aidha, kadi hizo zitambuliwe kwenye Hospitali/Vituo vya Afya na Zahanati binafsi kama ilivyo kwa aina nyingine za bima za afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kurudia, Serikali iwezeshe wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini walioamua kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (*CHF*), kutumia kadi hizo kupata huduma ya matibabu nje ya maeneo waliyosajiliwa. Aidha, kadi hizo zitambuliwe kwenye hospitali/vituo vya afya na zahanati binafsi kama ilivyo kwa aina nyingine za bima.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu; zoezi la kutambua na kuandikisha kaya maskini katika maeneo ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mradi wa ruzuku kwa kaya maskini, lifanyike mapema ili kaya maskini katika maeneo hayo ziweze kunufaika. Takwimu zinaonesha kuna maeneo ya Vijiiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambayo hayajafikiwa na mpango.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nne; Serikali iendelee kupunguza urasimu katika kuthibitisha Watumishi wa nafasi za uteuzi. Kamati imebaini kwamba, baadhi ya watumishi katika ofisi za umma wamekuwa wakikaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miaka miwili, kwa madai ya kusubiri upekuzi (*vetting*). Hali hiyo inawavunja moyo watumishi hao na kuathiri utendaji wao kwani hushindwa kufanya maamuzi ya msingi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tano; Halmashauri zitumie Maafisa Maendeleo ya Jamii kuelimisha wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini namna wanavyoweza kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kujkwamua kiuchumi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita; zoezi la kuhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, lîtekelezwe kwa uangalifu ili kuepuka uonevu na malalamiko kutoka kwa waathirika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sita; Serikali iongeze mshahara kwa watumishi wa umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka kila kukicha. Sote ni mashahidi kwamba, Serikali haijaongeza mshahara wa watumishi wa umma kwa mwaka wa tatu sasa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, saba; Serikali iongeze bajeti ya MKURABITA na kutoa kikamilifu na kwa wakati fedha inayotengwa, ili kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji wa ardhi na biashara za wananchi. Hadi mwezi Februari, 2019 MKURABITA ilikuwa hajapokea fedha yoyote ya maendeleo katи ya shillingi billioni 1.5 zilizoidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nane; Watendaji wa Halmashauri washirikiane na MKURABITA, katika kuandaa na kutekeleza Mpango bora wa matumizi ya ardhi na hivyo kupunguza au kuепusha migogoro ya ardhi baina ya makundi ya watumiaji katika jamii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tisa; Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Mtwara kiwezeshwe kumiliki viwanja Na. 41 na 46 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na hivyo kuondoa usumbufu wa wanafunzi wanaoishi nje ya chuo hicho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumi; Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (*Uongozi Institute*) iendelee kutoa mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwakumbusha juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kuitendaji na hivyo kuепusha migongano isiyo ya lazima. Kutolewa mafunzo hayo kumeanza kuzaa matunda ambapo vitendo vyta ukiukwaji wa sheria za kuitendaji vimepungua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati inapongeza juhudzi za Serikali kuitia TAKUKURU za kushughulikia wala rushwa wakubwa kwa kuwafikisha mbele ya sheria. Hata hivyo, Kamati inashauri juhudzi hizo pia zielekezwe kukabili vitendo vya rushwa ndogo ndogo zinazotendeka barabarani (askari polisi wa barabarani/madereva), hospitalini (Madaktari na wauguzi) na mahakamani/mabaraza ya ardhi (waendesha mashitaka/makarani/mahakimu) na kadhalika ambazo ni kero kwa wananchi. Aidha, Serikali iandae utaratibu wa kuingiza somo la maadili katika mitaala ya elimu ya msingi na sekondari ili kuandaa na kukuza kizazi chenye maadili na uzalendo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hitimisho; napenda kumpongeza Mheshimiwa Spika, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge kwa kuliongoza Bunge na kuendesha vikao vya Bunge hili vema na kwa weledi wa hali ya juu. Aidha, nawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii ambao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Naamini tutaendelea kushirikiana kikamilifu katika kutekeleza shughuli za Kamati na hivyo kutimiza wajibu wetu wa kuwawakilisha wananchi na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kamati hii inashughulikia mafungu mengi ya bajeti (mafungu 36) na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa wakati wa uchambuzi, ni wazi wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi wakati mwagine hadi jioni kabisa. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa namna yoyote kwao na badala yake walitekeleza jukumu la uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, ikiwa ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa umuhimu wa namna ya pekee ningetamani sana kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*).

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa niaba ya Kamati namshukuru Mheshimiwa Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) na Mheshimiwa Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Naibu Waziri, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa ushirikiano wao mkubwa ambao wamekuwa wakitupatia. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi hii wakiongozwa na Makatibu Wakuu; Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt. Lauren Ndumbaro (Utumishi) na Naibu Katibu Mkuu (Utumishi), Dkt. Francis Michael kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi kwa Mwaka wa Fedha 2018/2019 na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, shukrani zangu ziwaendee pia wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo vilivyo po chini ya Ofisi hii kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia.

MHE. VENANCE M. MWAMOTO - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai, kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi zake bila kukwama. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Athuman Hussein; Mkurugenzi Msaidizi, Ndugu Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati, Ndugu Chacha Nyakega na Ndugu Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndugu Modesta Kipiko, kwa kuratibu vizuri shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii. Vilevile, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge (*Hansard*) wakiongozwa na Bi.

Hanifa Masaninga kwa kuhakikisha taarifa hii inachapishwa kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofii*)

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA, KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO
YA MAPATO NA MATUMIZI KWA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1.0 UTANGULIZI

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2019/2020.

Kifungu cha 6 (4)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kinatoa wajibu

kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara zinazozisimamia. Jukumu hili la uchambuzi wa bajeti ambalo hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, hutanguliwa na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika mikoa ya Lindi na Mtwara, iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2018/2019 kuanzia tarehe 12 hadi 17 Machi, 2019. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 18 na 19 Machi, 2019.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina Mafungu Nane (8) ya bajeti kama ifuatavyo:-

- i) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;
- ii) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
- iii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
- iv) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- v) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- vi) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;
- vii) **Fungu 09:** Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na
- viii) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2018/2019;

iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa Fedha 2019/2020; na

iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

2.0 TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

2.1 Ufanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyokaguliwa

Mhesimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2018/2019, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa **shilingi 195,973,361,000/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu matano kama ifuatavyo:-

i) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri – Tshs. **175,055,489,000/=**;

ii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma – Tshs. **10,939,000,000/=**;

iii) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – **Tshs. 4,050,000,000/=**;

iv) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma - **Tshs. 750,000,000/=**; na

v) **Fungu 4:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa – **Tshs. 5,178,872,000/=**.

Mhesimiwa Spika, katika kuzingatia matakwa ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari 2016, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelawa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Miradi iliyotembelewa ni ile inayotekelawa chini ya Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA), Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC). Ufanuzi kuhusu miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

2.1.1 Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA).

Mheshimiwa Spika, mradi huu ultengewa **Shilingi 1,500,000,000/=** na unatekelezwa chini ya Kifungu 1003 “*Policy and Planning*” cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mpango huu unatekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa raslimali na uendeshaji wa biashara nchini kwa mujibu wa sheria. Mpango huu umewezesha wanyonge kurasimisha ardhi na biashara na kuvitumia kama dhamana ya kupata mikopo ambayo imewawezesha kukuza mitaji ya shughuli za kiuchumi.

Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilibainisha kwamba, MKURABITA imewajengea wakulima 362 na viongozi 88 wa vyama vya wakulima uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kupata mitaji katika benki na taasisi zingine za fedha katika halmashauri za wilaya za Mvomero na Magu. Kutohana na mafunzo hayo, wakulima 100 wameweza kufungua akaunti katika benki mbalimbali.

Aidha, vituo viwili vya urasimishaji wa biashara (*one stop formalization centre*) vimeanzishwa katika Halmashauri ya Mji wa Njombe na Halmashauri ya Manispaa ya Singida, ambapo huduma muhimu za utoaji wa leseni za biashara, namba ya utambulisho wa mlipa kodi (TIN), ujasili wa jina la biashara (BRELA), huduma za kibenki na mifuko ya hifadhi ya jamii zinapatikana. Aidha, wafanyabiashara 1,527 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara na katika kipindi hicho vituo hivyo vimesajili biashara 738 na wafanyabiashara 400 wamefungua akaunti katika benki kwa ajili ya kuweka akiba na kukopa fedha ili kuongeza mitaji.

Kwa upande wa Zanzibar urasimishaji wa biashara katika wilaya za Magharibi A, Unguja na Mkoani Pemba umeanza ambapo wafanyabiashara 100 watapata mafunzo na kusajiri biashara zao.

Aidha, kwa kushirikiana na Ofisi za Taifa za Takwimu, Tanzania Bara na Zanzibar, MKURABITA imefanya utafiti kuhusu sekta isiyo rasmi nchini kwa lengo la kubaini ukubwa na thamani ya sekta hiyo na maandalizi ya ripoti yako katika hatua ya ukamilishaji. Maeneo yaliyohusika katika utafiti huo ni mikoa ya Mbeya, Mwanza, Dodoma, Dar es Salaam, Tanga na Mtwara kutoka Tanzania Bara na Mjini Magharibi na Kusini Pemba, kutoka Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, vilevile MKURABITA imeingia makubaliano na Benki ya NMB kwa ajili ya utekelezaji wa miradi majaribio ya Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya. Utekelezaji umeanza katika Manispaa ya Iringa ambapo Serikali imeweka fedha za dhamana katika benki ya NMB ili kuziwezesha halmashauri kukopa na kuendesha shughuli za urasimishaji endelevu.

Mheshimiwa Spika, napenda kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa Kamati ilitembelea Halmashauri ya Wilaya ya Nachingwea, Mkoani Lindi ili kujiridhisha kuhusu hali ya utekelezaji wa MKURABITA.

2.1.2 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF)

Mheshimiwa Spika, mradi huu ilitengewa jumla ya **Shilingi 74,360,989,000** na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1003" *Administration and Human Resource Management*" cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri. Mfuko huu unatekelezwa katika mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar, na uko katika awamu ya tatu ya utekelezaji wake ambayo inasaidia kaya maskini za watanzania kukuza uchumi na hivyo kupunguza umaskini wa kipato; kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii, na kuhamasisha uwajibikaji na kuzingatia utawala bora.

Taarifa ya utekelezaji inaonesha kuwa, tangu kuanza kutekelezwa kwa awamu ya tatu ya TASAF takribani kaya maskini 1,007,588 zenye jumla ya watanzania **Milioni 5** zimeandikishwa na kunufaika.

Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2018 hadi Februari, 2019 kiasi cha **Shilingi Bilioni 135** kilitolewa kama ruzuku kwa idadi hiyo ya kaya ambayo inajumuisha Vijihi/Mitaa/Shehia 9,960 kutoka pande zote za Muungano.

Mheshimiwa Spika, taarifa zilibainisha kuwa mpango huu umetoa ajira kwa kaya za walengwa 288,837 kutokana na utekelezaji wa miradi 3,043 yenye thamani ya **Shilingi bilioni 14.2**. Miradi hiyo inatekelezwa katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar kwa kuhusisha Vijihi/Mitaa na Shehia 2,590.

Aidha, zoezi la uhakiki kwa lengo la kuondoa kaya zisizo na sifa kwenye mpango, liliendelea katika kipindi hicho cha kuanzia Julai, 2018 hadi Februari, 2019 ambapo kaya 4,840 zilindolewa kutokana na kukosa sifa au vigezo. Mionganoni mwa sababu za kaya hizo kupoteza sifa ni pamoja na mwanakaya au wanakaya kufariki, kaya kuhamia maeneo ambapo mpango haujaanza kutekelezwa au kaya kushindwa kujitekeza kupokea ruzuku mara mbili mfululizo.

Vilevile, TASAF imeandaa malipo kwa walengwa kwa njia ya kielektroniki kuititia mitandao ya simu na benki na majaribio kufanyika katika mamlaka za maeneo ya utekelezaji 16 ambazo ni Jiji la Arusha, Manispaa za Temeke, Kinondoni, Ilala, Kigoma Ujiji, Songea, Halmashauri za Bahi, Siha, Kilwa, Bagamoyo, Kisarawe, Mkuranga, Urambo, Muheza, Mpanda Mji na Halmashauri zote za Unguja na Pemba kwa upande wa Zanzibar. Hadi kufikia mwezi Februari, 2019 **Shilingi bilioni 16.2** zillipwa kwa walengwa 55,763.

Mheshimiwa Spika, ili kujiridhisha kuhusu utekelezaji wa mpango huu Kamati ilitembelea na kukagua Kijiji cha Namela kilichopo Kata ya Msanga Mkuu, Tarafa ya Ziwani, Halmashauri ya Wilaya ya Mtwara, Mkoani Mtwara.

2.1.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

Mheshimiwa Spika, chuo hiki kilianzishwa kwa lengo la kutoa mafunzo, ushauri na kufanya utafiti tumizi na kutoa

machapisho mbalimbali katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala. Aidha, chuo kinaendesha kozi za kitaaluma kwa ngazi ya astashahada, stashahada na shahada katika nyanja za Uhazili, Utunzaji Kumbukumbu, Menejimenti ya Raslimali Watu, Utawala na Manunuvi ya Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo katika Kampasi Sita (6) zilizoko katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Tanga, Singida, Mbeya na Mtwara.

Vile vile, chuo kiko mbioni kuanzisha Kampasi ya Dodoma ambapo jengo limepatikana na ukarabati utaanza muda si mrefu ili kuliwezesha kuwa katika hali bora ya kutumika kwa mahitaji ya chuo. Ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo hiki, Kamati ilitembelea Kampasi ya Mtwara ili kupata taarifa na kukagua mazingira ya chuo.

2.2 Matokeo ya Ukaguzi

Mheshimiwa Spika, ili kuwezesha tija ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha unaoisha, upo umuhimu wa kulifahamisha Bunge lako Tukufu kuhusu yaliyojiri kutokana na ukaguzi huo. Kwa madhumuni hayo taarifa hii imetumia njia kadhaa ikiwa ni pamoja na asilimia, majedwali, ulinganishaji na utofautishaji ili kubainisha hali ya utekelezaji wa miradi iliyo chini ya Ofisi hii. Ufafanuzi wa matokeo ya ukaguzi huo ni kama ifuatavyo:-

2.2.1 Mradi Na. 4921 - Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

Mheshimiwa Spika, katika Halmashauri ya Nachingwea Kamati ilipokea taarifa za utekelezaji wa mpango huu katika Vijiji vya Mbondo, Nahimba na Nakalonji, ambavyo kutokana na mafunzo ya vitendo jumla ya mashamba 2,328 yameweza kupimwa na Hati za Haki Miliki za Kimila 2180 kuandaliwa.

Aidha, MKURABITA imewezesha Vijiji 104 kati ya 127 katika halmashauri hiyo kupima mipaka yake na kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi hadi sasa.

Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa MKURABITA, katika Kijiji cha Mbondo ambapo upimaji wa mashamba 1,304 ulifanyika na jumla ya hati 750 kuandaliwa. Katika ziara hiyo mambo kadhaa yilibainika ikiwa ni pamoja na mafanikio na changamoto. **Jedwali Na. 01** linatoa muhtasari wa hali ya utekelezaji wa mpango huu katika Halmashauri ya Nachingwea.

Jedwali Na. 01: Mashamba yaliyopimwa katika Halmashauri ya Nachingwea, Mkoani Lindi

Na.	Kijiji	Mashamba yaliyopimwa	Hati zilizotolewa	Asilimia (%)
1.	Mbondo	1304	750	57.52
2.	Nahimba	505	341	67.52
3.	Nakalonji	519	256	49.33
Jumla		2328	1341	57.69

Chanzo: Taarifa za MKURABITA kuhusu urasimishaji wa ardhi na biashara.

Mheshimiwa Spika, mafanikio na changamoto viliwyobainika kutokana na urasimishaji ni pamoja na:-

(a) Mafanikio

- i) Kupungua kwa migogoro ya matumizi ya ardhi na mipaka ya miliki katika vijiji husika;
- ii) Kuongezeka kwa usalama wa milki ya ardhi kwa wananchi waliorasimisha ardhi yao;
- iii) Wanawake wamepata fursa ya ama kumiliki Hati za Haki Miliki ya ardhi peke yao au kwa kushirikiana na Waume zao;
- iv) Baadhi ya wananchi wamekuza mitaji ya kiuchumi kutokana na kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kama dhamana ya kupata mikopo katika benki na taasi nyingine za kifedha;
- v) Mafanikio katika vijiji vilivyotekeleza urasimishaji yamekuwa chachu ya kuendeleza zoezi hilo katika Viji 24 ambapo

mashamba 251 yamepimwa na utaratibu wa kuandaa hati unaendelea; na

vi) Kuongezeka kwa thamani ya ardhi ya wananchi katika maeneo yaliyorasimishwa.

(b) Changamoto

i) Uhaba wa fedha unahafifisha utekelezaji wa MKURABITA katika maeneo mengine ya Halmashauri ya Nachingwea;

ii) Halmashauri inashindwa kuendeleza urasimishaji hata baada ya watendaji wake kujengewa uwezo wa kimafunzo na MKURABITA;

iii) Ukosefu wa Wataalam wa kuandaa na kusajili Hati za Haki Milliki za Kimila, jambo linalochelewesha kukamilika kwa hati hizo. Kutokana na kukosekana kwa Afisa Ardhi Mteule, hati hizo zinalazimika kupelekwa Halmashauri za Ruangwa au Masasi kwa ajili ya maandalizi na usajili;

iv) Baadhi ya Wananchi kushindwa kugomboa Hati za Haki Milliki za Kimila za maeneo waliyopimiwa;

v) Wamiliki wa Hati za Haki Milliki za Kimila kukosa ujuzi wa kuandaa maandiko ya miradi ambayo yatawawezesha kupata mikopo kutoka benki na taasisi nyingine za kifedha; na

vi) Wamiliki wa mashamba kuuza kiholela mashamba yao baada ya upimaji na hivyo kukwamisha zoezi la utoaji Hati za Haki Milliki za Kimila kutokana na upimaji wa awali.

2.2.2 Mradi Na. 6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASA) - Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini

Mheshimiwa Spika, Kamati ilitembelea Kijiji cha Namela kilichopo Wilayani Mtwara ambacho ni miongoni mwa vijiji 99 vinavyonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini katika Wilaya hiyo. Kijiji hiki kina jumla ya Kaya 117

zinazonufaika na mpango huu. Kaya hizo zimepokea ruzuku ya **shilingi milioni 109.99** kutokana na awamu 30 za uhawilishaji tangu kuanza kwa mpango huo Julai – Agosti, 2014 hadi Januari – Februari, 2019.

Aidha, TASAF imewezesha Kijiji cha Namela kutekeleza miradi ya utoaji wa ajira za muda kwa kaya zote 117 za walengwa kwa kugharamia mradi wa upandaji wa mikoko katika eneo la ufukwe wa Bahari ya Hindi lenye ukubwa wa ekari 4 kwa gharama ya **shilingi milioni 14.46** na ujenzi wa kisima cha pete kwa gharama ya **shilingi milioni 14.89**. Jumla ya **shilingi milioni 7.12** zilitumika kwa ajili ya ununuzi wa vifaa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

Vile vile, kupitia mpango wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya ambao unalenga kuziwezesha kaya zilizo katika mpango wa kunusuru kaya maskini kuwa na uwezo wa kukuza mitaji kwa ajili ya shughuli za kiuchumi ili kuongeza kipato, kuona umuhimu wa vikundi na umuhimu wa kuweka akiba katika kaya, jumla ya vikundi 8 vya kuweka akiba za kukuza uchumi wa kaya vimeundwa. Hadi Kamati inatembelea kijijini cha Namela **shilingi milioni 2.98** zilikuwa zimewekwa kama akiba ya vikundi hivyo.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilishuhudia namna ambavyo baadhi ya wanufaika wa mpango wametumia fedha za ruzuku kujenga na kuboresha makazi yao. Miongoni mwa wanufaika hao ni Bw. Abdallah Ismail Hamadi Tungwalu (65) na Bi. Fatuma Shamte Abdallah (81), ambao wametumia ruzuku wanayoipata kuwa chachu ya kujenga na kuboresha makazi pamoja na hali ya uchumi wa familia.

Bi. Fatuma Shamte Abdallah, ambaye ni mjane anayeishi na wajukuu zake wawili anaeleza kwamba, mpango wa ruzuku umemuwezesha kuboresha hali ya maisha kwa kuendesha ufugaji wa mbuzi na kuku.

Wajumbe wa Kamati walishuhudia nyumba bora ambayo inajengwa na Bi. Fatuma kwa kutumia saruji, mawe na mchanga. Akiongea kwa kujiamini Bi. Fatuma anasema, "*TASAF ndiye bwana angu. Mimi na wajukuu wangu tumetoka*

kula mlo mmoja, hadi sasa tunakula milo mitatu. Ninavaa kitenge kizuri, wajukuu zangu wanasona bila hofu kwani wanapata mahitaji muhimu ya Shule”.

Kwa upande wake Mzee Hamad anasema ruzuku ya kaya maskini ilimuwezesha kuwa mfugaji wa mbuzi kwa kuanza na mbuzi wawili (2) tu, lakini sasa wamefika 17. Aidha, kupitia mpango huo mbali na kumudu milo mitatu kwa siku, anatekeleza ujenzi wa nyumba ya matofali na saruji ambayo iko katika hatua ya renta.

Mheshimiwa Spika, kutokana na ukaguzi huo, Kamati ilibaini mambo yafuatayo: -

a) Mafanikio;

- i) Kuongezeka kwa kiwango cha mahudhurio ya watoto shulenii hasa wanaotoka kaya za walengwa, tofauti na awali. Hii inatokana na kukua kwa uchumi na kipato cha kaya kupitia ruzuku na shughuli za mpango kwa watoto wanaosoma shule;
- ii) Kaya zote 117 za walengwa katika Kijiji cha Namela zimejiunga na huduma ya Bima ya Afya ya Jamii (CHF) na hivyo kuwezesha walengwa kupata huduma za afya kutoka vituo vya kutolea huduma kwa gharama nafuu;
- iii) Kaya za walengwa zimeboresha makazi kwa kukarabati makazi ya awali au kujenga mapya kutokana na fedha za ruzuku. Jumla ya Kaya 67 za walengwa zimeboresha makazi. Idadi hiyo ni sawa na asilimia 57.26 ya kaya zote za walengwa 117;
- iv) Kuongezeka kwa mahudhurio ya kliniki kwa watoto walio chini ya miaka mitano kutoka kaya za walengwa kutokana na kaya kupata ruzuku ya kuboresha na kujenga afya ya mtoto na ukuaji wake;
- v) Watoto kutoka kaya za walengwa wanapata mahitaji muhimu ya shule kutoka kwa wazazi kama vile sare, kalamu na madaftari;

- iv) Walengwa wa mpango wametumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi ya kiuchumi kama vile, ufugaji, kilimo, na biashara na kuongeza kipato ambacho kimewasaidia kuboresha maisha; na
- vi) Kupungua kwa ajira za watoto wadogo kwani sasa wanahudhuria Shule.

b) Changamoto;

- i) Ushirikiano hafifu kutoka kwa watoa huduma za afya na elimu, ambao husababisha ugumu katika kupata taarifa za watoto wa walengwa wanaopata huduma katika maeneo husika;
- ii) Malalamiko kutoka kaya maskini ambazo hazijaingizwa kwenye mpango;
- iii) Kuchelewa kwa vifaa vyta mpango wa kuweka na kuwekeza katika vikundi vilivyoundwa na walengwa na hivyo kusababisha vikundi kutunza fedha katika mazingira yasiyo salama;
- iv) Baadhi ya wanakamati wa CMC kulalamikia ujira/posho kidogo wanayoipata; na
- v) Baadhi ya wananchi kukosa uelewa wa kutosha kuhusu utekelezaji wa mpango.

2.2.3Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

Mheshimiwa Spika, chuo hiki kilianzishwa rasmi kama Wakala wa Serikali, Agosti, 2000 kwa Sheria ya Wakala za Serikali Na. 30 ya Mwaka 1997, baada ya kuunganishwa kwa vyuo viwili, Chuo cha Watumishi wa Serikali (*Civil Service Training Centre*) kilichokuwa Dar es Salaam na Chuo cha Uhazili Tabora (*Tabora Secretarial College*).

Uanzishwaji wa chuo hiki ulilenga kusaidia maboresho katika Utumishi wa Umma ili kuwe na matokeo na tija katika utoaji wa huduma.

Mheshimiwa Spika, tangu kuanzishwa kwake, chuo ambacho ni nguzo muhimu ya mafunzo ya kiutumishi kwa Watumishi wa Umma nchini, kimeweza kuongeza matawi hadi kufikia sita ambayo yako katika Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Singida, Mbeya, Tabora na Tanga. Katika ziara yake, kwenye Kampasi ya Mtwara Kamati ilibaini mambo yafuatayo:-

(a) Mafanikio

- i) Tawi liliidahili watumishi 20 kwenye Mitihani ya Serikali (PSE) na watumishi 287 kwenye mafunzo ya muda mfupi;
- ii) Tangu mwaka 2009, tawi limetoa wahitimu 8,560 katika fani mbalimbali kwa ngazi za astashahada na stashahada;
- iii) Tawi limepunguza watumishi wa mikataba kutoka asilimia 76 hadi asilimia 41;
- iv) Tawi limepata usajili kamili kutoka Baraza la Ithibati la Elimu ya Ufundji Tanzania (NACTE); na
- v) Tawi linamiliki viwanja (Plot Na. 47 na 49) katika eneo la Shangani. Hii ni tofauti na Kampasi nyingine ambazo zinatumia majengo ya kupanga;

(b) Changamoto

- i) Tawi linakabiliwa na uhaba wa mabweni, jambo linalokwamisha ongezeko la udahili wa wanafunzi;
- ii) Tawi lina upungufu wa vitabu 200 ambavyo vingewezesha kuwa na uwiano mzuri kati ya mwanafunzi na vitabu;
- iii) Majengo matatu ya tawi (Block A, B, na C) yameanza kuchoka na kumomonyoka, na hivyo kuhatarisha usalama wa watumiaji; na
- iv) Mwitikio hafifu kutoka Wizara na Taasisi za Umma katika kutumia huduma za Chuo hicho.

3.0 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, ni maoni ya Kamati kwamba: -

- i) Wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini wanaweza kujikwamua kiuchumi iwapo watatumia sehemu ya ruzuku kuanzisha miradi midogo midogo ya kiuchumi kama vile biashara, ufgaji au kilimo. Aidha, Idara ya Maendeleo ya Jamii katika halmashauri isaidie kuwaelimisha walengwa hao;
- ii) Iwapo TASAF itahakiki na kusajili kaya maskini zilizosahaaulika katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, itasaidia kupunguza au kuondoa malalamiko mionganoni mwa wanajamili;
- iii) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umechangia kuboresha mahudhurio ya watoto wa kaya maskini shulenii na kliniki;
- iv) Bajeti finyu kwa MKURABITA inaathiri utendaji wa mpango huo na hivyo kukwamisha zoezi la urasimishaji;
- v) Watendaji wa halmashauri waliojengewa uwezo na MKURABITA, wanaweza kuendeleza zoezi la urasimishaji iwapo watawezeshwa kwa kupatiwa vifaa na raslimali fedha;
- vi) Benki na Taasisi za fedha zikielimishwa kuhusu hadhi ya Hati za Hakimiliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo, zitatoa mikopo kwa wananchi wanaomiliki ardhi kwa hati hizo;
- vii) Halmashauri zikipatiwa Wataalam wa Ardhi, zitasaidia MKURABITA kuharakisha zoezi la kurasimisha ardhi na kutoa Hati za Hakimiliki kwa wahusika; na
- viii) Iwapo Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Mtwara kitawezeshwa kumiliki viwanja Na. 41 na 46 vilivyo

jirani na kampasi hiyo, kitaweba kujenga mabweni na hivyo kuondoa usumbufu kwa wanafunzi wanaolazimika kupanga vyumba mbali na chuo.

4.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019

4.1 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2018/2019

Mheshimiwa Spika, katika kuchambua Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 Kamati ilijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa ajili ya shughuli zillizopangwa.

Njia kubwa zilizotumiwa na Kamati wakati wa uchambuzi huu ni pamoja na kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

4.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2018/2019 na kiasi kinachotolewa na Hazina. Kutokana na uchambuzi huo, Kamati imebaini kuwa:-

- i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji fedha (cash flow plan);
- ii) Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo (matumizi ya kawaida asilimia 76 na maendeleo asilimia 46);

iii) Fedha hazipatikani kwa wakati na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Ofisi hii.

Maelezo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa fedha zilizopokelewa na mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoka hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2019 (robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2018/2019) na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi umebainisha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2019 Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, pamoja na mafungu yaliyo chini yake, ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 374, 706, 943, 857/=** kutoka Hazina kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kiasi hicho ni sawa na **asilimia 65.03** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge.

Kiasi hicho cha fedha kimepungua kwa takribani **shilingi 43,072,387,704** (sawa na asilimia **10.31**) ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018 ambacho kilikuwa ni **shilingi 417,779,331,561**.

Kwa upande wa fedha za maendeleo uchambuzi umeonesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2019, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na mafungu yake, ilikuwa imepokea jumla ya **shilingi 82,052, 427,230/=** kutoka hazina, sawa na **asilimia 46. 87** ya fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya maendeleo.

Kiasi hicho cha fedha ni pungufu kwa **asilimia 60.31** ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/18 kwa ajili ya maendeleo ambacho kilikuwa ni **shilingi 206,720,967,511/=**.

Aidha, imebainika kwamba, kwa ujumla mwenendo wa upatikanaji wa fedha haukuwa mzuri, kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani **asilimia 65.03** ya fedha zote zilizoidhinishwa. Kwa tafsiri rahisi ni kwamba, kiasi cha asilimia 25 kilichopaswa kupatikana kwa kila robo ya mwaka wa fedha hakikuweza kupatikana. Kwa kuzingatia kiasi hicho ilitarajiwa kwamba hadi kipindi hicho kiasi cha fedha

kilichoidhinishwa kilipaswa kuwa kimepatikana kwa takribani **asilimia 70.**

Vilevile, katika kipindi hicho jumla ya **shilingi 292,654,516,627/** = zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida, sawa na **asilimia 72.95** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo. Tafsiri ya mwenenendo huo ni kwamba, kiasi hicho ni pungufu kwa takribani asilimia 1.99 ikilinganishwa na **shilingi 298,604,842,833** zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2017/2018.

Hali hiyo inaweza kutafsiriwa kwamba, kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kinachotolewa na hazina kimeendelea kuwa kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Hali hii imejitokeza kwa miaka mitatu ya fedha mfululizo tangu mwaka 2016/17 hadi 2018/19.

Mheshimiwa Spika, kwa ujumla uchambuzi umebaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka hazina siyo mzuri ikilinganishwa na miaka iliyopita kwani, kiasi kinachotolewa kimeendelea kupungua mwaka hadi mwaka huku fedha za maendeleo zikiwa pungufu zaidi ya zile za matumizi ya kawaida.

4.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati Mheshimiwa Spika, wakati wa kupitia na kuchambua Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Kamati ilitoa ushauri katika mambo Kumi na Saba (17) kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imezingatia kikamilifu baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati na inaendelea kuzingatia yaliyosalia. Baadhi ya maoni na ushauri vilivyozingatiwa ni kuhusu:-

i) Serikali kupunguza urasimu katika kuthibitisha Watumishi wa nafasi za uteuzi, ambapo iliweza kuidhinisha asilimia 81 ya

nafasi za uteuzi zipatazo 1,332 na taratibu za uteuzi zinaendelea;

- ii) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) itoe mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwawezesha kutekeleza majukumu yao kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Miongozo ya kiutendaji na hivyo kuепusha migongano isiyo ya lazima ambayo inaweza kuibuka. Mafunzo yalitolewa kwa wakurugenzi wa serikali za mitaa, wakuu wa wilaya, wakuu wa mikoa na makatibu tawala wa mikoa na wlaya;
- iii) Benki na Taasisi za fedha zielimishwe kuhusu hadhi ya Hati za Haki Miliki za Kimila kutumika kama dhamana ya mikopo, ambapo baadhi ya benki na taasisi za fedha zimeanza kukubali hati hizo baada ya kuelimishwa. Aidha, wananchi zaidi ya 500 wametumia hati hizo kukopa **shilingi bilioni 4.9** kutoka Benki za CRDB, NMB, PSPF na Agricultural Inputs Trust Fund. Vilevile, vyama vya wakulima vimedhamini wakulima kukopa jumla ya **shilingi milioni 625.9**;
- iv) Kutambua na kuandikisha Kaya maskini katika maeneo ya Vijiji 4,408, Mitaa 1,189 na Shehia 96 ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mpango wa ruzuku kwa kaya maskini, ambapo maandalizi ya awamu ya pili ya utekelezaji wa TASAF III yako katika hatua za mwisho na maeneo yote hayo yatafikiwa; na
- v) Watendaji wa Halmashauri washirikiane na MKURABITA, katika kuandaa na kutekeleza mpango bora wa matumizi ya ardhi na hivyo kupunguza au kuепusha migogoro ya ardhi baina ya makundi ya watumiaji katika jamii; ambapo zoezi hilo linatekelezwa katika Halmashauri za Misungwi, Mpwapwa na Serengeti.

5.0 UCHAMBUZI WA MPANGO NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020

5.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, Taarifa ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inayojumuisha Mafungu Nane (20; 30; 32; 33; 67; 94; 09 na 04) imeandaliwa kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoanishwa katika:-

- (i) Ilani ya Uchaguzi ya Mwaka 2015 ya Chama Tawala,
- (ii) Mwongozo wa Taifa wa Kuandaa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na
- (iii) Maeneo muhimu ya kuzingatiwa kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla ofisi hii pamoja na mafungu yake imepanga kutekeleza malengo **177** katika mwaka wa fedha ujao malengo hayo ni pamoja na:-

- i) Kutoa huduma kwa Rais na familia yake;
- ii) Kutoa huduma za ushauri kwa Rais katika maeneo ya uchumi, siasa, masuala ya jamii, sheria, mawasiliano na habari kwa umma, mahusiano ya kikanda, kimataifa na maeneo mengine;
- iii) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) kwa kushirikisha wadau wa sekta ya umma na sekta binafsi;
- iv) Kuratibu,kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na Mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

- v) Kuratibu na kusimamia miradi ya maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF) na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA);
- vi) Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino, na kukarabati majengo ya ikulu ndogo za Mwanza; Arusha, Mbeya, Zanzibar, Lushoto na nyumba mbili za wafanyakazi Tabora;
- vii) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya 2007;
- viii) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;
- ix) Kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kuliflikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na hivyo kujenga jamii inayochukia rushwa;
- x) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi "Postgraduate Diploma in Leadership" kwa lengo la kuwajengea uwezo viongozi katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia raslimali watu na raslimali nyingine na kuimarisha sifa binafsi za kiongozi;
- xi) Kuendelea kuratibu na kuwezesha timu za kitaifa za majadiliano ya mikataba yenyе thamani kubwa kulingana na uhitaji;
- xii) Kuanzisha vituo vitano vyta urasimishaji biashara ili kuwawezesha wafanyakabiashara kupata huduma muhimu sehemu moja katika halmashauri za wilaya tano za Kahama, Tabora, Nyamagana, Songea na Babati. Aidha, mafunzo ya kurasimisha na kuendesha biashara yatatolewa kwa wafanyakabiashara 5000 kwa lengo la kuwawezesha kusajili biashara zao;
- xiii) Kuratibu na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya majaribio ya Mfuko Endelevu wa Urasimishaji wa Wilaya katika Manispaa ya Iringa na Halmashauri ya Wilaya ya Njombe;

- xiv) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini zipatazo 355,000 katika vijiji 4,408, mitaa 1,189 na shehia 96, ambazo hazikuflikiwa katika awamu ya kwanza;
- xv) Kuhamasisha mamlaka zote 187 za utekelezaji wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini kuingia kwenye mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya kielektroniki (kupitia mitando ya simu na benki), ili kuwahisha malipo na kupunguza gharama za uendeshaji;
- xvi) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa kitaifa;
- xvii) Kusimamia mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa kampuni ya ndege ya taifa (ATCL);
- xviii) Kusimamia ajira za watumishi wa umma ambapo katika mwaka wa fedha 2019/20 serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 57,807 wa kada mbalimbali na kupandisha vyeo watumishi 290,625 wa kada mbalimbali;
- xix) Kuendelea na mchakato wa kutumia wa ujazaji wa fomu za matamko ya raslimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa njia ya mtando (*online application*) baada ya kukamilika kwa mfumo wa kielektroniki wa menejimenti ya taarifa za kimaadili (*ethics management information system - EMIS*);
- xx) Kufanya uhakiki wa matamko ya raslimali na madeni kwa viongozi wa umma 2,000;
- xxi) Kuandaa taarifa nne (4) za gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kiwango cha mshahara wenye staha ili kuwezesha kushauri kuhusu kiwango kinachoendana na gharama halisi za maisha;
- xxii) Kufanya ukaguzi wa kawaida katika taasisi 150 na ukaguzi maalum katika taasisi 10 kwa lengo la kuangalia uzingatiaji wa sheria, kanuni, taratibu na miongozo ya usimamizi wa raslimali watu katika utumishi wa umma;

xxiii) Kukusanya taarifa na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka taasisi za umma na watu binafsi; na

xxiv) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za taifa kwa kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa ya kidijitali (*digital records and archives management and preservation systems*) ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi.

Mheshimiwa Spika, ili iweze kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishiwa jumla ya **shilingi 683,529,211,617**. Kati ya fedha hizo **shilingi 483,661,966,000**. ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida, na **shilingi 199,867,255,617** ni kwa ajilli ya miradi ya maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida, **shilingi bilioni 35.4** sawa na asilimia 7.31 ni kwa ajili ya mishahara na **shilingi bilioni 448.25** sawa asilimia 92.69 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwa kuidhinishiwa katika mwaka ujao wa fedha imeongezeka kwa **shilingi 14,434,665,608** sawa na asilimia 2.16 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishiwa katika mwaka wa fedha 2018/19 ambayo ilikuwa **shilingi 669,094,556,009**.

Ongezeko hilo la fedha limebadili mwenendo wa bajeti ya ofisi hii kwa miaka miwili ya fedha iliyopita (2017/18 na 2018/19) ambapo bajeti ilikuwa ikipungua.

Aidha, kwa upande wa fedha za maendeleo, uchambuzi umebaini kwamba kiasi kinachoombwa kuidhinishiwa nacho kimeongezeka kwa kwa **shilingi 3,893,894,617** sawa na asilimia 1.99 ikilinganishwa na kiasi cha **shilingi 195,973,361,000** kilichoidhinishiwa katika mwaka wa fedha 2018/19.

Uchambuzi zaidi umebaini kwamba, ingawa ongezeko hilo limebadili mwenendo wa bajeti ya maendeleo ambayo imekuwa ikipungua kwa miaka miwili ya fedha iliyopita (2017/18 na 2018/19), bado kiasi kilichoongezeka ni kidogo

ikilinganishwa na kiasi kilichoongezeka katika fedha za matumizi ya kawaida. Aidha, licha ya ongezeko, bajeti ya maendeleo kwa mwaka ujao wa fedha ni takribani asilimia 51.12 tu ya bajeti ya maendeleo iliyoidhinishwa na Bunge katika mwaka wa fedha 2017/2018.

5.2 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka wa Fedha 2019/2020

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Uchambuzi umelenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelvezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji, na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

- i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ni **shilingi bilioni 683** sawa na asilimia 2.06 ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2019/20 ni **shilingi bilioni 33,105**;
- ii) Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 1.93, ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka 2018/19; ilihali bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/20 imeongezeka kwa asilimia 2.16 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2018/19;
- iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 2.0 katika fedha za maendeleo, ambazo ni sawa na asilimia 37 ya bajeti ya Taifa kwa mwaka wa Fedha 2019/20, wakati bajeti ya maendeleo kwa Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, ambayo ni sawa na asilimia 0.60 ya Bajeti ya Taifa,


imeongezeka kwa asilimia 1.99 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2018/19. Aidha, **Jedwali Na. 02** linafafanua zaidi juu ya ulinganisho baina ya maeneo hayo mawili.

Jedwali Na. 02: Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais (UUB) dhidi ya Bajeti ya Taifa, kwa mwaka wa fedha 2019/20


BAJETI KUU YA TAIFA 2019/2020			BAJETI YA OFISI YA RAIS – UUB 2019/2020		
Mgawanyo	Bajeti Kuu (Tsh.Milioni)	Asilimia ya Jumla ya Bajeti kuu	Mgawanyo	Bajeti ya Wizara	Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya Wizara
OC	3,576,706	10.80	OC	448,258,391,640	65.58
Deni la Taifa	9,721,127	29.36	-	-	-
Mishahara	7,558,974	22.84	Mishahara	35,403,574,360	5.18
Maendeleo	12,248,602	37.009	Maendeleo	199,867,255,617	29.24
Jumla	33,105,409	100	Jumla	683,529,211,617	100

Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa, na Randama ya Ofisi ya Rais – UUB kwa mwaka wa fedha 2019/2020

Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yanaoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01** na **Na. 02** kama ifuatavyo:-



Chanzo: Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20



Chanzo: Randama ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa fedha 2019/2020

6.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa miradi ya Maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: -

- i) Serikali iongeze kiasi inachotoa kuchangia utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini, kwani mchango wake ni mdogo sana. Tangu kuanza kwa mpango huu katika mwaka wa fedha 2013/2014, hadi taarifa hii inaandaliwa Serikali imechangia **shilingi bilioni 4.35** tu kati ya **shilingi bilioni 66.5** ilizopaswa kuchangia, sawa **asilimia 6.54**. kwa ufanuzi ufuatao: -

Jedwali Na. 03: Mchango wa Serikali na kiasi ilichotoa

Na.	Mwaka wa Fedha	Kiasi kilichoahidiwa (Tshs. Bilioni)	Kiasi kilichotolewa (Tshs. Bilioni)	Bakaa (Tshs. Bilioni)
01.	2013/14	18.50	3.00	15.50
02.	2014/15	14.00	0.60	13.40
03.	2015/16	14.00	0.00	14.00
04.	2016/17	14.00	0.00	14.00
05.	2017/18	3.00	0.75	2.25
06.	2018/19	3.00	0.00	3.00
	Jumla	66.50	4.35	62.15

- ii) Serikali iwezeshe wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini walioamua kujiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii (CHF), kutumia kadi hizo kupata huduma ya matibabu nje ya maeneo waliyosajiliwa. Aidha, kadi hizo zitambuliwe kwenye Hospitali/Vituo vya Afya na Zahanati binafsi kama ilivyo kwa aina nyingine za bima za afya;
- iii) Zoezi la kutambua na kuandikisha kaya maskini katika maeneo ambayo hayakufikiwa katika awamu ya kwanza ya mradi wa ruzuku kwa kaya maskini, lifanyike mapema ili kaya maskini katika maeneo hayo ziweze kunufaika. Takwimu zinaonesha kuna maeneo ya vijiji 4,408, mitaa 1,189 na shehia 96 ambayo hayajafikiwa na mpango;
- iv) Serikali kuititia TASAF iandae utaratibu ambao utawezesha kuwaondoa walengwa wa mpango wa kunusuru kaya maskini ambao wamejenga uwezo wa kujitegemea kiuchumi kutoka katika mpango huo, ili watoe nafasi kwa kaya maskini ambazo haziko katika mpango huo kuingizwa na kuanza kunufaika. Aidha, utaratibu huu utawafanya wanufaika watambue kwamba, unufaika wao ni wa muda na mara wanapo Jimudu kiuchumi wanapaswa kuondoka katika mpango (*to graduate*);

- v) Serikali iendelee kupunguza urasimu katika kuthibitisha Watumishi wa nafasi za uteuzi. Kamati imebaini kwamba, baadhi ya watumishi katika ofisi za umma wamekuwa wakikaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miaka miwili, kwa madai ya kusubiri upekuzi (*vetting*). Hali hiyo inawavunja moyo watumishi hao na kuathiri utendaji wao kwani hushindwa kufanya maamuzi ya msingi;
- vi) Halmashauri zitumie maafisa maendeleo ya jamii kuelimisha wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa kaya maskini namna wanavyoweza kutumia sehemu ya ruzuku hiyo kujikwamua kiuchumi;
- vii) Zoezi la kuhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini, litekelezwe kwa uangalifu ili kuepuka uonevu na malalamiko kutoka kwa waathirika;
- viii) Serikali iongeze Mshahara kwa Watumishi wa Umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka kila kukicha. Sote ni mashahidi kwamba, Serikali haijaongeza mshahara wa watumishi wa umma kwa mwaka wa tatu sasa;
- ix) Serikali iongeze bajeti ya MKURABITA na kutoa kikamilifu na kwa wakati fedha inayotengwa, ili kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji wa Ardhi na biashara za Wananchi. Hadi mwezi Februari, 2019 MKURABITA ilikuwa hajapokea fedha yoyote ya maendeleo kati ya **shilingi bilioni 1.5** zilizoidhinishwa na Bunge;
- x) Watendaji wa Halmashauri washirikiane na MKURABITA, katika kuandaa na kutekeleza Mpango bora wa matumizi ya ardhi na hivyo kupunguza au kuepusha migogoro ya ardhi baina ya makundi ya watumiaji katika jamii;
- xi) Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania, Kampasi ya Mtwara kiwezeshwe kumiliki viwanja Na. 41 na 46 kwa ajili ya ujenzi wa mabweni na hivyo kuondoa usumbufu wa Wanafunzi wanaolazimika kuishi mbali na chuo hicho;

xii) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi (Uongozi Institute) iendelee kutoa mafunzo ya Uongozi na Utawala kwa Viongozi wanaoteuliwa ili kuwakumbusha juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kiutendaji na hivyo kuepusha migongano isyo ya lazima. Kutolewa mafunzo hayo kumeanza kuzaa matunda ambapo vitendo vya ukiukwaji wa sheria za kiutendaji vimepungua; na

xiii) Kamati inapongeza juhudi za Serikali kupitia TAKUKURU za kushughulikia wala rushwa wakubwa kwa kuwafikisha mbele ya sheria. Hata hivyo, Kamati inashauri juhudi hizo pia zielekezwe kukabili vitendo vya rushwa ndogo ndogo zinazotendeka barabarani (askari polisi wa barabarani/madereva), hospitalini (madaktari na wauguzi) na mahakmani/mabaraza ya ardhi (waendesha mashitaka/makarani/mahakimu) n.k ambazo ni kero kwa wananchi. Aidha, Serikali iandae utaratibu wa kuingiza somo la maadili katika mitaala ya elimu ya msingi na sekondari ili kuandaa na kukuza kizazi chenye maadili na uzalendo.

7.0 HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, napenda kukupongeza wewe binafsi, kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili vema na kwa weledi na umahiri wa hali ya juu. Nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha Maoni ya Kamati kwa niaba ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa.

Napenda kumpongeza Mheshimiwa Naibu Spika, Dkt. Tulia Ackson, Mb, kwa umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge na Wenyeviti wa Bunge kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha vikao vya Bunge. Wote kwa pamoja tunawaombea afya njema katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Aidha, ninawashukuru kwa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano wao katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii ambaao umewezesha kukamilika kwa taarifa hii. Ninaamini

tutaendelea kushirikiana kikamilifu katika kutekeleza shughuli za Kamati, na hivyo kutimiza wajibu wetu wa kuwawakilisha wananchi na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa shughuli za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati hii inashughulikia mafungu mengi ya bajeti (mafungu 36) na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa wakati wa uchambuzi, ni wazi wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa saa nyingi wakati mwiningine hadi jioni kabisa. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa namna yoyote kwao na badala yake walitekeleza jukumu la uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu, ikiwa ni ishara ya utayari wao katika kuwatumikia Wananchi, Bunge na Taifa kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wa namna ya pekee ningetamani sana kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kutokana na ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina hayo ni haya yafuatayo: -

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanne Ismail Mcemba, Mb – Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margareth Simwanza Sitta, Mb,
4. Mhe. Angelina Adam Malembeka Mb
5. Mhe. George Malima Lubeleje, Mb
6. Mhe. Hamad Salim Maalim, Mb
7. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb
8. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb
9. Mhe. Mwatum Dau Haji, Mb
10. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, Mb
11. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb
12. Mhe. Venance Methusela Mwamoto, Mb
13. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb
14. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
15. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
16. Mhe. Ursula Michael, Mb
17. Mhe. Mansoor Hilani Shanif, Mb
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb

19. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb
20. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
22. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohamedali Raza, Mb
23. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
24. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
25. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
26. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Kamati ninamshukuru Mhe. Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika, (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora kwa ushirikiano wao kwa Kamati katika kipindi chote cha kutekeleza majukumu yake.

Nawashukuru pia watendaji wa wote wa ofisi hii wakiongozwa wakiongozwa na Makatibu Wakuu Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt. Lauren Ndumbaro (Utumishi), na Naibu Katibu Mkuu (Utumishi) Dkt. Fransic Michael kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kupitia taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Aidha, shukrani zangu ziwaendee pia wakuu wa taasisi, idara na vitengo viliwyopo chini ya ofisi hii kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa utekelezaji wa majukumu yake.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndg. Stephen Kagaigai kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, namshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Athuman Husein, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Angelina Sanga, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega na Ndg. Eunike Shirima, wakisaidiwa na Ndg. Modesta Kipiko, kwa kuratibu vizuri shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya taarifa hii.

Vilevile, napenda kuwashukuru watendaji wote wa Kitengo cha Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard) wakiongozwa na Bi.

Hanifa Masaninga kwa kuhakikisha taarifa hii inachapishwa kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, kama yalivyowasilishwa na Mto Hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja.

Dkt. Jasson S. Rweikiza (Mb)

MWENYEKITI

**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA
NA SERIKALI ZA MITAA**

10 Aprili, 2019

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa namuita Msemaji Mkuu wa Kambi Rasmi ya Upinzani. (*Makofi*)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema, kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na matumizi ya fedha katika Ofisi ya Rais (TAMISEMI) kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwapa moyo viongozi wangu wakuu wa CHADEMA, nikianza na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe, na Mheshimiwa Esther Matiko ambao walikuwa wamezuiliwa katika Gereza la Segerea Jijini Dar es Salaam kwa zaidi ya siku 100 kutokana na hujuma na hila walizofanyiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, napenda pia kuwapa moyo viongozi wengine wakuu wa CHADEMA ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu wa CHADEMA, Dkt. Vincent Mashinji, Naibu Makatibu Wakuu wa CHADEMA Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar, Waheshimiwa John Mnyika na Salum Mwalimu pamoja na baadhi ya Wabunge wa CHADEMA ambaao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiandamwa na kesi mbalimbali zikiwemo za uchochezi, jambo ambalo limeathiri sana utendaji wao wa kazi za chama. Napenda kuwaambia kwamba haya ni mapito ya muda mfupi tu lakini mwisho wa yote haki lazima itatamalaki kwa kuwa wema haujawahi kushindwa na uovu na kesho ni imara kuliko jana. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee, napenda kuishukuru familia yangu pamoja na wananchi wa Moshi Mjini kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya Kibunge. Nawaahidi kwamba nitaendelea kushirikiana nao na kutekeleza ahadi zangu za chama chetu kwao bila kuchoka. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka huu wa fedha 2019/2020, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa kujenga taasisi imara kwa maendeleo endelevu *that means building strong institutions for sustainable development*. Sababu kubwa ya kuendelea na msisitizo huo ni kwamba ili kuwa na uendelevu (*sustainability*) katika jambo lolote, ni lazima kuwe na mifumo imara ya kitaasisi, kanuni, taratibu na sheria zitakazofuatwa juu ya namna ya kutekeleza jambo hilo na siyo kufuata matakwa ya mtu au kikundi cha watu fulani katika kufanya hivyo kwa kuwa watu ni wa kupita lakini taasisi na mifumo itabaki. Tukumbuke kwamba Mwalimu Nyerere alituachia Taifa moja ambalo limekuwa halibaguani kikabilal wala katika imani za dini lakini kwa sasa kuna viashiria vya ubaguzi ndani ya nchi yetu kwa mitazamo ya itikadi za vyama vyetu. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary, unasoma kutoka wapi? Kwa sababu kitabu nilichopewa mimi hayo unayosoma yote hayamo.

WABUNGE FULANI: Aaaa, yameenda wapi?

MWENYEKITI: Jikite katika hotuba hii, ndiyo utaratibu, endelea.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKO NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba Mwalimu Nyerere alituachia Taifa moja ambalo ililiwa halibaguani kikabila wala katika imani wala dini lakini kwa sasa kuna viashiria vya ubaguzi ndani ya nchi yetu kwa mitazamo ya itikadi za vyama vyetu vya siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kila mwananchi ana haki ya kujunga na chama chochote cha siasa kilichosajiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi. Hivyo ni makosa makubwa sana kama Serikali itaruhusu wananchi wake wabaguane kwa misingi ya itikadi zao. Jambo hilo ni bayu na mbegu hiyo ikikomaa mionganii mwetu italisambaratisha Taifa letu. Ni vizuri tulirejeshe Taifa letu kwenye misingi yake ya umoja na mshikamano ambayo utu wa mtu ulikuwa unapimwa kwa matendo yake na sio kutokana na chama anachoamini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana kwamba taasisi tulizonazo zimekuwa dhaifu sana na udhaifu huo umesababishwa na viongozi wanaopenda kutawala kwa kutumia njia za mkato, wasiopenda kufuata taratibu za kisheria za kitaasisi. Tumeshuhudia sheria zikivunjwa na viongozi kwa kutoa kauli au matamko ambayo ni kinyume na sheria, watu wananyimwa haki zao za Kikatiba za kisheria lakini taasisi husika zinazotakiwa kukemea mambo hayo zimekuwa zikikaa kimya. [Maneno Haya Siyo Sehemu ya Taarifa Rasmi za Bunge]

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana hii ya kujenga taasisi imara ina umuhimu mkubwa sana pia kwa Serikali za Mitaa. Inajulikana kwamba Serikali za Mitaa ni chombo kikuu kinachotakiwa kuimarisha demokrasia katika maeneo ya wananchi na kutumia demokrasia hiyo kuharakisha

maendeleo ya wananchi. Jambo la kushangaza ni kwamba Serikali za Mitaa haziheshimiwi na kila mara Serikali Kuu inazipoka madaraka yake na vyanzo vyake nya mapato licha ya kwamba zimepewa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 145 na Ibara ya 147.

Mheshimiwa Mwenyekiti, matokeo ya kuziingilia Serikali za Mitaa ...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary, unachoweka Mezani ndicho kinachotakiwa kisomwe na hiki ndicho kilichowekwa Mezani.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni *summary*. Naomba nikuthibitishie haya ndiyo yaliyoko huko ndani.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary, mimi sioni popote humu hayo unayosoma.

MBUNGE FULANI: Anasoma *summary*.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Nasoma *summary*.

MWENYEKITI: Hapana, unasoma *summary*...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Nasoma *summary* ya hicho kitabu.

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, Kiti kinazungumza wengine mnakaa kimya, utawala bora ni pamoa na nidhamu ya kukaa kimya. (*Makofii*)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nachosoma hapa ni *summary*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary, *with due respect*, haya ya Mwalimu Nyerere yote humu hakuna, mengine yote hakuna, sasa kwa mujibu wa taratibu zetu za Kibunge kinachowasilishwa hapa ndicho kinachoingia kwenye *Hansard*.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, natakiwa nifanyeje sasa kwa sababu hayo niliyosoma ndiyo niliyoandika hapo.

MWENYEKITI: Tuanze ukurasa wa 3; dhana ya utawala bora katika utekelezaji wa shughuli za Serikali.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna hotuba mbili; kuna hotuba ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuna hii hotuba yangu mimi.

MWENYEKITI: Sisi kwenye Meza hapa tumepata hotuba moja tu.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, basi ndiyo maana hatuelewani.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Selasini, unasemaje?

MHE. JOSEPH R. SELASINI: Mheshimiwa Mwenyekiti, inawezekana kwamba taarifa uliyonayo ni taarifa iliyohaririwa kutokana na...

MWENYEKITI: Hapana, kuna taarifa mbili; kuna Utawala Bora na TAMISEMI na mpaka sasa hivi iliyokuja hapa ni ya Utawala Bora, wewe unasoma ipi? Mheshimiwa Japhary.

WABUNGE FULANI: TAMISEMI.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwa na utaratibu mzuri wa uendeshaji wa shughuli za Bunge, kama taarifa hii imechelewa kuchapishwa na Bunge, aanze kusoma taarifa yule ambaye taarifa yake imeshawasilishwa ndani, wakati huo tunasubiri hivyo vitabu vyaa taarifa hiyo nyingine vikiingizwa Bungeni...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Sasa Mheshimiwa *Chief Whip* wa upande wa Upinzani, Kiti kimepokea taarifa ya Kambi Rasmi ya Upinzani, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Ruth uje usome.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Kiti kimeshatoa agizo, Mheshimiwa Ruth njoo usome, Mheshimiwa Japhary subiri ripoti yako utasoma baadaye, akimaliza Mheshimiwa Ruth utasoma wewe.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAGI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Sawa.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tunaendesha Bunge kwa mujibu wa Kanuni...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Hatujasema hamtasoma, tunaisoma taarifa ambayo iko kwenye Kiti, Mheshimiwa Heche, tuliza ball. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Ruth, endelea kusoma taarifa ya Utawala Bora.

MHE. RUTH H. MOLLEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa heshima kubwa, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuhusu utendaji kazi wa Serikali, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya ufinyu wa muda, naomba hotuba yote hii iweze kuingizwa katika *Hansard* kama tulivyoasilisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumshukuru Mungu pamoja na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe, Mbunge wa Hai na Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini, kwa jinsi Mungu alivyokuwa pamoja nao gerezani kwa takriban miezi mitatu na nusu na kutoka salama. Tuko pamoja nao katika safari ya mabadiliko na demokrasia ya kweli. Niwapongeze pia viongozi wote ambao kwa njia moja au nyingine wanafahamu na kutekeleza kwa vitendo dhana nzima ya

utawala bora bila kujali nafasi zao za uongozi katika kuwahudumia wananchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upekee, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wetu wa ngazi za Kanda hadi Misingi, hasa kwa Mikoa ya Kanda ya Pwani, kwa ukomavu wao katika kutambua hakizao za msingi katika kutekeleza majukumu yao ya kisiasa licha ya vitisho vingi wanavyokumbana navyo kutoka kwa Watendaji wanaolipwa kwa kodi za wananchi. Naomba niendelee kuwatia moyo kwamba Tanzania inapita katika kipindi cha mpito kuelekea demokrasia ya kweli, japokuwa tunarudi nyuma, uvumilivu ni muhimu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho lakini kwa umuhimu sana naishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kunipa moyo katika majukumu yangu haya ya Kibunge na kisiasa, ambayo kwa namna moja au nyingine naendelea kujifunza. Nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kaulimbiu ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni "Ujenzi wa Taasisi Imara kwa maendeleo endelevu". Ni dhahiri kwamba japokuwa hatuna Katiba Mpya ambayo ni nguzo kuu ya ujenzi wa taasisi imara katika usimamizi na uendeshaji wa Serikali lakini bado Ofisi ya Rais, hasa, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kutumia sheria zilizopo inatakiwa kuwa kioo cha jamii katika kutimiza majukumu yake ili kuhakikisha utawala bora unasimamiwa na kujenga utumishi wa umma uliotukuka wenyewe ari na utashi wa kufanya kazi kwa misingi ya utu, huku ukizingatia misingi ya sheria na kanuni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hotuba hii au hoja iliyombele ya Bunge lako Tukufu kwa siku ya leo imejikita katika mafungu saba ambayo yameainishwa katika (i)- (vii) katika ukurasa wa 4.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mafungu hayo, Ofisi hii ya Rais inasimamia pia Taasisi ya Kupambana na

Kuzuia Rushwa. Hata hivyo, nitazungumzia tu baadhi ya maeneo ambayo kwa maoni yangu yanahitaji msisitizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kutokana na uhaba wa taarifa au kukosekana kwa uwazi katika utendaji kwa baadhi ya mafungu, nitashindwa kuyatolea kauli kulingana na utendaji wake lakini naamini tutasaidiana na Waheshimiwa Wabunge wengine katika kutimiza wajibu wetu kuvisimamia Ofisi hii ili utendaji wake ufuate misingi na kanuni za utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana ya utawala bora katika utekelezaji wa shughuli za Serikali. Dhana nzima ya utawala bora imejikita katika matumizi ya mamlaka ya kisiasa na kiuchumi katika kusimamia masuala ya nchi kwenye ngazi zote. Hivyo basi, utawala bora ni matumizi ya mamlaka ambayo yanakuwa na uwazi, uwajibikaji, ushirikishwaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu na usawa unafuata utawala wa sheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatua ya Tanzania kujitoa rasmi katika Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (*Open Government Partnership*) ni hatua ambayo inazua wasiwasi kuhusu utekelezaji wa Sera ya Uwazi na Uwajibikaji ilioasisiwa na Rais Mstaafu Mheshimiwa Jakaya Kikwete mwaka 2011. Hatua hiyo ya kujitoa kwa Tanzania ina maana kwamba mipango yote ya Serikali itakuwa ikiendeshwa kwa usiri mkubwa, itafanyika gizani, hakutakuwa na uwazi tena. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema huu ni ushahidi wa wazi kwamba utawala bora kwa sasa ni jambo ambalo halipo na yote yanayofanyika tayari yanakuwa yamepangwa, hivyo, kuwanyima wananchi haki ya kuhoji matumizi sahihi ya rasilimali za watu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lengo mahsusili la utawala bora ni kukuza demokrasia na uwajibikaji katika jamii na kuhakikisha kuwa wananchi na viongozi wanawajibika ipasavyo kadri inavyowezekana katika majukumu yao na pia kuelekeza rasilimali za nchi kutoa matokeo chanya kwa ajili ya ustawi wa wananchi na maendeleo yao kwa ujumla. Hoja

ya msingi hapa ni je kweli utawala bora wenye kuzingataia sheria unatekelezwa na Awamu ya Tano? Tumeshuhudia baadhi ya maamuzi yanayokiuka kanuni za utawala bora na uwazi katika utendaji kazi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushahidi wa wazi ni kama kwa mfano, Bunge Tukufu kufanya kazi zake bila wananchi kuona nini kinafanywa na wawakilishi wao, hivyo kuwanyima wananchi haki yao ya msingi kufuatilia uwajibikaji wa Serikali na matumizi ya fedha zao. Pia kutofahamu jinsi gani Serikali inatatua kero zao kupitia wawakilishi wao Bungeni. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, usawa mbele ya sheria. Vyama vya upinzani kunyimwa haki ya kuwa na vikao kwa kisingizio cha taarifa za intelijensia ilhali chama tawala klinakutana na kuandamana chini ya ulinzi wa Polisi. Hii ni *double standard* na haikubaliki. Vilevile, wananchi kukamatwa holela kwa kisingizio cha uchochezi wanapokosoa utendaji wa Serikali. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa viashiria vilivyoainishwa hapojuu, utawala wa sheria unaendelea kuporomoka nchini. Hivyo basi ili kujenga umoja wa taifa, amani na utulivu, Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na usalama, haina budi kuzingatia utawala wa sheria ambao tumejiwekea kama nchi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza sheria zote kandamizi zinazozuia uhuru wa habari na demokrasia ya kweli zihuishwe ili Watanzania watembee kifua mbele katika nchi yao kuliko ilivyo sasa ambapo woga umekithiri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutekeleza dhana ya utawala bora mambo yafuatayo lazima yazingatiwe. Kwanza ni matumizi sahihi ya dola. Eneo hili bado linahitaji kufanyiwa kazi zaidi kwani pamekuwa na matukio mengi ya wananchi kupigwa, kujeruhwa na kufariki kwenye vituo vya polisi. Vilevile kubambikiziwa kesi na kuwekwa mahabusu kwa makusudi hata kwa kesi zinazodhaminika. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mbili, matumizi mazuri ya rasilimali kwa faida ya wananchi. Pamoja na juhudini zinazofanyika bado kuna ujisadi kwenye miradi mikubwa ya ujenzi, ukwepaji wa kodi na matumizi nje ya bajeti inayopitishwa na Bunge. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatu, matumizi mazuri ya madaraka. Baadhi ya viongozi wa kisiasa, hasa Wakuu wa Mikoa na Wilaya, wanavuka mipaka katika kutumia madaraka yao kwa kuweka raia rumande kwa zaidi ya saa 24 na 48 kwa mujibu wa Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 1997 bila kuwapeleka mahakamani na hakuna hatua zozote zinachukuliwa dhidi yao, matokeo yake chuki inajengeka kwa wananchi dhidi ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri yafuatayo:-

(a) Kutoa mafunzo ya mara kwa mara kwa wateule hao wa kisiasa waelewe jinsi Serikali inavyofanya kazi.

(b) Wafanyiwe upukuzi kabla ya kuteuliwa na wenye dosari za maadili na mwenendo usioridhisha hata katika maisha yao binafsi wasipewe madaraka.

(c) Serikali irejeshe mfumo wa zamani wa kuandaa viongozi kwa kutambua maafisa wenye viashiria vya uongozi (*leadership potentials*), waandaliwe mafunzo ya muda mrefu na mfupi na wakati huohuo mienendo yao inafuatiiliwa. Tunaamini mfumo huu ukiwa endelevu nchi yetu itapata viongozi bora wenye weledi, maadili, uzalendo na uadilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jinsia na utawala bora. Tunapozungumzia utawala bora, huwezi kuacha kuzungumzia usawa wa jinsia katika mgawanyo wa madaraka na rasilimali za nchi. Asilima 75 ya wanawake ndiyo wazalishaji wakubwa vijijini, hivyo basi, ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi ni jambo la msingi kabisa. Mtakubaliana nami kwamba mahitaji ya wanawake na wanaume ni tofauti kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa msingi huo, uwakilishi wa wanawake katika ngazi za maamuzi, hasa kwenye sera, sheria na kanuni itasaidia kujumuisha mahitaji ya wanawake na watu wenyewe mahitaji maalum. Pamoja na kwamba Kamusi ya Kiswahili ya *Oxford* inatafsiri jinsi kuwa ni "masuala yanayoambatana na mambo yanayohusu mwanamke na mwanamume" lakini kwa hali halisi wanawake ndiyo wenyewe uwakilishi mdogo. Hivyo basi, ili utawala bora uonekane kuwa upo katika jamii, usawa wa jinsia ni kipimo kimojawapo cha utawala bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba Kamusi ya Kiswahili ya *Oxford* inatafsiri jinsi kuwa ni "masuala yanayoambatana na mambo yanayohusu mwanamke na mwanamume" lakini kwa hali halisi wanawake ndiyo wenyewe uwakilishi mdogo. Hivyo basi, ili utawala bora uonekane kuwa upo katika jamii, usawa wa jinsia ni kipimo kimojawapo cha utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuzingatia Kipimo cha Tofauti ya Kijinsia, Tanzania iliporomoka nafasi nne kutoka 125 hadi ya 129 kati ya nchi 188 katika ripoti ya mwisho ya maendeleo ya binadamu duniani (*UNDP 2016*). Juhudi zimeendelea kufanywa katika kuongeza uwakilishi wa wanawake Bungeni, usawa wa kijinsia katika Elimu ya Msingi, ongezeko la wanawake katika kazi na kuongeza umri wa kuishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata Hivyo, tofauti bado imeendelea kuonekana katika uwiano wa wanawake katika nafasi za maamuzi katika ngazi za Mikoa na Serikali za Mitaabu na katika nafasi za uongozi wa juu na kati. Wakati huo huo, wanaume wanachukua takriban asilimia 82.6 ya nafasi za uongozi ikilinganishwa na asilimia 17.4 za wanawake.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchanganuo wa baadhi ya nafasi zilizoongezeka zinazoshikiliwa na wanawake tangu mwaka 2006 hadi 2010 kabla ya uchaguzi Mkuu ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulikuwa na Majaji 13 wakaongezwa wakawa 34; Mawaziri 4 wakawa 10; Makatibu Wakuu 7 wakawa 9; Makatibu Tawala za Mikoa 4 wakawa 10; Wakuu wa Wilaya 20 wakawa 25; Wakurugenzi wa Halmashauri 14 wakawa 35; na Wakurugenzi kwenye Wizara na Taasisi 19 hadi 133.

Aidha, kufuatia matokeo ya Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani uliofanyika Oktoba, 2010, idadi ya Wabunge wanawake ilifikia 126, sawa na asilimia 36 ya Wabunge wote 350 waliokuwepo wakati huo. Aidha, idadi ya Mawaziri wanawake ilikuwa ni asilimia 26.7 ya Mawaziri wote 30 waliokuwepo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Mtandao wa Jinsia Tanzania, Dkt. Shule wakati wa maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani, tarehe 8/3/2018 na kuandikwa kwenye gazeti la Nipashe la tarehe 15/3/2018 ilionesha kwamba ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi umeshuka kutoka 38% Awamu ya Nne hadi 19% Awamu ya Tano. Uwiano wa wanawake na wanaume katika ngazi za uongozi Serikalini ni 28:72 ikiwa ni wanawake 2,573 na wanaume ni 6,674.

Mheshimiwa Mwenyekiti, aidha, Baraza la Mawaziri, katika Serikali ya awamu ya nne lilikuwa na Mawaziri 57. Kati ya Mawaziri hao, idadi ya wanawake walikuwa ni 16 sawa na 28%. Baraza la Mawaziri katika Serikali hii ya Awamu ya Tano ni Mawaziri 35 kati yao wanawake ni 9 tu sawa na 25%. Idadi hii ni pungufu kwa 3%. Kwa upande wa Mabalozi katika Serikali ya Awamu ya Nne, idadi ya wanawake walikuwa ni 36% na Awamu ya Tano ni 21%. Wakuu wa Wilaya Awamu ya Nne wanawake walikuwa ni 40% na Awamu ya Tano ni 16%.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa Mtandao wa Kijinsia Lilian Liundi, baada ya utafiti wake aliona kuwa tathmini ya jumla ni kuwa ikilinganishwa na Awamu ya Nne, idadi ya Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wanawake imepungua kwa kiasi kikubwa. Takwimu za mwaka 2014 zinaonesha kuwa idadi ya

wanawake waliokuwa Makatibu Wakuu au Manaibu Katibu Wakuu ilikuwa 20 sawa na asilimia 37.7 huku wanaume wakiwa 33 sawa na asilimia 62.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika uteuzi uliofanyika Awamu ya Tano, Idadi ya Wabunge wanawake Bungeni kwa sasa ni 145 kati ya wabunge 392 waliopo, ikiwa ni ongezeko la Wabunge wanawake 19 sawa na asilimia 13.1 kulinganisha na waliokuwepo katika Bunge la Kumi. Jumla ya wanawake Makatibu Wakuu na Manaibu ni 10 sawa na asilimia 20 tu huku asilimia 80 inayobakia ikishikiliwa na wanaume. Kwa kuzingatia takwimu hizo, ni dhahiri kuwa idadi ya Makatibu Wakuu na Naibu Makatibu Wakuu wanawake imepungua kutoka asilimia 37.7 mwaka 2014 hadi asilimia 20 mwaka 2016. Hii ni tofauti ya asilimia 17.7 ambayo ni kubwa sana na hivyo kuongeza pengo la jinsia katika nafasi za kufanya maamuzi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa takwimu hizo, ni dhahiri uwakilishi wa wanawake kwenye ngazi za juu za maamuzi umeporomoka sana ilhali wanawake ni zaidi ya 50% ya Watanzania wote na pia ni zaidi ya 70% ya nguvu kazi katika uzalishaji wa chakula kinachotumika nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kurejea tena kwenye meza na kuongeza idadi ya wanawake kwenye ngazi ya maamuzi ili wanawake ambaao ni zaidi ya 50% ya Watanzania wapate uwakilishi. Wanawake ni jeshi kubwa kama wanavyotambuliwa kwenye Biblia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa taarifa hii, TAKUKURU inaangaliwa kama zana mojawapo ya kusimamia utawala bora katika nchi. Ili zana hii iweze kufanya kazi kwa ufanisi, inatakiwa iwe huru na kufanya kazi zake bila ya kuingiliwa na mamlaka yoyote ile. Aidha, lengo kuu la Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya 2007 imeainishwa katika kifungu cha 4 cha Sheria hii ikiwa ni kuhakikisha ustawi wa utawala bora na kuondoa rushwa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hii ni taasisi huru ya uchunguzi kwa mujibu wa sheria hiyo, lakini uhuru wake

hauonekani, kwani haiwezi kupeleka kesi Mahakamani hadi ipate kibali toka Ofisi ya Mwendesha Mashtaka. Hapa ndipo walakini wa zana hii unapotiliwa mashaka katika kadhia nzima ya uwazi na uwajibikaji kwa Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonesha kuwa hadi Septemba, 2016 kesi mpya zilizofunguliwa Mahakamani na TAKUKURU zilikuwa ni 338. Kati ya hizo washtakiwa walioachiwa huru na Mahakama ni 214 sawa na 63.3% na kesi zilizoondolewa Mahakamani ni 39 sawa na 11.53% na kesi 3 zilikatiwa rufaa. Kwa takwimu hizo ni kuwa, kesi zilizokuwa za halali ni 25.16% tu. Hii maana yake ni kuwa Taasisi hii inafanya kazi zake siyo kwa kuzingatia ushahidi uliopo bali ni kwa hisia. Jambo hili siyo tu linaondoa haki za watuhumiwa, bali pia linapoteza muda na fedha za walipakodi wa nchi hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa TAKUKURU isimkamate mtu yejote bila ya kuwa na ushahidi wa kutosha kumfikisha mhusika Mahakamani. Takwimu za walioshinda kesi ni ushahidi kuwa kesi nyingi zinafunguliwa bila ya ushahidi wa uhakika, matokeo yake ni kuathiri maisha ya wahusika na familia zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mashaka ya uhuru wa taasisi hii muhimu, unakuja pale inapowakamata watuhumiwa na kuwafikisha Mahakamani wakati huo huo huna ushahidi wa kutosha kuendesha kesi hiyo. Jambo hilo linasababisha watuhumiwa kukaa mahabusu kwa kipindi kirefu sana na kusababisha uvunjifu wa haki za msingi za wahusika. Hivyo basi, badala ya kuwa zana ya utawala bora inakuwa zana ya uvunjifu wa utawala bora. Hii ni hatari sana kwa nchi inayojenga mifumo huru ya utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kutenda haki na kutumia vyema kodi za wananchi, kuepuka usumbufu na uonevu kwa kushukiwa, TAKUKURU ikamilishe uchunguzi na kupeleka washukiwa Mahakamani badala ya rumande ili watuhumiwa wapate haki yao ya kuachilliwa huru au kuhukumiwa kwa sababu “*Justice denied is Justice delayed.*”

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona sasa ni muda muafaka kwa taasisi hii kuwa huru, kwa maana kuwa Watendaji wake Wakuu wasiteuliwe na Rais, bali waombe nafasi hizo na wafanyiwe usaili na jopo la wataalam na kuidhinishwa na Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa muktadha wa hotuba hii Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inatumika kama zana mojawapo ya kuonesha uwepo wa Utawala Bora katika nchi. Uwepo wa taasisi hii umeelezwa bayana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano Tanzania Ibara ya 129 na majukumu yake yameelezwu katika Ibara ya 130. Aidha, Tume ilianzishwa na sheria yake mahususi ambayo ni sura Na. 39 ya marejeo ya sheria ya mwaka 2002 ya sheria za Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tume hiyo imepewa majukumu mengi na ya muhimu katika kusimamia utawala bora na haki za binadamu ambazo ni pamoja na kufuatilia na kulinda haki za binadamu kama ambavyo zinælekezwa na Katiba yetu, pia kufanya uchunguzi kuhusu mambo yote yanayohusisha uvunjifu wa haki za binadamu hapa nchini. Tume hiyo pia ina majukumu ya kufanya utafiti ya haki za binadamu na utawala bora na kuielimisha jamii kuhusiana na mambo hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na mambo mengine, ukiukwaji wa haki za binadamu unatokea pia pale vyombo vyta dola vinapofanya matendo yanayokiuka haki za binadamu, kwa mfano, kupiga raia au watuhumiwa, kuwatesa, kuwanyima dhamana na kuwashikilia bila kuwafikisha Mahakamani kwa mujibu wa muda uliowekwa kisheria. Ili Tume iwe na mamlaka kama inavyotakiwa, ni muhimu sana mapendekezo yaliyotolewa katika Rasimu ya Pili ya Katiba ya Jaji Warioba kufuatwa katika kuifanya Tume kuwa chombo kinachosimamia pia mgawanyo wa madaraka baina ya vyombo vyta dola.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nakuja kwenye Sekretarieti ya Maadili. Maadili ni moja ya tunu muhimu zinazolitambulisha na kutofautisha Taifa moja na lingine. Maadili mema ni

kichocheo kikubwa cha maendeleo ya Taifa, hujenga umoja, amani, upendo, uvumilivu na mshikamano katika Taifa. Maadili yana umuhimu mkubwa sana katika utawala na maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kuwezesha Sekretariat kufanya kazi zake za kiuchunguzi, inaongozwa na sheria ili kutimiza majukumu yake, kifungu cha 27 cha Sheria Na. 13 ya mwaka 1995 kinamtaka Mheshimiwa Rais kuteua watu watatu ili kuunda Mahakama au Baraza kwa minajili ya kusimamia uchunguzi wa malalamiko dhidi ya viongozi wa Umma yanayowasilishwa kwenye chombo hiki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa hadi sasa wateule hao kwa ajili ya kusimamia uchunguzi wa malalamiko ya viongozi wa Umma bado hawajateuliwa, maana yake ni kwamba Sekretarieti halwezi kufanya kazi zozote za kiuchunguzi dhidi ya mienendo ya viongozi wa Umma yalivyowasilishwa kwa Tume.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba Mheshimiwa Rais atue Baraza hilo kwa mujibu wa Sheria Na.13 ya mwaka 1995 ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake, vinginevyo dhana ya Utawala bora haitafikiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Menejimenti ya Utumishi wa Umma fungu 32. Wateja wakubwa katika Utumishi wa Umma ni wananchi na mara zote wananchi wataendelea kudai huduma bora. Katika kutimiza matakwa hayo ya wananchi, Serikali inalazimika kuhakikisha watendaji katika Sekta ya Umma wanakidhi matakwa ya wateja ambao ni wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili kukidhi haya, kumekuwepo na kile kinachoitwa Mkataba wa huduma kwa wateja; ni makubalino ya kimaandishi baina ya taasisi itoayo huduma na wateja wake. Mkataba huu unafafanua huduma zote zinazotolewa na taasisi, kuweka viwango vya huduma, muda wa kutoa huduma hizo, majukumu na wajibu wa mteja na taasisi. Aidha, mkataba unapanga mbinu za kupata

majibu ikiwa ni pamoja na kushughulikia malalamiko ya Umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hoja ya msingi ya kuuliza hapa: Je, mikataba ya aina hiyo kuandikwa "huduma kwa wateja" zimeimarishwa katika utumishi wa Umma? Ukweli ni kwamba ni bado.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na mambo mengi mazuri ambayo yalikuwepo hapo awali ikiwemo la ugatuaji wa madaraka kwenda Serikali za Mitaa, lakini bado kukosekana mifumo imara ya ufuatiliaji na tathmini. Udhifu wa mifumo imara inasababisha Serikali kushindwa kupima malengo ambayo yamewekwa kulingana na utendaji binafsi wa mtumishi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ukweli kwamba iwe katika sekta binafsi au ya Umma pale penye mifumo imara ya ufuatiliaji na tathmini. Taasisi zimepiga hatua zaidi ya mifumo hiyo, inakuwa ni chachu katika utoaji wa huduma bora na matokeo chanya yanakuwa wazi kila mmoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uundwaji wa mifumo imara katika taasisi zetu ili kuwa na matokea chanya ni matokeo ya uwepo wa mipango thabiti katika taasisi zetu, lakini mipango ili iwe mipango ni lazima iandane na bajeti zilizopangwa katika utekelezaji wake. Kumekuwa na tatizo kubwa sana katika upatikanaji wa fedha za maendeleo kukidhi mahitaji ya ujenzi wa mifumo imara, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa linaathiri utendaji katika utumishi wa umma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano mzuri, fungu 32 kwa Ofisi ya Raisi miaka miwili yaani 2017/2018 na 2018/2019, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yenye majukumu ya kuimarisha Utawala Bora katika uendeshaji wa shughuli za Serikali, kwa kubuni Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji na usimamizi wa shughuli za utumishi wa umma pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa Umma ili watoe huduma bora kwa wadau wake. Kwa mwaka wa fedha 2017/2018 ilitengewa jumla ya

shilingi 33,695,038,000/=. Kati ya fedha hizo, fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zilikuwa ni shilingi 7,000,000,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mwaka wa fedha 2018/2019 fungu 32 lilitengewa jumla ya shilingi 12,947,029,261/= kama matumizi ya kawaida na shilingi 10,939,000,000/= kwa matumizi ya maendeleo. Kwa kufanya ulinganisho wa miaka hiyo miwili ni kwamba bajeti kwa fungu hilo 32 imepungua kwa shilingi 9,809,008,739/= sawa na asilimia 29.11. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinazopangwa na kuombewa idhini ya matumizi zitoke kama zilivyohitajika, kwani kinyume na hapo ni kuzorotesha mipango yote iliyokusudiwa kufanyika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya lengo kuu la maboresho ya Serikali za Mitaa ya kuhusiana na ugatuaji wa Madaraka ilikuwa ni kuwa na mfumo huru wa kiutawala katika ngazi ya Serikali ya Mitaa ambapo Baraza la Madiwani lilikasimiwa madaraka ya kusimamia sera na utoaji wa huduma na kusimamia watendaji katika ngazi hizo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mtazamo huo wa ugatuzi wa madaraka ilikuwa ni kujenga mfumo imara wa kiutawala ambao ungekuwa ni nguzo kuu ya kuimarisha utoaji wa huduma na utoaji wa maamuzi katika ngazi za Serikali za Mitaa. Ukiwa na uwezo wa kutoa maamuzi, maana yake una uhakika wa uendeshaji wa eneo husika bila ya kutegemea msaada wa aina yoyote kutoka ngazi yoyote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, malengo maalum ya Programu hiyo yalikuwa ni; kugatua madaraka ya Serikali na kuyapeleka kwenye Serikali za Mitaa; kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kuititia watumishi wa Umma; kuziwezesha Halmashauri kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake na kuwa na mfumo wa mgawanyo wa mapato kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa masikitiko makubwa ni kwamba uwekezaji wote huo uliofanywa wa kupeleka ugatuaji ambao uligharimu milioni za Kimarekani 150 ni kwamba uwekezaji wote huo uliofanywa na Serikali za Awamu ya Tatu na Awamu ya Nne umekuwa ni kazi bure, kwa sababu Serikali ya Awamu ya Tano imechukua vyanzo vikubwa vya mapato kama vile kodi ya majengo, malipo ya mabango, vile vile baadhi ya watumishi wa Wizara za Ujenzi, Ardhi, Maji, Kilimo wanasmamiwa moja kwa moja na Wizara husika kinyume kabisa na Sera ya *D by D*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tanzania ina kilometa za mraba 950,000. Hivyo ni vigumu sana Serikali Kuu kufika kila pembe ya nchi hii, ndiyo maana *D by D* lilibuniwa kuimarisha Serikali za Mitaa kwa kuwapatia fedha na wataalam ili huduma zitolewe na kusimamiwa kwa karibu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuendeleza mfumo wa *D by D* ulioanza kutekelezwa na Awamu zilizopita kwa kuimarisha mifumo ya uratibu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ambayo ndiyo majukumu ya msingi ya Serikali.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaruka kidogo nitakwenda kwenye rasilimali watu kwamba rasilimali ndiyo kichocheo kikubwa cha kuendesha nchi na katika sera yetu ya CHADEMA kwa kutambua umuhimu mkubwa wa Rasilimali watu/nguvukazi katika ukuaji wa uchumi na kuwa na maendeleo endelevu. Katika sera zake ukurasa wa 33 & 34 imeeleza kwa kina ni jinsi gani jambo hilo linatakiwa lipatiwe kipaumbele kutohana na ukweli kwamba idadi ya watu inazidi kuongezeka siku kwa siku.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kwamba pamoja na uwekezaji kwenye miradi mikubwa, kufikia lengo la Tanzania ya Viwanda, ni muhimu sana kwa Serikali kuainisha utaalam unaohitajika ili kukidhi mahitaji ya lengo la Tanzania ya viwanda.

Kuhusu maslahi ya Umma. Mshahara kwa mtumishi ni haki yake ya msingi kisheria na siyo hisani ya mwajiri. Aidha, mishahara mizuri ni motisha kwa watumishi kufanya kazini kwa hiari na ubunifu. Watumishi wanapolipwa mishahara inayotosheleza mahitaji ya msingi huchochea ukuaji wa uchumi kupitia kodi wanazolipa na wanaponunua bidhaa mbalimbali, hivyo kuchangia kuinua kipato cha watu wenye uchumi duni kwa kuongeza mzunguko wa fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha kwamba za *Employment and Earnings Survey* inayotolewa na *NBS* zinaonesha kwamba watumishi katika Sekta ya Umma ambao ni takriban 15.3% ya waajiriwa wote katika sekta iliyo rasmi wanapokea kati ya Shilingi 500,001/= na shilingi 900,000/= na takriban 8.1% inapokea mshahara wa kati ya 300,001/= na shilingi 500,000/=.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa viwango hivi vya madaraja ya mishahara ni vidogo mno kuweza kukidhi mahitaji ya msingi ya watumishi. Hivyo ni rai ya Kambi kuwa viwango vya mishahara vipangwe kulingana na hali halisi ya maisha ilivyo na pia vilinganishwe na dola au sarafu ambayo Serikali inafanya manunuzi yake nje kupitia sarafu hiyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukiwalipa vizuri wafanyakazi watakuwa na uwezo wa kufanya manunuzi ya bidhaa za kilimo kwa bei nzuri, hivyo kuinufaisha Sekta ya Kilimo, mkulima na pia viwanda kwa sababu watakuwa na uwezo wa kununua bidhaa na hivyo kuongeza ajira katika sekta binafsi na uchumi wa viwanda kukua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ujenzi wa uchumi wa viwanda unategemea sana uwezo wa wananchi kufanya manunuzi ili uzalishaji wa bidhaa kwa viwanda uwe endelevu. Viwanda haviwezi kuzalisha kwa kutegemea soko la nje tu. Tukumbuke, Tanzania kwa idadi yake ya watu ni soko kubwa kwa viwanda vyetu kama tu wananchi watakuwa na uwezo wa kufanya manunuzi. Kinyume cha hapo, ni kujidanganya kuwa tunajenga Tanzania ya viwanda wakati watanzania

hawana uwezo wa kufanya manunuzi kwa bidhaa tunazozalisha wenyewe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ili tutoke katika mkwamo huu, Serikali haina budi kuhakikisha inalipa vizuri mishahara kwa wafanyakazi na watumishi wa Umma ili kuongeza mzunguko wa fedha kwenye jamii. "*Purchasing power*" inatoa nguvu zaidi kwa wawekezaji kwenye Sekta ya Viwanda na zile zinazotoa huduma kwa jamii pia. Au kwa maneno mengine, ni kwamba mishahara mizuri inachochaea sekta nyingine za uzalishaji kwa kuongeza uwezo wa kufanya manunuzi na vile vile kufanya "*savings*."

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimezungumzia maslahi ya watumishi wa Umma. Toka Awamu ya Tano iingie madarakani, kumekuwa na kauli kinzani kuhusu watumishi kupandishwa mishahara. Mheshimiwa Rais akiongea katika Mkutano Mkuu wa 33 wa ALAT Oktoba 3, 2017 Jijini Dar es Salaam, alisema kuwa hatarajji kuongeza mishahara kwa wafanyakazi mpaka uchumi utakapokua japo haijulikani ni lini uchumi...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Malizia, malizia.

kwa upande mwengine, Waziri mwenye dhamana ye ye alisema Bodi ya Mishahara inaendelea kufanya kazi. Sasa tafsiri ya haraka ni kuwa Bodi ya Mishahara ifanye kazi na kuhakikisha watu wanalipwa mishahara kufuatana na kazi wanazolipwa na siyo kufuatana kuweka *standing* moja kwa moja kwamba kwa vile tupo cheo kimoja tulipwe mshahara mmoja. Watu wanatofautiana wapewe motisha wafanye kazi ili wajitume kwa ukamilifu zaidi.

Mheshimiwa mwenyekiti, naomba kuwasilisha.
(Makofii)

MWENYEKITI: Ahsante.

**HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI
WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA RUTH
HIYOB MOLLEL (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA
KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI (KRUB) KUHUSU BAJETI
YA OFISI HIYO, KWA MWAKA WA
FEDHA 2019/20 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge,
Toleo la Januari, 2016*

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, Kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu,kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hilli, kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu utendaji kazi wa Serikali, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha, katika Ofisi ya Rais- Utumishi na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/2020.
2. **Mheshimiwa Spika**, napenda kumshukuru Mungu pamoja na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Mbowe na Mbunge wa Hai na Mheshimiwa Esther Matiko, Mbunge wa Tarime Mjini kwa jinsi Mungu alivyokuwa pamoja nao gerezani kwa takriban miezi mitatu na nusu na kutoka salama. Tuko pamoja nao katika safari ya mabadiliko na demokrasia ya kweli. Niwapongeze pia viongozi wote ambao kwa njia moja au nyingine wanafahamu na kutekeleza kwa vitendo dhana nzima ya utawala bora bila kujali nafasi zao za uongozi katika kuwashudumia wananchi.
3. **Mheshimiwa Spika**, kwa upekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi wetu wa ngazi za Kanda hadi misingi hasa kwa mikoa ya Kanda ya Pwani kwa ukomavu wao katika kutambua haki zao za msingi katika kutekeleza majukumu yao ya kisiasa licha ya vitisho vingi wanavyokumbana navyo kutoka kwa watendaji wanaolipwa kwa kodi za wananchi. Naomba niendelee kuwatia moyo

kwamba Tanzania inapita katika kipindi cha mpito kuelekea Demokrasia ya kweli, japokuwa tunarudi nyuma, uvumilivu ni muhimu.

4. **Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini kwa umuhimu sana naishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kunipa moyo katika majukumu yangu haya ya Kibunge na Kisiasa, ambayo kwa namna moja au nyingine naendelea kujifunza. Nasema asante sana!

5. **Mheshimiwa Spika**, Kaulimbiu ya Kambi Rasmi ya Upinzani ni *“Ujenzi wa Taasisi Imara kwa maendeleo endelevu”* ni dhahiri kwamba japokuwa hatuna Katiba mpya ambayo ni nguzo kuu ya ujenzi wa taasisi imara katika usimamizi na uendeshaji wa Serikali, lakini bado Ofisi ya Rais, hasa, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kutumia sheria zilizopo inatakiwa kuwa kioo cha jamii katika kutimiza majukumu yake ili kuhakikisha utawala bora unasimamiwa na kujenga utumishi wa umma, uliotukuka wenyewe ari na utashi wa kufanya kazi kwa misingi ya utu, huku ukizingatia misingi ya sheria na kanuni.

6. **Mheshimiwa Spika**, hotuba hii au hoja iliyo mbele ya Bunge lako kwa siku ya leo imejikita katika mafungu yafuatayo yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais;

- i) Fungu 20 - Ofisi ya Rais (Ikulu);
- ii) Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
- iii) Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
- iv) Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- v) Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma,
- vi) Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma,

vii) Fungu 09-Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma,

7. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafungu hayo, Ofisi hii ya Rais inasimamia pia Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa.Hata hivyo, nitazungumzia tu baadhi ya maeneo ambayo kwa maoni yangu yanahitaji msisitizo zaidi.

8. **Mheshimiwa Spika**, kutokana na uhaba wa Taarifa au kukosekana kwa uwazi katika utendaji kwa baadhi ya mafungu nitashindwa kuyatolea kauli kulingana na utendaji wake, lakini ninaamini tutasaidiana na waheshimiwa wabunge wengine katika kutimiza wajibu wetu kuisimamia Ofisi hii ili utendaji wake ufuate misingi na kanuni za Utawala Bora.

2. DHANA YA UTAWALA BORA KATIKA UTEKELEZAJI WA SHUGHULI ZA SERIKALI

9. **Mheshimiwa Spika**, dhana nzima ya Utawala imejikita katika matumizi ya mamlaka ya kisiasa na kiuchumi katika kusimamia masuala ya nchi kwenye ngazi zote. Hivyo basi, Utawala bora ni matumizi ya mamlaka ambayo yanakuwa na uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu usawa na unafuata utawala wa sheria.

Aidha, kwa mujibu wa rasimu ya Katiba pendekezwa, ni kwamba misingi ya utawala bora katika Jamhuri ya Muungano itajumuisha: (a)uadilifu; (b) demokrasia; (c) uwajibikaji; (d) utawala wa sheria; (e) ushirikishwaji wa wananchi; (f) haki za binadamu; (g) usawa wa jinsia; (h) umoja wa kitaifa; (i) uwazi; na (j) uzalendo.

10. **Mheshimiwa Spika**, hatua ya Tanzania kujitoa rasmi katika Mpango wa Uendeshaji wa Shughuli za Serikali kwa Uwazi (Open Government Partnership-OGP) ni hatua ambayo inazua wasiwasi kuhusu utekelezaji wa sera ya uwazi na uwajibikaji iliyoasisiwa na Rais mstaafu Jakaya Kikwete mwaka 2011. Hatua hiyo ya kujitoa kwa Tanzania, ina maana kwamba mipango yote ya serikali itakuwa ikiendeshwa kwa usiri mkubwa (itafanyika gizani). Hakutakuwa na uwazi tena.

Kambi Rasmi ya Upinzani inasema huu ni ushahidi wa wazi kwamba Utawala bora kwa sasa ni jambo ambalo halipo na yote yanayofanyika tayari yanakuwa yamepangwa, hivyo, kuwanyima wananchi haki ya kuhoji matumizi sahihi ya rasilimali za umma.

11. Mheshimiwa Spika, Utawala bora kwa maana pana huhusisha uongozi unaofuata misingi na kanuni bora za ushiriki wa makundi mbalimbali katika jamii kwa ajili ya maendeleo chanya, hivyo basi, utawala bora unazingatia kwa makini mamlaka yanayotokana na sheria, taratibu na kanuni mbalimbali katika kusimamia rasilimali za nchi, ili kuboresha maisha ya wananchi.

12. Mheshimiwa Spika, Kitabu cha mwongozo wa wakufunzi wa mafunzo kwa viongozi na watendaji wa Serikali za mitaa, kimetoa tafsiri ya utawala wa sheria kwamba ni uwepo wa mfumo wa sheria unaotekelizwa kwa sawa kwa watu wote, kutoa ulinzi kwa watu wote pia na hasa makundi maalum. Aidha mwongozo huo unataka kuzingatia yafuatayo:-

- i. Mfumo wa sheria za nchi ulio wa haki na ambao umejengwa na sheria zisizo kandamizi;
- ii. Usawa mbele ya sheria; watu wote wawe sawa mbele ya sheria;
- iii. Ulinzi na haki sawa mbele ya sheria;
- iv. Uendeshaji wa shughuli za umma pamoja na maamuzi lazima vifanyike kwa kufuata sheria za nchi¹.

13. Mheshimiwa Spika, Lengo mahsusil la utawala bora ni kukuza demokrasia na uwajibikaji katika jamii na kuhakikisha kuwa wananchi na viongozi wanawajibika ipasavyo kadri inavyowezekana katika majukumu yao na pia kuelekeza rasilimali za nchi kutoa matokeo chanya kwa ajili ya ustawi wa wananchi na maendeleo yao kwa ujumla².

14. **Mheshimiwa Spika**, hoja ya msingi hapa ni je kweli utawala bora wenyewe kuzingataia sheria unatekelezwa na Awamu ya Tano? Tumeshuhudia baadhi ya maamuzi yanayokiuka kanuni za utawala bora na uwazi katika utendaji wa Serikali.

15. **Mheshimiwa Spika**, Ushahidi wa wazi kwenye hilo ni;

i. Bunge tukufu kufanya kazi zake bila wananchi kuona nini kinafanywa na wawakilishi wao (Kutokuonesha Bunge mubashara), hivyo kuwanyima wananchi haki yao ya msingi kufuatilia uwajibikaji wa Serikali na matumizi ya fedha zao. Pia kutofahamu jinsi gani Serikali inatatua kero zao kupitia wawakilishi wao Bungeni.

ii. Usawa mbele ya Sheria, vyama vya upinzani kunyimwa haki ya kuwa na vikao kwa kisingizio cha taarifa za intelijensia ilhalli chama tawala kinakutana na kuandamana chini ya ulinzi wa Polisi, hii ni “double Standard”

iii. Wananchi kukamatwa holela kwa kisingizio cha uchochezi wanapokosoa utendaji wa Serikali.

16. **Mheshimiwa Spika**, kwa viashiria vilivyoainishwa hapo juu, utawala wa sheria unaendelea kuporomoka nchini. Hivyo basi ili kujenga umoja wa Taifa, Amani na Utulivu, Serikali kupitia vyombo vyake vya ulinzi na Usalama, haina budi kuzingatia utawala wa sheria ambaao tumejiwekea kama nchi. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani, inapendekeza sheria zote kandamizi zinazozuia uhuru wa habari na kemokrasia ya kweli zihuishwe, ili watanzania watembee kifua mbele katika nchi yao kuliko ilivyo sasa ambapo woga umekithiri.

17. **Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza dhana ya utawala bora mambo yafuatayo lazima yazingatiwe:

i. Matumizi sahihi ya dola- Eneo hili bado linahitaji kufanyiwa kazi zaidi, pamekuwa na matukio mengi ya wananchi kupigwa, kujeruhiwa na kufariki kwenye vituo vya polisi. Vile

vile kubambikiziwa kesi na kuwekwa mahabusu kwa makusudi hata kwa kesi zinazodhaminika.

ii. Matumizi mazuri ya rasilimali kwa faida ya wananchi-Pamoja na juhudzi zinazofanyika bado kuna ujisadi kwenye miradi mikubwa ya ujenzi, ukwepajji wa kodi, matumizi nje ya bajeti inayopitishwa na Bunge.

iii. Matumizi mazuri ya madaraka yao- baadhi ya viongozi wa kisiasa hasa wakuu wa mikoa na wilaya wanavuka mipaka katika kutumia madaraka yao kwa kuweka raia rumande kwa zaidi ya masaa 24 na 48 kwa mujibu wa sheria ya Tawala za mikoa ya mwaka 1997 bila kuwapeleka mahakamani na hakuna hatua zozote zinachukuliwa dhidi yao matokeo yake chuki inajengeka kwa wananchi dhidi ya Serikali. Hivyo basi, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri yafuatayo yafanyike;

a. Kutoa mafunzo mara kwa mara kwa wateule hao wa kisiasa waelewe jinsi Serikali inavyofanya kazi

b. Wafanyiwe upekuzi kabla ya kuteuliwa na wenye dosari za maadili na mwenendo usioridhisha hata katika maisha yao binafsi wasipewe madaraka.

c. Serikali irejeshe mfumo wa zamani wa kuandaa viongozi kwa kutambua maafisa wenye viashiria vya uongozi (leadership potentials) waandaliwe mafunzo ya muda mrefu na mfupi na wakati huohuo mienendo yao inafuatiliwa. Tunaamini mfumo huu ukiwa endelevu nchi yetu itapata viongozi bora wenye weledi, maadili, uzalendo na uaminifu.

2.1 Jinsia na Utawala bora

18. Mheshimiwa Spika, unapozungumzia Utawala Bora, huwezi kuacha kuzungumzia usawa wa jinsia katika mgawanyo wa madaraka na Rasilimali za nchi. Asilima 75 ya wanawake ndio wazalishaji wakubwa vijijini, hivyo basi, ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi ni jambo la msingi kabisa na mtakubaliana na mimi, kwamba mahitaji ya

wanawake na wanaume ni tofauti kabisa, kwa msingi huo uwakilishi wa wanawake katika ngazi za maamuzi, hasa kwenye sera, sheria na kanuni itasaidia kujumuisha mahitaji ya wanawake na watu wenye mahitaji maalum. Pamoja na kwamba Kamusi ya Kiswahili ya Oxford inatafsiri jinsi kuwa ni "*masuala yanayoambatana na mambo yanayohusu mwanamke na mwanamume*" lakini kwa hali halisi wanawake ndio wenye uwakilishi mdogo. Hivyo basi, ili utawala bora uonekane kuwa upo katika jamii, usawa wa jinsia ni kipimo kimojawapo cha utawala bora.

19. Mheshimiwa Spika, ukiangalia taarifa ya **taarifa ya maendeleo ya binadamu iliyotolewa mwaka 2017** (Tanzania Human Development Report 2017) yenye kauli mbiu ya "*Sera ya Kijamii Katika Mukadha wa Mageuzi ya Kiuchumi*" kuhusu ushirikishwaji wa wanawake katika maendeleo ya nchi, Ukurasa wa 5 wa taarifa hiyo unaonesha kuwa; "Matokeo ya Kipimo cha Maendeleo ya jinsia (Gender Development Index-GDI) na Kipimo cha Tofauti ya kijinsia (Gender Inequality Index-GII) yanaonyesha kwamba wanawake wana nafasi kubwa zaidi ya kuathiriwa na ukosefu wa maendeleo ya binadamu kutokana na kukosekana kwa usawa baina ya wanawake na wanaume katika elimu, huduma za afya, na fursa za kiuchumi".

20. Mheshimiwa Spika, Kwa kuzingatia Kipimo cha Tofauti ya Kijinsia, Tanzania iliporomoka nafasi nne kutoka 125 hadi ya 129 kati ya nchi 188 katika ripoti ya mwisho ya maendeleo ya binadamu duniani (UNDP 2016). Juhudi zimeendelea kufanywa katika kuongeza uwakilishi wa wanawake bungeni, usawa wa kijinsia katika elimu ya msingi, ongezeko la wanawake katika kazi, na kuongeza umri wa kuishi.

21. Mheshimiwa Spika, Hata Hivyo, tofauti bado imeendelea kuonekana katika uwiano wa wanawake katika nafasi za maamuzi katika ngazi za mikoa na serikali za mitaa, na katika nafasi za uongozi wa juu na kati. Wakati huohuo, wanaume wanachukua takriban asilimia 82.6 ya nafasi za uongozi ikilinganishwa na asilimia 17.4 za wanawake.

22. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, mwaka 2010, Serikali iliendelea kuhakikisha uwepo wa uwiano wa kijinsia kwenye ngazi mbalimbali za uongozi nchini. Katika kipindi cha mwaka 2006 hadi 2010, uwiano wa wanawake kushiriki katika ngazi za maamuzi uliongezeka kutoka asilimia 26 mwaka 2006 hadi asilimia 31 mwaka 2010. Kiwango hiki ni juu ya lengo la MKUKUTA la asilimia 30 mwaka 2010 lakini chini ya lengo la SADC la asilimia 50.

23. Mheshimiwa Spika, mchanganuo wa baadhi ya nafasi zilizoongezeka zinazoshikiliwa na wanawake tangu mwaka 2006 hadi 2010 kabla ya uchaguzi Mkuu ni kama ifuatavyo: Majaji 13 hadi 34; Mawaziri 4 hadi 10; Makatibu Wakuu 7 hadi 9; Makatibu Tawala za Mikoa 4 hadi 10; Wakuu wa Wilaya 20 hadi 25; Wakurugenzi wa Halmashauri 14 hadi 35; na Wakurugenzi kwenye wizara na taasisi, 19 hadi 133. Aidha, kufuatia matokeo ya uchaguzi mkuu wa Raís, Wabunge na Madiwani uliofanyika Oktoba 2010, idadi ya wabunge wanawake ilifikia 126, sawa na asilimia 36 ya wabunge wote 350 waliokuwepo wakati huo. Aidha, idadi ya mawaziri wanawake ilikuwa ni asilimia 26.7 ya mawaziri wote 30 waliokuwepo.

24. Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Mwenyekiti wa Mtandao wa Jinsia Tanzania, Dr. Visencia Shule wakati wa maadhisho ya siku ya wanawake Duniani, tarehe 8/3/2018 na kuandikwa kwenye gazeti la Nipashe la tarehe 15/3/2018 ilionesha kwamba, ushiriki wa wanawake katika ngazi za maamuzi umeshuka kutoka 38% awamu ya nne hadi 19% awamu ya tano. Uwiano wa wanawake na wanaume katika ngazi za uongozi Serikalini ni 28:72 ikiwa ni wanawake 2,573 na wanaume ni 6,674.

Aidha, Baraza la mawaziri, katika serikali ya awamu ya nne ilikuwa na mawaziri 57, kati ya mawaziri hao, idadi ya wanawake walikuwa ni 16 sawa na 28%. Baraza la Mawaziri, katika serikali hii ya awamu ya tano ni mawaziri 35 kati yao wanawake ni 9 tu sawa na 25%. Idadi hii ni pungufu kwa 3%. Kwa upande wa mabalozi katika serikali ya awamu ya nne,

idadi ya wanawake walikuwa ni 36% na awamu ya tano ni 21%. Wakuu wa wilaya awamu ya nne wanawake walikuwa ni 40% na awamu ya tano ni 16%.

25. Mheshimiwa Spika, Kwa upande wake Mtendaji Mkuu wa Mtandao wa Kijinsia Tanzania (TGNP) Bi Lilian Liundi, baada ya utafiti wake aliona kuwa Tathmini ya jumla ni kuwa, ikilinganishwa na awamu ya nne, idadi ya Makatibu wakuu na Manaibu Katibu Wakuu wanawake imepungua kwa kiasi kikubwa. Takwimu za mwaka 2014 zinaonesha kuwa, idadi ya wanawake waliokuwa Makatibu wakuu au Manaibu Katibu Wakuu ilikuwa 20 sawa na asilimia 37.7 huku wanaume wakiwa 33 sawa na asilimia 62.3.

Katika uteuzi uliofanyika awamu ya tano, Idadi ya wabunge wanawake bungeni kwa sasa ni 145 kati ya wabunge 392 walopo, Ikiwa ni ongezeko la wabunge wanawake 19 sawa na asilimia 13.1 kulinganisha na waliokuwepo katika Bunge la 10. Jumla ya wanawake Makatibu Wakuu na Manaibu ni 10 sawa na asilimia 20 tu huku asilimia 80 inayobakia ikishikiliwa na wanaume. Kwa kuzingatia takwimu hizo, ni dhahiri kuwa, idadi ya Makatibu Wakuu na Manaibu Katibu Wakuu wanawake imepungua kutoka asilimia 37.7 mwaka 2014 hadi asilimia 20 mwaka 2016. Hii ni tofauti ya asilimia 17.7 ambayo ni kubwa sana na hivyo kuongeza pengo la jinsia katika nafasi za kufanya maamuzi.

26. Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizo ni dhahiri, uwakilishi wa wanawake kwenye ngazi za juu za maamuzi umeporomoka sana, ilhali wanawake ni zaidi ya 50% ya watanzania wote na pia ni zaidi ya 70% ya nguvu kazi katika uzalishaji wa chakula kinachotumika nchini.

27. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kurejea tena kwenye meza na kuongeza idadi ya wanawake kwenye ngazi ya maamuzi, ili wanawake ambaa ni zaidi ya 50% ya watanzania wapate uwakilishi. Wanawake ni jeshi kubwa kama wanavyotambuliwa kwenye Biblia takatifu.

2.2. Ufuatiliaji wa Matumizi ya Rasilimali za Umma-Public Expenditure Tracking Survey (PETS).

28. Mheshimiwa Spika, katika mfumo huru wa Serikali inayofuata na kutekeleza kanuni na misingi ya Utawala bora, mfumo wa ufuatiliaji wa matumizi ya rasilimali za umma ni jambo la muhimu. Mfumo huu unatakiwa uanzie kwa sisi wawakilishi wa wananchi kwa kufuatilia fedha zote zinazotengwa na Bunge kwa ajili ya shughuli zote za maendeleo. Ikishatoka kwetu inakwenda kwa wananchi au asasi za kiraia zinazojihusisha au ambazo ni mdau wa shughuli za maendeleo kwenye sekta husika.

29. Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla mfumo huu unakosa nguvu kutopteka na usiri mkubwa na vitisho katika upatikaji wa taarifa na mbaya zaidi ni kuweka sharti kuwa taarifa za Serikali ni siri. Vilevile kuna kuwa na mlolongo mrefu hadi kupatiwa taarifa husika na kuna uwezekano wa kukataliwa ijapokuwa umeiomba hiyo taarifa kwa kwa mujibu wa sheria na taratibu zilizowekwa.³

30. Mheshimiwa Spika, katika kufanya ufuatiliaji wa matumizi ya Rasilimali za umma, PETS ni zana mojawapo ya utawala bora. Kwa mujibu wa sheria, taarifa kutoka Serikalini na taasisi zake ni lazima zilipiwe. Inakuwaje sasa mdau anayefuatilia matumizi ya rasilimali za umma alipie upatikanaji wa taarifa husika? Kigezo cha kulipia taarifa ni ukiukwaji wa dhana ya utawala bora na uwazi. Utaratibu huo wa malipo utachangia kukatisha tamaa "frustrate" wadau wanaofanya PETS.

31. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kama kweli inautashi wa kuinua dhana nzima ya uwazi na uwajibikaji, ifanye marejeo ya sheria zote zinazotoa masharti ya upatikanaji wa taarifa zinazohusu matumizi ya fedha za umma.

2.3. Institutional Governance Review (IGR)

32. Mheshimiwa Spika, zana hii ya kupima utawala bora inatumika kutathmini utendaji wa taasisi za umma ambazo

hazifanyikazi kama inavyotakiwa. Taarifa ya kina (detailed report) inaibua chanzo cha utendaji mbovu wa taasisi na kujadiliwa na mwisho kutoa maamuzi juu ya utendaji wake⁴. Hata hivyo mifumo ya uratibu, Usimamizi na Udhhibit bado sio imara na hivyo kusababisha uanzishwaji wa taasisi mpya kwa gharama kubwa za fedha za walipa kodi. Mfano mzuri ni TARURA. Serikali imeshindwa kusimamia Serikali za Mitaa kujenga barabara zake, ikaona ufumbuzi ni kuanzisha TARURA chini ya Serikali kuu kusimamia ujenzi wa barabara za vijijini, jukumu ambalo kimsingi lilikuwa la Serikali za mitaa.

33. Mheshimiwa Spika, ni ukweli kwamba, Serikali imeshindwa kuweka mfumo madhubuti wa kusimamia taasisi zake, na sasa matokeo yake inahodhi majukumu ya taasisi hizo na kurudisha Serikalini ukiritimba ambao ulishindwa kuleta maendeleo hapo nyuma. Mifano ni mingi, lakini michache ni ifuatayo;

a. Ujenzi wa majengo ya Serikali umerudishwa kwa TBA, Suma JKT na Magereza na hivyo kuifanya Sekta binafsi kukosa kazi hivyo kuongeza idadi ya watu wasio na kazi na kupunguza mzunguko wa fedha.

b. Vyanzo vya mapato vya Halmashauri zetu kuporwa na Serikali Kuu, kama vile kodi za majengo, kodi za mabango n.k. jambo ambalo linapunguza uwezo wa Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa jamii kwa ufanisi kama vile maji, afya na shule.

34. Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Serikali ndiye mwekezaji mkuu katika taasisi, maana yake ni kuwa fedha zote za taasisi zinatakiwa kuingizwa kwenye mfuko mkuu wa Serikali, hela zikishaingia huko ni rahisi sana kupangiwa matumizi mengine na Taasisi husika kukosa kabisa fedha za maendeleo au kupewa kwa kuchelewa. Jambo hili litakwamisha taasisi hizo katika kutekeleza majukumu yao.

35. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema suluhu ya matatizo ya taasisi zetu za umma ni uwepo wa mifumo thabiti ya Uratibu, Ufuutiliaji na tathmini ya utendaji

kazi wa kila siku, kiasi kwamba mapato na matumizi yatakuwa yanasonic moja kwa moja kwenye kitengo husika Hazina. Vile vile hatua za kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya wote wanaoshindwa kutimizia wajibu wao.

36. Mheshimiwa Spika, zana hii ya IGR itumike kupima utendaji kazi wa Serikali ili kubuni mikakati ya kuboresha utendaji kazi, bila ya kuvuruga sera ya Ugatuaji wa madaraka ilyoasisiwa kwa muda mrefu na kwa kutumia fedha za walipa kodi wa nchi hii kwa njia ya mikopo.

37. Mheshimiwa Spika, zana hii IGR imekuwa ikitumika katika mataifa mbalimbali kufufua dhana nzima ya utawala bora na uwajibikaji kwa taasisi za umma. Lakini kwetu utekelezaji wa IGR umekuwa na changamoto kwa sababu maamuzi yanatolewa bila ya kufanya uchambuzi wa "processes na systems" kabla ya utekelezaji wa maamuzi husika. Wakati mwagine Serikali imetekeleza baadhi ya maamuzi ambayo utekelezaji wake ulishindikana kwenye awamu zilizopita.

38. Mheshimiwa Spika, kubadili maamuzi ya awamu zilizopita kabla ya matokeo chanya au hasi na kutoa maamuzi mengine ni kuchelewesa maendeleo kwa kuanza upya na pia ni upotevu wa raslimali fedha za umma ambazo zingetumika kuboresha huduma za jamii na kupunguza umasikini nchini.

2.4. Ukaguzi wa mapato na matumizi ya umma (Auditing)

39. Mheshimiwa Spika, utawala bora unahusisha haki ya kupata taarifa kwa wadau wote ili kuwawezesha kupata uhakika wa jinsi utendaji wa sekta ya umma ulivyo ili waweze kufahamu ni kwa vipi wateweza kushirikiana na Serikali au kufuatilia utendaji kazi wa Serikali na maamuzi yao kufanya kwa uwazi zaidi.

40. Mheshimiwa Spika, takriban nchi zote zilizoendelea na zinazoendelea zinatumia Ukaguzi au (Supreme Audit Institutions-SAIs) kama zana mojawapo ya uwazi na uwajibikaji

katika rasilimali za umma. Kwa miaka ya hivi karibuni mataifa mengi yaliyo chini ya SAI yameongezewa bajeti zao za utendaji kazi kutokana na ukweli kwamba kazi zao zinaimarisha utawala bora kwenye nchi husika. Lakini kwa bahati mbaya kuna mataifa ambayo pia yamepunguza bajeti kwa taasisi hizo za ukaguzi.

41. Mheshimiwa Spika, kati ya mataifa 129 yaliyofanyiwa utafiti mataifa 113 yalionegeza bajeti kwa taasisi za ukaguzi, mataifa ambayo bajeti iliongezeka sana ni: Iraq (1811%), Azerbaijan (804%), Angola (529%), Kazakhstan (523%), Macedonia (278%), Peru (244%), Belarus (221%), Ghana (212%) & Dominican Rep. (203%).

42. Mheshimiwa Spika, mataifa ambayo yalipunguza sana bajeti zao kwa taasisi za Ukaguzi ni; Madagascar (-93%), Zimbabwe (-82%), Argentina (-57%), Uruguay (-38%), Iran (-31%), Venezuela (-26%), Bolivia (-18%), Costa Rica (-14%), Philippines (-12%), Gambia (-10%).

Taarifa inaonesha kuwa kwa mwaka 2005, *Government Accountability Office (GAO) of the US* ilikuwa na bajeti kubwa ya takriban (\$ 474.5 million) na Madagascar ikiwa na bajeti ya chini ya (US \$ 100,784)⁵.

43. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inapenda kuuliza, kwa hoja hiyo, Taasisi ya Ukaguzi hapa Tanzania Bajeti yake ya kufanya kazi kama mojawapo ya zana na Utawala bora ikoje?

44. Mheshimiwa Spika, ukubwa wa bajeti ya taasisi ya ukaguzi sio ishara pekee ya utawala bora, lakini inaashiria dhamira ya mamlaka kusimamia utawala bora kwa kuhakikisha kodi za wananchi zinasimamiwa na kutumika ipasavyo.

45. Mheshimiwa Spika, kanuni ya uwazi ndiyo kanuni muhimu sana katika uwajibikaji, nchi yetu imekuwa ikiitumia sana Ofisi ya CAG kama zana mojawapo ya utawala bora na uwajibikaji. Lakini kwa hali isiyo ya kawaida kabisa imegundulika kwamba Ofisi ya Rais ambayo ndiyo inatakiwa

kuwa kinara katika utawala bora na kuwa mfano kwa taasisi zingine katika dhana nzima ya utawala bora na uwajibikaji, CAG amekuwa hafanyi kazi yake ya kuhakikisha utawala bora na uwajibikaji unafanya kama ipasavyo.

46. Mheshimiwa Spika, katika Tanzania taasisi pekee ambayo kikatiba imepewa nguvu ya kuhakikisha na kufuatilia matumizi ya fedha zote zinazopitishwa na Bunge zinatumika kama ilivyopangwa, ni Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) na kitendo chochote cha kumzuia CAG kufanya kazi yake katika taasisi yoyote ambayo inapokea fedha zilizopitishwa na Bunge ni kosa kubwa sana kwa mujibu wa sheria inayompa mamlaka CAG kufanyakazi yake.

2.5. Taasisi ya Kupambana na kuzuia Rushwa-TAKUKURU

47. Mheshimiwa Spika, kwa muktadha wa taarifa hii, TAKUKURU inaangaliwa kama zana mojawapo ya kusimamia utawala bora katika nchi. Zana hii ili iweze kufanya kazi kwa ufanisi inatakiwa iwe huru na kufanyakazi zake bila ya kuingiliwa na mamlaka yoyote ile. Aidha, Lengo kuu la Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Namba 11 ya 2007 imeainishwa katika kifungu cha 4 cha Sheria hii ikiwa ni kuhakikisha ustawi wa utawala bora na kuondoa rushwa nchini.

48. Mheshimiwa Spika, katika nchi yetu zana hii imeanza kupoteza maana halisi ya kuwa zana ya kuleta utawala bora kutokana na utendaji kazi wake ambao haifuati misingi ya kisheria na katiba ya nchi.

49. Mheshimiwa Spika, taasisi hii inafanyakazi chini ya uangalizi au maelekezo ya Ofisi ya Rais na ndio maana fungu lake liko chini ya Ofisi ya Rais Ikulu. TAKUKURU kama zana ya utawala bora inatakiwa kusisimamia taasisi zote na Ikulu ikiwa ni mojawapo ya taasisi hizo, lakini jambo hilo halifanyiki, na hivyo kuzidisha mashaka kwa wananchi kama kweli zana hii ya kusimamia utawala bora inafanya kazi kwa uhuru.

50. Mheshimiwa Spika, taasisi hii ni taasisi huru ya uchunguzi kwa mujibu wa sheria namba 11 ya mwaka 2007, lakini uhuru wake hauonekani kwani haiwezi kupeleka kesi

mahakamani hadi ipate kibali toka Ofisi ya Mwendesha Mashtaka. Hapa ndipo walakini wa zana hii unapotiliwa mashaka katika kadhia nzima ya uwazi na uwajibikaji kwa umma.

51. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa hadi Septemba 2016 kesi mpya zilizofunguliwa Mahakamani na TAKUKURU zilikuwa ni 338 kati ya hizo washtakiwa walioachiwa huru na Mahakama ni 214 sawa na 63.3% na kesi zilizoondolewa mahakamani ni kesi 39 sawa na 11.53% na kesi 3 zilikatiwa rufaa⁶. Kwa takwimu hizo ni kuwa kesi zilizokuwa ni za halali ni 25.16% tu. Hii maana yake ni kuwa Taasisi hii inafanyakazi zake sio kwa kuzingatia ushahidi uliopo bali ni kwa hisia, na jambo hili sio tu linaondoa haki za watuhumiwa bali pia linapoteza muda na fedha za walipa kodi wa nchi hii.

52. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kuwa TAKUKURU isimkamate mtu yeoyote bila ya kuwa na ushahidi wa kutosha kumfikisha mhusika mahakamani. Takwimu za walioshinda kesi ni ushahidi kuwa kesi nydingi zinafunguliwa bila ya ushahidi wa uhakika, matokeo yake ni kuathiri maisha ya wahusika na familia zao.

53. Mheshimiwa Spika, mashaka ya uhuru wa taasisi hii muhimu unakuja pale inapowakamata watuhumiwa na kuwfikisha mahakamani wakati huo huo haina ushahidi wa kutosha kuendesha kesi hiyo. Jambo hilo linasababisha watuhumiwa kukaa mahabusu kwa kipindi kirefu sana na kusababisha uvunjifu wa haki za msingi za wahusika. Hivyo basi, badala ya kuwa zana ya utawala bora inakuwa zana ya uvunjifu wa utawala bora. Hii ni hatari sana kwa nchi inayojenga mifumo huru ya utawala bora.

54. Mheshimiwa Spika, ili kutenda haki na kutumia vyema kodi za wananchi, kuepuka usumbufu na uonevu kwa kushukiwa, TAKUKURU ikamilishe uchunguzi na kupeleka washukiwa mahakamani badala ya rumande ili watuhumiwa wapate haki yao ya kuachilliwa huru au kuhukumiwa kwa sababu "Justice denied is Justice delayed".

55. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaona sasa ni muda mwafaka kwa taasisi hii kuwa huru, kwa maana kuwa watendaji wake wakuu wasiteuliwe na Rais bali waombe nafasi hizo na wafanyiwe usaili na jopo la wataalam na kuidhinishwa na Bunge.

2.6. Tume ya haki za Binadamu na Utawala Bora

56. **Mheshimiwa Spika**, kwa muktadha wa hotuba hii TUME ya Haki za Binadamu na Utawala Bora inatumika kama zana(tool) mojawapo ya kuonesha uwepo wa Utawala Bora katika nchi. Uwepo wa taasisi hii umeelezwa bayana na Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 129 na majukumu yake yameelezwa katika Ibara ya 130. Aidha, tume ilianzishwa na sheria yake mahususi, ambayo ni sura namba 39 ya marejeo ya sheria ya mwaka 2002 ya sheria za Tanzania.

57. **Mheshimiwa Spika**, Tume hiyo imepewa majukumu mengi na ya muhimu katika kusimamia utawala bora na haki za binadamu ambazo ni pamoja na kufuatilia na kulinda haki za binadamu kama ambavyo zinalekezwa na katiba yetu, pia kufanya uchunguzi kuhusu mambo yote yanayohusisha uvunjifu wa haki za binadamu hapa nchini.Tume hiyo pia ina majukumu ya kufanya utafiti juu ya haki za binadamu na utawala bora na kuelimisha jamii kuhusiana na mambo hayo.

58. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na mambo mengine ukiukwaji wa haki za binadamu unatokea pia pale vyombo vya dola vinapofanya matendo yanayokiuka haki za binadamu kwa mfano kupiga raia au watuhumiwa, kuwaresa, kuwanyima dhamana, na kuwashikilia bila kuwafikisha mahakamani kwa mujibu wa muda uliowekwa kisheria. Ili tume iwe na mamlaka kama inavyotakiwa ni muhimu sana mapendekezo yaliyotolewa katika Rasimu ya Pili ya Katiba ya Jaji Warioba kufuatwa katika kuifanya Tume kuwa chombo kinachosimamia pia mgawanyo wa madaraka baina ya vyombo vya dola.

59. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini kuwa haki za binadamu ni stahili ya kila mtu kama

zilivyoainishwa katika tamko la Kimataifa la haki za binadamu na mikataba ya kimataifa ya haki hizo. Hivyo basi Katiba mpya ya wananchi itaweka wazi mgawanyo wa madaraka baina ya mihimili mkuu ya dola na pia kuweka misingi ya kudhibitiana baina ya mihimili hiyo ili kulinda haki za binadamu, kama ilivyoainishwa kwenye Sera za Chadema kuhusu Katiba itakayotokana na matakwa ya wananchi.

3. SEKRETARIETI YA MAADILI YA UMMA

60. **Mheshimiwa Spika**, maadili ni moja ya tunu muhimu zinazolitambulisha na kutofautisha taifa moja na lingine. Maadili mema ni kichocheo kikubwa cha maendeleo ya taifa, hujenga umoja, amani, upendo, uvumilivu na mshikamano katika taifa. Maadili yana umuhimu mkubwa sana katika utawala na maendeleo ya nchi kwani; yanasaidia kujenga imani ya wananchi kwa viongozi na serikali kwa ujumla; kuhakikisha kuwa rasilimali za umma zinatumika kwa maslahi ya wote; yanasaidia kuongeza tija na thamani ya huduma zinazotolewa na Serikali; yanasaidia kujenga ujasiri wa kusimamia sheria na kanuni katika utumishi wa umma. Yanasaidia pia kudhibiti mianya na vitendo vya rushwa na kuepusha maamuzi yenye mgongano wa maslahi.

61. **Mheshimiwa Spika**, pamoja na uchunguzi wa kuimarisha utawala bora, taasisi hii inafuatilia mwenendo na tabia za viongozi, zinazoashiria ukosefu wa uaminifu au uadilifu, vitendo vinavyo chochea rushwa katika shughuli za umma au tabia inayohatarisha maslahi na ustawi wa jamii

62. **Mheshimiwa Spika**, ili kuwezesha Sekretariat kufanya kazi zake za kiuchunguzi inaongozwa na sheria ili kutimiza majukumu yake, kifungu cha 27 cha Sheria namba 13 ya mwaka 1995 kinamtaka Mheshimiwa Rais kuteua watu watatu ili kuunda mahakama au Baraza kwa minajili ya kusimamia uchunguzi wa malalamiko dhidi ya viongozi wa umma yanayowasilishwa kwenye Chombo hiki.

63. **Mheshimiwa Spika**, kwa kuwa hadi sasa Wateule hao kwa ajili ya kusimamia uchunguzi wa malalamiko ya viongozi

wa umma bado hawajateuliwa, maana yake ni kwamba Sekretarieti haiwezi kufanya kazi zozote za kiuchunguzi dhidi ya mienendo ya viongozi wa umma yalivyowasilishwa kwa Tume.

64. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri kwamba Mhe Rais atue Baraza hilo kwa mujibu wa sheria na13 ya mwaka 1995 ili kuiwezesha Tume kutekeleza majukumu yake, vinginevyo dhana ya Utawala bora haitafikiwa.

65. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani, inapendekeza kwamba uwepo wa Katiba mpya inayotokana na maoni ya wananchi ndio itakuwa muarubaini wa kuhakikisha mgawanyo kamili baina ya mihimili mitatu ya Serikali na baina ya taasisi zote na Serikali ili kuondoa muingiliano wa majukumu na mamlaka baina ya Serikali na Taasisi.

4. MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA-FUNGU 32

66. Mheshimiwa Spika, wateja wakubwa katika utumishi wa umma ni wananchi, na mara zote wananchi wataendelea kudai huduma bora. Katika kutimiza matakwa hayo ya wananchi, Serikali inalazimika kuhakikisha watendaji katika sekta ya umma wanakidhi matakwa ya wateja ambao ni wananchi.

67. Mheshimiwa Spika, ili kukidhi haya kumekuwepo na kile kinachoitwa Mkataba wa huduma kwa wateja, ni makubalino ya kimaandishi baina ya taasisi itoayo huduma na wateja wake. Mkataba huu unafafanua huduma zote zinazotolewa na taasisi, kuweka viwango vya huduma, muda wa kutoa huduma hizo, majukumu na wajibu wa mteja na taasisi. Aidha, mkataba unapanga mbinu za kupata majibu ikiwa ni pamoja na kushughulikia malalamiko ya umma.

68. Mheshimiwa Spika, hoja ya msingi ya kuuliza hapa ni je licha ya mikataba ya aina hiyo kuandikwa, huduma kwa wateja zimeimarishwa katika utumishi wa umma? Ukweli ni kwamba ni bado!!

- 69.** **Mheshimiwa Spika**, pamoja na mambo mengi mazuri ambayo yalikuwepo hapo awali ikiwemo la ugatuaji wa madaraka kwenda Serikali za mitaa, lakini bado kukosekana mifumo imara ya UFUATILIAJI na TATHMINI. Udhifu wa mifumo imara inasababisha Serikali kushindwa kupima malengo ambayo yamewekwa kulingana na utendaji binafsi wa mtumishi.
- 70.** **Mheshimiwa Spika**, ni ukweli kwamba iwe katika sekta binafsi au ya umma pale penye mifumo imara ya ufuatililaji na tathmini, Taasisi zimepiga hatua zaidi na mifumo hiyo inakuwa ni chachu katika utoaji wa huduma bora na matokeo chanya yanakuwa wazi kwa kila mmoja.
- 71.** **Mheshimiwa Spika**, uundwaji wa mifumo imara katika taasisi zetu ili kuwa na matokea chanya ni matokeo ya uwepo wa mipango thabiti katika taasisi zetu, lakini mipango ili iwe mipango ni lazima iandane na bajeti zilizopangwa katika utekelezaji wake. Kumekuwa na tatizo kubwa sana katika upatikanaji wa fedha za maendeleo kukidhi mahitaji ya ujenzi wa mifumo imara, jambo ambalo kwa kiasi kikubwa linaathiri utendaji katika utumishi wa umma.
- 72.** **Mheshimiwa Spika**, mfano mzuri fungu 32 kwa miaka miwili yaani 2017/18 na 2018/19 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yenye majukumu ya kuimarisha Utawala Bora katika uendeshaji wa shughuli za Serikali, kwa kubuni Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu za uendeshaji na usimamizi wa shughuli za utumishi wa umma pamoja na kuwajengea uwezo watumishi wa umma ili watoe huduma bora kwa wadau wake. Kwa mwaka wa fedha 2017/18 ilitengewa jumla ya shilingi 33,695,038,000/= kati ya fedha hizo fedha kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo zilikuwa ni shilingi 7,000,000,000/=
- 73.** **Mheshimiwa Spika**, kwa mwaka wa fedha 2018/19 fungu 32 lilitengewa jumla ya shilingi 12,947,029,261/- kama matumizi ya kawaida na shilingi 10,939,000,000/- kwa matumizi ya maendeleo. Kwa kufanya ulinganisho wa miaka hiyo miwili ni kwamba bajeti kwa fungu hilo 32 imepungua kwa shilingi

9,809,008,739/- sawa na asilimia 29.11, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuhakikisha kuwa fedha zinazopangwa na kuombewa idhini ya matumizi zitoke kama zilivyo hitajika, kwani kinyume na hapo ni kuzorotesha mipango yote iliyokusudiwa kwa kipindi hicho.

4.1 UGATUAJI WA MADARAKA- KATIKA SEKTA YA UMMA

74. Mheshimiwa Spika, Ugatuzi wa madara ni sera ya kukasimu madaraka kwa Serikali za Mitaa. Sera hiyo inawapa madaraka Serikali za mitaa kusimamia rasilimali fedha na watumishi moja kwa moja ili kurahisisha utoaji huduma kwa wananchi.

75. Mheshimiwa Spika, Moja ya lengo kuu la maboresho ya Serikali za Mitaa ya mwaka 1998 kuhusiana na ugatuzi wa madaraka ilikuwa ni kuwa na mfumo huru wa kiutawala katika ngazi ya Serikali ya Mitaa ambapo Baraza la Madiwani lilikasimiwa madaraka ya kusimamia sera na utoaji wa huduma, kusimamia watendaji katika ngazi zao.

76. Mheshimiwa Spika, Kwa mtazamo huo wa ugatuzi wa madaraka ilikuwa ni kujenga mfumo imara wa kiutawala ambaao ungekuwa ni nguzo kuu ya kuimarissha utoaji wa huduma na utoaji wa maamuzi katika ngazi za Serikali za mitaa. Ukiwa na uwezo wa kutoa maamuzi maana yake una uhakika wa uendeshaji wa eneo husika bila ya kutegemea msaada wa aina yoyote kutoka ngazi yoyote ya utawala.

77. Mheshimiwa Spika, Chini ya Sera hii, Programu ya Uboreshaji wa Serikali za Mitaa (Local Government Reform Programme- LGRP) ilianzishwa kwa dhamira ya kuimarissha Serikali za Mitaa ili kusukuma mbele utekelezaji wa Mkakati ya Kupunguza Umaskini yaani Poverty Reduction Strategy na baadaye MKUKUTA, na vile vile kuhakikisha kuwa Halmshauri za Miji na Wilaya zinatoa huduma bora kwa wananchi wake hususan huduma za Afya, Maji, Elimu, na huduma za ughani n.k. (angalia mpango wa "LGRP Medium Term Plan and Budget July 2005 – June 2008" OR – TAMISEMI: Juni 2005)

78. **Mheshimiwa Spika**, Malengo maalum ya Programu hiyo yalikuwa ni:

- i. Kugatua madaraka ya Serikali kuu na kuyapeleka kwenye Serikali za Mitaa (LGAs) ili ziwe na madaraka kamili (to create more autonomous Local Government Authorities), kupitia "political decentralization"
- ii. kuhakikisha ufanisi katika utekelezaji wa shughuli za Halmashauri kupitia watumishi wa umma wanaowajibika kwa Serikali za Mitaa zenyewe (*"de-linking of local authority staff from the respective line-ministries, making them accountable to the LGA who will be their employer, fully responsible for all human resource management"- Administrative Decentralization*)
- iii. Kuziwezesha Halmashauri kukusanya mapato kutoka kwenye vyanzo vyake na kuwa na mfumo wa mgawanyo wa mapato kati ya Serikali kuu na Serikali za Mitaa (financial decentralization)
- iv. Kwa umuhimu wa kipekee maboresha pia yalikuwa na dhamira kuu ya kubadilisha mfumo wa mahusiano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa, kutoka mfumo wa Serikali Kuu wa kuwa na *"control role* na hivyo kuwa na wajibu wa kutunga sera na kuweka vigezo vya ubora wa huduma; na kuziwezesha Serikali za Mitaa kutekeleza sera kwa kuwajengea uwezo na kuwapatia raslimali fedha na utaalamu ili ziweze kutoa huduma inayolingana na ubora uliowekwa na kukubalika.

79. **Mheshimiwa Spika**, Ikumbukwe kuwa, Programu ya Maboresho ya Serikali za Mitaa ilitekelezwa sambamba na programu nyingine za uboreshaji wa Sekta za Umma na Sekta Binafsi. Moja kati ya nyanja muhimu za uboreshaji wa Sekta ya Umma ni uboreshaji wa Utumishi wa Umma yaani Civil Service Reform Programme (CSRP 1998), ambayo baadaye iliboreshwaa na kutengeneza programu maalum ya miaka kumi na mitano Public Service Reform Programme (2000 -2015) yenye malengo makuu yafuatayo:

- i. Kuboresha utendaji kwa watumishi wa umma
- ii. Kuweka tabia ya kufuatilia, kupima na kutathmini utendaji katika utumishi wa umma na utoaji wa huduma za umma
- iii. Kuweka mifumo ya kuinua kiwango cha ubora wa huduma (quality improvement cycles).

80. Mheshimiwa Spika, Maboresho hayo yalidhamiria kuimarisha utawala na utoaji huduma, mambo ambayo ni muhimu sana katika kuiondoa nchi yetu kwenye umasikini na pia kufikia vigezo vya mpango wa Maendeleo ya Millenia ya kupunguza umasikini wa kipato na nchi yetu kuwa na uchumi wa kati. Aidha maboresho yalikuwa na lengo la kuipungizia mzigo Serikali Kuu na kurejesha uwezo kwenye Serikali za Mitaa katika muktadha mzima wa utumishi wa umma ambalo ilikuwa ni "vehicle" ya kuelekea kwenye ugatuzi wa maradaka (D by D) kutoka Serikali kuu na kurejesha madaraka kwa wananchi.

81. Mheshimiwa Spika, Kwa takwimu zilizopatikana kutoka kwenye taarifa ya tathmini ya Benki ya Dunia kama ilivyonukuliwa hapo juu ni kwamba; Progamu ilianza na kiasi cha USD milioni 60.8, na baadae zikaongezwa USD milioni 98 zilizoidhinishwa Juni 15, 2006 na hivyo kufanya mkopo kutoka shirika la IDA kufikia USD 141 Milioni, na USD milioni 3.9 kutoka kwa wakopeshaji wengine na USD milioni 4.9 kutoka LGAs/ Community contribution. Na hivyo kufanya gharama zilizotumika hadi program inafungwa kwa awamu hiyo kufikia USD 150 Milioni

82. Mheshimiwa Spika, katika program ya maboresho ya Serikali za Mitaa iliyochukua takriban miaka kumi kuanzia mwaka 1998 hadi 2008 ilikuwa inaenda sambamba na kuboresha sheria zinazohusika kuongeza vyanzo vya mapato kwa Serikali za mitaa kama ambavyo ziliviotungwa na Bunge hili Tukufu.

83. Mheshimiwa Spika, Kwa masikitiko makubwa ni kwamba uwekezaji wote huo uliofanywa na Serikali za

awamu ya tatu na awamu ya nne umekuwa ni kazi bure, kwa sababu Serikali ya awamu ya tano imechukua vyanzo vikubwa vya mapato kama vile kodi ya majengo, malipo ya mabango, vile vile baadhi ya watumishi wa Wizara za Ujenzi, Ardhi, Maji, Kilimo wanasmamiwa moja kwa moja na wizara husika kinyume kabisa na Sera ya D by D.

84. Mheshimiwa Spika, Tanzania ina Km za mraba 950,000 hivyo ni vigumu sana Serikali Kuu kufika kila pembe ya nchi hii, ndio maana D by D ilibuniwa kuimarisha Serikali za Mitaa kwa kuapatia fedha na wataalam ili huduma zitolewe na kusimamiwa kwa karibu.

85. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuendeleza mfumo wa D by D ulioanza kutekelezwa na Awamu zilizopita kwa kuimarisha mifumo ya uratibu, usimamizi, ufuatillaji na tathminni ambayo ndio majukumu ya msingi ya Serikali Kuu.

86. Aidha, Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaamini katika nguvu na madaraka ya umma katika kuongoza nchi, ugatuzi kamili wa madaraka kwa wananchi kupitia Serikali za Majimbo na mitaa ndio suluhisho la kuchochaea maendeleo kwa haraka. *Rejea Kitabu cha Sera za Chadema ukurasi wa 12 & 13*

5. RASLIMALI WATU

87. Mheshimiwa Spika, uchumi imara na endelevu katika nchi yoyote ile unategemea kwa kiwango kikubwa rasilimali watu iliyopo,hivyo basi, Rasilimali watu ndio msingi mkuu wa kuwepo kwa mfumo wa viwanda unaochochaea ukuaji wa uchumi.

88. Mheshimiwa Spika, uwekezaji katika Miradi mikubwa, vitu n.k ni muhimu, hata hivyo uwekezaji huo hautakuwa na tija endapo nyenzo muhimu ya Rasilimali watu haitapewa kipaumbele kwenye Nyanja ya Elimu, Ujuzi Ufundu na Uongozi.

89. Mheshimiwa Spika, katika mapitio ya bajeti za Wizara, ni kiasi kidogo sana kimetengwa kwa ajili ya mafunzo ya

watumishi. Mabadiliko ya mara kwa mara ya teknolojia na nadharia za utendaji kazi na mifumo yake, inahitaji watumishi wenye weledi na ujuzi wa nadharia mpya ili kuleta mageuzi katika utendaji ili kufikia uchumi wa kati ifikapo 2015.

90. Mheshimiwa Spika, Katika baadhi ya nchi za Afrika na Tanzania ikiwemo, wataalam wanapungua kutokana na vifo na wengine kuzihama nchi kufuata maslahi bora kwingine. Eneo la Afrika, Kusini mwa Jangwa la Sahara linahitaji kuongeza uwekezaji katika watu "investment in people" ili kufikia maendeleo ya kiuchumi yaliyo stahimivu na kuongeza ajira kukidhi idadi ya watu inayoongezeka, ili kufikia malengo ya Maendeleo ya Milenia na kupunguza pengo la Kiuchumi kati yak e na maeneo mengine.

91. Mheshimiwa Spika, CHADEMA kwa kutambua umuhimu mkubwa wa Rasilimali watu/nguvukazi katika ukuaji wa uchumi na kuwa na maendeleo endelevu, katika sera zake ukurasa wa 33 & 34 imeeleza kwa kina ni jinsi gani jambo hilo linatakiwa lipatiwe kipaumbele kutokana na ukweli kwamba idadi ya watu inazidi kuongezeka kila kukicha.

92. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kwamba, pamoja na uwekezaji kwenye miradi mikubwa, kufikia lengo la Tanzania ya Viwanda, ni muhimu sana kwa Serikali kuainisha Utaalam unaohitajika ili kukidhi mahitaji ya lengo la Tanzania ya Viwanda.

93. Mheshimiwa Spika, taaluma zinazohitajika ziwekwe bayana na idadi ya wanafunzi/wafanyakazi watakaopewa mafunzo kila mwaka ijlukane na mwisho Serikali itenye bajeti ya kutosha kwa ajili ya mafunzo.

6. MASLAHI YA WATUMISHI WA UMMA

94. Mheshimiwa Spika, mshahara kwa mtumishi ni haki yake ya msingi kisheria na sio hisani ya mwajiri, aidha, mishahara mizuri ni motisha kwa watumishi kufanyakazi kwa ari na ubunifu. Watumishi wanapolipwa mishahara inayotosheleza mahitaji ya msingi, huchochea ukuaji wa

uchumi kuititia kodi wanazolipa, na wanaponunua bidhaa mbalimbali, hivyo kuchangia kuinua kipato cha watu wenye uchumi duni kwa kuongeza mzunguko wa fedha katika jamii.

95. Mheshimiwa Spika, takwimu za Employment and Earnings Survey inayotolewa na NBS zinaonesha kuwa watumishi katika sekta ya umma ambao ni takriban 15.3% ya waajiriwa wote katika sekta ilio rasmi wanapokea kati ya Tshs 500,001 na 900,000 na takriban 8.1% inapokea mshahara wa kati ya Tshs 300,001 na 500,000. Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa viwango hivi vya madaraja ya mishahara ni vidogo mno kuweza kukidhi mahitaji ya msingi ya watumishi. Hivyo ni rai ya Kambi kuwa viwango vya mishahara vipangwe kulingana na hali halisi ya maisha ilivyo na pia vilinganishwe na dola au sarafu ambayo Serikali inafanya manunuzi yake nje kuititia sarafu hiyo.

96. Mheshimiwa Spika, Ukiwalipa vizuri wafanyakazi watakuwa na uwezo wa kufanya manunuzi ya bidhaa za kilimo kwa bei nzuri hivyo kuinufaisha sekta ya kilimo na mkulima, na pia viwanda kwa sababu watakuwa na uwezo wa kununua bidhaa na hivyo kuongeza ajira katika sekta binafsi na uchumi wa viwanda kukua.

97. Mheshimiwa Spika, ujenzi wa uchumi wa viwanda unategemea sana uwezo wa wananchi kufanya manunuzi ili uzalishaji wa bidhaa kwa viwanda uwe endelevu. Viwanda haviwezi kuzalisha kwa kutegemea soko la nje tu, na tukumbuke Tanzania kwa idadi yake ya watu ni soko kubwa kwa viwanda vyetu kama tu, wananchi watakuwa na uwezo wa kufanya manunuzi. Kinyume cha hapo ni kujidanganya kuwa tunajenga Tanzania ya Viwanda wakati watananzia hawana uwezo wa kufanya manunuzi kwa bidhaa tunazozalisha wenywewe.

98. Mheshimiwa Spika, ili tutoke katika mkwamo huu, Serikali haina budi kuhakikisha inalipa vizuri mishahara kwa wafanyakazi na watumishi wa umma ili kuongeza mzunguko wa fedha kwenye jamii. "Purchasing power" inatoa nguvu zaidi kwa wawekezaji kwenye sekta ya viwanda na zile

zinazotoa huduma kwa jamii pia. Au kwa maneno mengine, ni kwamba mishahara mizuri inachochaea sekta zingine za uzalishaji kwa kuongeza uwezo wa kufanya manunuzi na pale pale kufanya “savings”.

99. Mheshimiwa Spika, Nimezungumzia maslahi ya watumishi wa umma,toka awamu ya Tano iingie madarakani kumekuwa na kauli kinzani kuhusu watumishi kupandishwa mishahara. Mheshimiwa Rais akiongea katika mkutano mkuu wa 33 wa ALAT Oktoba 3, 2017 jijini Dar es Salaam,alisema kuwa hatarajji kuongeza mishahara kwa wafanyakazi mpaka uchumi utakapokua japo haijulikani ni lini uchumi utakua, kwa upande mwengine, Waziri mwenye dhamana ya utumishi wa umma alisema kuwa mishahara itaongezwa pindi uhakiki wa watumishi hewa na vyeti feki umalizike. Tarehe 6 January, 2018 TBC1 na Gazeti la Habari Leo, vilimnukuu Waziri Mkuchika akisema kuwa;

“Bodi ya Mishahara na Maslahi (HSRB) iko katika hatua za mwisho za kurekebisha mfumo mzima wa mishahara, utakaondoa tofauti ya uwiano wa mishahara katika taasisi za umma. Alisema kwa miaka mingi wafanyakazi wa umma wenyewe ujuzi, sifa na uzoefu sawa wamekuwa wakilipwa tofauti kulingana na ofisi anayofanya kazi”

100. Mheshimiwa Spika, kwa tafsiri ya haraka hapa ni kuwa Bodi ya mishahara inachokifanya ni kufanya kile alichokisema Mheshimiwa Rais kuwa kuna watumishi wengine wanalipwa sana na hivyo kuishi kama malaika sasa inabidi waishi kama mashetani. Kwani kuwianisha viwango (standardization) ni kumpunguzia wa juu na kumgawia wa chini ili wawe sawa. **Hizi ni sera na mtazamo wa kijamaa** ambao kwa miaka mingi ndio umetufikisha hapa tulipo, tukumbuke kuwa watu wa kuleta mageuzi katika utumishi wa umma ni lazima walipwe kulingana na mchango wao katika utumishi kwani uwezo na karama za watu zinatofautiana katika kutekeleza kazi.

101. Mheshimiwa Spika, tujiulize swali, ni kwa nini watumishi kwenye sekta binafsi wanafanya kazi kwa bidii, kujituma na kwa ubunifu? Hii ni kwa sababu malipo ya mishahara

hutegemea sana mchango wa mtumishi, na jinsi anavyobuni mikakati ya kuongeza tija kwenye taasisi. Kwa kipimo hicho hicho, watumishi wa umma wanapolipwa mishahara midogo, sio hivyo tu hata nyongeza zao za mwaka ambazo ni stahili zao hazilipwi, hawapandishwi vyeo, wanakopwa perdiem na mwajiri. Je, utategemea mtumishi ajitume afanye kazi kwa bidii, la hasha. Atafanya kile kinachostahili tu.

102. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kuongeza kiwango cha mishahara ya watumishi, ikidhi hali halisi ya maisha na “inflation” wapewe stahili zao za nyongeza ya mishahara na kulipwa madai yao yote, ili kuwatia moyo na kuongeza ari ya kufanyakazi.

103. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi inashauri pia kwamba, Serikali iboreshe zaidi mazingira ya uwekezaji kwa sekta binafsi. Uwekezaji ukiwa mkubwa tatizo la ajira kwa vijana linapungua sana.

104. Mheshimiwa Spika, Takwimu za NBS Employment and Earnings Survey(EES) iliyotolewa mwaka 2018 zinaonesha kuwa jumla ya watu 2,334,969 na watu 2,599,311 mwaka 2016 walikuwa wameajiriwa katika sekta rasmi kwa upande wa Tanzania Bara, ambalo ni ongezeko la watu 308,951 kulinganisha na mwaka 2015. Kati ya hao sekta ya umma ilikuwa imeajiri watu 766,803 mwaka 2015 na 850,616 mwaka 2016 na sekta binafsi ilikuwa imeajiri watu 1,568,165 mwaka 2015 na watu 1,748,695 mwaka 2016 ambao ni takribani nusu ya wale walio kwenye sekta ya umma.

105. Mheshimiwa Spika, takwimu hizo zinaonesha kuwa sekta binafsi kama itawekewa mazingira mazuri ni dhahiri kuwa uwezekano wa kuongeza ajira ni mkubwa zaidi na hivyo kupunguza mzigo kwa Serikali katika kutoa ajira na kuifanya Serikali kubakiwa na jukumu kuu la kuratibu utendaji wa Sekta binafsi.

106. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa kwa sasa vijana 900,000 wanaingia katika soko la ajira hapa Tanzania kila mwaka, Idadi hii inategemewa kuongezeka kwa

kadri idadi ya watu inavyozidi kuongezeka. Hata hivyo ni ajira mpya elfu 50-60 tu zinategemewa kutengenezwa katika sekta rasmi kila mwaka⁷.

107. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasema kuwa kuhusu ajira na ujira katika kitabu cha Sera za CHADEMA **rejea ukurasa wa 28 & 29** zinalezea kwa ufasaha ni jinsi gani tazito hili la ajira na ujira litakavyopatiwa ufumbuzi.

7. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA WA FEDHA 2018/2019 NA MAOMBI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/2020

108. Mheshimiwa Spika, kwa mwaka wa fedha 2018/19 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora fungu 32, walliomba na kupitishliwa na Bunge kiasi cha shilingi 10,939,000,000.00 kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo, sambamba na hizo pia walitengewa kiasi cha shilingi 30,464,499,261.00 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

109. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa hadi mwezi Februari, 2019 kiasi cha shilingi 26,022,270,741.84 ndicho kilikuwa kimepokelewa kutoka Hazina, na katika hizo fedha za miradi ya maendeleo zilizokuwa zimepokelewa ni shilingi 7,316,472,000.00, na shilingi 9,482,490,738.54 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

110. Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha shilingi bilioni 9.5 zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi mengine ni kwa ajili ya Wizara na Idara zake ambazo ni; Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC), Wakala wa Mafunzo kwa njia ya Mtandao (TaGLA), Wakala wa Serikali Mtandao(eGA).

111. Mheshimiwa Spika, ni dhahiri kwamba kwa kiasi hicho kilichotolewa, utendaji kazi kwa taasisi husika hautaleta tija kwa taifa, tija katika sehemu yoyote inaendana moja kwa moja na kiasi cha uwekezaji kinachokuwa kimewekwa. Tusitarajie muujiza katika kupata matokeo mazuri kutoka kwa taasisi zilizochini ya Ofisi hii ya Rais!!

112. Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha 2019/20 Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi 72,572,322,000.00 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na miradi ya Maendeleo. Katil ya fedha hizo shilingi 41,060,000,000.00 ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo, na katil ya kiasi hicho shilingi 4,000,000,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 37,060,000,000.00 ni fedha za nje.

113. Mheshimiwa Spika, kiasi hiki cha fedha za maendeleo ni ongezeko la asilimia 73.4 kulinganisha na kiasi kilichoombwa mwaka wa fedha 2018/19. Lakini kwa mwaka wa fedha 2018/19 hadi mwezi February 2019 fedha za maendeleo zilitokwa zimetolewa ni asilimia 67.8, hivyo tunaitaka Serikali kumalizia fedha zilitobakia ili ofisi hiyo itimiza majukumu yake kama yalivyopanqwa.

8. Mheshimiwa Spika, ukiangalia bajeti iliyoombwa kwa mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa umma, asilimia 90 ni fedha kutoka nje. Fedha hizi kutoka kwa wahisani hazina uhakika kutokana na baadhi ya maamuzi ya Serikali hapo awali kama, kujitoa katika mpango wa kimataifa wa uendeshaji wa Serikali kwa uwazi, sambamba na sheria ya uhuru wa vyombo vyaa habari unaopigwa kelele na wadau wengi wa habari bila kusahau sheria ya takwimu na vyama vyaa siasa iliyopitishwa hivi karibuni kukandamiza uendeshaji wa vyama vyaa siasa, kuna uwezekano mkubwa fedha hizo zisitolewe.

9. HITIMISHO

114. Mheshimiwa Spika, Ofisi hii ya Rais ina jukumu kubwa kusimamia utawala bora. Kuhakikisha wananchi wanalindwa na kusimamiwa kwa mujibu wa katiba, sheria, kanuni na taratibu tulizojiweke. Ofisi hii ina wajibu wa kuratibu na kusimamia watumishi wa umma, wafanye kazi zao kwa weledi, ujuzi na uadilifu. Hata hivyo watumishi watajituma bila shuruti endapo mishahara wanayolipwa inakidhi mahitaji yao ya msingi. Vinginevyo itakuwa "business as usual" kuna usemi kuwa; "*unaweza kumpeleka Punda kwenye maji na asinywe maji hayo*". Serikali ifanye hima, kazi inayofanywa na bodi

ya mishahara ikamilishwe, kwa kuzingatia ukweli kwamba hata kama watumishi wana sifa zinazolingana utendaji wao unatofautiana.

115. Mheshimiwa Spika, ile dhana ya "one size fits all" imeshindwa kuleta mageuzi katika eneo la kazi, historia hujirudia, watendaji wachapa kazi wataondoka kutafuta maslahi bora na utumishi wa umma utabakia na watumishi "mediocre" ambao wapo wapo tu.

116. Mheshimiwa Spika, teuzi nyingi za Ma-RAS, DAS na DED n.k zimefanyika bila kuzingatia utaratibu wa ajira Serikalini, baadhi yao hawana historia ya utumishi Serikalini, hiyo kusababisha ukiukwaji wa kanuni na taratibu za utumishi wa umma.

117. Mheshimiwa Spika, utumishi wa umma ndio nguzo "engine" kuu ya uendeleshaji wa Serikali yoyote Serikali ihakikishe watumishi wote tokea ngazi ya chini hadi juu, wanapatiwa mafunzo ya mara kwa mara ili kujenga utumishi wa umma wenye weledi, maadili, uaminifu na uzalendo.

118. Mheshimiwa Spika, wateule wa Rais mikoani na wilayani wazingatie mamlaka yao kwa mujibu wa sheria, kanuni na taratibu ili kuepuka migogoro, chuki kwa wananchi na wawekezaji. Aidha, wapatiwe mafunzo ya uendeshaji wa Serikali ili wawe chachu ya usalama na utulivu kwenye maeneo yao.

119. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....
Ruth H. Mollel (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI- OFISI YA
RAIS -MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA
BORA
10.04.2019**

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, kutokana na vitabu kutokupatikana kwa muda, kuna tatizo la kiufundi na ni utaratibu wa Kibunge kila hotuba ikisomwa watu wasome, nao wapitie kama nilivyokuwa nafanya mimi, nikagundua taarifa inasomwa tofauti ambayo mimi ninayo. Kwa hiyo, taarifa ya Kambi ya Upinzani kuhusu TAMISEMI tutaisoma saa 11.00. Baada ya hapo tutaanza kuchangia. Mchangiaji wetu wa kwanza atakuwa Mchungaji Msigwa, atafuatwa na Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

Wajumbe wote wa Ulinzi na Usalama mnatakiwa mwende chumba Na. 231 sasa hivi kuna kikao cha dharura.

(Saa 6.53 mchana Bunge lilisitishwa hadi saa 11.00 jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, tukae. Sasa namwita Msemaji wa Kambi ya Upinzani, Mheshimiwa Japhary.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, awali ya yote nimshukuru Mungu tena kwa kunipa nafasi ya kuweza kusimama hapa jioni hii, lakini la pili naomba hotuba yangu yote iingie kwenye Kumbukumbu za Bunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema kwa kunijaalia uhai, afya njema, na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda pia kuwatia moyo viongozi wangu Wakuu wa CHADEMA nikianza na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe na Mheshimiwa Esther

Matiko; ambao walikuwa wamezuiliwa katika Gereza la Segerea, Jijini Dar es Salaam kwa zaidi ya siku 100 kutokana na hujuma na hila walizofanyiwa, Aidha napenda pia kuwatia moyo, Viongozi wengine Wakuu wa CHADEMA ikiwa ni pamoja na Katibu Mkuu wa CHADEMA Dkt. Vincent Mashinji; Naibu Makatibu Wakuu wa CHADEMA, Tanzania Bara na Zanzibar Waheshimiwa John Mnyika na Salum Mwalimu pamoja na baadhi ya Wabunge wa CHADEMA ambao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiandamwa na kesi mbalimbali zikiwemo za uchochezi jambo ambalo limeathiri sana utendaji wao wa kazi za chama. Napenda kuwaambia kwamba hayo ni mapito ya muda mfupi tu lakini mwisho wa yote haki lazima itamalaki; kwa kuwa wema haujawahi kushindwa na uovu na kesho ni imara kuliko jana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu, pamoja na wananchi wangu wa Moshi Mjini kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge, nawaahidi kwamba nitaendelea kushirikiana nao na kutekeleza ahadi zangu na za chama chetu kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kujenga taasisi imara kwa maendeleo endelevu mwaka; huu wa fedha 2019/2020, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza umuhimu wa kujenga Taasisi Imara kwa Maendeleo Endelevu na sababu kubwa ya kuendelea na msisitizo huo ni kwamba ili kuwa na uendelevu katika jambo lolote ni lazima kuwe na mifumo imara ya kitaasisi, kanuni, taratibu na sheria zitakazofuatwa juu ya namna ya kutekeleza jambo hilo na sio kufuata matakwa ya mtu au kikundi cha watu katika kufanya hivyo kwa kuwa watu ni wa kupita lakini taasisi na mifumo itabaki.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tukumbuke kwamba Mwalimu Nyerere alituachia Taifa moja ambalo limekuwa halibaguani kikabilal wala katika imani za dini, lakini kwa sasa kuna viashiria vya ubaguzi ndani ya nchi yetu kwa mitazamo ya itakadi za vyama vyetu vya siasa. Kila mwananchi ana haki ya kuijunga na chama chochote cha siasa kilichosajiliwa

kwa mujibu wa sheria za nchi, hivyo ni makosa makubwa sana kama Serikali itaruhusu wananchi wake wabaguane kwa misingi ya itikadi zao. Jambo hilo ni baya na mbegu hiyo ikikomaa mionganii mwetu italisambaratisha Taifa letu. Ni vizuri tulirejeshe Taifa letu kwenye misingi yake ya umoja na mshikamano ambapo utu wa mtu ulikuwa unapimwa kwa matendo yake na sio kutokana na chama anachokiamini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni bahati mbaya sana kwamba taasisi tulizonazo zimekuwa dhaifu sana na udhaifu huo umesababishwa na viongozi wanaopenda kutawala kwa kutumia njia za mkato, wasiopenda kufuata taratibu...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary ushapewa maelekezo kuhusu *paragraph five*, iache twende *paragraph six*. Maelekezo ya Kiti ni hayo, twende *paragraph six*.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, umesema nisome *paragraph ipi*, ukurasa wa ngapi?

MWENYEKITI: *Six*, ukurasa wa pili.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Nianzie wapi sasa kusoma?

MWENYEKITI: Namba sita.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Sawa niambie *statement* ya kuanza kusoma.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Spika, dhana hii ya kujenga Taasisi imara..

MHE. JAPHARY R. MICHAEL - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Hapo naruhusiwa kusoma?

MWENYEKITI: Ndiyo, unaruhusiwa.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: .Mheshimiwa Mwenyekiti, dhana hii ya kujenga taasisi imara ina umuhimu mkubwa pia kwa Serikali za Mitaa. Inajulikana kwamba Serikali za Mitaa, ni chombo kikuu kinachotakiwa kuimarisha demokrasia katika maeneo ya wananchi na kutumia demokrasia hiyo kuharakisha maendeleo ya wananchi. Jambo la kushangaza ni kwamba Serikali za Mitaa haziheshimiwi na kila mara Serikali Kuu inazipoka madaraka yake na vyanzo vyake vya mapato licha ya kwamba zimepewa madaraka yake kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 145 na 147.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Matokeo ya kuziingilia Serikali za Mitaa ni kushindwa kutekeleza wajibu na majukumu yake. Mbaya zaidi Serikali za Mitaa zimekuwa na historia mbaya ya kuvunjwa na kurejeshwa tena kwa namna ambayo Serikali Kuu inataka. Mbaya zaidi kila Mkuu wa nchi anayekuja, anaendesha Serikali za Mitaa kwa matakwa na maono yake na sio kwa matakwa ya wananchi katika ngazi za chini kulingana na mipango yao ya maendeleo waliyoibua.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kudhoofishwa kwa Serikali za Mitaa, utaratibu wa kuteua Wakurugenzi na Wakuu wa Idara wa Halmashauri; pamoja na mamlaka ya kikatiba aliyonayo Rais ya kuteua Wakurugenzi wa Halmashauri, mamlaka hayo yanatumika vibaya kwa kuteua Wakurugenzi wasio na sifa jambo ambalo linadhoofisha halmashauri nyingi kiutendaji. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaelewa kwamba mionganoni mwa mambo ambayo yanapaswa kuzingatiwa kabla ya kuteua Mkurugenzi ni kumfanyia mhusika upukuzi (*vetting*) na mionganoni mwa vitu vinavyoangaliwa ni angalau mtu huyo awe amewahi kuwa

mtumishi wa umma kwenye idara kwa kipindi kisichopungua miaka nane.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tofauti na utaratibu huo wa kisheria, kigezo kikubwa kinachotumika kuwateua wakurugenzi wa Halmashauri katika Serikali hii ya awamu ya tano ni ukada wa Chama cha Mapinduzi. Ukurugenzi sasa umekuwa unatolewa kama zawadi kwa makada wa CCM walioshindwa katika kura za maoni ndani ya chama chao na wale walioshindwa katika chaguzi nyingi nyingine katika nchi. Kwa maneno mengine asilimia kubwa ya Wakurugenzi wa Halmashauri ni makada wa Chama cha Mapinduzi waliokataliwa na wanachama wenzao kwenye kura za maoni ndani ya chama chao, leo hii wamepewa madaraka ya kuwaongoza wananchi halafu tunatarajia halmashauri zifanye vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa vyovyyote vile uteuzi wa namna hii usiozingatia masharti yaliyowekwa na sheria ni mkakati wa kudhoofisha halmashauri zetu kwa kuwapatia Wakurugenzi ambaao uwezo wao na uzoefu wao unatia shaka, hivyo halmashauri nyingi zinakosa maendeleo kwa kuongozwa na Wakurugenzi wanao kosa, uwezo na uzoefu wa kiutendaji na weledi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaamini kwamba Serikali za Mitaa ni mhimili muhimu sana katika kuchochaea maendeleo ya nchi, hivyo inapaswa kusimamiwa na watendaji wenye weledi mkubwa ili kuleta ustawi wa wananchi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wakala wa Ujenzi wa Barabara Vijijini (*TARURA*); *TARURA* ni wakala ulioundwa kwa kupitia Tangazo la Serikali la mwaka 2017 kwa madhumuni ya kuhudumia barabara zote zilizokuwa zinahudumiwa na Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji. Hivyo basi, mfumo mzima wa uanzishwaji wake ukiangalia kwa undani haukuwa wazi kiasi kwamba unaacha maswali mengi sana yasiyo na majibu juu ya utendaji wa Halmashauri zetu za hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba ni Azimio la Bunge lako Tukufu lililopelekea kuanzishwa kwa *TARURA* lakini ujio wake umekuwa wa haraka na haukuwa shirikishi, kwa kiwango cha kuridhisha. Mpaka sasa kuna mkanganyiko mkubwa kati ya watendaji wa *TARURA* na Madiwani pamoja na watendaji wa halmashauri hapa nchini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maeneo yenze utata zaidi ni:-

(i) Kutoshirikishwa kwa Mabaraza ya Madiwani katika hatua yoyote ya mchakato wa utengenezaji wa barabara ikiwemo vikao vya maamuzi mpaka usimamizi wa miradi ya barabara;

i. Kutolazimika kuzingatiwa kwa barabara vya vipaumbele vya Mabaraza ya Madiwani ambao ndio wawakilishi wa wananchi;

ii. Kukosekana kwa Bodi ya *TARURA* kama ilivyo Bodi ya *TANROADS*;

iii. Uwezo mdogo wa fedha za dharura kwa ajili ya kukabiliana na uharibifu wa mara kwa mara unaotokana na majanga kama mafuriko na mengine kama hayo. Hali hii imefanya madaraja, makalavati na barabara nyingi kwenye vijiji na mitaa kuwa katika hali mbaya ya uharibifu kutokana mvua zinazonyesha katika maeneo mengi hapa nchini; na

iv. Kiwango cha asilimia 30 kinachotengwa kutoka katika Mfuko wa Barabara hakiwiani na urefu wa barabara za mijini na vijijini ambazo *TARURA* wanapaswa kusimamia hivyo kufanya barabara nyingi ziendelee kuwa na hali mbaya zaidi ya uharibifu kuliko hata zilipokuwa zinasimamiwa na Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri mambo yafuatayo ili kuboresha hii hali ya *TARURA*:

i. Lazima *TARURA* washirikishe halmashauri katika hatua mbalimbali za mchakato wa kutengeneza miundombinu ya

barabara kwa vile Madiwani na Mkurugenzi ndio wanaofahamu barabara zenyeku;

ii. Iwepo Bodi ya *TARURA* ambayo itaundwa katika ngazi ya Halmashauri;

iii. Bajeti ya *TARURA* longezwe kuwa asilimia 40 kutoka katika Mfuko wa Barabara badala ya asilimia 30 ya sasa ili kuifanya *TARURA* iwe na uwezo wa kutimiza wajibu wake kwa kiwango cha kuridhisha;

iv. *TARURA* ili ijiendeshe, Serikali isinyang'anye Halmashauri vyanzo vyake vichache vya mapato vilivyobaki ambavyo ndivyo vinasaidia kuendesha shughuli za kila siku za Halmashauri katika kutoa huduma kwa wananchi;

v. Lazima *TARURA* iwe suluhisho la kilio cha Wabunge cha muda mrefu cha kutaka barabara zao zipandishwe daraja ili zihudumiwe na *TANROAD* vinginevyo lengo kuu la kuanzishwa kwa *TARURA* litakuwa halijafikiwa; na

vi. Lazima iwepo bajeti ya dharura kwa kuhudumia barabara za vijiji na mitaa zinazoharibika kutohakana na majanga mbalimbali ya asili kama vile mafuriko.

Mheshimiwa Mwenyekiti, maandalizi ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa mwaka 2019, madai ya Tume Huru ya Uchaguzi; Kambi Rasmi ya Upinzani inafahamu kuwa mfumo wa uchaguzi wa nchi hii unasimamiwa na TAMISEMI. Kwa sababu Tume inawatumia Wakurugenzi wa Halmashauri kusimamia uchaguzi. Pia ikumbukwe kuwa tulishaeleza kuwa Wakurugenzi wengi wa halmashauri walioteuliwa na Rais ni makada wa Chama cha Mapinduzi ambao walishindwa ama kwenye kura za maoni ndani ya chama chao au walishindwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 74 (14) inakataza maofisa wanaohusika na uchaguzi kujihusisha na Siasa, licha ya katazo hilo tumeshuhudia Wakurugenzi wengine wakishiriki vikao vya

CCM na kupokea maelekezo mbalimbali bila kificho. Wakurugenzi hao wa Halmashauri, kwa kuwa ni makada wa CCM wanapokuwa wasimamizi wa uchaguzi, ama kwa utashi wao au kwa kulazimishwa wanatangaza mgombea wa CCM ambaye hajashinda uchaguzi na kumnyima haki yule aliyeshinda kwa vile tu ni wa chama cha upinzani. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni lini Serikali italeta Muswada hapa Bungeni kwa ajili ya kupitia upya mfumo wa uchaguzi nchini ili kuepusha madhara yanayoweza kutokea kutokana na upungufu uliomo katika uchaguzi ukizingatia kwamba uchaguzi ni zoezi muhimu sana kwa ajili ya kujenga demokrasia na utawala bora.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Ofisi ya Rais, TAMISEMI iko chini ya Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi. Mfumo mzima wa uchaguzi ndani ya CCM uko chini yake moja kwa moja. Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini ambaeo ni waratibu na wasimamizi wa chaguzi hizo ni wateuliwa wa Rais na bila shaka ni wana-CCM kwa kuwa haitegemewi Rais kuteua timu inayompinga kufanya nayo kazi. Aidha, upo ushahidi wa wazi kuwa Wakurugenzi wa Halmashauri ni makada wa CCM walioshindwa katika kura za maoni na kupewa zawadi ya ukurugenzi na wana maelekezo ya Rais kuwa wasiwatangaze wagombea wa upinzani hata kama wameshinda katika chaguzi. Rais alinukuliwa akisema: “*Mkurugenzi atakayemtangaza Mpinzani wakati amepewa nyenzo zote za utendaji na Serikali atakuwa hana kazi.*” (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sura hiyo, Ofisi yake haiwezi kuendesha kwa haki uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambaeo unajumuisha vyama vingi. Hii sababu yake ni rahisi, ye ye ni refa na ni mchezaji kwa wakati huohuo hivyo hawezi kutenda haki katika mchezo. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani bado inatafakari mantiki ya kushiriki uchaguzi kama mfumo uliopo sasa hautarekebishwa. Aidha, Mheshimiwa Rais

anapaswa kushauriwa na wasaidizi wake kufuta kauli yake ya kwamba Mkurugenzi aliyemtangaza Mpinzani atafutwa kazi. Kwa uzito wa mamlaka ya Mheshimiwa Rais kauli hiyo ikiachwa ilivyo inaweza kutumiwa vibaya na wakurugenzi jambo ambalo linaweza likasababisha fujo. Vinginevyo itakuwa ni fujo na matokeo yake ni machafuko ya kisasa. Hivyo, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kuwa Serikali kushughulikia jambo hilo mapema ili kuepuka uvunjifu wa amani unaoweza kutokea.

Mheshimiwa Mwenyekiti, posho za Wenyeviti wa Serikali za Mitaa; katika bajeti zilizopita Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikishauri Serikali kuzielekeza halmashauri zipandishe viwango vya posho za Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, Vijiji na Vitongoji kufika shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa mwezi pamoja na kuanzisha posho ya mkono wa kwa heri wa shillingi laki tano pale wanapomaliza muda wao. Hii inatokana na ukweli kwamba kundi hii la uwakilishi linafanya kazi kubwa ya kuwashudumia wananchi katika ngazi za chini kabisa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani ilishauri kuanzishwa kwa posho ya shillingi elfu 30 kwa Wajumbe wa Vijiji, Vitongoji na Mitaa ili kuwapa ari ya kutekeleza majukumu yao ambayo ni magumu sana ya kuwashudumia wananchi wa kada ya chini kabisa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na majibu ambayo yametolewa hapa Bungeni na Naibu Waziri, TAMISEMI kwa kudhani kwamba, Viongozi wa Serikali za Mitaa wakiwa na kazi nyingine za kuingiza kipato basi hawastahili kulipwa posho. Tunapenda kusitiza na kuishauri Serikali hii kwamba Wenyeviti wa Mitaa ni viongozi wa kuchaguliwa kama walivyo Wabunge na Madiwani ambao wanapata posho. Hivyo, stahiki za posho kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa ni stahiki zao kwa kazi wanazofanya bila kujali shughuli zao binafsi za kuwaingizia kipato.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusitiza umuhimu na ulazima wa kupandisha posho hizo na kwamba lazima viwango vya

posho vilingane kwa Halmashauri zote. Aidha, Serikali iache kuchukua vyanzo nya mapato ya halmashauri ili kuziwezesha halmashauri hizo kuwa na mapato mengi na ziweze kutekeleza wajibu wa kulipa posho kwa Wenyeviti wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali imeshindwa kusimamia elimu ya msingi; ni wazi kwamba...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary utanisaidia ukiwa unaruka tu, soma hizo page na nini ili Wabunge wote waweze kufuatilia.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ukurasa wa 17, sawa, naruhusiwa kuendelea?

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. JAPHARY R. MICHAEL - MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ni wazi kwamba baada ya Serikali kutamka kwamba elimu msingi itatolewa bila malipo ya ada, kumekuwa na ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi kwa shule za msingi na sekondari ambazo ziko chini ya uratibu wa Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Pamoja na neema hii kwa wananchi, jambo hili limekumbwa na changamoto kubwa ya uhaba wa walimu, miundombinu, vifaa nya kufundishia na zaidi sana bajeti ndogo ya maendeleo katika kutatua changamoto hizo ili kuweza kuhudumia idadi kubwa ya wanafunzi mashulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, upungufu wa kutisha wa Walimu katika shule za msingi na sekondari; Kambi Rasmi ya Upinzani kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita imekuwa ikiikumbusha Serikali hii ya CCM kwamba, hakuna elimu bila Walimu. Sarakasi na mbwembwe zote za kisiasa za elimu bure, elimu bila malipo na sasa elimu bila ada hazitasaidia

chochote kama hakuna idadi ya kutosha ya Walimu wenye weledi na motisha wa kufanya kazi ya kufundisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa takwimu za *BEST* za mwaka 2016 na 2017, idadi ya walimu kwa shule za msingi imeshuka kutoka walimu 191,772 mwaka 2016 hadi kufikia walimu 179,291 mwaka 2017 ikiwa ni anguko la asilimia 6.5 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuwa 1.50. Aidha, katika shule za awali, idadi iliyopungua ni walimu 1,948 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuongezeka kutoka 1:135 mwaka 2016 hadi kufikia 1:159 mwaka 2017 badala ya 1:25 ambao ni uwiano unaokubalika.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika shule za sekondari kuna uhaba mkubwa wa walimu kwa baadhi ya masomo kama ifuatavyo: Hisabati kuna upungufu wa walimu 7,291, Baiolojia kuna upungufu wa walimu 5,181, Kemia kuna upungufu wa walimu 5,373 na Fizikia kuna upungufu wa walimu 6,873. Hii ni kwa mujibu wa takwimu za *BEST* za 2016. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mujibu wa Takwimu za Elimu Msingi za Mikoa walimu 7,743 wanatarajiwa kustaafu kati ya mwaka 2018 na 2019. Aidha, takriban walimu zaidi ya 30,000 wana umri wa zaidi ya miaka 51 ya kuzaliwa; hivyo na wao wanatarajiwa kustaafu muda mfupi ujao. Kwa kuzingatia ukweli kwamba bila walimu hakuna elimu, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu ni kitu gani kimesababisha upungufu mkubwa wa walimu ukizingatia kwamba kuna idadi kubwa ya wahitimu wa fani ya ualimu katika vyuo mbalimbali vya ualimu vilivyopo nchini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hivi karibuni Serikali imetangaza ajira 4000 za walimu. Waliojitokeza kuomba nafasi hizo ni zaidi ya watu 90,000. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge ni kwa nini Serikali haikutoa nafasi nyingi zaidi za ajira kwa walimu ili kukabiliana na upungufu huu wa walimu wa kutisha? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kujivekea mpango mkakati wa kuajiri angalau walimu 15,000 kila mwaka kwa

muda wa miaka mitano ili kupunguza kwa kiwango kikubwa upungufu wa walimu mashulenii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, uhaba mkubwa wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari nchini. Mazingira bora ya kufundisha na kujifunza yanategemea sana uwepo wa miundombinu rafiki na wezeshi. Ni jambo ambalo haliwezekani kutegemea kupanda kwa ubora wa elimu ikiwa hakuna jitihada zozote za kuboresha miundombinu itakayosaidia zoezi la kufundisha na kujifunza kufanikiwa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna uhaba mkubwa sana wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari za umma, jambo linalopelekea mazingira magumu ya kufundisha na kujifunza na hivyo kushusha viwango vya ubora wa elimu. Kwa mujibu wa takwimu za *BEST*, 2016 na 2017 ni kwamba uhaba wa maktaba katika shule za msingi umeongezeka kutoka asilimia 88 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 91.1 mwaka 2017.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu hizo zinaonyesha pia kwamba upungufu wa maabara katika shule za sekondari unatofautiana kulingana na masomo husika. Kwa mfano, upungufu wa maabara za somo la Bailojia ni asilimia 51.5, Fizikia ni asilimia 54.3 na Kemia ni asilimia 43.3.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu zinaonyesha pia kwamba kuna upungufu wa nyumba za walimu 186,008 sawa na asilimia 83.1 na upungufu wa majengo ya utawala 10,943 sawa na asilimia 83.4. Aidha, uwiano uliopo sasa wa matundu ya vyoo na wanafunzi wa kike ni 1:53 wakati uwiano unaoshauriwa ni 1:20 na kwa wavulana uwiano uliopo ni 1:56 na unaoshauriwa ni 1:25. Hivyo kufanya upungufu wa mashimo ya vyoo kwa wasichana kuwa 62% na kwa wavulana kuwa 56%. Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2016 inaonyesha kwamba ni asilimia 41 tu ya shule za msingi na sekondari nchini Tanzania zenye miundombinu inayokidhi viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, takwimu nilizozitaja hapo juu zinatiliwa nguvu na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2016/2017 inayoonyesha kwamba shule za msingi zina upungufu wa madarasa kwa asilimia 85, upungufu wa vyoo asilimia 66 na upungufu wa nyumba za walimu asilimia 14. Kwa upande wa sekondari kuna upungufu wa vyumba vyta madarasa asilimia 52, upungufu wa maabara asilimia 84, upungufu wa madawati asilimia 86, upungufu wa nyumba za walimu asilimia 85, upungufu wa mabweni asilimia 88 na upungufu wa matundu ya vyoo asilimia 83. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wakati nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wako kwenye mpango wa kuwapatia wanafunzi wote wa shule za msingi Kompyuta Mpakato (*Laptops*) sisi Tanzania bado tunazungumzia uhaba wa matundu ya vyoo. Ni alibu sana kwa Serikali hili inayojitapa kwamba inatoa elimu bure wakati mazingira ya kutolea elimu hiyo ni mabaya na yanachangia kwa kiwango kikubwa kushuka kwa ubora wa elimu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali inafahamu upungufu huu kwa kuwa takwimu zilizotumika ni za Serikali. Swali ni, je, kwa nini upungufu huu umekuwa ukiongezeka? Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulielea Bunge imepunguza tatizo la uhaba wa miundombinu mashulenii kwa kiwango gani hadi sasa? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza imetenga bajeti kiasi gani katika mwaka wa fedha 2019/2020 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mashulenii ili kukabiliana na uhaba ulipo sasa?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kupungua kwa bajeti ya sekta ya elimu. Pamoja na Serikali hii ya Awamu ya Tano kuuaminisha umma kwamba elimu ni kipaumbele chake, kwa kutangaza kwamba itatoa elimu msingi bila malipo ya ada azma hiyo hionekani katika upangaji wa bajeti ya elimu. Pamoja na ukweli kwamba tangu Serikali hii iingie madarakani, bajeti kuu ya Serikali imekuwa ikiongezeka lakini ongezeko hilo limekuwa halina manufaa yoyote katika sekta ya elimu kwa kuwa bajeti ya elimu imekuwa ikipungua kila

mwaka kwa miaka yote mitatu ya utawala wa Serikali hii ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, wakati Bajeti kuu ya Serikali iliongezeka kutoka shilingi trillioni 29.5 mwaka 2016/2017 hadi trillioni 31.7 mwaka 2017/2018 na kufikia shilingi trillioni 32.4 mwaka 2018/2019, bajeti ya sekta ya elimu imekuwa ikishuka kutoka shilingi trillioni 4.77 hadi shilingi trillioni 4.706 mpaka shilingi trillioni 4.628 kwa mtiririko huohuo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya sekta ya elimu iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/2019 ya takribani shilingi trillioni 4.628 ni pungufu kwa asilimia 1.7 ukilinganisha na bajeti ya elimu ya shilingi trillioni 4.706 iliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2017/2018. Upungufu wa asilimia 1.7 unaweza kuonekana mdogo lakini asilimia hiyo ni sawa na shilingi bilioni 78 zillizopungua kwenye bajeti hiyo. Fedha hizo zingeweza kujenga mabweni zaidi ya 500 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 40 kila moja na madarasa 1,000 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 45 kila moja. Hii ina maana kwamba kama ingetakiwa kutumia fedha kuboresha mazingira ya kujifunza kwa mtoto wa kike, zaidi ya watoto wa kike 12,500 ambaao hutembea umbali mrefu kwenda na kurudi kutoka shulenii wangepata malazi katika mabweni hayo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, licha ya bajeti ya elimu kuwa na mwelekeo wa kupungua, utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika sekta hii una hali mbaya zaidi. Hii ni kwa sababu zaidi ya asilimia 90 ya bajeti ya elimu inayopelekwa TAMISEMI ni ya Matumizi ya Kawaida na asilimia kidogo tu ndiyo hutekeleza Miradi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2016/2017 bajeti ya Matumizi ya Kawaida iliyopelekwa TAMISEMI kwenye sekta ya elimu ilikuwa ni asilimia 93 huku Bajeti ya Maendeleo ikiwa ni asilimia 7 tu. Aidha, mwaka uliofuata wa 2017/18 bajeti ya Matumizi ya Kawaida ilikuwa ni asilimia 93.4 huku ya Maendeleo ikishuka

hadi asilimia 6.6. Kwa hiyo, kwa wastani, kwa miaka miwili ya kwanza ya Serikali hii ya Awamu ya Tano, Serikali imekuwa ikitenga wastani wa asilimia 6.5 ya jumla ya bajeti ya sekta ya elimu katika Ofisi ya Rais, TAMISEMI kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo na zaidi ya asilimia 94 kwa Matumizi ya Kawaida.

Mheshimiwa Mwenyekiti, utengaji huo hafifu wa bajeti ya Maendeleo hauwezi hata kidogo kutatua changamoto kubwa za upungufu wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, uhaba wa walimu, maabara na nyenzo nyingine za kufundishia kama nilivyoainisha hapo kabla. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Serikali itaongeza bajeti ya maendeleo ya elimu msingi chini ya TAMISEMI hadi angalau ifikie asilimia 30 ya bajeti inayotengwa kwa ajili ya elimu msingi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nahitimisha hotuba yangu kwa kusema mambo makubwa mawili. Jambo la kwanza, narudia tena umuhimu wa kujenga taasisi imara kwa maendeleo endelevu. Taasisi zetu za kiserikali zingekuwa imara hii migogoro na vurumai katika Halmashauri zinazosababishwa na Wakuu wa Wilaya na Mikoa wasio na karama za uongozi zisingetokea. Naikumbusha tena Serikali kutoa mwongozo wa mipaka ya kazi kwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa kama Bunge lilivyoazimia katika Mikutano iliyopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la pili la kuzingatia ni vyanzo vya mapato ya ndani ya Halmashauri zetu ili taasisi ziwe imara kama tunavyotamani ziwe ni lazima ziweze kuwa na vyanzo vya kutosha vya mapato ili ziweze kuijendesha kwa uhuru na mamlaka za Serikali za Mitaa ziweze kuwa timilifu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha, ahsante sana. (*Makofii*)

HOTUBA YA MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI
BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – TAMISEMI, MHESHIMIWA
JAPHARY RAPHAEL MICHAEL (MB), AKIWASILISHA BUNGENI
MAONI YA KAMBI RASMI YA UPINZANI KUHUSU MAKADIRIO
YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KATIKA OFISI HIYO,
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 - KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI

*Inatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Kudumu za
Bunge, Toleo la Januari, 2016*

UTANGULIZI

1. **Mheshimiwa Spika**, kwanza kabisa napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwangi wa rehema, kwa kunijalia uhai, afya njema na kunipa nguvu na uwezo wa kusimama mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu makadirio ya mapato na matumizi ya fedha katika Ofisi ya Rais - TAMISEMI kwa mwaka wa fedha 2019/2020.

2. **Mheshimiwa Spika**, napenda pia kuwatia moyo viongozi wangu wakuu wa CHADEMA nikianza na Mwenyekiti wa CHADEMA Taifa na Kiongozi wa Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikaeli Mbewe na Mheshimiwa Esther Matiko; ambaao walikuwa wamezuiliwa katika gereza la Segerea jijini Dar Es Salaam kwa zaidi ya siku 100 kutohana na hujuma na hila walizofanyiwa, Aidha napenda pia kuwatia moyo, Viongozi wengine wakuu wa CHADEMA ikiwa ni pamoa na Katibu Mkuu wa CHADEMA Dkt. Vincent Mashinji; Naibu Makatibu Wakuu wa CHADEMA – Tanzania Bara na Zanzibar Waheshimiwa John Mnyika na Salum Mwalimu pamoa na baadhi ya wabunge wa CHADEMA ambaao kwa nyakati tofauti wamekuwa wakiandamwa na kesi mbalimbali zikiwemo za uchochezi jambo ambalo limeathiri sana utendaji wao wa kazi za chama. Napenda kuwaambia kwamba; hayo ni mapito ya muda mfupi tu lakini mwisho wa yote haki lazima itatamalaki; kwa kuwa wema haujawahi kushindwa na uovu na kesho ni imara kuliko jana.

3. **Mheshimiwa Spika**, Kwa namna ya pekee napenda kuishukuru familia yangu; pamoja na wananchi wa Moshi Mjini kwa ushirikiano mkubwa wanaoendelea kunipatia katika kutekeleza majukumu yangu ya kibunge, nawaahidi kwamba nitaendelea kushirikiana nao na kutekeleza ahadi zangu na za chama chetu kwao.

KUJENGA TAASISI IMARA KWA MAENDELEO ENDELEVU

4. **Mheshimiwa Spika**, mwaka huu wa fedha 2019/20, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza juu ya umuhimu wa *Kujenga Taasisi Imara kwa Maendeleo Endelevu (Building Strong Institutions for Sustainable Development)*; Na Sababu kubwa ya kuendelea na msisitizo huo ni kwamba ili kuwa na uendelevu (sustainability) katika jambo lolote ni lazima kuwe na mifumo imara ya kitaasisi, kanuni, taratibu na sheria zitakazofuatwa juu ya namna ya kutekeleza wa jambo hilo; na sio kufuata matakwa ya mtu au kikundi cha watu katika kufanya hivyo kwa kuwa watu ni wa kupita lakini taasisi na mifumo itabaki. Tukumbuke kwamba Mwalimu Nyerere alituachia Taifa moja ambalo limekuwa halibaguani kimakabila wala katika imani za dini; lakini kwa sasa kuna viashiria vya ubaguzi ndani ya nchi yetu kwa mitazamo ya itakadi za vyama vyetu vya siasa. Kila mwananchi ana haki ya kujunga na chama chochote cha siasa kilichosajiliwa kwa mujibu wa sheria za nchi; hivyo ni makosa makubwa sana kama Serikali itaruhusu wananchi wake wabaguane kwa misingi ya itikadi zao. Jambo hilo ni baya na mbegu hiyo ikikomaa miongoni mwetu italisambaratisha Taifa letu. Ni vizuri tulirejeshe taifa letu kwenye misingi yake ya umoja na mshikamano ambayo utu wa mtu ulikuwa unapimwa kwa matendo yake na sio kutokana na chama anachokiamini.

[MANENO YA AYA YA 5 HADII 7 YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]

8. **Mheshimiwa Spika**, Tofauti na utaratibu huo wa kisheria; kigezo kikubwa kinachotumika kuwateua wakurugenzi wa Halmashauri katika Serikali hii ya awamu ya

tano; ni ukada wa Chama Cha Mapinduzi. Ukurugenzi sasa umekuwa unatolewa kama zawadi kwa makada wa CCM walioshindwa katika kura za maoni ndani ya chama na wale walioshindwa katika chaguzi nyingine. Kwa maneno mengine asilimia kubwa ya Wakurugenzi wa Halmashauri ni makada wa chama cha mapinduzi waliokataliwa na wanachama wenzao kwenye kura za maoni ndani ya chama chao, leo ndio wamepewa madaraka ya kuwaongoza wananchi halafu tunatarajia halmashauri zifanye vizuri.

9. Mheshimiwa Spika, kwa vyovypote vile; uteuzi wa namna hii usiozingatia masharti yaliyowekwa na sheria ni mkakati wa kudhoofisha halmashauri zetu kwa kuwapatia wakurugenzi ambao uwezo wao na uzoefu wao unatia shaka, hivyo Halmashauri nyingi zinakosa maendeleo kwa kuongozwa na wakurugenzi wanao kosa, uwezo na uzoefu wa kiutendaji na weledi.

10. Mheshimiwa Sipika Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaanini kwamba Serikali za Mitaa ni mhimili muhimu sana katika kuchochaea maendeleo ya nchi hivyo inapaswa kusimamiwa na watendaji wenye weledi mkubwa ili kuleta ustawi wa wananchi.

**a) VYANZO VYA MAPATO VYA HALMASHAURI
KUCHUKULIWA NA SERIKALI KUU:**

11. Mheshimiwa Spika, ili halmashauri ziwe na uwezo wa kuleta maendeleo endelevu mbali na mgawo unaotoka Serikali kuu, ni lazima na muhimu kwa halmashauri kuwa na vyanzo vya ndani vya mapato na fedha hizo kuzitumia kulingana na mahitaji na mipango inayopangwa kuanzia Serikali za vijiji.

12. Mheshimiwa Spika, Vyanzo vya mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa vimeainishwa katika vifungu Na. (6) hadi (9) vya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa Na. 9 ya mwaka 1982 yaani (The Local Government Finance Act, No. 9 of 1982).Kulingana na Sheria ya Fedha Na. 9 ya mwaka 1982 ya Serikali za Mitaa iliyorekebishwa na Sheria ya Fedha Na. 15

ya mwaka 2003 yaani (The Finance Act No. 15 of 2003), Serikali za Mitaa hazitozi kodi ya Mapato bali kodi hiyo hutozwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania(TRA). Ni muhimu Serikali kuu hasa awamu ya tano iache utaratibu wake iliouanzisha tangu iingie madarakani wa kupora vyanzo vya mapato vya halmashauri.

13. Mheshimiwa Spika, tangu serikali hii ya awamu ya tano iingie madarakani imechukua vyanzo mbalimbali vya mapato kutoka katika halmashauri nchini na kuvihamishia serikali kuu. Baadhi ya vyanzo hivyo ni kodi ya majengo (property tax) ambayo sasa, Serikali kuu imekichukua chanzo hiki na kukiweka chini ya Mamlaka ya Mapato nchini TRA. Serikali pia hairejeshi asilimia 30 ya mapato yanayotokana na kodi ya ardhi. Ikumbukwe kuwa ardhi ndiyo rasilimali pekee ambayo kila Halmashauri katika nchi inaimiliki. Ardhi ndiyo chanzo cha mapato cha uhakika kwa kila Halmashauri ya nchi hii, hivyo kitendo cha Serikali Kuu kuchukua chanzo hiki ni kuzifanya halmashauri zishindwe kabisa kutoa huduma za msingi kwa wananchi wake.

14. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kutazama upya uamuzi wake wa kuchukua vyanzo vya mapato vya Halmashauri. Ni vema Serikali ikarejesha vyanzo hivyo kwa Halmashauri kwa kuwa Halmashauri zina uwezo wa kukusanya mapato kutoka vyanzo hivyo kwa umahiri zaidi. Aidha, kurudisha vyanzo hivyo kwa Halmashauri kutaimarisha zaidi ile dhana ya ugatuaji wa madaraka (D by D).

b) KUANZISHWA VITAMBULISHO VYA UJASIRIAMALI

15. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais wakati akizungumza na maafisa kutoka Mamlaka ya Mapato nchini TRA, katika ukumbi wa mikutano wa Mwalimu Julius Kambarage Nyerere, alitumia mikutano huo, kulitangazia taifa kuwepo kwa vitambulisho vya wajasiriamali wadogo ambavyo kwa maelezo yake mwenyewe alisema amevitengeneza yeye. Maelezo na maelekezo ya Mheshimiwa Rais ni kwamba, vitambulisho hivyo,

vilivytengenezwa na lkulu vinauzwa kwa gharama ya shilingi 20,000/- kwa mwaka na kwamba wafanyabiashara wasiolipia mapato Mamlaka ya Mapato nchini (TRA) wanapaswa kuwa na vitambulisho hivyo.

16. Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alieleza ubora wa vitambulisho kutokana na teknolojia aliyotumia kutengeneza vitambulisho hivyo, huku akitweta kuwa ni mkombozi wa wajasiriamali ambao wamekuwa kwa kipindi kirefu sasa wananyanyaswa na kubughudhiwa.

17. Mheshimiwa Spika, Maelekezo hayo ya Mheshimiwa Rais, yalitakiwa yaende sambamba na mipango ya Serikali ya kuwajengea wajasiriamali hawa mazingira rafiki ya kujipatia mitaji na masoko ili waweze kulipa kodi za serikali kwa ufanisi. Kwa maneno mengine, ni kama Serikali inang'ang'anlia kumkamua ng'ombe maziwa bila kumlisha, huku ikitarajia kupata maziwa mengi zaidi.

18. Mheshimiwa Spika, wajasiriamali hawa, ambao wengi wao ni kundi la vijana na wanawake, ni kundi linalojishughulisha na biashara za kimachinga, mama lishe, wafanya biashara barabarani, minadani na mtaani ambao wamekuwa wakinyanyaswa na baadhi ya watendaji wa Serikali kama vile Wakuu wa Wilaya na Mikoa, Wakurugenzi wa Halmashauri na wasaidizi wao katika ngazi za chini, wafanyabiashara wamekuwa wakipata vipigo kutoka kwa Mgambo wa Halmashauri; Wafanyabiashara hao wanahitaji kujengewa na Serikali mazingira mazuri na rafiki. Wanahitaji mazingira ya kuwezesha kiuchumi, kwa kupewa mikopo na maeneo ya kuuzia bidhaa zao kuliko kutozwa kodi bila kuwajengea uwezo wa ki biashara; na hivyo kuifanya Serikali ionekane kwamba inajielekeza zaidi kupata fedha kutoka kwa wajasiriamali wadogo.

19. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, inaitaka serikali kuiga sera mbadala kwa kuwa na uchumi wa soko jamii ambao unazingatia maendeleo na ustawi wa jamii. Katika mfumo huu msingi mkubwa wa uchumi wa soko jamii itakuwa soko huria lililojikita katika ushirikishwaji na

mshikamano, ambapo jamii inatakiwa kusimama pamoja wakati wote na kushiriki katika masuala ya maendeleo. Katika muktadha huu mfumo wa kodi lazima usaidie keki ya Taifa kutumika kwa manufaa ya watu wote chini wakiwemo wajasiriamali hawa tunaowauzia vitambulisho hivi.

- **Utaratibu Holela wa kutoa Vitambulisho vya Ujasiriamali.**
- 20. **Mheshimiwa Spika**, Utoaji wa Vitambulisho ulikiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma (Public Procurement Act) Kwa mujibu wa Sheria ya Manunuzi ya Umma ya Na. 7 ya mwaka 2011 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2016 miradi yote ya Serikali hutekelezwa kupitia zabuni. Kwa sababu hiyo, utaratibu wa kutoa vitambulisho vya wajasiriamali ultakiwa kutangazwa kwa wazabuni ili washindanishwe na mzabuni aliyeshinda apatiwe zabuni hiyo ya kutengeneza vitambulisho hiyo.
- 21. **Mheshimiwa Spika**, hali haikuwa hivyo; vitambulisho vimetengenezwa, - hakuna zabuni iliyotangazwa, haijulikani ni kampuni gani ilifanya kazi hiyo na ilishindanishwa na kampuni zipo na ilishinda zabuni kwa thamani ya shilingi ngapi. Taarifa hizi ni muhimu kwa kuwa kukosekana kwake kunaashiria kunaifanya Serikali ionekane kutofuata taratibu za kisheria katika mchakato mzima na pia kunaashiria kukosekana kwa utawala bora.

 - **Kudhoofika kwa mapato ya Halmashauri nchini.**

- 22. **Mheshimiwa Spika**, Vitambulisho vya mjasiriamali ni nyenzo ya kudhoofisha Halmashauri zetu nchini. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaanmini kwamba zoezi hili lina lengo la kuua halmashauri zetu kwa kuzinyang'anya kila chanzo ambacho kilikuwa kinazisaidia kujidesha na kuziingizia mapato ya ndani. Kwa utaratibu huu sasa Halmashauri hizi hazitozi ushuru kutoka kwa wajasiriamali hawa kwenye masoko na minada mbalimbali. Aidha, minada na masoko ilikuwa ni sehemu ya kuziingizia mapato Halmashauri nyingi nchini na kwa kuwa wafanyabiashara katika minada hiyo ni

hawa wajasiriamali wadogo, wakishapata vitambulisho hivyo hawatalipa ushuru tena. Ikumbukwe kwamba masoko mengi katika Halmashauri ni vitega uchumi vilivyojengwa kwa mikopo kutoka taasisi za fedha kwa ajili ya kuzipatia Halmashauri mapato. Hivyo, kuzikosesha Halmashauri mapato ni kuzifanya zishindwe kujiedesha na kulipa madeni. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka serikali kuu kutafakari upya uamuzi wake wa kuzibana Halmashauri kimapato. Ibuni vyanzo vipyta vya mapato bila kuathiri serikali za Mitaa ili kuziwezesha kutimiza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi kwa ufanisi.

23. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kuangalia upya mpango huu wa vitambulisho vya wajasiriamali ili lifikie malengo yake ya kusaidia wajasiriamali wadogo bila kuathiri mapato ya halmashauri za ndani ya Tanzania.

c) WAKALA WA UJENZI WA BARABARA VIJIJINI-TARURA

24. Mheshimiwa Spika, TARURA ni wakala iliyoundwa kwa kupitia Tangazo la Serikali (Government Notice no. 211 ya Juni 2017, kwa madhumuni ya kuhudumia barabara zote zillizokuwa zinahudumiwa na Halmashauri za wilaya, miji, manispaa na majiji. Hivyo basi, mfumo mzima wa uanzishwaji wake ukiangalia kwa undani haukuwa wazi kiasi kwamba utaacha maswali mengi sana yasiyo na majibu juu ya utendaji wa Halmashauri zetu hapa nchini.

25. Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba ni Azimio la Buge lako tukufu lilopelekea kuanzishwa kwa TARURA lakini ujio wake umekuwa wa haraka na haukuwa shirikishi, kwa kiwango cha kuridhisha. Mpaka sasa kuna mkanganyiko mkubwa kati ya watendaji wa TARURA na Madiwani pamoja na watendaji wa halmashauri hapa nchini.

26. Mheshimiwa Spika, maeneo yenye utata zaidi ni:-

i. Kutoshirikishwa kwa Mabaraza ya Madiwani katika hatua yoyote ya mchakato wa utengenezaji wa barabara

ikiwemo vikao vya maamuzi mpaka usimamizi wa miradi ya barabara.

ii. Kutolazimika kuzingatiwa kwa Barabara za vipaumbele vya Mabaraza ya Madiwani ambao ndio wawakilishi wa wananchi.

iii. Kukosekana kwa Bodi ya TARURA kama ilivyo Bodi ya TANROADS

iv. Uwezo mdogo wa fedha za dharura kwa ajili ya kukabiliana na uharibifu wa mara kwa mara unaotokana na majanga kama mafuriko na mengine kama hayo. Hali hii imefanya madaraja, makalavati na barabara nyingi kwenye vijiji na mitaa kuwa katika hali mbaya ya uharibifu kutokana mvua zinazonyesha katika maeneo mengi hapa nchini.

v. Kiwango cha asilimia 30 kinacotengwa kutoka katika Mfuko wa Barabara hakiwiani na urefu wa barabara za mijini na vijijini ambazo TARURA wanapaswa kusimamia hivyo kufanya barabara nyingi ziendelee kuwa na hali mbaya zaidi ya uharibifu kuliko hata zilipokuwa zinasimamiwa na Halmashauri.

27. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri mambo yafuatayo ili kuboresha hiki cha TARURA:-

i. Lazima TARURA washirikishe halmashauri katika hatua mbalimbali za mchakato wa kutengeneza miundombinu ya barabara kwa vile Madiwani na Mkurugenzi ndio wanaofahamu barabara zenye kero.

ii. Iwepo Bodi ya TARURA ambayo itaundwa katika ngazi ya Halmashauri.

iii. Bajeti ya TARURA iongezwe kuwa asilimia 40 kutoka katika Mfuko wa Barabara badala ya asilimia 30 ya sasa ili kuifanya TARURA iwe na uwezo wa kutimiza wajibu wake kwa kiwango cha kuridhisha.

iv. TARURA ili ijiendeshe, Serikali isizinyang' anye Halmashauri vyanzo vyake vichache nya mapato vilivyobaki ambayo ndivo viñasadia kuendesha shughuli za kila siku za Halmashauri katika kutoa huduma kwa wananchi.

v. Lazima TARURA iwe suluhisho la kilio cha Wabunge cha muda mrefu cha kutaka barabara zao zipandishwe daraja ili zihudumiwe na TANROAD vinginevyo lengo kuu la kuanzishwa kwa TARURA litakuwa halijafikiwa.

vi. Lazima iwepo bajeti ya dharura ya kuhudumia barabara za vijiji na mitaa zinazoharibika kutokana na majanga mbalimbali ya asili kama vile mafuriko.

28. Mheshimiwa Spika, Kwa mujibu wa hotuba ya Waziri Mkuu ya 2017/2018 ni kwamba barabara zilizokuwa chini ya TARURA ni Kilomita 108, 946.2; mwaka 2018/ 2019 TARURA ilisimamia matengenezo ya Kilomita 4,183.3 tu. Hii maana yake ni kwamba ingeichukua TARURA muda wa miaka 26 kuweza kukamilisha ujenzi wa barabara zote zilizopo chini ya TARURA. Badala ya kuchukua mapendekezo Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kutokana na uchache wa barabara zilizokuwa zimetengenezwa, sasa serikali kupitia Bodi ya Mfuko wa Barabara inadai imeunda timu ya uhakiki wa mtandao wa barabara zilizochini ya TARURA na kwamba zoezi hilo bado halijakamilika, Bado Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatoa rai kwa serikali ya kuongeza fedha kwa mamlaka hii ili malengo yake yaweze kufikiwa.

d) MAANDALIZI YA CHAGUZI ZA SERIKALI ZA MITAA 2019
▪ Madai ya Tume Huru ya Uchaguzi

29. Mheshimiwa Spika, Serikali imetangaza kwamba Uchaguzi wa Serikali za Mitaa utafanyika mwezi Oktoba, mwaka huu wa 2019. Kama ilivyo ada, uchaguzi unatanguliwa na maandalizi mbalimbali yakiwemo maandalizi ya kanuni za uchaguzi huo, ambapo kwa mwaka huu, wadau wamekutana hapa Jijini Dodoma. Aidha uchaguzi huu unafuatia uchaguzi wa mwaka 2014, uchaguzi ambaa Serikali pia ilikutanisha wadau wanaohusika na

Uchaguzi wa Serikali za Mitaa vikiwemo Vyama vya Siasa Mjini Morogoro kwa ajili ya kupokea maoni yao kuhusu Kanuni za uchaguzi huo. Moja ya changamoto zilizoibuliwa wakati huo ilikuwa ni uchaguzi wa Madiwani kufanyika tofauti na uchaguzi wa Serikali za Mitaa na wakati huo huo Diwani ni Mwenyekiti wa Kamati ya Maendeleo ya Kata (WDC) ambapo Wajumbe wake ni Wenyevitii wa Vijiji au Mitaa katika Kata husika.

30. Mheshimiwa Spika, katika maandalizi hayo, hoja ya uchaguzi wa Serikali za Mitaa kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi kuanzia kwenye uandikishaji wa wapiga kura mpaka siku ya uchaguzi ilijitokeza. Serikali kupitia kwa Waziri wa TAMISEMI wakati huo Mheshimiwa Hawa Ghasia ilikubali na kuahidi kuwa Serikali ingewasilisha muswada Bungeni ili kufanya marekebisho ya utaratibu wa Uchaguzi wa Serikali za Mitaa ili kufanya uchaguzi wa Serikali za Mitaa kusimamiwa na Tume ya Uchaguzi na pia uchaguzi wa Madiwani kufanyika pamoja na Serikali Mitaa ifikapo mwaka 2019. Sasa mwaka 2019 umeshafika bila Serikali kuwasilisha msawaada wowote mbele ya Bunge hili kama ilivyoahidi, hali inayoashiria kwamba huenda Taifa hili litaingia kwenye uchaguzi pamoja na mapungufu na malalamiko ya muda mrefu ambayo Serikali imekuwa ikiahidi kuyafanya kazi bila mafanikio kutoka uchaguzi mmoja hadi uchaguzi mwingine.

31. Mheshimiwa Spika, Pamoja na mapungufu ya kimfumo na kisheria yaliyopo kwenye Tume ya Uchaguzi ya sasa, ni vema Serikali ikaona umuhimu wa kutekeleza ahadi yake ilioitoa kwa Vyama vya Siasa Mjini Morogoro mwaka 2014 ili kuzifanya kazi changamoto za Uchaguzi wa Serikali za Mitaa unaotarajia kufanyika mwakani.

32. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inafahamu kuwa kimfumo uchaguzi wa nchi hii unasimamiwa na TAMISEMI kwa sababu Tume inawatumia Wakurugenzi wa Halmashauri kusimamia uchaguzi, na ikumbukwe kuwa tulishaeleza kuwa Wakurugenzi wengi wa Halmashauri walioeteuliwa na Rais ni makada wa Chama cha Mapinduzi ambao walishindwa ama kwenye kura za maoni ndani ya

chama chao au walioshindwa kwenye Uchaguzi Mkuu wa mwaka 2015.

33. Mheshimiwa Spika, Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ibara ya 74 (14) inakataza maofisa wanaohusika na uchaguzi kujihusisha na Siasa, licha ya katazo hilo tumeshuhudia Wakurugenzi wengine wakishiriki vikao vya CCM na kupokea maelekezo mbalimbali bila kificho. Wakurugenzi hao wa Halmashauri, kwa kuwa ni makada wa CCM; wanapokuwa wasimamizi wa uchaguzi, ama kwa utashi wao au kwa kulazimishwa wanatangaza mgombea wa CCM ambaye hajashinda uchaguzi na kumnyima haki yule aliyeshinda kwa vile tu ni wa chama cha upinzani.

34. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inahoji ni lini Serikali italeta muswada hapa Bungeni kwa ajili ya kupitia upya mfumo wa uchaguzi nchini illi kuepusha madhara yanayoweza kutokea kutokana na mapungufu yaliyopo kwenye uchaguzi ukizingatia kwamba uchaguzi ni zoezi muhimu kwa ajili ya demokrasia na utawala bora.

35. Mheshimiwa Spika, Hitaji la Tume Huru ya Uchaguzi ni hitaji na kilio cha muda mrefu cha Taifa tangu mfumo wa vyama vingi urejeshwe mwaka 1992 na hoja hii imeletwa bungeni kila mwaka kwa njia mbalimbali. Tume huru ya Uchaguzi ni msingi wa haki, amani, demokrasia na maendeleo endelevu. Ni bahati mbaya sana, bado serikali ya CCM imeendelea kupuuza jambo hili na kuendelea kuwa na tume ambayo muundo na weledi wake unapalilia na kutengeneza bomu litakalovuruga sana nchi yetu siku si nydingi hatua za makusudi zisipochukuliwa.

36. Mheshimiwa Spika, ukiachilia mbali utawala wa sheria, kujali na kutetea haki za binadamu ambayo ni mionganoni mwa misingi mikuu ya demokrasia, sifa nydingine kuu ya demokrasia duniani ni chaguzi huru na za haki. Chaguzi huru na za haki ndizo zinazodhahirisha mamlaka ya wananchi katika kuamua namna wanavyotaka utawala wa nchi yao uwe. Kwa maneno mengine, chaguzi huru na za haki ndizo kitambulisho halisi cha demokrasia ya kweli.

- 37.** **Mheshimiwa Spika**, mamlaka yoyote inayopatikana kwa njia nyingine yoyote bila kupitia chaguzi huru na za haki; mamlaka hiyo haiwezi kuwa ya kidemokrasia. Kwa vyovoyote vile, mamlaka hiyo itakuwa ni ya ki-imla (udikiteta) yenye kujali na kusimamia maslahi ya wachache na sio maslahi ya wananchi au maslahi ya taifa.
- 38.** **Mheshimiwa Spika**, ili chaguzi ziweze kufikia malengo yaliyokusudiwa – ya kuweka uongozi au mamlaka halali inayokubalika na wananchi walio wengi, ni lazima chaguzi hizo ziratibiwe na chombo kinachoaminika na pande zote zinazoshiriki katika chaguzi hizo; chombo ambacho ni huru kisichoegemea upande wowote ili kujenga muafaka wa kitaifa na mustakabali mwema wa nchi. Chombo hicho si kingine bali ni Tume Huru ya Uchaguzi.
- 39.** **Mheshimiwa Spika**; kuhusu uchaguzi wa Serikali za Mitaa: - Yalikuwa ni madai ya siku nyingi ya vyama vyatia upinzani kwamba uchaguzi huo usisimamiwe na Ofisi ya Rais – TAMISEMI na badala yake usisimamiwe na Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Na sababu ya kutaka iwe hivyo, ni kutokana na kwamba Ofisi ya Rais – TAMISEMI ina maslahi katika uchaguzi huo na kwa maana hiyo haitatenda haki kwa wadau wengine wa uchaguzi.
- 40.** **Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais – TAMISEMI iko chini ya Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Taifa wa Chama cha Mapinduzi. Mfumo mzima wa uchaguzi ndani ya CCM uko chini yake moja kwa moja. Wakurugenzi wote wa Halmashauri nchini – ambao ni waratibu na wasimamizi wa chaguzi hizo ni wateuliwa wa Rais na bila shaka ni wana-CCM kwa kuwa haitegemewi Rais kuteua timu inayompinga kufanya nayo kazi. Aidha; upo ushahidi wa wazi kuwa wakurugenzi wa halmashauri ni makada wa CCM walioshindwa katika kura za maoni na kupewa zawadi ya ukurugenzi; na wana maelekezo ya Rais kuwa wasiwatangaze wagombea wa upinzani hata kama wameshinda katika chaguzi. Rais alinukuliwa akisema “Mkurugenzi atakayemptangaza Mpinzani wakati amepewa nyenzo zote za utendaji atakuwa hana kazi” Kwa sura hiyo;

Ofisi yake haiwezi kuendesha kwa haki uchaguzi wa Serikali za Mitaa ambao unajumuisha vyama vingi. Na hii sababu yake ni rahisi – yeye ni refa na ni mchezaji kwa wakati huohuo; hivyo hawezi kutenda haki katika mchezo.

41. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani bado inatafakari mantiki ya kushiriki uchaguzi kama mfumo uliopo sasa hautarekebishwa; Aidha Mh. Rais anapaswa kushauriwa na wasaidizi wake kufuta kauli yake kwamba Mkurugenzi atakayemtangaza Mpinzani atafutwa kazi. Kwa uzito wa mamlaka ya Mhe Rais kauli hii ikiachwa ilivyo inaweza kutumiwa vibaya na wakurugenzi jambo ambalo linaweza likasababisha fujo. Vinginevyo itakuwa ni fujo na matokeo yake ni machafuko ya kisiasa. Hivyo, ni Rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni Kwa Serikali kushughulikia jambo hili mapema ili kuepuka uvunjifu wa amani unaoweza kutokea.

e) POSHO ZA WENYEVITI WA SERIKALI ZA MITAA

42. Mheshimiwa Spika, katika bajeti zilizopita Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imekuwa ikishauri Serikali kuzielekeza halmashauri zipandishe viwango vya posho za wenyeviti wa Serikali za mitaa, vijiji na vitongoji kufika shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa mwezi pamoja na kuanzisha posho ya mkono wa kwaheri wa shiling laki tano pale wanapomaliza muda wao. Hii inatokana na ukweli kwamba kundi hii la uwakilishi linafanya kazi kubwa ya kuwashudumia wananchi katika ngazi za chini kabisa. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani ilishauri kuanzishwa kwa posho ya shilingi elfu 30 kwa wajumbe wa vijiji, vitongoji na mitaa ili kuwapa ari ya kutetekeza majukumu yao ambayo ni magumu sana ya kuwashudumia wananchi wa kada ya chini kabisa.

43. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasikitishwa na majibu ambayo yametolewa hapa bungeni na Naibu Waziri TAMISEMI kwa kudhani kwamba, viongozi wa serikali za mitaa wakiwa na kazi nyingine za kuingizia kipato basi hawastahili kulipwa posho, tunapenda kusisitiza na kuishauri Serikali hii kwamba wenyeviti wa mitaa ni viongozi wa kuchaguliwa kama walivyo wabunge na madiwani ambao wanapata posho hivyo, stahiki za Posho kwa

wenyeviti wa Serikali za Mitaa ni stahiki zao kwa kazi wanazofanya bila kujali shughuli zao binafsi za kuwaingizia kipato. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaendelea kusisitiza umuhimu na ulazima wa kupandisha posho hizo na kwamba lazima viwango vya Posho vilingane kwa Halmashauri zote. Aidha serikali iache kuchukua vyanzo vya mapato ya Halmashauri ili kuziwezesha halmashauri hizo kuwa na mapato mengi na ziweze kutekeleza wajibu wa kulipa posho kwa wenyeviti wa serikali za Mitaa.

f) FEDHA ZA MRADI YA MAENDELEO KUTOFIKA KWA WAKATI KATIKA HALIMASHAURI

44. Mheshimiwa Spika, Katika kujiletea maendeleo raslimali fedha toka Serikali kuu ni muhimu sana lakini kuna tatizo la Serikali kushindwa kupeleka fedha zinazopitishwa na Bunge kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwenda kwenye Halmashauri zetu kwa ukamilifu wake na kwa wakati. Hata pale zinapopelekwa kwa ukamilifu kuna tatizo kwamba zinakwenda kwa vipande vipande kiasi kwamba utekelezwaji wa miradi unashindikana, kutokana na mazingira halisi yanayokuwepo kwa wakati huo.

45. Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ni kupeleka fedha za miradi katika robo ya mwisho ya mwaka, jambo linalopelekea kushindwa kutumika kwa fedha hizo kutokana na utaratibu mzima wa kufuata sheria ya manunuzi ambayo inahitaji kutimizwa kwa masharti. Hivyo kupelekeea fedha hizo kurudishwa Serikali kuu.

g) KUCHELEWESHWA KWA MIONGOZOYA BAJETI NA UKOMO WA BAJETI

46. Mheshimiwa Spika, Kumekuwepo kwa kuchelewa sana kutolewa kwa miongozo ya bajeti na ukomo wa bajeti(**Budget guidelines and ceilings**) kwenda ngazi za halmashauri pamoja na Serikali za Vijiji na hivyo kupelekeea hizo guidelines zinapowafikia tayari wanakuwa wameshakaa na kumaliza mchakato wa mipango yao na vipaumbele vya kupanga miradi katika maeneo yao. Sambamba na hilo, kuna tatizo la kutorejesha taarifa za mabadiliko ya

vipaumbele vya taifa na vile vya wananchi katika ngazi za chini. Hili ni tatizo kubwa sana ambalo linaenda sambamba na wananchi kuona kuwa wamepokwa haki yao za msingi ya kupanga na kutekeleza miradi yao kulingana na mahitaji yao.

47. Mheshimiwa Spika, hapa jambo kubwa na haraka linalohitajika ni kuimarisha mifumo yetu ya uwajibikaji, na jambo hili haliwezi kuwa ni suala la watawala tu bila watawaliwa kushirikishwa. Kambi Rasmi ya Upinzani inamini kwamba Katiba mpya ndio suluhisho la utengenezaji wa mifumo mipyä ya uwajibikaji ambayo haitachezewa kwa matakwa ya yule atakayepewa ridhaa ya kuisimamia.

h) UTARATIBU WA BAJETI YA SERIKALI

48. Mheshimiwa Spika, utaratibu wa bajeti ya serikali unakumbwa na changamoto kadhaa ambazo huathiri utekelezaji wa bajeti hiyo hata baada ya kuitishwa na Bunge. Inatambulika kuwa maandalizi ya Bajeti ya mwaka wa fedha unaofuata huanza mapema baada tu ya kuanza mwaka wa fedha mpya. Aidha, inafahamika kuwa bajeti hutakiwa kuanzia kwenye ngazi za Vijiji na Mitaa kwa mfumo wa kuibua fursa na changamoto katika maendeleo (O and OD) na baadaye kwenda Halmashauri na ngazi ya Mkao. Hata hivyo uzoefu unaonesha kuwa mambo yamekuwa yakipangwa kuanzia ngazi ya Halmashauri pekee na sio shirikishi kama inavyotakiwa. Hata utofauti wa takwimu kwenye vitabu vya bajeti ambao Kambi Rasmi ya Upinzani ilionesha kwa miili mfululizo huenda unasababishwa na utaratibu wa Halmashauri kujipikia takwimu na miradi bila kushirikisha ngazi za chini katika mipango.

49. Mheshimiwa Spika, bajeti ya serikali kwa namna moja ama nyiningine imekua ikiathiriwa na maelekezo ya mara kwa mara yanayotolewa na viongozi wa kisiasa wa Serikali. Mathalani kama Halmashauri ilipanga kukusanya kodi kuitia kwenye masoko au mazao inaathiriwa na agizo linalotolewa katikati ya mwaka wa fedha kuwa vyanzo hivyo visiendelee kutozwa kodi. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuacha kutoa maelekezo ambayo yanaathiri bajeti za

Halmashauri na wakati huo huo ni Serikali hiyo hiyo iliyokubali mipango ya Halmashauri hizo kabla ya kupitishwa na Baraza la Madiwani.

i) MATAMKO BILA MKAKATI WA UTEKELEZAJI

50. **Mheshimiwa Spika**, wananchi wamepokea tamko la Waziri wa TAMISEMI kuwa kila mkoa ujenge viwanda 100. Hiki ni kitu kikubwa kinachotakiwa kiwe na Sera itakayoonesha wadau watashiriki vipi katika ujenzi huo wa viwanda 100 na sera hiyo itengenezewe Mkakati wake na chini yake Bunge litunge sheria yake pamoja na Kanuni kwa kueleza wazi katika mkoa viwanda vya aina gani vya kimkakati vijengwe na ushiriki wa kila Halmashauri, Kata na Kijiji na namna ya kupata Raslimali za viwanda hivyo 100.

51. **Mheshimiwa Spika**, sambamba na hilo ni kuwa viwanda hivyo 100 vitatumia teknolojia gani na soko la bidhaa zake litakuwa ni wapi ukizingatia kwamba kuna ushindani mkubwa sana wa soko kikanda na kimataifa na Soko la ndani halitawenza kubeba bidhaa za viwanda hivyo iwapo kweli vitajengwa kama Mheshimiwa Waziri alivyoagiza.

52. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kwamba dhana hii ya ujenzi wa viwanda lazima iwe shirikishi na usiwe mtazamo wa mtu mmoja ikiwemo kushirikisha wataalamu waliobobea katika sekta hiyo. Aidha, lazima dhana hii langalie miaka zaidi ya 50 ijayo, hivyo ni muhimu sana kujenga taasisi imara itakayosimamia mpango huu ili uwe endelevu na usije ukashindwa kama ulivyoshindwa miaka ya nyuma.

j) SERIKALI IMESHINDWA KUSIMAMIA ELIMU MSINGI

53. **Mheshimiwa Spika**, ni wazi kwamba baada ya Serikali kutamka kwamba elimu msingi itatolewa bila malipo ya ada; kumekuwa na ongezeko kubwa la udahili wa wanafunzi kwa shule za msingi na Sekondari ambazo ziko chini ya uratibu wa Ofisi ya Rais- TAMISEMI. Pamoja na neema hii kwa wananchi; jambo hili limekumbwa na changamoto kubwa ya uhaba wa walimu, miundombinu, vifaa vya kufundishia na zaidi sana bajeti ndogo ya maendeleo katika kutatua

changamoto hizo ili kuweza kuhudumia idadi kubwa ya wanafunzi mashuleni.

i. **Upungufu wa Kutisha wa Walimu katika Shule za Msingi na Sekondari**

54. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kwa zaidi ya miaka kumi iliyopita imekuwa ikiikumbusha Serikali hii ya CCM kwamba; hakuna elimu bila walimu. Sarakasi na mbwembwe zote za kisiasa za elimu bure; elimu bila malipo na sasa elimu bila ada hazitasaidia chochote kama hakuna idadi ya kutosha ya walimu wenyewe weledi na motisha wa kufanya kazi ya kufundisha.

55. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa takwimu za BEST za mwaka 2016 na 2017; idadi ya walimu kwa shule za msingi imeshuka kutoka walimu 191,772 mwaka 2016 hadi kufikia 179,291 mwaka 2017 ikiwa ni anguko la asilimia 6.5 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuwa 1:50. Aidha, katika shule za awali, idadi iliyopungua ni walimu 1948 na kufanya uwiano wa mwalimu na wanafunzi kuongezeka kutoka 1:135 mwaka 2016 hadi kufikia 1:159 mwaka 2017 badala ya 1:25 ambao ni uwiano unaokubalika.

56. **Mheshimiwa Spika**, katika shule za Sekondari kuna uhaba mkubwa wa walimu kwa baadhi ya masomo kama ifuatavyo:

- i. Hisabati – kuna upungufu wa walimu 7,291
- ii. Baiolojia – kuna upungufu wa walimu 5,181
- iii. Kemia – kuna upungufu wa walimu 5,373
- iv. Fizikia – kuna upungufu wa walimu 6,873 (Hii ni kwa mujibu wa takwimu za BEST, 2016)

57. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa takwimu za Elimu Msingi za Mikoa (BEST Regional Data, 2017); walimu 7,743 wanatarajiwa kustaafu kati ya mwaka 2018 na 2019. Aidha, takriban walimu zaidi ya 30,000 wana umri wa zaidi ya miaka 51 ya kuzaliwa; hivyo na wao wanatarajiwa kustaafu muda mfupi ujao.

- 58. Mheshimiwa Spika;** kwa kuzingatia ukweli kwamba bila walimu hakuna elimu; Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kutoa majibu Ni kitu gani kimesababisha upungufu mkubwa wa walimu ukizingatia kwamba kuna idadi kubwa ya wahitimu wa fani ya ualimu katika vyuo mbalimbali vya ualimu vilivyopo nchini?
- 59. Mheshimiwa Spika,** hivi karibuni Serikali imetangaza ajira 4000 za walimu. Waliojitokeza kuomba nafasi hizo ni zaidi ya watu 90,000. Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kulieleza Bunge hili; ni kwanini Serikali haikutoa nafasi nydingi zaidi za ajira kwa walimu ili kukabiliana na upungufu huu wa walimu wa kutisha? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kujiwekea mpango mkakati wa kuajiri angala walimu 15,000 kila mwaka kwa muda wa miaka mitano ili kupunguza kwa kiwango kikubwa upungufu wa walimu mashulenii.
- ii. **Uhaba Mkubwa wa Miundombinu katika Shule za Msingi na Sekondari Nchini**
- 60. Mheshimiwa Spika;** mazingira bora ya kufundisha na kujifunza yanategemea sana uwepo wa miundombinu rafiki na wezeshi. Ni jambo ambalo haliwezekani kutegemea kupanda kwa ubora wa elimu ikiwa hakuna jitihada zozote za kuboresha miundombinu itakayosaidia zoezi la kufundisha na kujifunza kufanikiwa.
- 61. Mheshimiwa Spika,** kuna uhaba mkubwa sana wa miundombinu katika shule za msingi na sekondari za umma, jambo linalopelekea mazingira magumu ya kufundisha na kujifunza na hivyo kushusha viwango vya ubora wa Elimu. Kwa mujibu wa takwimu za BEST, 2016 na 2017; ni kwamba uhaba wa maktaba katika shule za msingi umeongezeka kutoka asilimia 88 mwaka 2016 hadi kufikia asilimia 91.1 mwaka 2017.
- 62. Mheshimiwa Spika,** takwimu hizo zinaonyesha pia kwamba; upungufu wa maabara katika shule za sekondari unatofautiana kulingana na masomo husika. Kwa mfano

upungufu wa maabara za somo la Bailojia ni asilimia 51.5, Fizikia ni asilimia 54.3 na Kemia ni asilimia 43.3

63. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha pia kwamba kuna upungufu wa nyumba za walimu 186,008 sawa na asilimia 83.1 na upungufu wa majengo ya utawala 10,943 sawa na asilimia 83.4. Aidha, uwiano uliopo sasa wa matundu ya vyoo na wanafunzi wa kike ni 1:53 wakati uwiano unaoshauriwa ni 1:20 na kwa wavulana uwiano uliopo ni 1:56 na unaoshauriwa ni 1:25. Hivyo kufanya upungufu wa mashimo ya vyoo kwa wasichana kuwa 62% na kwa wavulana kuwa 56%. Ripoti ya Benki ya Dunia ya mwaka 2016 inaonyesha kwamba; ni asilimia 41 tu ya shule za msingi na sekondari nchini Tanzania zenyenye miundombinu inayokidhi viwango vinavyotakiwa.

64. Mheshimiwa Spika, takwimu nilizozitaja hapo juu zinatiliwa nguvu na Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ya mwaka wa fedha 2016/17 inayoonyesha kwamba shule za msingi zina upungufu wa madarasa kwa asilimia 85; upungufu wa vyoo asilimia 66; na upungufu wa nyumba za walimu asilimia 14. Kwa upande wa sekondari kuna upungufu wa vyumba vya madarasa asilimia 52, upungufu wa maabara asilimia 84; upungufu wa madawati asilimia 86; upungufu wa nyumba za walimu asilimia 85; upungufu wa mabweni asilimia 88 na upungufu wa matundu ya vyoo asilimia 53

65. Mheshimiwa Spika, wakati nchi washirika wa Jumuiya ya Afrika Mashariki wako kwenye mpango wa kuwapatia wanafunzi wote wa shule za msingi Kompyuta Mpakato (Laptops) sisi Tanzania bado tunazungumzia uhaba wa matundu ya vyoo. Ni aibu sana kwa Serikali hii inayojitapa kwamba inatoa elimu bure wakati mazingira ya kutolea elimu hiyo ni mabaya na yanachangia kwa kiwango kikubwa kushuka kwa ubora wa elimu.

66. Mheshimiwa Spika, Serikali inafahamu upungufu huu kwa kuwa takwimu zilizotumika ni za Serikali. Swali ni je; kwanini upungufu huu umekuwa ukiongezeka? Kambi Rasmi ya

Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kulieleza Bunge; imepunguza tatizo la uhaba wa miundombinu mashulenii kwa kiwango gani hadi sasa? Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kueleza imetenga bajeti kiasi gani katika mwaka wa fedha 2019/20 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu mashulenii ili kukabiliana na uhaba ulipo sasa?

iii. **Kupungua Kwa Bajeti ya Sekta ya Elimu**

67. Mheshimiwa Spika, pamoja na Serikali hii ya awamu ya tano kuuaminisha umma kwamba elimu ni kipaumbele chake; kwa kutangaza kwamba itatoa elimu msingi bila malipo ya ada; azma hiyo hionekani katika upangaji wa bajeti ya elimu. Pamoja na ukweli kwamba tangu Serikali hii iingie madarakani, bajeti kuu ya Serikali imekuwa ikiongezeka; lakini ongezeko hilo limekuwa halina manufaa yoyote katika Sekta ya Elimu kwa kuwa bajeti ya elimu imekuwa ikipungua kila mwaka kwa miaka yote mitatu ya utawala wa Serikali hii ya awamu ya tano. Kwa mfano wakati Bajeti kuu ya Serikali iliongezeka kutoka shilingi trilioni 29.5 mwaka 2016/17 hadi trilioni 31.7 mwaka 2017/18 na kufikia shilingi trilioni 32.4 mwaka 2018/19; bajeti ya sekta ya elimu imekuwa ikishuka kutoka shilingi trilioni 4.770 hadi shilingi trilioni 4.706 mpaka shilingi trilioni 4.628 kwa mtiririko huohuo.

68. Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Sekta ya Elimu iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2018/19 ya takribani shilingi trilioni 4.628 ni pungufu kwa asilimia 1.7 ukilinganisha na bajeti ya elimu ya shilingi trilioni 4.706 iliyoidhinishwa mwaka wa fedha 2017/18. Upungufu wa asilimia 1.7 unaweza kuonekana mdogo lakini asilimia hiyo ni sawa na shilingi bilioni 78 zilizopungua kwenye bajeti hiyo. Fedha hizo zingeweza kujenga mabweni zaidi ya 500 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 40 kila moja na madarasa 1000 yenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 45 kila moja. Hii ina maana kwamba, kama ingetakiwa kutumia fedha kuboresha mazingira ya kujifunza kwa mtoto wa kike, zaidi ya watoto wa kike 12,500 ambaao hutembea umbali mrefu kwenda na kurudi kutoka shuleni wangepata malazi katika mabweni hayo.

69. Mheshimiwa Spika, licha ya bajeti ya elimu kuwa na mwelekeo wa kupungua; utekelezaji wa bajeti ya maendeleo katika sekta hii una hali mbaya zaidi. Hii ni kwa sababu zaidi ya asilimia 90 ya bajeti ya elimu inayopelekwa TAMISEMI ni ya matumizi ya kawaida na asilimia kidogo tu ndiyo hutekeliza miradi ya maendeleo. Kwa mfano, katika mwaka wa fedha 2016/17 bajeti ya matumizi ya kawaida iliyopelekwa TAMISEMI kwenye sekta ya Elimu ilikuwa ni asilimia 93 huku bajeti ya maendeleo ikiwa ni asilimia 7 tu. Aidha, mwaka uliofuata wa 2017/18 bajeti ya matumizi ya kawaida ilikuwa ni asilimia 93.4 huku ya maendeleo ikishuka hadi asilimia 6.6. Kwa hiyo, kwa wastani, kwa miaka miwili ya kwanza ya Serikali hii ya awamu ya tano, Serikali imekuwa ikitenga wastani wa asilimia 6.5 ya jumla ya bajeti ya sekta ya elimu katika Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo; na zaidi ya asilimia 94 kwa matumizi ya kawaida.

70. Mheshimiwa Spika, utengaji huo hafifu wa bajeti ya maendeleo hauwezi hata kidogo kutatua changamoto kubwa za upungufu wa vyumba vya madarasa, matundu ya vyoo, uhaba wa walimu, maabara, na nyenzo nyingine za kufundishia kama nilivyoainisha hapo kabla. Ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzini kwa Serikali kuongeza bajeti ya maendeleo ya elimu msingi chini ya TAMISEMI angalau ifikie asilimia 30 ya bajeti inayotengwa kwa ajili ya elimu msingi.

71. Mheshimiwa Spika, tatizo jingine kuhusu bajeti ya sekta nzima ya elimu, ni bajeti hiyo kutolewa kwa wizara zaidi ya moja jambo ambalo linaweka mazingira magumu ya ufuatiliaji wa utekelezaji wake. Bajeti hiyo hutolewa kwa Wizara ya Elimu, Ofisi ya Rais – TAMISEMI na sehemu kidogo Wizara ya Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto. Tofauti na mchanganuo wa fedha bajeti ya elimu inayopelekwa Wizara ya Elimu, kwa maana ya matumizi ya kawaida na ya maendeleo; fedha ya elimu inayopelekwa TAMISEMI haionyeshi mchanganuo wa ni kiasi gani (kwa maana ya fedha taslimu - tarakimu halisi)kinachokwenda kwenye miradi halisi ya maendeleo. Kambi rasmi ya Upinzani Bungeni inaitaka Serikali kuonyesha katika randama mchanganuo wa matumizi ya fedha za kawaida na za

maendeleo za sekta ya elimu inayosimamia na Ofisi ya Rais – TAMISEMI.

k) MIGOGORO KATIKA HALMASHAURI MBALIMBALI NCHINI

72. Mheshimiwa Spika, naomba ieleweke kuwa, kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, ibara ya 145 na 146, imeunda Serikali za Mitaa na kutamka bayana kuwa Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi ambavyo vipo katika ngazi za chini za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vyombo hivi huundwa, huendeshwa, husimamiwa na kuwajibika kwa wananchi wenyewe.

73. Mheshimiwa Spika, Aidha, Sheria Na. 8 ya mwaka 1982 inazungumzia uundaji wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika maeneo ya mijini, ambazo ni Halmashauri za Miji, Manispaa na Majiji. Tunatambua kuwa Halmashauri zote Tanzania zimeundwa kwa mujibu wa sheria hii.

74. Mheshimiwa Spika, napenda kutoa taarifa katika Bunge lako tukufu kuwa kumekuwa na migogoro ndani ya Halimashauri mbalimbali ambayo vyanzo vyake ni maagizo yanayotolewa na au Wakuu wa Wilaya na au Wakuu wa Mikoa, maagizo hayo kwa kiasi kikubwa huwa hayazingatia Sheria za uendeshaji wa Halmashauri.

75. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inashindwa kuelewa malengo ya wateule hawa wa Mheshimiwa Rais dhidi ya mamlaka za Serikali za Mitaa, maelekezo yao ya hovyo na kuingilia utendaji wa Halmashauri yamesababisha migongano mingi bila sababu za msingi kwa kupenda kutaka umaarufu wa muda kwa kuvunja sheria na taratibu za Taifa hili.

76. Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inatambua kwamba yapo maelekezo ambayo yamekuwa yakitolewa na Waziri mwenye dhamana mara anapopata taarifa za vitendo hivyo, lakini mara nyingine wakuu wa wilaya

huwa hawatekelezi maelekezo hayo kwa sababu zinazofahamika kwao tu.

I) UHUSIANO WA TAMISEMI NA SEKTA ZINGINE ZA UZALISHAJI

77. Mheshimiwa Spika, unaposema TAMISEMI maana yake ni taasisi ambayo inahusika moja kwa moja kuinua hali ya maisha kwa watanzania wote hususani waishio vijiji ambaao ni zaidi ya asilimia 85. Aidha, asilimia 75 ya idadi hiyo ni nguvukazi inajishughulisha na sekta ya kilimo.

78. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonyesha kwamba; Sekta ya kilimo ambayo inahusisha, mazao, mifugo na uvuvi ilikuwa ilikua kwa asilimia 2.3 mwaka 2015, na asilimia 2.1 mwaka 2016. Ni dhahiri kuwa ukuaji huu wa asilima 2.1 hauwezi kuwa na matokeo chanya katika kuondoa umasikini kwa watanzania wanaotegemea sekta hii.

79. Mheshimiwa Spika, kwa takwimu hizo za Ofisi ya Taifa ya Takwamu ni kujaribu kuonyesha tu umuhimu wa sekta hiyo kwa maisha ya watanzania na Tanzania kwa ujumla. Sasa kama sekta hiyo ingepata umuhimu wa kutosha kama vile, Sera ya kilimo ya mwaka 1997 kabla ya kuhuishwa mwaka 2013 kwamba huduma za ugani (EXTENSION SERVICE) kwa sekta ya kilimo ni jukumu la Halmashauri zetu (TAMISEMI), ni wazi kuwa kilimo kingeweza kukua kwa zaidi ya asilimia 4 na mchango wake katika mauzo nje ya nchi yangeongezeka maradufu na mchango wake katika pato la Taifa ungeongezeka na hivyo kuwa kwenye mwelekeo sahihi wa kuondoa umasikini wa kipato kwa watanzania.

80. Mheshimiwa Spika, sekta ndogo ya uvuvi ambayo kwa mujibu wa taarifa ya wizara ya uvuvi⁸ inaonesha kuwa Tanzania ina wavuvi wapatao 183,800, na watu wapatao 4,000,000 wanategemea kuendesha maisha yao kutokana na sekta hii. Sambamba na hilo ni kuwa Tanzania inaukanda wa bahari upatao kilometa 1,424 kwa mikoa ya (Tanga, Pwani, Dar, Lindi na Tanga), kwa takwimu za mwaka 2015 ni kuwa samaki wanaovuliwa ni tani 51,912 sawa na 14%

na maziwa yote kwa pamoja yenye ukubwa wa kilometa za mraba 64,500 (Kagera, Mwanza, Geita, Simiyu, Mara, Kigoma, Sumbawanga, Ruvuma, Mbeya na Njombe), samaki wanaovuliwa ni tani 314,062 sawa na 85%. Wahuksika wakuu wa samaki hizi na wavuvi wadogo wadogo lakini hatuwaheshimu na kuwalea ili wawe ni wavuvi wakubwa, hii ni aibu kubwa sana kwa walio na dhamana kwa kuhakikisha nchi inakuwa ya uchumi wa kati

81. Mheshimiwa Spika, maeneo yote hayo, Halmashauri husika zinapata mapato yake ya ndani kwa kutegemea shughuli zinazofanywa kutokana na uvuvi, lakini wavuvi hasa wadodgo wanapata madhila makubwa sana ambayo yanawafanya badala ya kuondoa umasikini yanawaongezea umasikini na hivyo mapato ya halmashauri yanapotea kutokana na kukosa taasisi imara za kusimamia sekta hii.

82. Mheshimiwa Spika, operation ilioendeshwa na bado inaendelea katika Ziwa Viktoria ya kukamata wavuvi ambao wanatumia nyavu ambazo kikosi kazi cha Operation hiyo kinahisi sio mwafaka imeleta kilio kikubwa sana kwa wavuvi na kuwaletea umasikini wa ghafla.

83. Mheshimiwa Spika, sheria inasema nyavu zitakazotumika kuvulia ziwani ni lazima ziwe na matundu yenye inchi 6 na kuendelea, lakini katika Ziwa Viktoria kuna samaki wadogo chini ya inchi 6. Mfano; Furu, Gogogo(ngore) na Ningi. Hawa ni samaki maarufu sana katika Ziwa Viktoria. Kambi Rasmi ya Upinzani inauliza hawa wanavuliwa na Nyavu za inchi ngapi?

84. Mheshimiwa Spika, kutokuwepo au kupatikana kwa nyavu zinazokubalika kisheria kwa ajili ya uvuaji wa dagaa imekuwa ni usumbufu mkubwa sana na hivyo kutoa mwanya kwa watendaji kudai rushwa na kuwabambikizia kesi wavuvi. Mfano dhahiri ni walioendesha Operation katika visiwa vya Irugwa-Ukerewe kudai fedha nyingi kuliko thamani halisi ya mali walizonazo wavuvi na wakishindwa wanakamatwa na kufunguliwa kesi za uvuvi haramu.

85. **Mheshimiwa Spika**, ukweli ni kuwa zaidi ya 60% ya wavuvi wa dagaa wameshindwa kuendelea na shughuli zao kwa sababu nyavyu zilizopo hazina ubora wa kuweza kuhimili kazi za kila siku. Jambo hilo linazidi kupunguza mapato kwa halmashauri zetu.
86. **Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa wavuvi wa Ukanda wa Pwani, nao wanapata madhila makubwa sana kutokana na makatazo ambayo hayaangalii hali halisi ya ukuaji wa sekta hii na hivyo kuongeza mapato kwa halmashauri zilizo katika ukanda wa Bahari. Wavuvi wengi wadogo wanatumia uvuvi wa Mtanda "ring net" na ni lazima uzame ukiwa na mtungi wa gesi ya Oxygen.
87. **Mheshimiwa Spika**, kwa bahati mbaya watendaji wasiofahamu uvuvi unafanyikaje wanashindwa hata kukaa na wahusika ili wajifunze, matokeo yake ni kuwafanya wavuvi kuwa masikini kwa kuteketeza mitungi na kupora engine za boat na wavuvi kukamatwa. Kwa upande wa Nyavyu wanasema nyavyu zenye ukubwa wa mm 38 au Inchi 2 ndizo zinazotakiwa. Sasa dagaa watavuliwa na nyavyu zenye matundu ya ukubwa huo?
88. **Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa takwimu za mapato kama yalivyotolewa na "**kundi la Fungamano la vyama na vikundi vya sekta ya uvuvi**" katika soko la samaki Magogoni/Ferry na maeneo mengine, ni kwamba Wastani wa mapato yanayochangiwa na wadau wa sekta ya uvuvi kwa Taifa kwa soko la samaki Magogoni/Feri kwa mwaka mmoja ni Tshs. 8,663,294,000/- hizi ni stahiki za Serikali peke yake bado mzunguko wa biashara kwa wananchi. Aidha, vyombo vikubwa vinavyotumika katika mwambao wa Dar na Pwani ni vikubwa 3000 na vidogo 650, lakini wamiliki wanashindwa kufanyakazi kutokana na mazingira magumu wanayowekewa na Watendaji na hivyo kupelekea Halmashauri zetu na Serikali kukosa stahiki za mapato kwa maendeleo ya nchi.
89. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaitaka Serikali kuiangalia vizuri sekta hii ya uvuvi hasa wavuvi

wadogo, wasinyanyaswe ili wawewe kuzalisha zaidi na mapato kwa Serikali hususani halimashauri yaweze kuongezeka.

m) MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO 2018/19 NA MAOMBI YA UTEKELEZAJI YA FEDHA KWA MWAKA 2019/20

90. **Mheshumiwa Spika**, kwa mujibu wa Randama, Ofisi ya Rais - TAMISEMI imegawanyika katika maeneo yafutayo; OR-Tamisemi na Taasisi zake (Chuo cha Serikali za Mitaa (LGTI)-Hombolo, Shirika la Elimu Kibaha-(KEC), Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka (DART), Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa(LGB). 2. OR-Tamisemi Makao Makuu, 3. Tume ya Utumishi wa Waalimu, 4. Fungu 26 kwa Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

91. **Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa randama ya Mpango na Bajeti Fungu 56, illyotolewa Machi, 2019, Ofisi ya Rais-TAMISEMI na Taasisi zake, shirika la Elimu Kibaha, Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, Chuo cha Serikali za Mitaa Hombolo, Wakala wa Usafiri wa Haraka Dar Es Salaam na program mbalimbali Kwa mwaka wa fedha 2018/19 iliiidhinishiwa kiasi cha shilingi **387,981,784,000.00**, kati ya hizo shilingi **345,113,541,000.00** zilikuwa ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Aidha, kati ya fedha zilizoidhinishwa kwa ajili ya miradi ya maendeleo, fedha za ndani zilikuwa shilingi **283,642,430,000.00** na fedha za nje shilingi **61,471,111,000.00**. Takwimu za randama zinaonesha kwamba, hadi kufikia February, 2019 fedha za nje zilizokuwa zimepokelewa zilikuwa ni **3,183,360,076.00** sawa na 5.2% ya fedha zote za kutoka nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

92. **Mheshimiwa Spika**, wakati hali iko hivyo kwa mwaka wa fedha 2018/2019, Randama, inaonesha katika uk 73, wizara hii kwa mwaka huu wa fedha 2019/2020 inaomba kuidhinishiwa jumla ya shilingi **498,921,060,910.00**, kati ya fedha hizo shilingi **463,563,123,910.00** ni kwa ajili ya maendeleo. Aidha fedha za ndani ni shilingi 253,738,400,000.00 na fedha za nje ni 209,824,723,910.00. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kujua mambo yafuatayo

- i. Sababu za kupanda makadirio ya fedha za kugharamia miradi ya maendeleo kutokana na wafadhili wa nje kutoka shilingi **61,471,111,000.00** kwa mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia shilingi **209,824,723,910.00** mwaka huu sawa na ongezeko la Shilingi **148,353,612,910.00**?
- ii. Ni kwanini katika mwaka wa fedha 2018/2019 hadi kufikia mwezi February 2019, fedha za kugharamia miradi ya maendeleo kutoka nje zilikuwa zimepatikana shilingi **3,183,360,076.00** kati ya shilingi **61,471,111,000.00** sawa 5.2%?
- iii. Ni sababu zipy zilizowafanya wafadhili wa miradi ya maendeleo kuchelewesha fedha kwa ajili ya miradi ya maendeleo na je, sababu hizo zimetatuliwa namna gani?

93. **Mheshimiwa Spika**, takwimu hizi zinatuonesha kuwa kasi ya wafadhili wa miradi ya maendeleo kutoka nje inatia shaka, Pamoja na ukweli huo, bado Serikali imeweka miradi 16 ambayo ni chachu ya kuboresha elimu na afya kuendelea kutegemea wahisani ambaeo Serikali hii imekuwa inawaita mabeberu. Kitendo hiki ni kuiweka rehani Elimu ya Taifa hili na Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka kupata maelezo ni kwa nini miaka zaidi ya hamsini baada ya uhuru wa Taifa hili, bado tunagemea hisani ya wafadhiri kujenga matundu ya vyoo kwa shule za watoto wetu?

94. **Mheshimiwa spika**, Ukitosoma Randama ya Mpango na Bajeti, Fungu 56, Aya ya 3.4 uk.73 OR-TAMISEMI inaomba kuidhinishiwa shilingi **463,563,123,910.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo kati ya fedha hizo, Shilingi 253,738,400,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 209,824,723,910.00 ni fedha za nje. Ukitosoma kwenye sura ya tatu ya Randama, Aya 3.7 Mpango na Bajeti ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020 wizara inasema inaomba kuidhinishiwa **345,113,541,000.00** kwa ajili ya miradi ya maendeleo. Kati ya fedha hizo shilingi 283,642,430,000.00 ni fedha za ndani na shilingi 61,471,111,000.00 ni fedha za nje.

95. **Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inataka Wizara kutoa ufanuzi wa shilingi **118,449,582,910.00**

ambazo henzieleweki eleweki kutokana na mkanganyiko unaopatikana kwenye maeleo ya Wizara kupitia Randama yake. Fedha hizi zinapatikana baada ya kuchua shilingi **463,563,123,910.00** zinazotajwa kwenye Randama uk 73 na Shilingi **345,113,541,000.00** zinazotajwa kwenye Randama uk 130 fedha ambazo zote zinatarajiwa kugharamia miradi ya maendeleo kwa Wizara hii lakini zote zikiwa ni kugharamia miradi ya maendeleo kwa kipindi cha mwaka 2019/2020. Pili, kiasi cha fedha kutoka kwa wafadhiri nje ni kipi kati ya shilingi **61,471,111,000.00** zinazotajwa uk 130 wa Randama sawa na kiasi kilichokuwa kimetengwa mwaka wa fedha 2018/2019 au ni shilingi 209,824,723,910.00 zinazotajwa katika Randama Uk 73?

Tatu, hata kama kiasi tarajiwa kutoka kwa wafadhili ni kile kilichotajwa kwenye Randama Uk 73 shilingi 209,824,723,910.00 badala ya shilingi 61,471,111,000.00 zinazotajwa kwenye Randama uk 130 Aya 3.7, Je, ni kwa nini mwaka huu wa fedha 2019/2020 kiwango kipande kwa shilingi 148,353,612,910.00 zaidi?

Nne, ikiwa mwaka 2018/2019 fedha za nje zilikuwa 61,471,111,000.00 na fedha zilizopatikana ni 5.2% mwaka 2019/2020 ambapo serikali imekadiria shilingi 209,824,723,910.00 inatarajia kiwango kipande kutokana na mikakati ipi iliyowekwa na serikali ya kuwashawishi wahisani?

n) HITIMISHO

96. **Mheshimiwa Spika**, Nahitimisha hotuba yangu kwa kusema mambo makubwa mawili, Jambo la kwanza, narudia tena umuhimu wa kujenga taasisi imara kwa maendeleo endelevu. Taasisi zetu za kiserikali zingekuwa imara hii migogoro na vurumai katika halmashauri zinazosababishwa na Wakuu wa Wilaya na Mikoa wasio na karama za uongozi zisingetokea. Naikumbusha tena Serikali kutoa mwongozo na mipaka ya kazi kwa Wakuu wa Wilaya na Mikoa kama Bunge liliivoazimia katika Mikutano iliyopita.

97. **Mheshimiwa Spika**, jambo la pili la kuzingatia ni vyanzo vyaa mapato ya ndani ya halmashauri zetu. Ili taasisi

ziwe imara kama tunavyotamani ziwe ni lazima ziweze kuwa na vyanzo vyatunayi kutosha vyatunayi mapatao ili ziweze kuijendesha. Uhuru na mamlaka za Serikali za Mitaa hauwezi kuwa timilifu:-

- i. Ikiwa Serikali Kuu itaendelea kuchukua vyanzo vyatunayi mapatao vyatunayi halmashauri'
- ii. Ikiwa Serikali Kuu haitatimiza wajibu wake wa kuzipelekea Halmashauri fedha za uendeshaji (OC na maendeleo) kwa wakati na kama zilivyoidhinishwa na Bunge;
- iii. Ikiwa hakuna utawala bora unaozingatia Katiba na Sheria zinazongoza halmashauri zetu
- iv. Ikiwa kodi za halmashauri zinazokusanywa na Serikali kuu kupitia TRA hazitarejeshwa kwenye Halmashauri husika kama sheria zinavyoolekeza.

98. Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba kuwasilisha.

Japhary Raphael Michael (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI
KATIKA OFISI YA RAIS – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA
MITAA (TAMISEMII)**

10 Aprili, 2019

MWONGOZO WA SPIKA

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, mwongozo.

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE,
KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kuniona.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba mwongozo wako, nilikuwa napitia Sheria ya Utekelezaji wa Shughuli na Kazi za Rais, Sheria Na.15 ya mwaka 1984, Sheria Na.9 ya mwaka 1992 na Sheria Na.34 ya mwaka 1994. Pia nilikuwa napitia Sheria Na.15 ya mwaka 1984 na Sheria Na.3 na Na.6 ya mwaka 2000 inayohusu kuanzisha mamlaka na uteuzi wa watendaji ambapo sheria hizi zinaenda na Ibara ya 37(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ambayo imesema wazi kabisa kwamba mbali na kuzingatia masharti yaliyopo katika Katiba hii na sheria za Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika utendaji wa kazi na shughuli zake Rais atakuwa huru.

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile Katiba Ibara 36(1), bila masharti mengineyo yaliyomo katika Katiba hii na sheria nyinginezo, Rais atakuwa na mamlaka ya kuanzisha na kufuta nafasi za madaraka ya namna mbalimbali katika utumishi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Ibara ya 36(2) Rais anayo madaraka ya kuteua watu na kushika nafasi za madaraka ya viongozi wanaowajibika chini yake, sitaki kumalizia.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini nilikuwa naangalia Kanuni zetu zinazotuongoza, ukienda Kanuni ya 64(1)(e) inatukataza pia Waheshimiwa Wabunge kuzungumzia mwenendo wa Rais wetu. Mwenendo ambao Rais anaruhusiwa kuzungumzwa ndani ya Bunge ni lazima uwe umeletwa kwa hoja mahsusni na umewekwa ndani ya Bunge kuhusu jambo hilo mahsusni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nilikuwa napitia hotuba ya Kiongozi wa Kambi ya Upinzani ukurasa wa 3, kuna maeneo mawili ambayo nitayaombea mwongozo wako. Eneo la kwanza, katika ukurasa wa 3, paragrafu ya juu, Mheshimiwa Rais, Mkuu wa Nchi, anatuhumiwa kwamba anaendesha Serikali za Mitaa kwa matakwa na maono yake na siyo kwa matakwa ya wananchi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *paragraph* nyingine inayofuata...

MWENYEKITI: Hebu Mheshimiwa *Chief Whip*rudia tena ni ukurasa gani?

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyeekiti, ni ukurasa wa 3, *paragraph* ile juu kabisa, nadhani tunakwenda pamoja.

MWENYEKITI: *Okay.*

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyeekiti, pia *paragraph* ya 7, kwa kadri ya kitabu nilichonacho inasema, pamoja na mamlaka ya kikatiba aliyonayo Rais ya kuteua Wakurugenzi wa Halmshauri, mamlaka hayo yanatumiaka vibaya. Hizo ni tuhuma nzito kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na ni tuhuma ambazo zinapingana na sheria hizi nilizosizoma na madaraka aliyopewa Mheshimiwa Rais kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Muungano wa Tanzania. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyeekiti, kunapotokea jambo hili ambalo ni la Kikatiba na Kikanuni na Kisheria kwa mujibu wa sheria nilizosizoma, kwa nini *paragraph* hizi zisiondolewe na zisiwe kumbukumbu...

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyeekiti, kumbumbuku za shughuli hizi za Bunge ama vinginevyo hatua nyingine zichukuliwe za kutaka uthibitishwaji wa maneno yaliyojionyesha katika hotuba hii. (*Makofi*)

MHE. JOHN W. HECHE: Tutakuletea.

WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU: Mheshimiwa Mwenyeekiti, uthibitishwaji wa tuhuma hizi ambazo

Mheshimiwa Rais anapewa kupitia hotuba Rasmi ya Kambi ya Upinzani. Naomba Mwongozo wako. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Japhary kwanza umesoma vizuri taarifa yako, *flow* yako ilikuwa nzuri, lakini nakuomba maneno ya paragraph ya 6 na 7 uyafute. Mheshimiwa Mnyika kaa chini, nazungumza na Mheshimiwa Japhary.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, utuongoze vizuri.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mnyika, nakuongoza vizuri, kwanza kaa chini.

MHE. JOHN J. MNYIKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, halafu utanipa nafasi na mlimi.

MWENYEKITI: Kaa chini Mheshimiwa Mnyika. Mheshimiwa Japhary *paragraph* ya 6 na 7 zifute tu basi.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kitabu hii kimepita kwa Spika akapunguza vile ambavyo...

MWENYEKITI: Kwani wewe hujawahi kuona penati inarudiwa? (*Kicheko*)

WABUNGE FULANI: Aaaaa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Japhary, wewe ni mtu mzima futa haya maneno.

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMADI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maelekezo yako pia kiondoke hiki.

MWENYEKITI: *Paragraph 6 na 7.*

MHE. RAPHAEL J. MICHAEL – MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo kiondoke hamna shida. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Ahsante.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, sasa tutulie penati zinakosewa na zinarudiwa, mipira mingine mpaka leo hajatua. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaanza uchangiaji na Mheshimiwa Msigwa, Mheshimiwa Lubeleje na Mheshimiwa Bonnah Kamoli.

MHE. MICH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana kwa kunipa nafasi lakini nalidhani Serikali ingekuwa inavumilia ikatujibu kwenye hoja, sisi ndivyo tunavyoona, hayo ni maoni ya Kambi ya Upinzani. Naona mnaogopa kivuli chenu wenyewe huku mnasema mmejipanga na tupo tayari kutoa ushahidi. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Msigwa, jambo likishafanyiwa maamuzi usilete ushabiki ambao hauna maana. (*Makofii*)

MHE. MICH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Toka Serikali ya Awamu ya Tano imeeingia madarakani imefanya maamuzi makubwa matatu na maamuzi madogo madogo mengi ambayo kwa ujumla wake siyo chini ya 10. Serikali ya Awamu ya Tano ilifanya maamuzi ya Kikokotoo, korosho, Muswada wa Habari, Muswada wa Takwimu, kutokufanya kazi na CAG, Muswada wa Vyama Siasa, *Stiegler's Gorge*, SGR, ununuzi wa ndege na kuhamia Dodoma. *Is a major decision* toka Serikali ya Awamu Tano imeedingia madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja ya sifa za viongozi duniani ni pamoja na kufanya maamuzi (*decision making*), sina tatizo na hilo lakini tunapaswa tujue kama Taifa kwamba *consequences are more important than decisions*. Matokeo ya maamuzi tunayoyafanya ni ya muhimu zaidi kuliko maamuzi tunayoyafanya. *We don't live by decisions we live by consequences*, hatuishi kwa maamuzi tunayoyafanya dakika moja tunaishi kwa matokeo ya maamuzi tunayoyafanya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kabla ya kufanya maamuzi watu wenye busara, wenye hekima wanaoongoza lazima wajifunze *consequences*. *You have to study the consequences before you make decisions*. Unafanya *research*, unatafuta *information*, unatafuata *historical data*, unatafuta watu wengine wamefanya maamuzi gani katika mambo unayokwenda kuyafanya na unajifunza kwa watu wengine katika maamuzi unayokwenda kuyafanya. nimezungumza tumefanya maamuzi makubwa sana kama Serikali na Serikali tunazungumzia masuala ya utawala bora na Serikali za Mtaa, haya mambo yote lazima yawe *synchronized* ili tupate matokeo yaliyo bora. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tukienda kwenye Kikokotoo, Mheshimiwa Jenista anahuksika. Mlikuha hapa na nyimbo nyingi sana kuhusu Kikokoto na kwa mujibu wa taratibu ili sheria ije Bungeni inapitia hatua mbalimbali. Inaanza kwenye Wizara husika, inakuja kwenye Cabinet Secretariat, inakuaja kwenye MMC, Makatibu, inaenda kwenye Baraza la Mawaziri, inaenda kwa wadau inakuja Bungeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa baada ya kufanya maamuzi ya Kikokotoo tukapitisha kwa nyimbo nyingi sana hapa na tuliwaambia humu ndani, baada ya miezi mitatu mkaweka *U-turn*. Swali la kuijiliza, *are we capable to lead this country?* Kama kupitia hatua zote hizi mmefanya haya mambo yote ndani ya miezi kadhaa Kikokotoo kikageuka, mkarudi na ngonjera zingine za kukipinga Kikokotoo ninyi wenyewe hapo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais, ameteua wengine hapa Maprofesa, Madaktari, *degree holders* wanaoweza ku-scrutinize vitu, kuona kama vina hoja; *think tank* ya lkulu, nasi Wabunge tunaowawakilisha wananchi hapa, tukaimba ngonjera nyingi bila kuangalia *consequences*. Tunaitumbukiza nchi kwenye matatizo. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama hiyo haitoshi, liliuja suala la Korosho hapa, tunasema tunataka tuwe na maendeleo, mkaondoka mpaka na azimio la kusifu maamuzi ya Korosho. Baada ya muda mfupi, leo tunaambiwa kangomba hawana makosa. Tuliitwa Kangomba sisi huku. *You guys did you study the consequences of the decision you are making? (Makof!)*

MHE. JOHN W. HECHE: Mnaita mhindi anunue kilo ngapi...

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi ambao mnasema mko *fit* kuiongoza nchi hii, *did you study the consequences?* Kama hiyo haitoshi, Muswada wa habari, nilitegemea maswali; kama nilivyo sema inapitia maeneo yote hayo; Muswada wa Habari, mnataka kuniambia Mawaziri walikuwa hawajui kwamba unakinzana na Jumuiya ya Afrika Mashariki? Mmekuja hapa mmelazimisha, mnataka kusema mlikuwa hamjui, kama unakinzana na Jumuiya ya Afrika Mashariki! (*Makof!*)

MHE. JOHN W. HECHE: Na mli-*ratify* wenyewe.

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ninyi wenyewe Baraza zima la Mawaziri, mlileta hapa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama haitoshi, mkaleta takwimu, tukapitisha na azimio la kusema hatufanyi kazi na CAG. Leo vitabu vyake viko hapa na sahihi iko hapa. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, swali langu kwenu, ninyi mnapofanya maamuzi, huwa mnajifunza *consequences?* Do

you do research? Maprofesa mko hapa, huwa mnafanya *research* ili mfanye hayo maamuzi. Leo tumefanya maamuzi makubwa. Nia na dhamira nzuri ya *Stiegler's Gorge* na *Standard Gauge* ni mambo mazuri ya kuhamia Dodoma na kununua ndege, vyote ni vitu vizuri. Ila *consequences* zinazotokea sasa hivi kwa maamuzi hayo makubwa ambayo tulikuwa hatuna *priorities*, ndiyo maana tunaona hamwezi kuajiri wafanyakazi wapya. *Those are the consequences* na hamkuliandaa Taifa kwamba hatutaajiri wafanyakazi wengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hakuna *increment* kwa wafanyakazi, mishahara haiongezeki, hakuna motisha. Halafu haya mambo makubwa mnategemea *staffwataleta positive result* katika mambo haya ambayo hamkufanya *study?* Asimame mtu hapa atuambie *what are the consequences* na *tuta-suffer* kipindi hiki bila kuajiri wafanyakazi wapya *for how long?* Leo mnasimama hapa mnasema, ukisikiliza hotuba za Mheshimiwa Rais, ni *contrary* kabisa na ninyi Mawaziri mnavyofanya kazi hapa, zote! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama kuna Wizara moja tu ambayo mimi naiona Mheshimiwa Rais hazungumzi ni Wizara ya Ulinzi. *The rest*, kwenye mikutano yake huko, Wizara karibu zote, tulizungumza na Mheshimiwa Mpango, hayupo hapa leo; tulimwambia utaratibu wa kodi unaofanya haufai, leo Mheshimiwa Rais anasema yale yale tuliyosema. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tulizungumza mambo ya msingi mengi hapa hamkutusikiliza. Leo mnasema wawekezaji. Tuliwaambia mnafukiza wawekezaji, leo Mheshimiwa Rais ndiye analalamika kwamba wawekezaji wanakimbia. *Why do you expect wawekezaji waje* katika nchi ambayo hakuna *democracy*, hakuna *good governance*, hakuna kuelewana! Mnataka kupuuza kwamba sisi wote hatuna *social capital* katika nchi hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mnataka kupuuza Kiongozi wa Kambi ya Upinzani kwamba hana *social capital* katika nchi hii? Hatuna wafuasi katika nchi hii? Nani atakuwa na

confidence ya kuleta mitaji hapa nchini aweze kuwekeza kwenye nchi hii ambapo hakuna uhuru wa mawazo, hatuwezi kuji-express? Nani ataleta mitaji katika nchi ili mambo yaende vizuri mahali ambapo Wakurugenzi, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, kila mtu anaenda njia yake? Mheshimiwa Rais anatoa maagizo haya, Mkurugenzi anatoa haya, Waziri anasema haya. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hatuwezi kuleta mabadiliko na tabia za kama Manaibu Waziri akina Mheshimiwa Waitara hapa, ambao kila saa anadhani tuko kwenye Mikutano ya Siasa. Changamoto tulizonazo zinahitaji *big brain*. Tanzania tuna matatizo makubwa kutoka hapa tulipo. Hatupo kwenye Mikutano ya Kisiasa hapa ndani. Uliondoka CHADEMA, *is over. Do the job, mwonyeshe Mheshimiwa Rais kwamba you are capable. Show your talent! Show your ability.* (Kicheko/ Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hapa mambo ya kusema nilikuwa CHADEMA, mipasho, haitusaidii. Mheshimiwa Rais amewapa hiyo kazi, hebu tuonyesheni uwezo wa kututoa hapa tulipo. Nchi hii haina mashimo ya vyoo sasa hivi, mnasema huko, vyanzo vyote kwenye hotuba yetu tumezungumza, vimehamishwa vyote vimekuja Serikali Kuu, lakini hela hiyo hairudi kwa wananchi.

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Reverend Msigwa. (Makofi)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Nimemaliza! (Makofi)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Lubeleje, halafu wajiaandae Mheshimiwa Bonnah Kamoli na Mheshimiwa Njalu Silanga.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hoja hizi mbili; TAMISEMI pamoja na Utumishi na Utawala Bora.

Kwanza kabisa nawapongeza Waheshimiwa Mawaziri wote wawili, Waziri wa TAMISEMI, Waziri wa Utumishi, Manaibu Mawaziri, Wakuu wa Vitengo na Makatibu Wakuu kwa kazi nzuri wanayofanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze na suala la Mapato ya Serikali za Mitaa. Mapato ya Serikali za Mitaa ndiyo uhai wa Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato haya yanasaidia sana kulipa Watendaji wa Vijiji...

MWENYEKITI: Utulivu ndani ya Bunge tafadhali. Kuna *Senate* anatoa mchango wake.

MHE. GEORGE M. LUBELEJE: Mheshimiwa Mwenyekiti, mapato haya yanasaidia sana kulipa Watendaji wa Vijiji wale ambao wameajiriwa na Serikali za Mitaa, mapato haya vilevile yanasaidia kulipa posho za Madiwani, Wenyeviti wa Vijiji pamoja na Wenyeviti wa Vitongoji na Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni kweli Halmashauri zetu zilikuwa na vyanzo vingi vya mapato, lakini bahati mbaya sana vyanzo vingi vimechukuliwa na Serikali. Vyanzo hivi ndiyo vingesaidia sana kuongeza mapato katika Halmashauri zetu. Kwa mfano, hivi karibuni *TRA* wamechukua kodi ya majengo. Mimi sipingi, lakini ule utaratibu kwamba wakusanye mwaka mzima, miezi 12, halafu ndipo wazigawie Halmashauri. Hili kwa kweli mimi sikubaliani nalo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu Halmashauri zina miradi na miradi ile inaendelea mwaka mzima. Sasa fedha ikae *TRA* mwaka mzima halafu baadaye ndiyo Halmashauri ziweze kupata hizo fedha. Kwa hiyo, nilikuwa namshauri Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, hili mngeliangalia upya angalau miezi sita Halmashauri ziweze kupata mgao wa fedha zao.

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la pili, ni kuhusu barabara. Naipongeza sana *TARURA*, inafanya kazi nzuri sana,

Iakini changamoto kubwa ya *TARURA* ni fedha. Tumeishauri Serikali kwamba hii asilimia 30 haitoshi, kwa hiyo, waongezwe angalau ifike asilimia 40. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara za Vijijini ni muhimu sana kwa ajili ya kusafirisha mazao na kusafirisha abiria. Kwa hiyo, naishauri sana *TAMISEMI* ijitahidi sana kuongeza fedha kwa ajili ya Wakala wa Barabara Vijijini na Mjini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Waziri amefika Mpwapwa na kuona barabara ya kutoka Gulwe, Berege, Chitemo, Mima, Chazima mpaka Igoji moja mpaka Seluka. Amepita hii barabara; barabara hii mbaya sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti ya mwaka 2018 ambayo inaendelea sasa, tulitengewa shilingi millioni 148. Barabara ile inahitaji zaidi ya shilingi bilioni moja ili iweze kutengenezwa kwa kiwango cha matengenezo makubwa. Sasa naomba sana mwongeze fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara ile pamoja na barabara ya kutoka Mima kwenda Mkanana. Vilevile Mkanana Mheshimiwa Waziri, pamoja na kwamba mmesitisha kugawa maeneo ya Utawala, Iakini Mkanana iko milimani kilometra 35 kutoka milimani kuja Makao Makuu ya Kata ambayo ni Chitemo. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri wa *TAMISEMI* kwamba Mkanana nao wapate Kata yao. Nitashukuru sana kwa hilo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu mambo ya *TASAF* na *MKURABITA*. *TASAF* wanafanya kazi nzuri sana, imesambaa nchi nzima. Ombi langu Viongozi wa *TASAF* ni kwamba, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa, tumeshatoa mapendekezo kwamba lengo la *TASAF* Awamu ya Tatu ni kuboresha au kunufaisha kaya masikini, Iakini sasa kuna baadhi ya maeneo tumegundua fedha hizi zinakwenda kwa watu wenye uwezo. Tumeagiza chombo kinachohusika, wote ambao wameorodheshwa kwenye daftari waondolewe, kwa sababu wana uwezo, hawawezi wakapata fedha za *TASAF*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, fedha za *TASAFT* tunasaidiwa na Wafadhili na Wafadhili wakigundua kwamba kaya masikini hawapati, wanapata wananchi ambao wana uwezo, wanaweza kuleta maamuzi ambayo yatatuletea matatizo makubwa sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, MKURABITA ni kurasimisha mali, kwa mfano mashamba. Kuna Kijiji changu pale Jimbo la Mpwapwa kinaitwa Inzomvu MKURABITA walipima mashamba, baada ya kupima mashamba, hawakujenga ile Ofisi ya Masijala na ule mradi haujakamilika. Namwomba Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, afike kijiji kile, wanalamika sana, akajibu ye ye mwenyewe hoja. Mimi siwezi kukosa kura za pale kwa sababu mradi wa MKURABITA haujatekelezwa, hapana. Namwomba sana Mheshimiwa Waziri aende akawaambie ye ye mwenyewe kwamba kwa nini mradi ule umekwama? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lingine ni kuhusu upungufu wa watumishi. Kuna upungufu wa watumishi hasa kwenye Sekta ya Afya. Wilaya ya Mpwapwa ina upungufu wa watumishi katika Sekta ya Afya zaidi ya 450. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri, atusaidie tupate watumishi wa kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwisho ni Bodi ya Mikopo Serikali za Mitaa. Bodi ya Mikopo Serikali za Mitaa, ni chombo cha Serikali za Mitaa, ni chombo cha Halmashauri. Chombo hiki, wadau wakubwa ni Halmashauri na ndiyo wanakichangia hiki chombo. Kulikuwa na mpango wa kuanzisha Benki ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa. Sasa Mheshimiwa Waziri: Je, mpango huu umefika wapi? Kama mpango huu haupo, basi Halmashauri ziruhusiwe kukopa kama zamani ili kujenga masoko, barabara, stendi na mambo mengine.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono kwa asilimia mia moja. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Silanga, jiandae Mheshimiwa Kamoli.

MHE. NJALU D. SILANGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba ya Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Utawala Bora. Nianze kuwapongeza sana Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kazi kubwa na nzuri wanayoifanya wakiongozwa na Waziri na Katibu Mkuu, pamoja na Wataalam wote kwa ujumla.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa ushauri katika sehemu ya Watumishi wanaolipwa mapato ya ndani. Watumishi wanaolipwa mapato ya ndani wanafanya kazi kubwa katika Halmashauri zetu. Ni vyema wangechukuliwa nao sasa walipwe katika Mfuko wa Serikali Kuu ili waondokane na suala la kusubiria fedha za mapato ya ndani. Kazi kubwa wanafanya, ni vyema sasa nao hawa wakaingia katika utumishi kama wengine kwenye maeneo yetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa shukrani kubwa sana katika Wizara ya TAMISEMI. Kazi wanayoifanya ni kubwa sana. Ni mfano tosha katika kitabu hiki ukikiangalia kwenye jalada hili, Kituo cha Afya cha Magu na maeneo mengine na kwangu Ikindilo na sehemu nyingine, shilingi milioni 500 nakumbuka katika enzi zilizopita ilikuwa ni suala la kufanya upembuzi yakinifu, hela inaisha; lakini leo fedha hizi zinafanya kazi ya kuonekana. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepata shilingi bilioni 1.5 kwenye Halmashauri zetu 67. Ukizunguka katika maeneo hayo, utakuta zile shilingi bilioni 1.5 ujenzi unakaribia kwisha kwa majengo saba. Niseme tu ndugu zangu Waheshimiwa Wabunge, viongozi wetu kazi kubwa wanazozifanya, tuwatie moyo na tuwatie nguvu. Wanafanya kazi kubwa ya kunusuru maisha ya Watanzania, lakini nao hawalali kwa ajili ya kutufanyia kazi zetu nzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala la elimu. Serikali ya Awamu ya Tano, pamoja na mengi tunayoyazungumza, lakini kama ni kazi, viongozi wetu wanafanya kazi kubwa sana na nzuri sana. Ni suala la kufika mahali nasi kama viongozi, kama Wawakilishi wa wananchi, tuwatie moyo na pale kuliko na

upungufu tuwaongezee maarifa wafanye kazi yao vizuri sana.
(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hajawahi kutokea, nakumbuka mimi nikiwa kule kijijini, shilingi milioni 50, shilingi milioni 40 ilikuwa darasa moja na haliishi. Leo shilingi milioni 15, madarasa katika kitabu hiki utaona yapo mfano hapa katika Wilaya yangu ya Gangabilili, ni mfano wa kuigwa. Leo tukiingia katika Bunge hili tunaona kama kazi hazifanyiki.
(Makof)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Vituo vya Afya na Zahanati, nashukuru na ninaipongeza Wizara kwa kusajili Vituo vya Afya vinne Ikunguilipu, Mwamwita, Maderana na Ndoleji; na kwa ujumla naiomba Serikali pale itakapokamiliika watupatie Wauguzi katika Kada hii ili wananchi waweze kupata huduma katika maeneo husika. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika hotuba ya Waziri ya Mkuu kuna Wabunge walichangia, wanasema Idara ya Maji, hajafanya kazi. Mimi nataka nitoe ushuhuda katika Mkoa wetu wa Simiyu hususan katika Jimbo langu la Itilima. Tangu nchi iumbwe, Makao Makuu ya Lagangabilili tulikuwa hatuna maji. Leo Laganganilili, Nkoma, Kabale, Mwamungesha na Habia yamejengwa machujio ya kuweza kubeba takribani lita 200,000. Kusema ukweli Serikali hii inafanya kazi kubwa na lazima tuipongeze. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, Wilayani kwangu pale Itilima tulikuwa hatuna nyumba ya watumishi, jengo la utawala. Tulipata shilingi bilioni 1.5, leo jengo limekamiliika na watu wanaendelea kufanya kazi. Naipongeza sana Wizara imenitengea shilingi milioni 900 kwa ajili kumalizia vitu vingine vilivyopo mle. *(Makof)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile nampongeza Mheshimiwa Waziri kwa kunitengea shilingi milioni 500 kwa ajili ya kumalizia Hospitali ya Wilaya. Nami nimhakikishie mwezi wa Nane au wa Kumi njoo ufungue Hospitali ya Wilaya ianze

kuwatumikie wananchi wa Itilima. Haya ndiyo matunda tunayohitaji ya Serikali ya Awamu ya Tano. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naiomba *TARURA* ituongezee bajeti yake. Wilaya yangu ya Itilima ina mtandao wa barabara wa kilometra 562, fedha iliyotengwa ni kidogo, lakini vilevile yako maeneo korofsi ambayo hayawesi yakaendana na bajeti hii. Naomba Ofisi ya TAMISEMI pale ambapo wataalam wetu watakapoleta maandiko, basi watusaidie katika maeneo mawili muhimu sana. Tuna daraja la solo ambalo linaunganika na kwa Mheshimiwa Ndassa na daraja la Mwabuki. Tukiunganishiwa hayo, tutakuwa tumefanya kazi nzuri katika maeneo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niseme tu kwamba Wizara ya TAMISEMI imefaa. Zamani walikuwa wanasesma mzigo mzito mpe Mnyamwezi, kumbe na Wazaramo wanaweza. Mnachapa kazi vizuri na kazi inaonekana na mwenye macho haambiwi tazama. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Kamoli, jiandae Leah Komanya.

MHE. BONNAH M. KALUWA: Mheshimiwa Mwenyekiti Ahsante, kwanza naomba nichukue nafasi hii kuipongeza Wizara ya TAMISEMI, lakini pia kuwapongeza Mawaziri wote pamoja na Serikali nzima kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kuhakikisha kwamba wanalitoa Taifa letu kwenye uchumi wa chini na kulipeleka kwenye uchumi wa kati ifikapo 2025. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa *speed* ambayo inaonekana, sina mashaka kabisa, 2025 kama tutakuwepo, basi tutakuwa wote tunaona tumefika kwenye uchumi wa kati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, sana naomba nichangie mchango wangu kwenye upande wa *TARURA*. *TARURA* kama walivyosema wenzangu, inapewa asilimia 30, lakini *TARURA* ina kilometra 130,000 na *TANROAD* wana kilometra 30,000. Sasa *TARURA* wana kuwa hawawezi kufanya kazi zao vizuri kwa sababu bajeti ni ndogo sana.

Mheshimiaw Mwenyekiti, kwa sababu sheria hizi zilivyokuwa zinatungwa zamani, ilikuwa bado hawaajaunganisha zile barabara mkoa kwa mkoa, lakini kwa sasa hivi watu wa *TANROAD* wameshaunganisha barabara zao mkoa kwa mkoa na nyingine wameshaunganisha wilaya kwa wilaya. Kwa hiyo, naomba niishauri Serikali iweze kubadilisha sheria ili watu wa *TARURA* waweze kuongezewa fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kumekuwa kuna tatizo kubwa sana hasa sisi Wabunge tunapoenda kufanya mikutano yetu. Tunaenda kufanya mikutano yetu tunaahidi wananchi kwamba hapa sehemu hii itajengwa barabara na ndivyo tunavyokuwa tumeaambiwa na watu halmashauri pia na watu wa *TARURA* wanakuwa wamepanga bajeti yao, lakini ukiangalia sana unakuta kwamba *TARURA* wana matatizo ya bajeti. Dar es Salaam kuna matatizo makubwa ya barabara, ukiangalia barabara za Jimbo la Segerea tuna barabara moja ambayo iko Kata ya Kimanga, sasa hivi hiyo barabara inajengwa kwa miaka mine, lakini tatizo kubwa ni bajeti, *TARURA* haina pesa ya kumalizia ile barabara iweze kumalizika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia tuna barabara nyingi mfano kama Jimbo la Ukonga barabara ziko kwenye hali mbaya, barabara ya Pugu, barabara ya Majohé, Barabara ya Kitunda – Banana, barabara zote hizo zinasubiri *TARURA*, lakini *TARURA* hawana bajeti walipanga mwaka jana hizo barabara zitajengwa, lakini haziwezi kujengwa kwa sababu bajeti hakuna. Sasa nataka nishauri Serikali kwamba hii sheria ibadilishwe, *TARURA* waongezewe fedha ili waweze kupanga kuendana na mipango yao wanayoipanga, lakini kama tutaendelea hapa kwamba *TARURA* watakuwa wanapewa

asilimia 30, haiwezekani, itakuwa mipango yetu ya kusema kwamba tunajenga barabara Fulani, barabara hazitajengwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hali ni mbaya sana ukiangalia Kata ya Kipawa pale tuna *terminal one, two na three* tunategemea kufungua *airportya* kisasa *terminal three*, lakini *opposite* na hiyo *airport* barabara ni mbovu sana, sasa tunasema kwamba tunakaribisha wawekezaji, wanapokuja hapa inatakiwa pia miundombinu iwe mizuri. Sasa mwekezaji anatoka tu *airport* anakutana na barabara mbovu, kwa kweli hiyo inamkatisha tamaa. Niwaombe sana tuangalie hili suala la kuongeza fedha kwenye Mfuko wa *TARURA*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kingine ninachotaka kuongelea ni kuhusiana na ushirikiano wa hizi taasisi mfano *TARURA, DAWASA*, Wizara ya Maji pamoja na *TANESCO*, unakuta barabara imetengenezwa, *TARURA* wametengeneza barabara baada ya miezi miwili *DAWASA* wanakuja wanachimba wanapitisha miundombinu yao, mashimo yale yanakaa miezi hata sita hayajawahi kuzibwa. Sasa huu pia ni upotevu wa mapato ya Serikali kwa sababu baada ya kuchimba wanakuja wanaziba ni kutengeneza vitu mara mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kama inawezekana, kama kuna mradi ambao unafanyika sehemu Fulani, taasisi hizi za Serikali ziweze kuwasiliana ili wakae waone kwamba hapa tunapitisha mradi fulani, waweze kuweka miundombinu yao kwa pamoja, sio barabara imejengwa *TANESCO* wamekuja, *DAWASA* wamekuja *TANESCO* wanakuja ooh hapa tunapitisha nguzo, kwa hiyo inabidi tubomoe barabara. Naomba sana hilo jambo lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo nataka kuongelea ni kuhusiana na suala la elimu. Tumekuwa tuna tatizo kubwa sana, watoto wetu wanapoanza shule darasa la kwanza. Sasa kama sasa hivi mwaka jana wamemaliza wanafunzi 22,285, mwaka huu wameingia

wanafunzi 44,656, tunajua hawa wanafunzi wameingia na sasa hivi Serikali imeleta utaratibu kwamba wanafunzi wote wanakuwa kwenye *system*. Sasa Serikali inashindwajwe kujua kwamba mwaka 2020 mwezi wa Kwanza wataingia watoto fulani ili sasa tusije tukaanza yale mambo ya zima moto. Kwa hili kwa kweli nichukue nafasi hii kuwapongeza sana viongozi wa Dar es Salaam, Mkuu wangu wa Wilaya Sophia Mgema, Mkurugenzi wangu pia na Mkuu wa Mkoa wamekuwa wakifanya kazi kubwa kuhakikisha madarasa ya zimamoto yanajengwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa kwa sababu tusiwe tunafanya kazi kwa zimamoto tuna hesabu sasa hivi za watoto ambao wameanza shule ya awali, lakini pia tuna hesabu ya watoto ambao wanaanza darasa la kwanza, tunajua kwamba baada ya muda gani watoto watamaliza shule. Sasa kuepukana na haya matatizo ya kufanya kazi kwa zimamoto tuiombe sana TAMISEMI iweze kuandaa miundombinu na tukisema miundombinu hatusemi tu miundombinu ya madarasa tunahitaji tupate miundombinu ya vyoo, kama sasa hivi kuna watoto wengi wanakuwa kwenye shule moja tunahitaji tupate miundombinu ya vyoo lakini tupate miundombinu mingine ambayo itawawezesha wale watoto waweze kusoma vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niongelee kuhusiana na zahanati au vituo vyा afya. Kwanza nichukue nafasi kumshukuru sana Mheshimiwa Jafo kwa kuleta milioni 500 kwenye kituo chetu cha *Plan International* lakini nataka tu nikwambie Mheshimiwa Jimbo la Segerea lina wakazi milioni moja elfu kumi na sita, tuna kituo kimoja tu cha afya. Sasa kwa kuwa na kituo kimoja tu cha afya kwa jimbo zima kama lile na lenye wakazi kama wale bado tuna changamoto kubwa. Tunaomba tupate kituo kingine na tuna maeneo makubwa mfano kama zahanati ya Seregea ina eneo kubwa sana la kujenga kituo cha afya. Pia ukienda Kinyerezi pia kuna zahanati pia ina eneo kubwa la kujenga kituo cha afya na Tabata. Tungeomba tupate hivi vituo vyा vinne ambavyo vinaweza vikatusaidia katika Jimbo la Segerea kwa sababu

mambo mengine yote yanaweza yakaishia kwetu kwenye Jimbo la Segerea kabla hatujaenda Amana.

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Leah Komanya, jiandae Mheshimiwa Zainab Mndolwa.

MHE. LEAH J. KOMANYA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi nami niweze kutoa mchango katika hoja za Wizara hizi mbili. Kwanza nipende kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuweza kunipa kibali chake na kuniwezesha kusimama mbele kuweza kutoa mchango. Pia nipongeze kazi nzuri inayofanywa na Mawaziri wote wawili na wasaidizi wao kazi zao ni nzuri tunazona kwa vitendo, maneno wanayoyatao hapa katika Bunge ndivyo kazi inavyofanyika. (*Makofî*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nianze mchango wangu kwa kuongelea idadi kubwa ya Wakuu wa Idara wanaokaimu kwa muda mrefu bila kuthibitishwa katika nafasi hizi. Kumekuwa na idadi kubwa sana ambayo ikiongezeka siku hadi siku ya Wakuu wa Idara katika Halmashauri zetu wanaokaimu kwa kipindi kirefu bila kuthibitishwa. Nakubaliana na kwamba zoezi la uchunguzi ni muhimu sana ili kuweza kupata wakuu wa idara. Zoezi hili limekuwa likichukua muda mrefu sana. Ningependa kutoa ombi katika idara inayohusika kuwepo na muda maalum hata kama mtumishi ana mambo mengi anatakiwa kuchunguzwa kuwepo na muda maalum kwamba itachukua miezi mingapi kuchunguzwa kama hana matatizo mengi itachukua kipindi gani, kuwe na *time frame*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema hivyo kwa sababu gani Kamati ya LAAC tumetembelea halmashauri nyingi kwa mfano, Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba Wakuu wa Idara wanaokaimu sita, Bukombe sita, Mbogwe sita, Ngara wanne kwa kigezo kwamba wanasubiri kufanyiwa *vetting*. Hii inapunguza ufanisi kwa wakuu wa idara kwa sababu wanaona hawana uhakika na kesho yao. Mara nyingi imekuwa ikitokea anakaimu mpaka mwaka mzima mwisho wa siku analetwa mkuu wa idara mwingine kutoka sehemu

nyingine. Hii inavunja moyo sana kwa sababu upande wa Serikali bajeti ya mishahara ya wakuu wa idara ipo kwa kila halmashauri, kinachochelewesha ni suala la *vetting*, naomba kuwe na *timeframe*. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sambamba na hilo kuna upungufu mkubwa sana wa wahandisi wa majengo katika wilaya zetu kwa sababu wahandisi wengi wameenda TARURA. Kwa hiyo kazi za majengo zimekuwa zikifanywa na ma-local fundi bila kuwepo na ufuatilaji wa wahandisi wa halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia nishukuru na kupongeza kazi nzuri sana inayofanywa na mradi wa TASAF pamoja na MKURABITA. TASAFinafanya kazi nzuri sana na wananchi wetu wanapata fedha, wasio na uwezo na wengi imewasiadnia pla kuanza kujlongezea biashara ndogondogo. Naomba nishauri, fedha hizi zimekuwa zikiletwa halmashauri na kuingia katika kapu kuu la halmashauri, hivyo kupelekeea fedha nyingine kutumika kwa matumizi yasiyotarajiwaa na kuchelewesha utekelezaji wa shughuli za TASAF.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa lengo la Serikali la kudhibiti akaanti nyingi, lakini naomba kwa fedha hizi za wafadhili zingepewa *special account* kwa sababu mwisho wa siku utekelezaji wa miradi unachelewa na baadaye wanapata hoja za ukaguzi. Hofu yangu ni kuweza kuleta shida kwa wafadhili wetu. Katika Wizara hii hii kuna mradi pia wa MKURABITA, zote ziko chini ya Wizara ya Utumishi. Hata hivyo, MKURABITA wenyeewe wamekuwa wakisubiri tu fedha kutoka kapu kuu la Mfuko Mkuu wa Hazina wakati TASAF wanaandika maandiko na kuweza kupata ufadhili. Mwanzo MKURABITA walikuwa wanaandika maandiko na kupata ufadhili, sasa sielewi tatizo limekuwa lipo upande gani. Nashauri pia katika Wizara ya Utumishi katika OPRAS zao kiwe kigezo pia cha kuangalia kwa nini hawa wameshindwa kutafuta namna ya kujipatia fedha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu pia naomba nichangie vigezo vinavyotumika katika kupata

fedha za EP4R katika halmashauri zetu. Kigezo kikuu kimekuwa kikitumika ili halmashauri zipate fedha kwa ajili ya kujenga madarasa, maabara na shughuli zingine, ni Mwalimu kuhudumia darasa lenye wanafunzi 40 hadi 50. Kigezo hiki katika halmashauri zetu ni changamoto kubwa sana kwa kuwa Halmashauri zinatofautiana mazingira. Nashauri vigezo hivi vingekuwa categorized kwa halmashauri kwa mfano manispaa na majiji zikawa na vigezo vyake na halmashauri za wilaya zikawa na vigezo vyake. Bila kufanya hivyo fedha nyingi zitakwenda sana kwenye Halmashauri za Majiji na Manispaa kwa sababu wenyewe wanakidhi vigezo vya Mwalimu kuhudumia wanafunzi 40 hadi 55. Katika halmashauri za wilaya kigezo hiki ni kigumu. Ombi langu kwa Serikali ziwapelekee Walimu wa kutosha hizi halmashauri ama ziwhamishe kule walikojaa na kuletwa ambako kuna upungufu wa Walimu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hata kama halmashauri zitapewa zile asilimia 10 za msawazisho wa ikama fedha hii haitoshi kwa sababu, kwa mfano, Halmashauri ya Wilaya ya Meatu asilimia 10 inayolekwa inaweza ikafanya msawazisho kwa Walimu 10 ikawahamisha, lakini na hiyo siyo solution...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, kengele ya pili hiyo. Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Zainabu Mndolwa, ajiandae Mheshimiwa Sophia Mwakagenda.

MHE. ZAINAB A. MNDOLWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana kwa kunipa fursa hii ili niweze kuchangia katika wizara hizi mbili, Wizara ya TAMISEMI pamoja na Wizara ya Utawala Bora. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyeumba mbingu na ardhi pia kwa kunipa afya njema nami niweze kuchangia kwa siku hii ya leo

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitaanza kwenye elimu, elimu bila malipo ni suala zuri katika Serikali yetu, lakini wakati inaanizisha elimu bure bila malipo Serikali haikufanya utafiti

wa kina. Watu walihamasika sana kuwapeleka watoto wao kuijandikisha, lakini ukatokea upungufu wa madarasa, ofisi za Walimu, vyoo na maabara. Naishauri Serikali hususani mijini maeneo ni madogo ya shule zetu ijenge madarasa kwa *style* ya ghorofa ili iweze kuchukua idadi kubwa ya wanafunzi kuliko sasa wanafunzi wanaingia kwa *session*, wengine wanakuja asubuhi wengine jioni na inapelekea wale wanaokuja jioni hususan katika Jiji la Dar es Salaam kuchelewa kurudi majumbani na wakati mwingine mpaka nyakati za usiku unakuta watoto wako barabarani wanasubiri usafiri wa kurudi nyumbani. Naishauri Serikali sasa itenye fungu maalum ambalo litafika kwa wakati ili liweze kujenga madarasa ya kutosha, vyumba vyya Walimu, vyoo pamoja na maabara. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika barabara zetu hizi za mijini na vijijini Serikali imejitahidi sana hususani katika wilaya yangu ninayotoka ya Temeke imejenga barabara za kiwango cha lami, lakini bado kuna changamoto kubwa sana katika barabara za lami hizo hakuna alama za barabarani hususani katika maeneo yetu, hupeleka magari makubwa ambayo kwa mfano Dar es Salaam kuna barabara ya Mandela, kipindi cha jioni kunakuwa na foleni kubwa sana katika daraja la Mfugale kupelekea magari makubwa kupita katika barabara za mitaani ambazo hazina alama za kuonyesha ni tani gani ya kiasi gani cha gari inatakiwa kupita kwenye eneo hilo. Kwa hiyo nashauri Serikali iweze kuweka alama za barabarani kwenye barabara zetu ambazo zimejengwa kwa kiwango cha lami. Pia iongeze fungu kwa *TARURA* kama walivyosema wenzangu kwa sababu kila mtu anahitaji barabara ya lami, lakini kutokana na uchache wa fungu hilo ndio maana kuna maeneo mengi wanajenga barabara za changarawe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni kuhusu hospitali zetu za wilaya, vituo vyya afya na zahanati. Naishauri Serikali ipeleke vifaa tiba vyya kutosha katika hospitali hizo kwa sababu tunaona kuna msongamano mkubwa katika hospitali za rufaa, endapo Serikali itapeleka vifaa tiba vyya kutosha Madaktari Bingwa wakawepo pia na wauguzi wa kutosha

katika vituo vyetu vya afya na hospitali za wilaya hakutakuwa na msongamano mkubwa katika hospitali ya rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natolea mfano, sasa hivi Hospitali ya Temeke imekuwa hospitali ya rufaa, lakini kunakuwa na msongamano kutokana na hospitali hiyo inahudumua Wilaya ya Kigamboni, pia inahudumia wagonjwa kutoka Wilaya ya Mkuranga na vituo vingine vya jirani. Kwa hiyo naishauri Serikali itenge fedha za kutosha ili kupeleka miundombinu ikiwepo vifaa tiba vya kutosha katika vituo vya afya kuondoa msongamano katika hospitali zetu za rufaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia katika hospitali hizo siyo wote wanaoenda kutibiwa wana uwezo wa kulipa gharama ya bili, wengi wanalipia kwa *cash* na pia hupelekea kutibiwa ugonjwa wao kwa gharama kubwa sana na wakati mwingine wagonjwa hao hypoteza maisha. Naishauri Serikali kupitia TAMISEMI iondoe ile tozo ya maiti kwa sababu ni kero kwa Watanzania, ni kero kwa walipa kodi. Ikumbukwe kwamba marehemu huyo pia alikuwa analipa kodi kwenye Serikali wakati akiwa ananunua bidhaa mbalimbali, hivyo basi katika tozo zote tunashauri Serikali iondoe tozo katika huduma ya kuhifadhi maiti, imekuwa ni kero kwa sababu tunaona maeneo mengi ndugu zetu walioondokewa na ndugu zao huchelewa kuchukua miiili yao kwenye *mortuary* kutokana na kiwango kikubwa cha kulipia. Naishauri Serikali katika bajeti yao iangalie suala hili ni muhimu sana na ni kero kwa wananchi wetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia katika eneo la watumishi. Mheshimiwa Waziri hapa amesema kwamba watumishi lazima wapewe elimu na watumishi hawa wamesema baada ya kuajiriwa wanatakiwa walipe. Naongeza kwa kusema kwamba, sio tu wale ambao wameajiriwa pia wateuliwa wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, wapate elimu ya kutosha ya kujua mamlaka yao ni mwisho wapi kuongoza, kwa sababu tunaona kabisa kuna maeneo mengi ambapo wanatumia mihemko ya kisiasa. Wewe kama kiongozi wa

nchi, kama kingozi wa eneo, kama kiongozi wa mkoa, wilaya unapaswa kufuata maadili au *ethic* za uongozi, hata kama una itikadi ya chama, lakini hupaswi kuionesha hadharani.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumesikia hivi karibuni kuna Mkuu wa Mkoa anatoa tamko kwamba nitahakikisha kwamba Serikali za Mitaa zote, majimbo yote yatakuwa chini ya CCM. Kwa kweli jambo hilo kama ni kiongozi na umesomea uongozi kabisa huwezi kutamka hivyo.

Kwa hiyo tunaomba wapatiwe elimu jinsi ya kuongoza kwa sababu hata Rais wetu anaongoza watu tofauti na huduma anatoa na kama ni maendeleo ni maeneo yote bila kujali itikadi. Kwa hiyo elimu si kwa wale ambao wameajiriwa tu pia kwa wateule. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuchangia eneo moja la watumishi. Kuna watumishi ambao ni kina mama ambao hupata ujauzito na kujifungua, siyo wote ambao wanajifungua kwa njia ya kawaida, wengine hujifungua watoto wa chini ya umri, watoto njiti (*pre-mature*) lakini wanapewa likizo sawasawa na yule aliyejifungua kwa kawaida na likizo hiyo ni ya miezi mitatu tu. Ikiwa mwanamke amejifungua mtoto wa miezi mitano, anahitajika kukaa hospitali kwa miezi minne, unakuta likizo ya uzazi inaishia pale pale hospitalini. Mwingine *mashallah* Mwenyezi Mungu amemjalia akapata watoto wawili, watatu mpaka wanne lakini likizo ni ile ile ya miezi mitatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naishauri Serikali watumishi wa Serikali wanaotakiwa kukaa likizo ya uzazi, kwa wale wenye mahitaji maalum kama hao, waipitie sheria ile na kuweza kuongeza angalau wapewe muda maalum wa kuweza kukaa na kuwahudumia wale watoto, kwa sababu muda mwingi unakuta wako pamoja hospitalini na wengine wamezaa watoto zaidi ya mmoja tofauti na mwanamke mwingine. Kwa hiyo, naishauri Serikali ione haja sasa ya kupitia sheria na kuongeza muda kwa akina mama ambao wamejifungua watoto njiti au mtoto zaidi ya mmoja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni la kukaimishwa, sehemu nydingi wafanyakazi wamekaimu. Kwa hiyo, naishauri Serikali, kwa sababu kuna *shortage* ya wafanyakazi na watu wako *competent* mmeshawakaimisha mnajua kabisa wana uwezo wa kufanya hizo kazi, iwaajiri moja kwa moja kwenye nafasi zao na siyo kuwakaimisha kwa muda mrefu. Huwezi kuwa kwenye nafasi ya kukaimu zaidi ya miaka miwili, mitatu. Kwa hiyo, naishauri Serikali, sioni haja ya kuendelea kuwa na makaimu wakati uwezo wa kazi wanao, naomba wawaajiri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ni hali ngumu ya maisha kwa wananchi wetu, kila kukicha afadhali ya jana. Naishauri Serikali ione haja sasa ya kuongeza kipato cha mwananchi wa kawaida hasa mfanyakazi. (*Makofii*)

(Hapa kengele lilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Tunaendelea na Mheshimiwa Sophia Mwakagenda, ajiandae Rehema Migilla halafu atakuja Mheshimiwa Marwa Ryoba na Mheshimiwa Hamoud Jumaa ajiandae.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami nashukuru kupata muda wa kuchangia Wizara hizi mbili, kwanza kabisa nitaanza kuzungumzia TAMISEMI.

Mheshimiwa Mwenyekiti, zaidi ya asilimia 60 ya fedha za elimu zinaenda katika Wizara hii ya TAMISEMI na hasa kwa ajili ya majengo na *infrastructure* zote za mambo yanayohusu elimu. Sisi sote tunafahamu TAMISEMI inashughulika na elimu ya msingi na sekondari na hapo ndiyo kwenye msingi hasa wa kutengeneza Taifa la kesho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ripoti ya *CAG* ya mwaka 2016/2017, inaonesha mapungufu yaliyopo katika Wizara ya TAMISEMI ambapo asilimia 85 ni madara, asilimia 52 ni upungufu wa madawati, asilimia 86 ni vyoo na mashimo na

matundu lakini asilimia 88 ni kwa ajili ya mabweni. Tunapozungumzia *infrastructure* kwa ajili ya elimu ya watoto wetu wa msingi na sekondari, ni lazima kama Wizara ijipange upya na kujua kwamba watoto hawa ambao tunawatengeneza kuwa Taifa zuri la kesho tuwawekee mazingira mazuri ya kuweza kujisomea. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mpaka sasa bajeti tunayopitisha sisi Wabunge, ndugu zetu wa TAMISEMI hawapati zote. Naomba Serikali wanavyokuja kujibu waniambie kwa nini bajeti haiendi yote maana tunapopanga bajeti sisi kama Wabunge, tunataka kusaidia jamii na hasa wananchi tunaowaongoza waweze kufikia malengo tuliyoyakusudia. Kwa hiyo, natoa ushauri kwa Wizara na Serikali pia, tunahitaji asilimia 25 zaidi ya bajeti iliyopangwa ili iweze kukidhi mahitaji yanayohitajika katika Wizara hii. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, shule za msingi zina upungufu, na hii natoa kwenye ripoti ya CAGya mwaka 2016/2017. Katika shule za msingi kuna upungufu wa madarasa zaidi ya 85,000. Hii ni idadi kubwa sana kwa nchi yenyewe watu wengi kama Tanzania.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mwaka 2018, Serikali kupitia Waziri wa TAMISEMI, aliahidi kujenga madarasa mapya 10,140 lakini mpaka leo hakijafanyika chochote. Serikali inapoahidi na ilizungumzia kwamba itatoa zaidi ya shilingi bilioni 29 lakini mpaka leo hazijatolewa. Tunajua kweli tunanunua ndege na vitu vingine lakini usipowapa elimu watoto wako na tayari tuko kwenye Jumuiya ya Afrika Mashariki, ushindani wa ajira utakuwa mgumu sana miaka mitano au kumi ijayo. Ndiyo hapo tunakuja kusema lazima tuwe na mipango ya muda mrefu kwa ajli ya kusaidia kizazi chetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejaribu kuainisha vitu muhimu na vipaumbele kama Taifa tunavyotakiwa kuvifanya. Kwanza lazima bajeti iongezwe na mazingira ya kujisomea lazima yawe mazuri. Walimu ambao wao ndiyo wanaosimamia hawa watoto, muda mrefu

hawajapandishwa madaraja, mishahara haijaongezwa, tusitegemee hawa watu watafanya kazi kwa bidii na kwa ubunifu. Sote tunafahamu mwalimu anayefundisha mtoto wa darasa la 1 mpaka 5, ni lazima awe mwalimu anayejitolea na kujituma na kufanya kazi kwa uaminifu ili kujenga msingi wa mtoto mdogo. Sisi Wabunge hapa wengi tunapeleka watoto wetu kwenye shule ambazo zinalipa vizuri labda ndiyo maana hatuoni uchungu kwa ajili ya watoto ambao wako chini na wanasoma bila kuwa na mpangilio mzuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Tuongeze ajira kwa walimu, uwiano wa watoto na walimu ni tofauti. Mwalimu mmoja shule *standard* watoto 30 - 35, naijua Shule ya Msingi Majimatitu ina watoto 200 mwalimu mmoja, hiyo siyo sawa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile ni muhimu kuweka uwazi wa Wizara katika programu na mipango mbalimbali endelevu kwa ajili ya kusaidia watoto wetu. Tunaomba Wizara husika itafute wadau iweze kujifunza, pamoja na kukataa takwimu ambazo sisi Bunge tulikataa lakini bado tunahitaji wadau watupe hali halisi ya takwimu kule chini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye elimu tulizungumzia habari ya kuondolewa kwa VAT katika taulo za kike Bunge lililopita. Hakuna utekelezaji uliofanyika wa kupunguza bei kwenye taulo za kike. Tunaiomba Wizara aidha, irudi nyuma tena, irudishe VATlakini itamkwe kwamba tunatoa VATkwa wale wanaopeleka taulo za kike kwenye shule za msingi na sekondari tu, vinginevyo tumewapa faida wafanyabiashara ambao wameendelea na lile punguzo la tozo ya VATlakini wakati huo huo watoto wetu hawapatii huo msaada wa taulo za kike. Tunaomba Serikali na hasa Wizara ya TAMISEMI isimamie suala hili. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie posho za Wenyevitii wa Serikali za Mitaa pamoja na Madiwani. Hawa watu ndiyo wanakaa na wananchi chini zaidi kuliko sisi Wabunge lakini posho zao, mpaka sasa kuna baadhi ya Halmashauri zimekopa, Madiwani hawajalipwa vikao

mbalimbali, ikiwemo na viongozi wetu wa vitongoji na vijiji na Serikali za Mitaa. Tusitegemee ufanisi wa kazi kama hatuwezi kuwalipa, sisi Wabunge maslahi yetu tunayapigania na yanafanikiwa. Tunaomba pia Serikali muwatazame watu hawa muweze kuongeza posho na mishahara yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa niende kwenye suala la utawala bora. Tatizo la viongozi sisi Watanzania, tunafikiri tuonavyo sisi ndivyo ambavyo na watu wa kawaida wanaona. Watanzania wa leo siyo wa jana, watu wa Tanzania wanaona, tuna teknolojia, watu wanaangalia simu nchi nyininge wanafanyaje. Leo hii mukutano wa Chama cha Upinzani unazuiliwa, mita 15 kutoka kwenye huo ukumbi unaozuiwa watu wa CCM wanafanya mukutano, tusijenge chuki zisizokuwa na maana. (*Makofi*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango wako, kengele ya pili hiyo. Tunaendelea na Mheshimiwa Rehema Migilla halafu Mheshimiwa Marwa Ryoba, Mheshimiwa Hamoud Jumaa na Mheshimiwa Azza Hamad wajandae.

MHE. REHEMA J. MIGILLA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipata nafasi nami jioni hii nichangie hotuba iliyopo mbele yetu. Awali ya yote, napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa nanyi jioni hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia napenda kuwashukuru wanachama wa Chama cha Wananchi *CUF*, kwani kwa kupitia wao kwenye Mkutano wetu wa Saba tumeweza kumchagua Mheshimiwa Prof. Ibrahim Haruna Lipumba kuwa Mwenyekiti wetu mpya. Hakika wana-*CUF* tunaweza na Mheshimiwa Prof. Lipumba ndiyo Mwenyekiti wetu halali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, moja kwa moja, naomba nijielekeze kwenye mada na nitajikita kwenye suala la upandishwaji wa mishahara ya watumishi wa umma. Ni ukweli

ulio wazi kwamba tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani watumishi hawa wa umma hawajaweza kuongezwa mshahara wao. Itambulike kwamba *annual increment* ni takwa la Kikatiba kwa mujibu wa *Standing Order* lakini watumishi hawa wa Tanzania kwa miaka mitatu mfululizo hawajaongezwa mshahara kama Katiba inavyosema. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunataka tujue ni lini sasa Serikali yetu itawaongeza mishahara hawa watu ambao wanafanya kazi katika mazingira magumu na wanafanya kazi pasipo motisha wa aina yoyote? Nataka niiulize Serikali, kwa sababu kupandishwa mishahara ni takwa la kisheria, je, iko tayari sasa kuwapa mishahara yao kwa mkupuo ambayo wame-delay kuwapa kwa miaka mitatu? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine nataka nijikite kwenye vitambulisho vya wajasiriamali. Hivi karibuni Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Maguful alitoa vitambulisho 670,000, lengo ikiwa ni kuwatambua hawa wajasiriamali wadogo lakini pia ni kuwatafutia mahali ambapo watafanya biashara zao pasipo kubughudhiwa kwa aina yoyote. Mimi sikudhani kama hili lilikuwa ndiyo hitaji lao haswa la kuwatambua hawa wafanyabiashara ns wajasiriamali wadogo. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nasema haya nikiwa na sababu kwamba wafanyabiashara hawa kwanza wanatakiwa walipe Sh.20,000 ambayo baadhi yao ni kubwa mno. Unamkuta mama anauza mbogamboga, mtaji wake ni Sh.3,000 lakini unamtaka mjasiriamali huyu mdogo ali pe Sh.20,000 anaitoa wapi? Hata kama tunataka tuongeze mapato siyo kwa namna hii. Nashauri Serikali ifanya tathmini itambue, je, hawa wajasiriamali wadogo wanahitaji kutambuliwa au wanahitaji mitaji? (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na kwamba lengo ni kuwatambua na kuwatafutia mahali pa kufanya biashara wafanyabiashara wadogo lakini bado maeneo ya kufanya biashara hawana, wanatembea hovyo na bado huko

mitaani wakitembea wanasumbuliwa na Mgambo, bado watendaji wetu huko wanawasumbua. Kwa hiyo, niiombe Serikali sasa iweze kutumiza lengo lake la kuwatambua, lakini pia waweze kuwatafutia mahali pa kufanya biashara ili waweze kufanya biashara kama wafanyabiashara wengine. Kama itawezekana, hii Sh.20,000 ni kubwa sana, tunaiomba Serikali hawa wafanyabiashara wapunguziwe iweze kuendana na mitaji yao. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni upandishwaji wa vyeo na madaraja kwa wafanyakazi *especially* walimu. Suala la kupandishwa madaraja kwa walimu sasa hivi limewekewa masharti magumu sana. Leo hii walimu wanaambiwa watapandishwa madaraja kwa kuangalia bajeti ya Serikali, lakini pia wataangalia *Performance Appraisal* ya huyu mwalimu na uwezo wa Halmashauri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunajua wazi kabisa vyanzo vingi vya mapato vimechukuliwa na Serikali Kuu, baadhi ya Halmashauri hazina vyanzo vya mapato vya kueleweka. Kwa hiyo, kama hizi Halmashauri hazina vyanzo, leo tunawaambia hawa wafanyakazi watapandishwa kwa kuangalia bajeti ya Halmashauri, ni lini hawa walimu sasa au Halmashauri zitawenza kujikidhi mpaka ziweze kuwapandisha hawa walimu madaraja? (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaposema *Performance Appraisal*, kazi ya mwalimu ni kufundisha lakini suala la kusema kumpima kwa kuangalia wanafunzi wamefaulu kwa kiasi gani, hilo suala halimhusu mwalimu. Hivi vigezo vilivyowekwa kwa ajili ya kumpandisha huyu mtumishi naomba viangaliwe kwa jicho lingine tena kwa sababu ni kumbana mwalimu na kumpotezea haki zake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni kuangalia posho za Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji. Kama walivyosema wenzangu, hawa Wenyeviti wa Mitaa na Vitongoji ndiyo viongozi wa kwanza katika maeneo yetu. Hawa watu wanasumbuliwa usiku kucha, watu wakipigana huko na wake zao kwa Mwenyekiti wa Mtaa, mtu amekosea

njia, amepotea anakwenda kwa Mwenyekiti wa Mtaa, amlishe na amfanyie kila kitu lakini mtu huyu hana posho wala kitu chochote. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo nilimsikia Mheshimiwa Waitara pale anasema ni kazi za kujitolea na wawe na shughuli nyingine. Kama Serikali imepanga hadi bajeti ya kuweza kusimamia Uchaguzi wa Serikali za Mitaa, ina maana tunawatambua hawa watu lakini leo hii tunasema ni kazi ya kujitolea. Kama ni kazi ya kujitolea basi kulikuwa hakuna haja ya kutenga hata bajeti kwa ajili ya uchaguzi wa kuwachagua viongozi hao. Naiomba Serikali iwatambue watu hawa, wao ndiyo wanafanya kazi kubwa na ndiyo hata sisi tunapopatia kura zetu huko. Naomba tuwaangalie hawa watu kwa jicho la tatu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni elimu bure. Suala hili ni zuri sana, kwanza limeweza kusaidia watoto wa kimaskini waweze kwenda shule kwa wingi lakini pia wazazi wamepunguza baadhi ya gherama kwa elimu bure. Hata hivyo, hili suala la elimu bure haliendi sambamba na uongezekaji wa miundombinu. Sasa hivi asilimia ya wanafunzi itakuwa ni kubwa sana lakini miundombinu ni ile ile, madarasa yale yale na matundu ya vyoo yale yale. Kama tutakuwa tunajisifu tu tuna elimu bure ilhali tunachofanya pale ni kuongeza idadi ya wanafunzi lakini *quality education* haipo. Ili tuweze kupata *quality education* ni lazima basi hii elimu bure iende sambamba na ongezeko la wanafunzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, vilevile kumekuwa na matatizo sana sasa hivi wanafunzi wengi wamechelewa kuanza kidato cha kwanza kwa sababu madarasa hayakuwepo na ndiyo maana wadau wengi wa elimu wamejishirikisha kwa njia moja au nyingine kuhakikisha madarasa yanapatikana. Niiombe Serikali kama kweli tunataka kuboresha elimu yetu, tutumie takwimu za maoteo, takwimu zipo zinafanya kazi gani? Kama kweli takwimu zinafanya kazi leo Serikali ingekuwa haina mzigo wa kujua wilaya fulani kuna upungufu wa madarasa ama nini, ni kwa sababu tu hizi takwimu za maoteo hazitumiki. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, suala lingine ni *TASAF*. Tunaelewa kabisa kwamba *TASAF* ni mpango wa kunusuru kaya zilizo maskini na mradi huu ni mradi unaofadhiliwa na mashirika ya nje ya nchi lakini nachokiona kwenye *TASAF* bado hatuna nia ya dhati kabisa ya kuwasaidia hawa watu wa kaya maskini. Unakuta pesa anayopata mtu wa Dar es Salaam ni sawasawa na anayopata mtu Ulindwanoni huko Kaliua. Tuelewe kabisa kwamba tuna lengo la kuzisaidia hizi kaya maskini lakini hizi kaya maskini ziko maeneo tofauti na zina mahitaji tofauti. Kama tunawapa pesa ambayo inatolewa kwa kiwango kile kile, kwa maeneo tofauti, tunakuwa hatufanyi sawa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo Dar es Salaam ...

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante. Sasa ni zamu ya Mheshimiwa Marwa na Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, Mheshimiwa Azza, Mheshimwa Mgimwa na Mheshimiwa Frank Mwakajoka wajiandae.

MHE. MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushuru sana. Naomba nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kunipa uzima niweze kuchangia leo tena hapa kwenye hii hoja ya TAMISEMI. Kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, ni moja ya Mawaziri ambao wako *very humble and mobile*.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kipindi nikiwa ng'ambo ile, Mheshimiwa Jafo alitutembelea Wilaya ya Serengeti akaona jitihada zetu kwenye Hospitali ya Wilaya ya Serengeti, Jafo hakusita akatuletea fedha na hospitali inaendelea vizuri. Nikushukuru sana kwa mwaka huu Mheshimiwa Jafo umetupa shilingi milioni 500, Mungu akubariki sana lakini pia naomba unifikishie salamu hizi kwa Mheshimiwa Rais. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukisoma Biblia Zaburi ya 11:3 Biblia inasema, "Kama misingi ikiharibika, mwenye haki

atafanya nini?" Hakuna ubishi kwamba nchi huko nyuma ilikokuwa inaenda ilikuwa inaenda kubaya kweli kweli. Upande wa kule ng'ambo walikuwa na nguvu sana kwa sababu kwa kweli mambo hayakuwa mazuri. Nakumbuka kabla sijawa Mbunge, nikiwa Diwani na wanasiasa wengi waliojifunzia upande wa kule kama mimi, hoja kubwa waliyokuwa wanaitumia ni ujisadi. Ujisadi ulikuwa ni tiketi ya wewe kuhakikisha unaing'oa CCM. (*Kicheko/Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ndugu zangu tukubaliane ukweli, kwa mfumo ambao Mheshimiwa Rais Magufuli amekuja nao, kwanza kwa kuanzisha kitu kinaitwa *Treasury Single Account* ni mfumo bora ambao hakuna kiumbe yejote anaweza ku-*temper* nao kirahisi. Unalipa kila mtu anaona; Serengeti wamelipa hiki, wamefanya hiki na kinakuwa *evaluated*. Kwa hiyo, namshukuru sana Mheshimiwa Dkt. Magufuli. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza Mbunge mmoja ng'ambo ile anasema kwamba, *decision making* iliyofanywa na Chama cha Mapinduzi, chini ya Mwenyekiti, Rais wetu Mheshimiwa Dkt. Magufuli kununua ndege kwamba ni maamuzi mabaya. Ngoja niwaambie, wakati wengine tukiwa nje ya Bunge hili kipindi kilichopita, waliokuwa wanaipinga Serikali kwa nini hakuna ndege za nchi, mmojawapo alikuwa Mheshimiwa Mch. Msigwa. Akasema nchi gani hii hatuna ndege! Alikuwa Mheshimiwa Mch. Msigwa huyu. Ndege zimenunuliwa anaanza kupiga kelele. Hawa watu vinyonga hawa. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukikaa ukamsikiliza Mheshimiwa Mch. Msigwa, kila siku anaongelea uwanja wa Nduli, hivi uwanja wa Nduli uko Jimbo gani? Si Iringa? Anasema watengeneze uwanja wa Nduli. Sasa watapeleka ndege gani? Hawa ndege wanyama au! Ndege wa angani ndiyo wataenda kwenye uwanja wa Nduli! Si lazima tununue ndege ziende kule ili kuleta watalii watakaoenda *Ruaha National Park*. Watalii wataendaje *Ruaha National Park* bila ndege? Kwa hiyo, lazima tununue ndege. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuna mtu unapinga *Stieglers Gorge*. Hivi jamani, si tumeona kila siku, sisi tunajua hapa, si tunaelewa! Mheshimiwa Rais amesema tunataka umeme rahisi. Umeme rahisi ni wa maji. Labda ile Kambi wangesema sisi Kambi ya Upinzani tumefanya utafiti, tumegundua umeme rahisi ni wa gesi. Hizo tafiti mlizofanya ziko wapi Mheshimiwa Mch. Msigwa? Serikali ya Chama cha Mapinduzi imefanya utafiti wa vyanzo vyote vya umeme, imegundua umeme rahisi ni wa maji. Leo utatokea wapi? Ni *Stieglers Gorge*, yaani unapinga na hiyo? Aaaah mura! (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niwaambie Serikali ya Chama cha Mapinduzi ni Serikali sikivu. Kweli kabisa ni sikivu. *Issue ya kikokotoo*, ni kweli ilipita sheria hapa, tulipitisha Wabunge wote, si na wewe!

MBUNGE FULANI: Eeh!

MHE MARWA R. CHACHA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ilipitishwa hapa. Mheshimiwa Rais alivyo msikivu, Mwenyekiti wa Chama cha Mapinduzi akasikiliza wafanyakazi akasema, hakuna, hii rudisha huko. Sasa hiyo nayo unapinga tena kwamba eti ni maamuzi mabaya! Aaah mura! (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemsikiliza mwingine anasema, Serikali ya Chama cha Mapinduzi waongo, waliahidi mwaka jana shilingi bilioni 29 za maboma, ziko wapi? He, unaishi wapi wewe? Mheshimiwa Dkt. Magufuli alishatoa hela, yaani huko madarasa yanafunikwa, madarasa yanakamilishwa na hakuna watoto watakaoshindwa kwenda shule. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Hamoud Abuu Jumaa, wajiandae Mheshimiwa Azza, Mheshimiwa Mgimwa, Mheshimiwa Mwakajoka, Mheshimiwa Kalanga.

MHE. HAMOUD A. JUMAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze

kuchangia kwenye bajeti hii muhimu. La kwanza kabisa, nichukue fursa hii ya kumpongeza Rais wetu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa ambayo anaifanya na sisi wote ni mashahidi. Kwa sababu hiyo najikumbusha mbali kidogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Bunge liliopita lile 2010/2015 nilisimama Bungeni hapa na nikasema, kule kwetu mimi ni Mganga wa Kienyeji na nilitabiri kwamba CCM itaendelea kutawala miaka 200. Kwa dalili hizi ambazo naona, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kazi alizozifanya, kwa hiyo, utabiri wangu naona utakamilika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na Chama cha Mapinduzi kitaendelea kuongoza kwa miaka mingi. Kuongoza ni kufanya kazi nzuri ambayo wananchi wanaridhika na chama kile ambacho kiko madarakani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, upo ushahidi wa kazi kubwa ambazo zinafanywa na Mheshimiwa Rais na wasaidizi wake; Mawaziri, kazi kubwa wanazozifanya katika nchi yetu, sisi wote ni mashahidi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nachukua fursa hii ya kipekee kumpongeza Mheshimiwa Waziri Jafo kwa kazi kubwa ambayo anaifanya nchi nzima. Sisi ni mashahidi, kila kona anazunguka kuhakikisha mambo yanakwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nina ushahidi kidogo tu. Kwenye Jimbo langu naishukuru Serikali nimepata fedha shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya hospitali ya Wilaya; pia nimepata fedha shilingi milioni 500 kwa ajili ya Kituo cha Afya. Kituo cha Afya hiki kiko Madindu, lakini nimepata fedha tena shilingi milioni 500 ya Kituo cha Afya cha Mlandizi. Haya yote ni mafanikio ya Serikali hii ya Awamu ya Tano. Ninajivunia, tumepata fedha karibu shilingi bilioni saba kwa ajili ya ujenzi wa soko pale Mlandizi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumepata fedha kwa ajili ya kujenga mabweni shilingi milioni 720. Sasa leo ukisema kwamba Serikali haifanyi kitu napata taabu kidogo. Vile vile tumepata gari la Kituo cha Afya Mlandizi pale, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Ummy kwa kazi kubwa ambayo amefanya tumepata pale gari. Haya yote ni mafanikio makubwa sana katika Halmashauri yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, liko jambo moja nataka kuzungumzia. Kuna ujenzi wa bandari kavu pale Kwala, nadhani na Mheshimiwa Jafo anafahamu, lakini liko tatizo moja kubwa pale. Tatizo la pale, tukipata barabara ile ya kutoka Vigwaza mpaka Kwala itatusaida sana kule kusukuma mambo kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili, Waheshimiwa Wabunge wenzangu wameongelea sana suala la *TARURA* kuhusu kuongezewa bajeti, nami naunga mkono suala hili. Kwenye Jimbo langu kuna tatizo kubwa sana la *TARURA* kukosa vyombo vyaya usafiri ili waweze kufanya kazi zao vizuri. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa Jafo, kama mambo yako sawasawa kule atuangalie Jimboni kwetu tupate gari liweze kutusaidia mambo yaweze kwenda vizuri. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninalo jambo moja tu la mwisho, kuna suala zima la Walimu. Pale Jimboni kwangu ni tatizo kubwa, Walimu wanalamika kuhusu kupandishwa madaraja. Kwa hiyo, naomba sana upande huu nao tuweze kuangalia mambo yaende vizuri katika Jimbo pale kwa sababu kama walimu ndiyo wapiga kura wetu na sisi wote tunafahamu, lakini kuna malalamiko makubwa, kwa hiyo, tukiangalia Walimu hawa na yako maeneo mengine wanapandishwa madaraja, lakini sisi bado hatujapanda daraja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nichukue fursa hii ya kipekee tu kuipongeza Halmashauri yangu. Halmashauri yangu mwaka 2018 imekuwa ya kwanza Kitaifa katika ukusanyaji wa mapato. Nawapongeza Madiwani kwa kazi kubwa

ambayo wameifanya kuhakikisha kwamba Halmashauri yetu inaweza kukusanya mapato. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nawapongeze wananchi wa Jimbo la Kibaha Vijiji na mimi mwenyewe kwa kazi kubwa ambazo tunazifanya kwenye Jimbo. Tumeweza kuleta *container* ya vitabu pale lenye thamani ya dola 250,000; juzi tumeshusha *container* moja la Vifaa vya Afya pale hospitali shilingi milioni 400; na tunaisaidia hospitali pale kujenga ukuta ule, karibuni milioni 200. Fedha hizo zote zinasaidiwa na nchi na Mbunge.

Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya kusema hayo, nakushukuru sana. Ahsante sana. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Azza, halafu wajiandae Mheshimiwa Mgimwa na Mheshimiwa Mwakajoka. (*Makof*)

MHE. AZZA H. HAMAD: Mheshimiwa Mwenyekiti, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Awali ya yote nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu, mwingi wa rehema kwa kunijaalia afya na uzima na hatimaye nimeweza kusimama ndani ya ukumbi wako huu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nami nianze kuchangia bajeti ya Ofisi ya Rais TAMISEMI. Leo nitakuwa tofauti sana na mlivyonizoea, nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa kazi kubwa ya utekelezaji wa miradi mikubwa ya Kitaifa ndani ya miaka mitatu. Ununuzi wa ndege, reli ya *standard gauge*, mradi mkubwa wa umeme wa Mto Rufiji, Vituo vya Afya 352 na elimu bure shilingi bilioni 20.8 kila mwezi. Mheshimiwa Rais anastahili pongezi kubwa. Kikubwa kwake tumwombee dua kwa Mwenyezi Mungu, ampe afya njema, umri mrefu aende kuwatumikia wananchi wa Tanzania. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa Jafo, Naibu Mawaziri na Watendaji wote katika

ofisi yake. Mmikuwa mkifanya kazi kubwa ndani ya ofisi ya TAMISEMI. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimejionea mambo makubwa ambayo yamefanya katika Mkao wa Shinyanga na Serikali ya Awamu ya Tano. Nianze kwenye elimu. Mkao wa Shinyanga katika Shule za Sekondari na Shule za Msingi kila mwezi tunapata shilingi milioni 594, kwa nini nisisimame na kumpongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Mkao wa Shinyanga kwa mwaka huu wa fedha uliokwisha tumepata fedha za kujenga na kukamilisha maboma shilingi bilioni tatu ndani ya Mkao wa Shinyanga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, haitoshi, nimetazama ndani ya kitabu cha Mheshimiwa Jafo, hata mwaka huu tumepangiwa fedha tena kwenda kukamilisha maboma kwenye shule zetu, shilingi milioni 425. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niende kwenye ujenzi wa Vituo vya Afya. Katika vituo 352 vilivyojengwa nchi nzima, Mkao wa Shinyanga tumepata vituo tisa ambavyo vimejengwa. Thamani yake ni shilingi bilioni 3.9. Naishukuru sana Serikali na ninampongeza sana Mheshimiwa Rais. Mheshimiwa Jafo, peleka salamu za wananchi wa Shinyanga kwa Mheshimiwa Rais. Wananchi wa Shinyanga na wanawake wa Mkao wa Shinyanga tunamshukuru sana kwa kazi kubwa ambayo ameifanya. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kusema kwamba toka nimeingia ndani ya ukumbi huu wa Bunge, mitaa hii hapa ninayokaa nilikuwa nikisimama tu kuchangia TAMISEMI wanasema, Hospitali ya Wilaya. Hilo ndilo lilikuwa neno langu kubwa. Hakuna mwaka ambao nikisimama na nisiseme ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Shinyanga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, natumia fursa hii kuishukuru sana Serikali, imetupatia fedha, shilingi bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Shinyanga. Haitoshi, katika Halmashauri ya Wilaya ya Ushetu tumepatiwa pia shilingi

bilioni 1.5 kwa ajili ya ujenzi wa Hospitali ya Wilaya. Haitoshi, Halmashauri ya Msalala tumepewa shilingi milioni 500 kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Wilaya ya Shinyanga. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini bado nimetazama katika kitabu cha Hotuba ya Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI, tumetengewa shilingi milioni 400 kwa mwaka huu wa fedha kwa ajili ya kwenda kuboresha Vituo vyetu vya Afya. Nitumie fursa hii kuishukuru Serikali na kuipongeza kwa kazi kubwa ambayo wameifanya. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, aombaye hupewa na abishae hufunguliwa. Baada ya shukurani zangu hizo, namwomba sasa Mheshimiwa Jafo, kwa yale mambo yote makubwa ambayo wameyafanya ndani ya Mkoa wa Shinyanga na Halmashauri zake zote, kuna zahanati ambazo zillanzishwa kwa lengo la kuwa Vituo vya Afya; na alipokuja Makamu wa Rais, Mheshimiwa Mama Samia nilizisema zahanati hizi katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga; Zahanati ya Solo na Zahanati ya Ihalo. Wananchi kwa nguvu zao wamejenga majengo mengi, wodi za wazazi na watoto. Tunaomba angalau tupate hata shilingi milioni 200 ili zahanati hizi ziende zikafanye kazi kubwa ya kuwashudumia wananchi wetu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, bado haitoshi, alipokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu mwaka 2018 niliomba katika Halmashari ya Wilaya ya Kishapu Kituo cha Afya cha Nobola. Kituo kile kinahudumia Tarafa nzima katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Naombe nao muwafikirie waweze kupata fedha kile kituo kiweze kuboreshwa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa upande wa elimu kwa Mkoa wa Shinyanga, namwomba sana Mheshimiwa Jafo, katika Shule za Sekondari, tuna shule ambazo nimekuwa nikizisemea; Shule ya Sekondari Samuye, shule hii iko katika Halmashauri ya Wilaya ya Shinyanga. Tatizo kubwa la shule hii, hii ni Shule ya Kitarafa, wanafunzi wengi wanatoka mbali. Ombi langu kwako ni bweni tu wala sina ombi lingine. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuiombea Shule ya Sekondari ya Ukenyenge ambayo pia ni Shule ya Kitarafa iliyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Ombi kubwa katika shule hii ni bweni. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwekiti, haitoshi. Katika Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga nitumie fursa hii kuiombea fedha Shule ya Sekondari ya *Old Shinyanga* ambayo pia ni Shule ya Kitarafa. Ombi langu kubwa ni ujenzi wa bweni ili tuwaondoe wasichana kurubuniwa barabarani wanapokuwa wanaenda shule na kurudi majumbani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nitumie fursa hii kuzisemea shule zetu za msingi. Alipokuja Mheshimiwa Waziri Mkuu tukiwa Kishapu niliombea Shule ya Msingi Beredi na Shule ya Msingi Mwangili. Mheshimiwa Waziri Mkuu allilipokea na aliyekuwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Kakunda aliahidi kwamba shule hizi zitaletewa fedha. Shule hizi zina msongamano mkubwa...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Mgimwa, halafu wajiandae Mheshimiwa Mwakajoka na Mheshimiwa Kalanga. (*Makofii*)

MHE. MAHMOUD H. MGIMWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nichukue fursa hii kumshukuru sana Mwenyezi Mungu aliyeiwezesha kusimama mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa namna ya kipekee, naomba nichukue fursa hii kumpongeza sana Rais wetu mpendwa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri ya kizalendo anayoifanya katika nchi yetu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jafo na Mheshimiwa Mkuchika, kwa kazi nzuri wanazozifanya, bila kuwasahau Naibu

Mawaziri; mjomba wangu Mheshimiwa Kandege na ndugu yangu Mheshimiwa Mwita Waitara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, mchango wangu utajielekeza katika maeneo makubwa manne. La kwanza ni barabara. Sisi Wabunge tunaotoka vijiji ni ndio tuna mtandao mkubwa sana wa barabara kuliko wanaotoka mjini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, bajeti inayopelekwa *TARURA* ni ndogo sana kuliko bajeti inayopelekwa kwenye miundombinu. Ifike wakati sasa hizi bajeti ziwe 50 kwa 50. *TARURA* wapate asilimia 50 pamoja na miundombinu wapate asilimia 50.

Mheshimiwa Mwenyekiti, tuna sababu za msingi kusema hayo. Kwenye vijiji ndiyo kwenye wakulima na ndiyo kwenye wananchi waliokuwa wengi. Kwa hiyo, malighafi na chakula vinatoka vijiji. Kwa hiyo, tusipoboresha barabara za vijiji ni tatizo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Jafo ni shahidi, nimekwenda Wizarani kwake nikiwa na Mwenyekiti wangu wa Chama cha Mapinduzi Wilaya ya Mufindi kumlalamikia miundombinu ya barabara iliyoko katika vijiji vyetu. Barabara ya kutoka Mtili – Ifwagi – Mdabulo – Ihanu – Isipii mpaka Tazara mpaka Mlimba ni barabara mbaya sana. Toka *TARURA* wameingia madarakani hawajawahi kutengeneza zaidi ya kilometra 30.

Mheshimiwa Mwenyekiti, barabara hii inaunganisha mikoa miwili, Mkoa wa Morogoro na Mkoa wa Iringa. Tumemwomba Waziri aje kwenye barabara hii, lakini hajafika, lakini najua leo atakapokuwa ana-*wind up* atatuambia lini atafika Mafinga, atafika Mufindi kukagua barabara hii, kusudi aweze kuwasaidia wananchi wa maeneo yale wapate usafiri wa uhakika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye eneo hili watu wanakufa kwa sababu miundombinu imematika. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri alione hili jambo.

Kwenye eneo hili tuna vijiji zaidi ya 30, tuna kata zaidi ya tisa, miundombinu haipitiki, kwa hiyo namwomba sana Mheshimiwa Jafo afike kwenye eneo hili. Bahati nzuri alipata nafasi ya kufika Mdabulo Sekondari, akaona hali halisi ya hiyo barabara, yeche ni shahidi. Kwa hiyo, tunamwomba afike kwenye eneo hili na watu wa Mufindi wanataka kusikia kauli yake kuhusu barabara hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine la barabara ni la Tambalang'ombe, Uyole, Ugwenza, Ikweha na Kwatwanga, nalo ni tatizo. Ukienda kwenye Jimbo la Mufindi Kaskazini, haya maeneo hayapitiki kwa sababu yanasmamiwa na TARURA na TARURA hawana fedha hatuwezi kuwalaumu. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri afike kwenye maeneo haya aone hali halisi na aone malighafi za wananchi zinavyoharibika kwenye maeneo haya. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni matumaini yangu Waziri atatembelea kwenye maeneo haya na atajionea hali halisi. Hata hivyo, tunamwomba sana Waziri atuletee upya tuiangalie Sheria ya TARURA, kwa sababu sisi kama Wabunge hatuna *control* ya TARURA, Madiwani hawana *control* ya TARURA, TARURA hawawajibiki kwa Madiwani, hawawajibiki kwa Wabunge, kwa hiyo, TARURA wenyewe ndiyo wanaamua barabara gani itengenezwe. Sisi tuna matatizo ya barabara kama wangkuwa wanahuksika kwa Wabunge au kwa Madiwani, tungewaambia anzeni na barabara hii, hii acheni. Kwa hiyo, kwa utaratibu huu, wanatengeneza barabara wanazozitaka wao, siyo tunazozitaka sisi wawakilishi wa wananchi. Kwa hiyo, Sheria ya TARURA, ibadilishwe, tuiangalie upya, kwamba wawe wanawajibika kwenye Kamati za Fedha za Halmashauri, kusudi tuweze kuwashauri tuanze na barabara gani. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo naomba kuchangia ni eneo la afya. Jimbo la Mufindi Kaskazini lina tarafa nne (4), lakini tuna kituo kimoja tu cha afya na mwaka jana tuliahidiwa kupelekewa milioni 300 kwenye kituo kimoja cha afya, lakini mpaka leo hazijafika. Kwa hiyo, pamoja na kazi nzuri aliyoifanya Mheshimiwa Jafo

ya kutupelekea milioni 400 kwenye kituo cha afya cha Ifwagi, tunaomba kwenye kile kituo kiwepo, tupelekewe milioni 300 na hii ilikuwa ni ahadi ya kipindi kilichopita.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini tusiishie hapa, kwa sababu tuna tarafa nne, *at least* kwenye kila tarafa tupate kituo Kimoja cha afya, tutakuwa tumefikia jinsi gani ya kuwasaidia wananchi. Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Jafo kwenye kila tarafa moja, tupate kituo kimoja cha afya.

Mheshimiwa Mwenyekiti, eneo lingine ambalo nataka kuchangia...

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante, umezungumza sana kwenye barabara muda wako umekwisha. (*Makofi*)

Hongera kwa mchango mzuri. Mheshimiwa Mwakajoka, wajiandae Mheshimilia Kalanga, Mheshimiwa Chatanda na Mheshimiwa Mwijage.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa fursa hii. Awali ya yote nitumie fursa hii kwanza kumpongeza sana Mwenyekiti wetu wa Chama cha Demokirasia na Maendeleo (CHADEMA), Mheshimiwa Freeman Aikael Mbwe, Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, lakini pia nimpongeze pia Waziri Kivuli aliyewasilisha taarifa hii vizuri na naomba tu kwamba taarifa hii kwa jinsi ambavyo imeandaliiwa vizuri, Mawaziri waichukue itasaidia kujenga Taifa hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kuzungumzia sana kuhusiana na utawala bora, mambo yote yanayozungumzwa, maendeleo hakuna na mambo mengine, kama Taifa litakuwa halina utengamano, kutakuwa hakuna maendeleo na maendeleo hayatapatikana. Kwa sababu tunachokizungumza hapa sasa hivi, kila mmoja

analia, leo tukiangalia bajeti za Mawaziri wote, karibu zote hakuna bajeti ambayo imefikia asilimia 70, karibu bajeti zote ziko asilimia 30, 40, na 47 mwisho. Kwa hiyo, tutazungumza sana hapa, kinachohitajika ni fedha, zikipatikana fedha miradi itakwenda kutekelezwa vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tatizo kwa nini miradi hii haiwezi kutekelezwa vizuri na kwa nini fedha haziwezi kupatikana? Sababu ni kwamba tumesahau jambo moja. Katika Taifa hili utawala bora limekuwa ni jambo ambalo ni tatizo kubwa sana na lazima tuliangalie kwa umakini mkubwa sana. Tumefika humu ndani ya Bunge tunafanya siasa, tumefika ndani ya Bunge badala ya kujenga hoja za msingi za kutatua tatizo, ni kwa nini hatupati fedha ni kwa nini hatusongi mbele, tunaendelea kufanya siasa katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Wananchi waliotutuma, hawajatutuma kuja kufanya siasa za namna hii.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka kusema, unapozungumzia utawala bora, una mapana yake, ukizungumzia utawala bora tafsri yake ni kwamba unazungumzia mambo mengi sana ambayo yanahuksiana na maisha ya kawaida ya wananchi. Hata hivyo, unategemeaje maendeleo, kama wananchi wanabaguana, unategemeaje maendeleo kama kuna baadhi ya kikundi kinaonekana ni bora kuliko watu wengine, hayo maendeleo yatatoka wapi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashangaa sana, Mheshimiwa Rais sasa hivi anakozunguka kote huko, ameanza kuwanyooshea vidole Waheshimiwa Mawaziri, anasema hamfanyi kazi vizuri, ameongea na Wizara ya Fedha amesema wamekosea, kwa nini wanaendelea kupandisha kodi, anawaambia *TRA* kwa nini wanafanya hivi, haya yote tumeshayashauri sana, lakini wakatupuuza wakasema sisi hatufai, tunafanya mambo ya hovyo na sisi ni watu ambao hatuwezi kulijenga Taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, lakini ukweli tu, hata angezunguka huko, anachokizunguimza Mheshimiwa Rais ni kitu kidogo sana, lakini kitu kikubwa ambacho lazima tukiangalie, ni kuhakikisha kwamba Taifa linakuwa pamoja. Kama Taifa halijakuwa pamoja, tusitegemee maendeleo katika Taifa hili, tusitegemee wawekezaji katika Taifa hili, kama hatutakuwa pamoja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siasa ni jambo kubwa sana, demokrasia ni jambo kubwa katika maisha ya binadamu, demokrasia ni maendeleo, lakini leo demokrasia katika Taifa hili, kila wanachofanya CCM huku na Serikali yao wanafanya kwa ajili ya uchaguzi ujao, ndicho wanachokifanya, hawafanyi kwa sababu ya maendeleo na ahadi walizotoa kwenye llani yao ya Uchaguzi. Wanafanya mambo yote kwa sababu ya siasa ya kesho ili waweze kufanya vizuri katika uchaguzi unaokuja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, wananchi wanazidi kulia na sasa hivi utawashangaa sana Watanzania, kwa nini Watanzania hawasemi, Walimu wamekaa kimya, hawajapandishiwa mishahara muda mrefu, lakini wamekaa kimya wanawatazama tu. Ukienda kwa wakulima, wamekaa kimya, mazao yao hayanunuliki, soko limeshuka wamekaa kimya wanawaangalia tu. Kwa sababu wakizungumza wanawakamata wanawaweza ndani, wameamua kuwanyamazisha na wao wamekaa kimya, wanataka waone wanaelekea wapi. Wafanyabiashara wamekaa kimya, wananyanyaswa wafanyabiashara katika nchi hii, wamekaa kimya, hawazunguzi kabisa. Leo wanasiasa wameamua kutunyamazisha pia tukae kimya, waendeshe nchi hii kwa hivi wanavyotaka wao, lakini nataka niwaambie, tunakutana kwenye bajeti kila mwaka, tunaangalia utekelezaji wao kwenye bajeti, kila siku, kila Wizara tunakuta wametekeleza chini ya asilimia 50, chini ya asilimia 40, wanatekeleza bajeti hii. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba leo Mawaziri waweke *commitment* hapa, ndani ya Bunge, mbele ya Rais, wamwambie Mheshimiwa Rais, tunataka tutekeleze bajeti

inayokuja kwa asilimia 80. Mbona Halmashauri zetu wamezipa masharti, kwamba kila Halmashauri ihakikishe kwamba inatekeleza kwa asilimia 80, lakini kwa nini Mawaziri hawataki kuiwekea malengo hayo ya kutekeleza kwa asilimia 80. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo lingine ambalo tunaendelea kuwashangaa, wameendelea kujichanganya, wameanza kuchekana wenyewe. Leo mnasema Serikali ya Awamu ya Tano, ina maana Serikali ya Awamu ya Nne, illikuwa ni Serikali ya CHADEMA? Haikuwa Serikali ya CCM? Kwa nini wasizungumze mipango yao ya miaka inayokuja, lakini wanaanza kuzomeana wenyewe, wanasma Awamu ya Tano imekuwa nzuri kuliko Awamu ya Nne. Awamu ya Nne imefanya kazi kubwa, hivi nyie Awamu ya Tano wangejenga chuo cha Dodoma hiki hapa, tungelala na kunywa maji kweli! (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa nini hawawezi kuangalia, kwa nini hawawezi kuweka mipango ya muda mrefu. Serikali ni ya kwao, chama ni cha kwao, muda wote wamepewa madaraka ya kuongoza Taifa hili, leo wameanza kuzoemeana, Awamu ya Nne imefanya vibaya, lakini nataka nikwambie...

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwakajoka subiri kuna taarifa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: We dogo vipi wewe!

MHE. SEIF K. S. GULAMALI: Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumpa taarifa rafiki yangu, muda mrefu wa speech yake aliyokuwa anazungumza hapa au maeleo yake, mengi yanazungumzia kukosoa. Nilitegemea angalau katika muda ambao anazungumza angeweka maombi mawili matatu au ushauri katika maombi ya jimboni kwake, angalau maji, barabara, lakini yote anayozungumza ni siasa ambayo haina

faida kwenye jimbo lake na yeye ni mwakilishi ambaye anatoka kwenye jimbo ambalo... (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante. Mheshimiwa Mwakajoka taarifa hiyo. (*Kicheko*)

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, huyu bwana mdogo siwezi kupokea taarifa yake naona ana matatizo huyu bwana mdogo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kukwambia, ndio maana nimetangulia kusema, leo kila mmoja anazungumza hapa, Waziri wa Fedha alikuja hapa akasema, hakuna fedha. Sasa unaposema kwamba hakuna fedha halafu unataka mimi nianze kusema eti nasifia, nasifia kitu gani wakati hakuna kazi iliyofanyika, hakuna kazi iliyofanyika nasifia kitu gani?

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, jambo kubwa nililolizungumza tunahitaji utawala bora katika Taifa hili. Utawala bora ukiwepo, wawekezaji tunaowataka, wanaweza kuja kuwekeza katika Taifa hili na wakalipa kodi na nchi ikapata fedha.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Taarifa.

MWENYEKITI: Taarifa Mheshimiwa Frank subiri.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, linda muda watu wanana...

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji, unaposema Waziri wa Fedha akisimama anasema hakuna fedha, lakini amesikia, vituo vya afya zaidi ya 352 vimejengwa ndani ya mwaka mmoja. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshatoa zaidi ya shilingi trilioni mbili kwa ajili ya ujenzi wa reli ya kisasa. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tayari tumeshatoa bilioni 1.5 kwa hospitali za halmashauri 67. Anatakiwa aseme mambo ambayo yana ukweli ambayo wananchi wanayaona kwa macho yao, kwamba fedha ipo na Serikali inaendelea kutekeleza miradi ya maendeleo katika majimbo yote likiwemo na jimbo lake ye ye mwenyewe. (*Makofii*)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Frank, taarifa hiyo.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nilifikiri kama Waziri wa Fedha, kwa sababu ndiye anayewaambia Mawaziri wengine kwamba hamtatekeleza kwa asilimia mnazozihitaji kwa sababu fedha hakuna amekusanya chini ya kiwango na anayekusanya fedha ni ye ye. Cha kushangaza, namshangaa, lakini pia kama mama, tukiangalia takwimu za mwaka jana za vifo vyta wanawake na watoto, kati ya vizazi laki moja katika nchi hii, watu wanaopotiza maisha ni vizazi elfu sitini na tano, kwa hiyo, elfu 44 wanakuwa wazima. Sasa huwezi kuniambia kwamba, eti umejenga vituo, unajenga vituo madawa hakuna, unajenga vituo vifaa hakuna, ee, una maana gani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo hii ukijaribu kuangalia kwenye shule zetu za msingi, watoto wanakaa zaidi ya 250 kwenye shule za msingi. Hizo ndizo takwimu ambazo tunazo, lakini leo anatuambia kwamba, eti anasema kwamba fedha zinatoka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninachotaka kuzungumza ni kwamba, lazima tutengeneze utawala bora na nawaambia ndugu zangu, viongozi wa Chama Cha Mapinduzi, Mawaziri pamoja na Mheshimiwa Rais, asikie, wananchi wamekaa kimya, hawajakaa kimya eti kwa sababu wameridhika na utawala huu, wamekaa kimya na wanapata taarifa kwamba mnategemea kwenye uchaguzi ujao mtapeleka polisi wengi, mtapeleka majeshi mengi, lakini wamesema hawatagombana na jeshi la polisi, watakwendwa sasa kujuana na ndugu zao ambao watasababisha wapigwe. Sawa jamani! (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, nataka niwaambie, lazima tuelewane, wanataka kuleta machafuko katika Taifa hili kwa sababu ya uroho wa madaraka. Haiwezekani wamekubali demokrasia, leo wanataka wabaki peke yao, wakati wananchi hawakubaliani na ninyi, wanahitaji upinzani ndani ya nchi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, jana nilikuwa namsikia Mheshimiwa Jenista Mhagama, anasema watu ambao wamechangia kuhusiana na Katiba Mpya, anasema ni watu wawili, watatu.....

MHE. MAULID S.A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Frank taarifa.

MHE. MAULID S. A. MTULIA: Mheshimiwa Mwenyekiti, namheshimu sana mzungumzaji kaka yangu Mwakajoka, lakini nataka nimpe taarifa, si kweli kwamba wananchi hawaipendi au hawakipendi Chama cha Mapinduzi, ni kwamba wananchi wetu huko tunakotoka wameridhika, wanakipenda Chama cha Mapinduzi na mwaka 2020, hali itakuwa mbaya sana kipande cha kule.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hiyo ndiyo taarifa yangu.

MWENYEKITI: Taarifa, Mheshimiwa Frank.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza huyo bwana Akwirina anamlilia sana. Kwa sababu ndiye aliyesababisha Mkurugenzi wake akazuia viapo vya...

MWENYEKITI: Mheshimiwa Frank elekeza hoja yako kwenye kuchangia.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti taarifa.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naendelea....

MWENYEKITI: Taarifa nyingine, Mheshimiwa Frank kaa, taarifa ya mwisho hiyo.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka nimpe Mheshimiwa Frank taarifa kwamba, anayoyasema ni ya kweli, kwamba bila jeshi la polisi CCM haitafika madarakani na uthibitisho upo, Mheshimiwa Frank kwa mfano Kata ya Turwa Tarime, tuliwashinda CCM kwa kura zaidi ya 76 lakini walitupiga mabomu wakachukua wakajitangaza. (*Makof*)

MWENYEKITI: Ahsante, Mheshimiwa Frank.

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, napokea na mimi kwenye kata ya Ndarambo kule kwetu Momba, Mkurugenzi alikuja na polisi zaidi ya 100 ndani ya chumba na akanyang'anya matokeo na akaondoka nayo, kwa hiyo, hili lipo. Kama kweli Mtulia anasema kwamba eti CCM inapendwa na wananchi, wekeni mpira chini...

MWENYEKITI: Ahsante, nilikuongeza dakika moja. (*Makof*)

Mheshimiwa Kalanga atafuatiwa na Mheshimiwa Chatanda na Mheshimiwa Mwijage, Mheshimiwa Amina Makilagi na Mheshimiwa Mbogo wajiandae.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia jioni ya leo. Nianze kwa kuunga mkono hoja, lakini niseme, namshukuru Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kazi kubwa anayoifanya ya kulijenga Taifa letu na kujenga uchumi wa nchi yetu kwa kipindi chake. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, pia naomba nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, TAMISEMI, kwa kazi kubwa

ya kizalendo anayoendelea kuifanya, waendelee kufanya kazi Watanzania wanaona huduma ambayo Wizara yake inafanya kwa Watanzania. Katika wanaopiga kelele hakuna jimbo hata moja la kwao ambalo hajafika na kuweka alama ya utumishi katika miradi mbalimbali ya maeneo yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, ukiangalia wakati mwingine hawasemi, wale wananchi, wanyonge wa Taifa hili wanaohitaji afya, wanaohitaji elimu uliowahudumia ni shukrani mbele za Mungu na wao wanakushukuru. Kwa hiyo, msikatishwe tamaa na maneno ya watu waliokata tamaa wenyewe. (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ukimkuta binadamu asiyeshukuru hata moja jema, ujue binadamu huyo aidha amekata tamaa mwenyewe, au hajui hata anachotakiwa kushukuru au kukipinga. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, ni ngumu sana kuamini kwamba wapinzani wote kwenye Bunge hili wana akili sawa, kwamba wote.....

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Eee, taarifa!

MHE. PASCAL Y. HAONGA: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kumpa taarifa mzungumzaji wa sasa kwamba, anaposema kuna watu wamekata tamaa, ni kwamba yeye ndiye amekata tamaa kwa sababu alikimbia mapambano amekwenda kujisalimisha upande wa pili.

MWENYEKITI: Hiyo siyo taarifa, endelea.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niseme mambo machache kuhusu eneo la jimbo langu, kwamba Mheshimiwa Waziri nakushukuru kwa sababu umetupa milioni 800 kwa ajili ya vituo vya afya. Hata hivyo, Mheshimiwa Waziri akumbuke ana deni la kituo cha

Naalarami, alienda mwenyewe alifika, lakini ana deni kubwa la soko la Mto Mbu, ambalo yeye aliahidi lakini sijaona kwenye kitabu, kwa hiyo, wakati anajibu, naomba anisaidie kwamba ni lini soko hilo tutalijenga.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nataka niseme mambo machache, nimemsikiliza Mheshimiwa Msigwa, kaka yangu, amezungumza akasema, Rais amefanya uamuzi na lazima tuangalie uamuzi tunaofanya na matokeo ya uamuzi huo. Naomba nimtajie mambo kumi aliyofanya Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa miaka hii michache na matokeo yake kwa Taifa hili, kwa sasa na vizazi vijavyo. Halafu mwisho wapime na Watanzania wapime, kama wao hawakubaliani na haya ambayo anafanya, Watanzania watapima mwaka 2020 na watafanya uamuzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa kwanza wa Serikali hii...

MHE. FRANK G. MWAKAJOKA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Frank kaa, muda wetu umekwisha, Mheshimiwa muda wetu umekwisha kaa, taarifa nilishafunga, kaa Mheshimwa Frank kaa chini.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, muda wangu. Rais amefanya uamuzi wa kulifufua Shirika la Ndege, ili kusaidia usafiri wa ndani na nje ya nchi kwa ajili ya utalii na kupata mapato ya Taifa hili. Nataka mmoja asimame aseme ndege haina faida kwenye nchi hii ili Watanzania wapime ni nani anayesema ukweli na nani mchawi wa maendeleo yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Taifa hili ili liwe na uhakika wa uendelezaji wa viwanda na uchumi endelevu, lazima tuwe na umeme wa uhakika. Rais amefanya uamuzi ili tutafute umeme wa maji kwa ajili ya uchumi wa Taifa hili na hao na wao kama wajasiriamali watatumia umeme huo,

nataka atuambie, ni nani kati yenu ambaye hataki umeme kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Rais na Serikali imefanya uamuzi wa kujenga miundombinu ya *Standard Gauge* kwa ajili ya kusafirisha mazao na kusafirisha na kujenga uchumi wa nchi yetu. Nani kati yao ambaye hakubaliani na miundombinu salama kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu na uwekezaji wa taifa hili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la tano, Mheshimiwa Rais wa nchi hii amefanya uamuzi wa kutengeneza taifa la watu wenyewe afya njema, kwa kuamua kujenga vituo vya afya 300 na zaidi ya hospitali za wilaya zaidi ya 60 ili Watanzania wapate afya njema, afanye kazi kwa ajili ya uchumi wa nchi yetu. Nani hataki afya ya Taifa hili iweze kutengemaa. (*Makof*)

WABUNGE FULANI: Oyeee. (*Makof*)

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la sita, Katiba ya nchi yetu inasema, elimu ni haki ya msingi ya kila Mtanzania. Mheshimiwa Rais amefuta ada watoto wetu wanasoma elimu bure ili kupata haki kwa aliye na fedha na asiye na fedha. (*Makof*)

MHE. MCH. PETER S. MSIGWA: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, na sisi Waheshimiwa Wabunge...

MWENYEKITI: Muda wetu umekwisha, Mheshimiwa Msigwa, nilishatoa taarifa tatu huku na huku nne.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: *Don't question me.*

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Rais amefanya uamuzi wa elimu bure ili Mtanzania asiyé na fedha na mwenye fedha waweze kupata haki yao ya Kikatiba ya kupata elimu. Tusijilinganishe tulioko ndani tunaweza kulipa ada kuna Watanzania walioko vijiji ambao hata Sh.5,000 kwa siku ni tabu kwake, hivi leo tubeze uamuzi ambao ukienda kwenye kitabu hiki, ukurasa wa 198, Mheshimiwa Mwakajoka anajua ni kiasi gani cha fedha cha elimu bure kimeenda katika Jimbo lake. Kama ninyi ni waungwana simameni waambieni wapiga kura wetu wakatae elimu bure, wakatae fedha zinazopelekwa kwenye Majimbo yenu ili irudi tuamini kwamba hamthamini elimu bure. (*Makof*)

MBUNGE FULANI: Yes.

MHE. JULIUS K. LAIZER: Mheshimiwa Mwenyekiti, jambo la saba, moja ya tatizo liliopo kwenye nchi yetu ni uchumi wetu haukulindwa na rasilimali zetu zilitumika vibaya. Tumetunga sheria hapa ya kulinda rasilimali za Taifa, leo husikii habari ya utoroshaji wa madini, husikii habari ya ujangili kwa wanyama wetu, halafu ninyi mnataka kuona siyo uamuzi? Nataka tupime matokeo kwa kupata wanyama wazuri pamoja na utalii kwa ajili ya uchumi wa Taifa letu. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, uamuzi wa kutunga Sheria ya Kudhibiti Madawa ya Kulevy na uamuzi kutoa ardhi kwa ajili ya wakulima na mimi nasema Taifa hili liko salama... (*Makof/Vigelegele*)

(Hapa kengele illilia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante kwa mchango mzuri. Tunaendelea na Mhehimiwa Chatanda jiandae Mhehimiwa Mwijage. (*Makof*)

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hotuba mbili; TAMISEMI, Utumishi na Utawala Bora. Nianze kwa kuunga

mkono hotuba hizi lakini naomba uniruhusu ninukuu kutoka kitabu cha Mithali 15:2 inasema kwamba: "Ulimi wa mwenye hekima hutamka maarifa vizuri; bali vinywa vyatapumavu humwaga upumbavu". Mwisho wa kunukuu. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mwenyezi Mungu anisaidie nitumie ulimi wa mwenye hekima katika kumpungeza Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi kubwa ambayo ameendelea kuifanya ndani ya nchi hii. Nampongeza Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mawaziri, Naibu Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wasaidizi wao kwa kazi kubwa ambayo wameendelea kuifanya katika nchi hii.

KUHUSU UTARATIBU

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu utaratibu.

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, mwambie akae chini.

MWENYEKITI: Kuhusu utaratibu na msiingie na uchochoro wa utaratibu.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nasimama kwa mujibu wa Kanuni ya 64(1)(e). Tunapenda kuitumia Kanuni hii lakini labda ama waliyoitunga hawakuitunga vizuri au hatuilewi. Kanuni inasema: "Bila ya kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba inayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge, (e) hatazungumzia mwenendo wa Rais..."

MWENYEKITI: Hebu, rudia Kanuni ya 64 ngapi?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(e).

MWENYEKITI: Endelea.

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, inasema kwamba: "Mbunge, hatazungumzia mwenendo wa Rais, Spika, Mbunge na kuendelea."

Mheshimiwa Mwenyekiti, humu ndani tumekuwa tukizungumzia mwenendo wa Rais. Tofauti yetu sisi upande na huu na upande ule, huku tumekuwa tukizungumzia mwenendo wa Rais ambao tunaona una upungufu na wale wanazungumzia mwenendo wa Rais wanaoona hauna upungufu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, tukabaliane na Kanuni ya 64(1)(e) kwamba ama wote tusizungumzie mwenendo wa Rais au kila mtu azungumzie mwenendo wa Rais kwa kadri anavyoona. Kwa mtazamo wangu naona Kanuni hii inakiukwa. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Soma Kanuni ya 68(10).

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 68(10) inasema: "Uamuzi wa Spika kuhusu suala lolote la utaratibu utakuwa ni wa mwisho."

WABUNGE FULANI: Aaa, sasa mmeamua nini?

MHE. SALOME W. MAKAMBA: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo?

MWENYEKITI: Ndiyo, uamuzi wa Spika ni wa mwisho.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Sikilizeni jamani, hizi Kanuni hazisomwi kama unasoma gazeti, zinasomwa kwa mtiririko.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Kaa chini, endelea Mheshimiwa.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MHE. MARY P. CHATANDA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru. Naona mwanangu alikuwa ananipotezea muda tu lakini naendelea kuwaambia kwamba wananchi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanaridhika na utendaji wa Serikali ya Chama cha Mapinduzi. Kwa kuthibitisha hayo, wananchi wa Korogwe wanaridhika na mwenendo mzima wa utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi unaofanywa na Serikali hii kwa sababu tumeletewa fedha kwa ajili ujenzi wa vyumba vya madarasa, mabweni, za matengenezo ya barabara kwa kiwango cha changarawe na kiwango cha lami na za kumalizia maktaba katika chuo cha ualimu, kwa nini wasiwe na imani na Serikali ya Chama cha Mapinduzi? Naendelea kuwaombea viongozi wetu hawa Mwenyezi Mungu aendelee kuwapa afya njema ili waendelee kusimamia utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika ujenzi wa vituo vya afya, Korogwe Mjini tulipata Kituo cha Afya kimoja cha Majengo. Tunashukuru tulipata shilingi milioni 500 lakini niombi na Mwenyezi Mungu ikiwezekana aendelee kuwapa afya njema mkipata fedha muweze kunisaidia niweze kupata Kituo cha Afya Mgombезi, tuweze kupandisha Zahanati ya Mgombезi iwe Kituo cha Afya. Kule Mgombезi ni nje ya Mji wa Korogwe na kuna mashamba ya m Konge, wananchi wengi wako kule, ni vijiji sita viko pale Mgombезi. Kwa hiyo, tukiwapa kituo cha afya kitawasaidia wao katika matibabu kwa sababu akina mama wajawazito na watoto wanapopata shida usiku ni shida sana kwenda Mjini. Kwa hiyo, wakipewa Kituo cha Afya kule Mgombезi itawasaidia kupata huduma kwa urahisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, halikadhalika, nina Kata ya Kwamsisi, iko nje ya mji, ni mbali na Kituo cha Afya cha Majengo na Hospitali ya Magunga. Nao napenda Mwenyezi Mungu akijalia basi niombi angalau waweze kupata fedha kwa ajili ya kujenga Kituo cha Afya kule Kwamsisi. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nimshukuru sana Waziri wa TAMISEMI, bajeti iliyopita walinipa shilingi bilioni 1.5 nijenge hospitali. Kwa bahati nzuri au mbaya hospitali ambayo ilikuwa ya Korogwe Vijijini iko kwenye Jimbo langu, mkasema hiyo hospitali ibaki mjini wakapewa zile fedha ambazo nilikuwa nimetengewa mimi kwenye Halmashauri yangu ya Mji wa Korogwe. Wenzangu wanajenga hospitali, hospitali ile ambayo imebaki sasa ni ya mwaka 1947, naomba sana muweze kuikumba hospitali hii angalau kupewa fedha kwa ajili ya ukarabati wa majengo hayo makuukuu. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwamba mmetupa fedha tumefanya ukarabati wa shule kongwe ya Korogwe *Girls*, majengo yanapendeza lakini kwa bahati mbaya sana jengo moja la bweni limeshindikana kabisa kukarabatiwa kwa sababu lina nyufa kubwa ambapo Mhandisi amesema halitawezekana kabisa kufanyiwa ukarabati lijengwe moja kwa moja.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kuwa watoto waliokuwa wanakaa kwenye bweni lile ni 120 wamehamishiwa kwenye mabweni mengine, wamesambazwa huko, niombe basi ikiwezekana na Naibu Waziri wa Fedha alifika akaona lile jengo, tupewe fedha ili tuweze kujenga jengo jipya la bweni pale Korogwe *Girls* ili kusudi wale watoto waweze kurudi kwenye lile bweni lao kama walivyokuwa wanakaa mle. (*Makof!*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie masuala ya watumishi, lipo tatizo la watumishi kupandishwa madaraja halafu hawalipwi zile fedha zao baada ya kuwa wamepandishwa yale madaraja. Niombe wanapopandishwa madaraja watumishi hawa basi fedha zao walipwe.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MWENYEKITI: Mheshimiwa Chatanda kwa kujali Jimbo lako, umeongea vizuri sana. (*Makof!*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Mwijage na Mheshimiwa Makilagi na Mheshimiwa Mbogo wajiandae.

MHE. CHARLES J. P. MWIJAGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nikushukuru kwa kunipatia fursa ya kuchangia Wizara hizi muhimu katika maendeleo ya Watanzania. Awali ya yote, niwashukuru Waheshimiwa Mawaziri kwa wasilisho zuri, masilisho lenye vielelezo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, siwezi kuchukua muda mwingi kuzungumzia hilo kwa sababu natoka kijijini kama ni shule nimeziona. Wale waliosafiri kwenda kwetu, Kaitu Kaila kuna misemo inasema mtenda kazi ndiye huleta kazi, mtenda kazi aliyeamua watoto wote waende shule ndiyo aliyeleta kazi. Kwa hiyo, ukiona watoto wako wengi shule hawana madarasa ni kwa sababu mtenda kazi amesema wote waende shule na nina imani mtenda kazi atawafuata kule wale watoto atawapatia madarasa, vyoo na mambo yatakwenda mbele. Kama mtenda kazi asingesema muende shule wala msingewaona na hali ingekuwa siyo nzuri. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, niishauri Serikali miundombinu ya shule inayotakiwa ni mingi, pamoja na jithihad za kujenga miundombinu Serikali itoe vivutio kwa sekta binafsi iingie kwenye kuendesha shule. Vyumba 85,000 Serikali hatutavimaliza kesho sasa sekta binafsi ihamasishwe, ipewe vivutio vya kila namna kusudi na wao waingie kwa sababu vijana hawa hawatasubiri, waweze kwenda kwenye shule hizi walipe pesa kidogo kidogo. Hilo la elimu nimelimaliza na nishukuru kwa kazi zote ambazo mmeefanya kwenye Jimbo langu la Muleba Kaskazini. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, nzungumzie suala la afya. Napokuja kwenye afya niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Muleba Kaskazini lakini niwashukuru wadau wangu wa maendeleo, katika Jimbo langu tumetengeneza zahanati 12. Unajua mtoto anapoanza kufyeka shamba mzazi unamwekea msingi, naiomba Serikali katika maeneo yangu yenye maeneo hararishi kama Kisiwa cha Bumbile ambako kuna shughuli za uvuvi na kuna mapato mengi tunaomba

tuwekewe kituo cha afya. Kuna sehemu za *low lands* upande wa Magharibi mpakani na Karagwe, sehemu za Ngenge tungeweka kituo cha afya kuwasaidia watu wa eneo lile ambao wao wanatembea siyo chini ya kilometa 30, 40 kuweza kupata huduma ama kwenda Muleba au Bukoba Vijijini.

Mheshimiwa Mwenyekiti, napomaliza hilo nizungumzie suala la *TARURA*, tofauti na wenzangu waliozungumza mimi sitawaliwi na asilimia. *TARURA* mnapoijijenga upya mfanye tathmini ya uhalisia wa barabara zenu mlizo nazo na sisi Wabunge tupewe fursa ya kutengeneza Mfuko wa Barabara za Vijijini. *TARURA* amepata ngapi, *TANROADS* amepata ngapi haina tija, tija itokane na kutenga mfuko wa kuweza kutengeza barabara. Kimsingi hata mgao huu unaofanyika unakuta Wilaya moja anapewa pesa nyingi mwingine anapewa kidogo bila kuzingatia uhalisia wa barabara. Kwa hiyo, *solution* ni mfuko yaani shida ya jirani yako isikufanye wewe ufurahi, *TANROADS* apate pesa za kutosha na *TARURA* apate pesa za kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nizungumzie suala la mikopo wanayopewa vijana na akina mama na hili nizungumze nikihusisha na shughuli ya Wizara hii ya TAMISEMI kuhusu suala la viwanda. Nakumbuka katika kitabu kimoja nimewahi kusoma kinachozungumzia mwongozo wa ujenzi wa viwanda katika Tawala za Mikoa na Vijijini kinaeleza watu weledi na maeneo yako kule vijijini. Kwenye vitabu inaonyeshwa kwamba shilingi bilioni 62 zinatumika kuwapa watoto na akina mama, nashauri Serikali mngechukua shilingi bilioni 62 sehemu yake mkanunua matrepta, kwa sababu vijana wengi wako vijijini wapeni matrepta, muwape viwanda badala ya kuwapa shilingi laki mbili mbili, wanakwenda kugawana umaskini. Nichukue fursa nikushukuru Mheshimiwa Jafo namna unavyoendelea kuhamasisha viwanda. Mimi niliachaa viwanda 3,540 nimesikia wewe una 4,000, unanitia moyo, endelea kuhamasisha viwanda. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu suala la watumishi, nichukue fursa hii kuiomba Serikali kwenye sekta ya afya na

elimu tuwatafutie watumishi, pelekeni watumishi kule. Mimi chumba cha darasa hakinipi shida, unaweza kutengeneza makuti ukaweka pale. Nimewahi kulisema na nalisema tena, Muadhama Laurean Cardinal Rugambwa ye ye alianzisha...

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa
Mzungumzaji)*

MWENYEKITI: Ahsante. Muda wetu umekwisha, Mheshimiwa Makilagi dakika tano na Mheshimiwa Mbogo dakika tano.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli nilitaka kusema kama ni dakika tano niongee kesho kwa sababu nina salamu za wanawake wa Tanzania ambao mimi ndiyo wapiga kura wangu.

MWENYEKITI: Basi utaongea kesho, Mheshimiwa Mbogo malizia dakika kumi hizo. Mheshimiwa Richard Mbogo, umejitoa? Sikusikii, naona unainama, unakaa.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ameomba niendelee, amenipa zake zimekuwa kumi.

MWENYEKITI: Haya.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante na nimshukuru sana kaka yangu Mheshimiwa Mbogo na nichukue nafasi hii kukupa pole na msiba mkubwa uliokupata wa kuondokea na mama.

Mheshimiwa Mwenyekiti, ninaona maneno mengi yanazungumzwa humu ndani sasa nimesimama Mbunge ninayewakilisha wanawake wa Tanzania na Jimbo langu ni Tanzania nzima. Hapa naleta salama za wanawake wa wa Tanzania ambao wamekuwa wakifariki kwa kujifungua kwa sababu ya kukosa huduma, ambao wamekuwa wakitembea umbali mrefu kwenda kutafuta huduma za afya, ambao vituo vilikuwa ni duni havitoi huduma kikamilifu, wakienda leba

wanafariki, kwa uongozi wa Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli Serikali imewajengea vituo zaidi ya 350.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wamenituma nilete salama za ahsante kwa Mheshimiwa Rais. Wanasema ahsante kwa Serikali ya Chama cha Mapinduzi na wanamshukuru sana Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli na wanasema achutame maana ukiwa kwenye maji unaoga akija mwendawazimu haumfukuzi na akutukanaye hakuchagulii tusi. Wanaosema Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli hajafanya kitu tuwasamehe maana hawajui watendalo, ndiyo salamu walizonipa. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, wanamshukuru Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli kwa sababu Mikoa ya Geita, Simiyu, Kigoma, Mwanza, iko sita ambayo wanawake wallikuwa wanafariki kwa kujifungua kwa sababu ya kukosa huduma, kwenye taarifa ya Mheshimiwa Jafo imeeleza ambavyo Serikali inakabiliana na changamoto hizo. Kwa hiyo, ukisikia mtu anabeza tena bahati mbaya wanaongea ni wale ambao hawakwenda leba, tunasema akutukanaye hakuchagulii tusi na ukiwa kwenye maji unaoga akija mwendawazimu haumfukuzi. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kumwambia Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli endelea na kazi, tunakuona unahangaika Nyanda za Juu Kusini, leo umefungua vituo vya afya, umekwenda Mikoa ya Mtwara, leo uko Njombe, umekwenda Ruvuma na unakwenda Katavi, unakwenda Tanzania nzima kuwalettea wananchi maendeleo. Chapa kazi baba, tuko nawe na wanawake wa Tanzania na leo nimekuja na *book* hili ndiyo kazi ulizozifanya na nimewauliza wanasema tukipiga kura leo anashinda kwa asilimia 100. (*Makofii*)

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, wanasema atapita bila kupingwa.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kuhusu Utaratibu.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, baada ya utangulizi huo, napenda kuchukua nafasi hii...

MWENYEKITI: Kuhusu Utaratibu.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti...

MWENYEKITI: Kanuni.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Kanuni ya 64(1)(a), inasema: "Bila kuathiri masharti ya Ibara ya 100 ya Katiba yanayolinda na kuhifadhi uhuru wa mawazo na majadiliano katika Bunge, Mbunge, hatatoa ndani ya Bunge taarifa ambazo hazina ukweli". (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa anayechangia ametoa taarifa ambazo si za kweli. Tunajua kwamba Tanzania tuna kata zaidi ya 4,000 na kwa Sera ya Afya inatakiwa kila kata iwe na kituo cha afya. Kwa takwimu tu alizozitoa mwenyewe amesema vimejengwa vituo mia tatu thelathini na kitu na nadhani vilikuwa kama 400 hivi. Kwa hiyo, ukitoa utaona zaidi ya kata 3,000 ambazo zina *suffer* wanawake wanakufa. Hata ukipitia taarifa vifo vya mama na mtoto ni vingi sana kama Taifa bado hatujavipunguza. (*Makof*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, pamoja na kwamba amepotosha anazungumzia wanawake wote ambao...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa kaa chini.

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa kaa chini. Mheshimiwa Makilagi, endelea. (*Makofi*)

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, inabidi nicheke tu kwa sababu ni mwanangu ana stress naomba tumsamehe kwa sababu ni juzi tu alikuwa na shida. Mimi kama mama nina kazi ya kufanya *counseling* nitaendelea kwa sababu kama angekuwa.....

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ana uchungu na anajua kuna pengo angeanza kuonesha Tarime ambayo inapata fedha nyngi kutokana na madini lakini...

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, afute kauli yake.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee nimesema kama mama nitaendelea kumlea mwanangu, nitazungumza naye...

MBUNGE FULANI: Afute kauli yake.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Ni juzi alikuwa na shida nahitaji kumsaidia.

WABUNGE FULANI: Afute kauli yake.

(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba niendelee kwa kusema kwamba Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli amefanya kazi nzuri...

*(Hapa baadhi ya Wabunge walizungumza bila kufuata
utaratibu)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Sophia Mwakagenda,
Mheshimiwa Salome Makamba *last warning*.

MBUNGE FULANI: Mheshimiwa Mwenyekiti, taarifa.

MWENYEKITI: Kiti hakijasikia bado.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa
Mwenyekiti, taarifa.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Maryam, kaa
chini.

MHE. MARYAM SALUM MSABAHA: Mheshimiwa
Mwenyekiti, sasa nikae viperi chini?

MWENYEKITI: Hutaki kukaa chini?

MBUNGE FULANI: Huyo mama ajiheshimu.

MWENYEKITI: Sema tena hutaki kukaa chini?

WABUNGE FULANI: Sema.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Makilagi, endelea na
mchango wako.

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti,
ahsante kwa kunipa nafasi. Naomba niendelee kujielekeza
katika mchango wangu kama ambavyo nimejiandaa.
Naendelea kumpongeza Dkt. John Pombe Magufuli kwa kazi
mzuri, Tanzania nzima maana kwenye llani ya CCM aliahidi
na ametekeleza kwamba tutajenga sekondari, shule za
msingi, watoto watasoma bure na ukisikia watu wazima
wanapiga kelele wameshikwa pabaya, leo nimekuja na
takwimu zinazoonesha kila shule imepata nini. (*Makofii*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwenye Mkoa wetu wa Mara peke yake Serikali yetu imetupelekea zaidi ya shilingi bilioni 1.7; kwenye hospitali zetu zote za Wilaya kila kila Halmashauri tumepata shilingi bilioni 1.5; kwenye vituo vya afya, hivi ninavyozungumza anajiaandaa kujenga siyo hivi vilivyomalizika sasa hivi vingine vipyta kwenye Mkoa wa Mara peke yake shilingi bilioni 2 zinakwenda na Mikoa yote ya Tanzania karibu shilingi bilioni 65. Tumpe nini Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli zaidi ya kumpa kura za ndiyo uchaguzi utakapofika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, tunaipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi na nichukue nafasi hii kuipongeza Bunge letu la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania chini ya maelekezo ya Mheshimiwa Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli alisema tuwawezeshe wanawake kiuchumi. Tumewahamasisha wamejiunga katika vikundi vya vijana na wanawake na watu wenye ulemavu na kupitia Bunge hili tulipitisha sheria ili sasa suala la kutoa fedha kwa asilimia kumi ya wanawake na vijana isiwe jambo la hiari liwe ni la lazima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, napenda kuchukua nafasi hii kusema karibu Halmashauri nyingi zinafanya vizuri. Hata hivyo, naomba nitoe ushauri, kuna Halmashauri wanakaidi kutekeleza agizo hili, naomba nitumie nafasi na Mheshimiwa Jafo tunakuamini ni mtendaji hodari na mahiri, hebu orodhesha Halmashauri zote ambazo zimeshindwa kutekeleza Azimio la Bunge na matakwa ya sheria ya kutenga asilimia 10 kwa ajili ya vikundi vya wanawake na vijana ili hatua zinazostahili ziweze kuchukuliwa na vikundi vya wanawake na vijana viweze kupata mkopo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, baadhi ya Halmashauri zetu ziko taabani, hazina vyanzo vizuri vya mapato kutohana na hali halisi ya Mikoa yao. Nashauri...

MWENYEKITI: Ahsante Mheshimiwa Makilagi kwa mchango mzuri. (*Makofi*)

MHE. AMINA N. MAKILAGI: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante, mengine nitachangia kwa maandishi. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Waheshimiwa Wabunge, hakuna nchi isiyokuwa na changamoto, hata Marekani kuna changamoto, hata Uchina na utajiri waliokuwa nao bado kuna sehemu zina changamoto. Kinachofanywa na Serikali ni kuzitattua na kuzipunguza changamoto hizo, ndiyo hatua ya mpango wa miaka mitano, mitano. Hata mbuyu ulianza kama mchicha na hatimaye tutafika tutakuwa mbuyu.

Waheshimiwa Wabunge, la mwisho, mwenye vivu ajinyonge. Naahirisha Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi. (*Makofi/Kicheko*)

*(Saa 1.44 Usiku Bunge liliahirishwa hadi Siku ya Alhamisi,
Tarehe 11 Aprilli, 2019 Saa Tatu Asubuhi)*